

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 17 Mei, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. MUSSA R. SIMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA VIWANDA, BIAHARA NA UWEKEZAJI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

Na. 219

**Madai ya Wazabuni**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE (K.n.y. MHE. BERNADETA K. MUSHASHU)** aliuliza:-

Wazabuni wanaotoa huduma shuleni wanaidai Serikali fedha nyingi kwa huduma walizotoa miaka iliyopita.

(a) Je, Serikali inadaiwa fedha kiasi gani na kwa miaka ipi na wazabuni hao?

(b) Je, ni lini madai hayo yatalipwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa wapo wazabuni mbalimbali ambao wanaidai Serikali baada ya kutoa huduma Serikalini. Wapo wazabuni waliotoa huduma za vyakula katika shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum za msingi na shule za bweni za sekondari na wazabuni waliochapisha na kusambaza vitabu shuleni. Kiasi cha shilingi bilioni 54.86 zinadaiwa na wazabuni waliotoa huduma ya chakula, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 9.907 ni za wazabuni waliotoa huduma ya uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya shule za msingi. Hivyo jumla ya deni ni shilingi bilioni 64.767.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa madeni haya ni yale yaliyojitokeza kabla ya Serikali kuanza kutekeleza elimu msingi bila malipo. Kwa kutambua umuhimu wa kuwalipa wazabuni hawa Serikali kupitia Wizara ya Fedha imeshalipa jumla ya shilingi bilioni 13.239 hadi kufikia Mei, 2016. Wazabuni wengi ambao madeni yao hayajalipwa hadi sasa wataendelea kulipwa kwa awamu kwa kadri ya uwezo wa Serikali na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba wazabuni hawa wawe na uvumilivu kama ambavyo wamekuwa wakifanya wakati Serikali ikiendelea kulipa madeni haya ikiwa ni pamoja na madeni mengine ya ndani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali. Pamoja

na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa wapo wazabuni ambao walitoa huduma hiyo ya kusambaza vyakula na vifaa mbalimbali katika shule zetu zikiwemo na shule za watoto wenye ulemavu, lakini wazabuni hao wengi wao wana miaka zaidi ya mitano hawajaweza kulipwa pesa yao na walio wengi wamekopa benki na wengine nyumba zao zimeuzwa na wengine ziko hatarini kuuzwa. Je, Serikali iko tayari kufanya uhakiki wa madeni hayo ili kuweza kuwalipa wazabuni hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa wapo wazabuni wapya ambao walitoa huduma ya kusambaza vyakula shuleni wao wamelipwa lakini wazabuni wa zamani hawajalipwa. Je, Serikali iko tayari kuwalipa wazabuni wa zamani ambao walitoa huduma ya kusambaza vyakula shuleni ambao hawajalipwa lakini wapya wamelipwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza la kufanya uhakiki wa madeni haya ili walipwe, ndiyo maana nimesema kwamba ni kweli, kuna madeni mbalimbali hasa wazabuni waliotoa vyakula katika shule zetu kabla programu ya elimu bila malipo kuanza. Jambo hili kweli limesababisha wazabuni wengi kupata mtikisiko lakini ndiyo maana ilibidi Serikali kuyapitia madeni haya yote tukijua wazi kwamba lazima kuna mengine siyo sahihi maana katikati hapo tulibaini baadhi ya madeni mengine ni hewa.

Kwa hiyo, Serikali imefanya mchakato wa ku-*analyse* madeni yote haya ili kutambua deni halisi la Serikali. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wazabuni wote waliotoa vyakula shuleni kwamba Serikali itafanya kila liwezekanalo kuwalipa.

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika hii *concern* kwa nini wazabuni wapya wanalipwa lakini wa zamani hawajalipwa ni kama nilivyosema kwamba utaratibu wa sasa tunapeleka fedha moja kwa moja kule shuleni. Kwa hiyo, kila mwezi mgao wa Serikali ukipeleka kule na fedha ya chakula inakuwepo. Ndiyo maana sasa hivi sitarajii sana kuona kwamba kuna wazabuni watadai kwa sababu fedha zote ambazo zinatakiwa zielekezwe katika ulipaji wa chakula tunazipeleka kila mwezi.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tunalibeba na sisi kama Watanzania na Serikali tutahakikisha kwamba wazabuni wetu wa ndani lazima tuwalinde ili waendeele kufanya biashara yao kwa sababu ndiyo watajenga uchumi wao katika nchi yetu hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wazabuni wanaohudumia chakula *Mpwapwa High School, Mazai Girls' School* pamoja na *Berege Secondary School form five na six* sasa ni zaidi ya miaka miwili hawajalipwa na bado wanahudumia na wamekopa benki. Mheshimiwa Naibu Waziri amefika Mpwapwa sekondari na ameona hali ilivyo na wanataka kukamatiwa nyumba, je, hawa wazabuni watalipwa lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lubeleje, *Senior MP* wa Bunge hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na kwa bahati mbaya kwa Halmashauri ya Mpwapwa siyo kesi ya wazabuni wa chakula peke yake isipokuwa kuna kesi ya wakandarasi mbalimbali ambao wamefanya kazi pale Mpwapwa lakini bado hawajalipwa. Hili napenda hasa nimuelekeze Mkurugenzi wetu wa Halmashauri ya Mpwapwa kwamba madeni mengine ambayo hayajalipwa ni suala la kuangalia Menejimenti ya Kurugenzi yake jinsi gani itafanya kuweza kuyalipa.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lubeleje kwamba Mpwapwa ndiyo maeneo ya *priority* kwa sababu ofisini kwangu hata watu wa *CRDB* walifika kulalamikia Halmashauri ya Mpwapwa. Hata hivyo, ukiachia hizo fedha kutoenda lakini kuna mambo mengine ya ziada lazima tuyasimamie. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba tutafanya kila liwezekanalo hasa kwa wazabuni wa Mpwapwa na maeneo mengine ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuweze kuwalipa fedha hizi ili wasije wakataifishiwa mali zao na mabenki ambazo ziliwekwa kama dhamana wakati wanachukua mikopo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, swali fupi.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini napenda afahamu kwamba tunapozungumzia wazabuni tuisahau kwamba tunawazungumzia wafanyabiashara. Mara nyingi kama walivyosema wenzangu wafanyabiashara hawa wanapata pesa zao kutoka kwenye mabenki lakini maelezo yake anasema kwamba wale ambao hawajalipwa watalipwa pindi Serikali inapopata pesa. Napenda kujua ni lini? Ni vizuri jambo hili sasa likawekewa mkakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu inatambua umuhimu wa kuwalipa

wazabuni hawa lakini kama alivyosema Mheshimwa Naibu Waziri wa TAMISEMI kwamba sasa hivi tuliji-engage kwenye kuyahakiki madeni haya. Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaambie jambo moja kwamba Serikali ina nia njema. Tulipokea madeni haya kwa ajili ya shule tu ya shilingi bilioni 21.64 baada ya uhakiki tumekuta ni shilingi bilioni sita tu ambazo ni halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana Serikali inaomba muda maalum ili tuweze kumaliza uhakiki. Hii itasaidia Serikali kulipa yale madeni ambayo ni halali kwa ajili ya wazabuni waliotoa huduma na siyo kuwahi kulipa wakati kuna vitu vingine vya kufanya na tutajikuta tunalipa madeni hewa. Tunasisitiza dhamira ya Serikali ni njema na tutalipa madeni yote yale ambayo ni halali tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, mtusaidie basi hayo madeni ambayo yako halali myalipe kwa sababu malalamiko yako mengi sana. Wabunge wanaandikiwa barua na hao wazabuni, sasa mtusaidie hayo ambayo mmeshahakiki myalipe basi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 220

### **Kuanzisha Vituo Vingine vya Mabasi Yaendayo Mikoani**

**MHE. ZAYNABU M. VULU** aliuliza:-

Kwa sasa kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani cha Ubungo Jijini Dar es Salaam kimezidiwa uwezo wa kutoa huduma kwa ufanisi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vituo vingine kikanda ili kuboresha huduma za usafiri wa mabasi yanayoingia na kutoka mikoani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ipo katika mipango ya kuanzisha vituo vingine mbadala vya mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani baada ya kituo kikuu cha mabasi cha Ubungo kuzidiwa uwezo wa kutoa huduma kwa ufanisi kama ifuatavyo:-

(a) Kituo cha mabasi Mbezi Luis, chenye eneo la mita za mraba 68,000 kitahudumia mabasi yatokayo katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Rukwa, Iringa, Ruvuma na Njombe); Kanda ya Ziwa (Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Geita na Simiyu); Kanda ya Kati (Dodoma, Singida na Manyara); Kanda ya Magharibi (Tabora, Kigoma na Katavi) na nchi za jirani za Malawi, DRC, Burundi, Rwanda, Zimbabwe na Zambia.

(b) Kituo cha mabasi cha Boko Dawasa chenye eneo la mita za mraba 63,121 kitahudumia mabasi yatokayo mikoa ya Kanda ya Kaskazini na Mashariki (Arusha, Kilimanjaro na Tanga) na nchi za jirani za Kenya na Uganda.

(c) Kituo cha mabasi cha Kanda ya Kusini, kitatafutiwa eneo sehemu ya Kongowe kwa ajili ya kuhudumia mabasi yatokayo Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Vulu, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.



Kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri inaelekea Serikali haijajipanga kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo. Kwa kuwa suala la ujenzi wa kituo cha mabasi cha Mbezi Luis ni la miaka mingi na kwa kuwa msongamano uliokuwepo pale Ubungo umekithiri na halleti sura nzuri kwa sababu sasa hivi nchi yetu inatakiwa iwe na kituo chenye hadhi ya Kimataifa. Swali la kwanza, je, ni lini Serikali iko tayari kuanza kujenga kituo cha mabasi katika maeneo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyataja kwa maana ya mabasi ya Kusini, Kaskazini na yanayotoka Kanda ya Kati na nchi jirani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa katika maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kituo cha mabasi ya Kusini kinatarajiwa kujengwa Kongowe na ukiangalia eneo la Kongowe halina nafasi ambayo watajenga kituo bila kutumia pesa nyingi za Serikali.

Je, atakubaliana na mimi kwamba majibu haya hayako sahihi kwa sababu vikao vimeshaanza kufanywa kati ya Wizara ya Maliasili na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga? Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuanza kufanya upembuzi yakinifu katika hilo eneo la Vikindu au Mwanambaya huko Mkuranga? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la dada yangu Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano imejipanga sana na ndiyo maana nilisema pale awali mipango yoyote lazima ipangwe katika utaratibu sahihi. Wiki iliyopita nilijibu swali la Mheshimiwa Mnyika linalofanana na swali hili. Kinachotokea ni nini? Serikali kupitia Jiji la Dar es Salaam imeweza kupata eneo la Mbezi Luis. Bahati nzuri Kamati yenye kuhusika ya Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa iliamua kwenda kujihakikishia na imejiridhisha kuwa ni eneo muafaka. Bahati nzuri sasa *LAPF* wameshakubali uwekezaji wa kituo hicho cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo kuna mambo ya msingi lazima yafanyike. Wiki iliyopita Jiji pamoja na *LAPF* na wadau wengine walikaa kikao kujadili ujenzi wa kituo hicho ambao utagharimu takribani shilingi bilioni 28. Walikuwa wanajadili katika hicho kituo cha Mbezi Luis daraja litapita juu au chini kwenda katika kile kituo cha mabasi cha kawaida cha daladala. Hiyo haitoshi, tarehe 19 Mei, Kamati hii itakutana tena kufanya mjadala mpana kuona ni jinsi gani kituo hiki kinaenda kujengwa. Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano imejipanga sana na tutahakikisha tunajenga vituo katika Jiji la Dar es Salaam ili kusaidia wananchi waweze kupata usafiri mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kituo cha watu kutoka Kusini ni kweli, Jiji la Dar es Salaam sasa hivi linafanya tafakari kwa sababu yeye anaangalia mipaka yake. Walivyoangalia eneo lililokuwepo la Kongowe waliona kwamba ni lazima kulipa fidia. Kwa hiyo, kwa mkakati unavyokwenda, kwa mfano Kongowe mbele pale Vikindu kuna eneo kubwa, Serikali itaangalia jinsi gani *stand* ile itaweza kujengwa pale kwa watu wa Kanda ya Kusini na itahakikisha mipango hii yote inafanyika vizuri. Hata hivyo, agenda hii itaenda awamu kwa awamu lakini lazima tumalize kujenga vituo vyote.

Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaweza kujenga vituo imara kabisa kama tulivyojenga pale Msamvu, Mpanda na maeneo mengine. Lengo kubwa ni wananchi waweze kusafiri vizuri katika nchi yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Bulembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa kituo cha Mbezi Luis kimeshapata mwekezaji LAPF, Serikali inatuambiaje kuhusu kituo cha Boko na cha Temeke, wamewatafuta akina nani watakaosaidia kujenga vituo hivi kwa haraka ili kuondoa msongamano Dar es Salaam? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bulembo, Mbunge Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana swali la Mheshimiwa Mbunge na ndiyo maana nimesema Mbunge Maalum kwa sababu ana hadhi maalum katika nchi hii kutokana na nafasi zake alizokuwa nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi Serikali tumepata wadau wetu wa LAPF tumeanza na kituo kile lakini hata hivyo tunaenda kutafuta wadau wengine kwa ajili ya kujenga kituo kile katika eneo la Boko na kituo cha Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, niwaelekeze wenzetu wa Jiji la Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na wadau wengine hasa Meya wa Jiji la Dar es Salaam, ikiwezekana wakae na Halmashauri ya Mkuranga, kwa sababu eneo la kimkakati tayari lipo ambalo halina haja ya kulipa fidia kuona ni jinsi gani tuta-*fast track* hiki kituo ambacho tunaweza tukakijenga eneo la Mkuranga kwa watu wa Kusini ili wakapata unafuu zaidi.

Kwa hiyo, tunachukua mambo yote haya kwa kushirikisha wadau mbalimbali lengo ikiwa ni kujenga vituo ambavyo vitasaidia suala la usafiri katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mohammed, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize suala moja Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inatilia mkazo suala la kukusanya mapato kwa njia ya kielektroniki. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana mpango gani wa kuhakikisha katika kituo cha Ubungo wanakusanya mapato kwa njia ya kielektroniki wakati abiria wakiingia na wakati magari yakitoka? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tumetoa maelekezo kwamba siyo maeneo ya vituo vya mabasi pekee isipokuwa maeneo yote, utaratibu wa Serikali ni kwamba tunaenda kukusanya mapato yote kwa njia ya kielektroniki.

Naomba nisisitize sana na nimuelekeze Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam ambapo eneo lile lipo, kama kuna upungufu kwamba sehemu zingine wamekusanya kwa njia ya kielektroniki na nyingine hawajakusanya washughulikia changamoto hiyo. Naomba niagize na mimi najua kwamba hilo zoezi limeshaanza katika Jiji la Dar es Salaam, kwamba ili kuziba mianya yote ile ya upotevu wa fedha, mifumo yote ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika vituo ya mabasi, hospitali na maeneo mengine ni kwa kutumia mifumo ya kielektroniki na si vinginevyo.

**NAIBU SPIKA.** Mheshimiwa Ulega, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kuhusiana na ujenzi wa kituo cha mabasi ya Kusini katika eneo la Jimbo la Mkuranga; na kwa kuwa uratibu wa zoezi zima la ujenzi wa kituo cha mabasi ya Kusini linasimamiwa pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kuhakikisha wanashirikiana vema, Wizara ya TAMISEMI, Maliasili na nyingine zinazohusika kuhakikisha kituo hiki cha mabasi ya Kusini kinapatikana kwa haraka katika eneo la Wilaya ya Mkuranga hasa maeneo ya msitu ule wa Vikindu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ujenzi wa vituo hivi vya mabasi ni uwekezaji mkubwa sana na ni vyanzo vikubwa vya mapato kwenye Halmashauri zetu. Ukizingatia Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, huwezi kwa namna yoyote ile ukafanya mradi kwenye mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika na mradi ule ukawa na wadau wengi nje ya utaratibu wa kuibua na kutekeleza mradi ule kutoka kwenye Halmashauri husika.

Kwa hiyo, kwa kuzingatia dhana ya ugatuaji wa madaraka *(D by D)*, katika kusimamia sisi kama TAMISEMI tutajaribu sana kuhakikisha kwamba miradi hii ya vituo vya mabasi itafanywa na mamlaka za Serikali za Mitaa husika kwa kushirikiana na wadau wowote *whether* ni PPP au kwa kushirikiana na taasisi zetu za Mifuko ya Jamii, kwa vyovyote vile lakini mwenye mradi na mmiliki wa mradi atakuwa ni Halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kumueleza kwamba sisi kama Serikali kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Maliasili tutakuwa tu ni *facilitator* lakini pia kuwaondolea vikwazo ili waweze kutekeleza mradi huo. Hii naisema ni kwa maeneo yote, kwa Mbezi Luis lakini pia kwa Boko, utaratibu utakuwa ni huo huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 221

**Utaratibu wa Kuwapanga na Kuwahamisha  
Watumishi wa Umma**

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani maalum wa kuwapanga na kuwahamisha sehemu za kazi watumishi wake?

(b) Je, ni vigezo gani huzingatiwa katika kuwapanga au kuwahamisha watumishi sehemu za kazi?

(c) Je, ni kwa namna gani Serikali inahakikisha watumishi wake wanafanya kazi kwa ufanisi katika maeneo waliyopangwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA  
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha watumishi wa kada ya ualimu na wale wa kada za afya ambao utaratibu wao wa kuajiriwa ni wa kupangiwa vituo vya kazi mara tu wanapohitimu mafunzo yao, utaratibu wa ajira kwa kada nyingine hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria hii, mchakato wa ajira hufanywa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ambayo hutangaza kazi kulingana na mahitaji ya waajiri, kufanya usaili na kuwapeleka katika vituo vya kazi waombaji waliofaulu usaili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamisho ndani ya utumishi wa umma hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa

Umma, Sura 298 ikisomwa kwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Toleo la mwaka 2009 ambapo Katibu Mkuu (Utumishi) amepewa mamlaka ya kufanya uhamisho wa watumishi wa umma kutoka kwa mwajiri mmoja na kwenda kwa mwingine kwa lengo la kuimarisha utendaji ndani ya Utumishi wa Umma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vinavyotumika kuwapanga au kuwahamisha vituo vya kazi watumishi wa umma ni pamoja na:-

(i) Mahitaji ya kila taasisi kutokana na kuwepo ikama na bajeti ya mishahara ya watumishi kwa mwaka wa fedha husika.

(ii) Sifa za kitaaluma kama zilivyoainishwa kwenye Miundo ya Maendeleo ya Utumishi kama inavyotolewa mara kwa mara na Serikali.

(iii) Umuhimu wa kuimarisha utendaji wa kazi na kuongeza ufanisi katika utumishi wa umma.

(iv) Kupangiwa kazi au uhamisho kutokana na mtumishi kupata maarifa/taaluma mpya (*re-categorization*).

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha watumishi wanafanya kazi kwa ufanisi katika maeneo waliyopangwa, zipo Mamlaka za Ajira na Nidhamu ambazo zimewekwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298. Kwa mujibu wa sheria hii, mamlaka hizi zinapaswa kuhakikisha kuwa kila mtumishi anapangiwa majukumu kulingana na mpango mkakati wa kila taasisi, ambapo kila mwisho wa mwaka upimaji wa wazi wa utendaji kazi hufanyika. Pale mtumishi anapoonekana hajatimiza malengo yake kwa sababu yoyote ile, anapaswa kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazoongoza usimamizi wa utumishi wa umma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Mngwali, swali la nyongeza.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Niseme tu majibu ya Serikali yamekuwa ni yale ya *ought to be, rather than what is the real situation*. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, je, Serikali inasema nini pale ambapo watendaji maalum kama *DED, DAS, RAS* na walimu wanapohamishwa kila baada ya muda mfupi katika Wilaya husika? Na mfano ni Wilaya Mafia ambapo katika miezi michache ma-*DED* walihamishwa na tukapata wapya kama watatu na hii ilitokana zaidi na jinsi walivyoendesha uchaguzi na kuusimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ufanisi sio tu kutunga sheria za kusimamia, hivi Serikali haioni kwamba masuala kama ya kuhakikisha watumishi wanapata makazi bora, wanalipwa stahiki zao ipasavyo na vilevile wana uhakika wa kuwa na *periodic training* za ku-*upgrade* zile nafasi zao ni namna za kujenga ufanisi katika utendaji kazi? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuzungumzia alipokuwa anasema kwamba tumejibu tu namna inavyotakiwa kuwa na siyo uhalisia. Sisi tunasimamia Menejimenti nzima ya Utumishi wa Umma na ndiyo maana tunatoa miongozo na taratibu mbalimbali na kuifuatilia. Ndiyo maana nimemueleza utaratibu kwa sababu yeye ameuliza utaratibu na vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza kwamba ni kwa nini unakuta watumishi wengine wanahamishwa bila kufuata taratibu. Tumekuwa tukitoa nyaraka mbalimbali za kiutumishi, tumetoa Waraka kwa TAMISEMI mwaka 2006, tumetoa pia Waraka mwaka 2007 kwa



Makatibu Tawala wa Mikoa kueleza ni namna gani na masuala gani yanayotakiwa kuzingatiwa wakati wanapohamisha watumishi. Pia katika jibu langu la msingi nimemueleza muuliza swali, lengo kubwa ni kuangalia manufaa ya umma, kuangalia uwiano katika Halmashauri zetu na katika sehemu zetu za kazi na si kwa kumkomesha mtu wala kwa lengo lolote, lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha kwamba ikama na bajeti ya fedha imetengwa ili kuhakikisha kwamba mtumishi wa umma hapati usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumuongezea Mheshimiwa Mngwali, hata Mheshimiwa Rais ameweza kutoa msisitizo zaidi tarehe 1 Mei, 2017 wakati wa siku ya wafanyakazi. Maelekezo yamekuwa yakitoka lakini ameweka mkazo kwamba kuanzia sasa hakuna kumhamisha mtumishi yeyote wa umma kama gharama zake za uhamisho hazijatengwa na pia kama hakuna manufaa katika uhamisho huo na hakuna ufanisi wowote ambao unaenda kuongezeka katika kuboresha ikama hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la makazi pamoja na umuhimu wa mafunzo, niseme tu katika Sera ya Menejimenti ya Ajira katika Utumishi wa Umma pamoja na Sera ya Mafunzo, tunatambua umuhimu wa kuwa na mafunzo na watumishi wetu wa umma kuwa na makazi bora. Ndiyo maana kama Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania, *Watumishi Housing*, Shirika la Nyumba la Taifa, *TBA* na mashirika mengine tumekuwa tukiweka msisitizo na kuhakikisha kwamba nyumba zinajengwa kwa ajili ya watumishi wetu wa umma.

Vilevile katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wamekuwa mwaka hadi mwaka wakitenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi wetu. Lengo kubwa likiwa ni kuwaboresha watumishi wetu wa umma makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya yote nitoe rai kwa waajiri wetu kuona ni namna gani wanaweza kuweka vivutio mbalimbali ili kuhakikisha kwamba wanavutia watumishi waweze kufanya kazi katika maeneo yao ya kazi.

Zaidi katika mafunzo pia ni vema waajiri wakahakikisha kwamba kila mwaka wanatenga bajeti kwa ajili ya kuwapatia mafunzo watumishi wao na kuwaendeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alex Gashaza, swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kutoa miongozo na maelekezo mbalimbali kuhusu uhamisho wa watumishi, Halmashauri mbalimbali ikiwemo Halmashauri yangu ya Wilaya ya Ngara wameendelea kufanya uhamisho huo bila kulipa stahiki za uhamisho za watumishi hao na hivyo kuzalisha madeni. Je, Serikali inachukua hatua gani juu ya watendaji hawa ambao hawazingatii maelekezo wala mwongozo wa Serikali? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza tumekuwa tukitoa maelekezo katika nyakati mbalimbali lakini nimefanya *reference* ya maelekezo ya mwisho ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 1 Mei, 2017. Tumekuwa tukichukua hatua na mifano ya karibuni tu ni katika Halmashauri ya Kilombero na Bagamoyo ambapo wale ambao hawakuzingatia taratibu hizi waliweza kuchukuliwa hatua mbalimbali za kiutumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuwaeleza Wakurugenzi wetu na Mamlaka za Ajira wazingatie maelekezo haya. Ni lazima pindi wanapofanya uhamisho wawe wametenga fedha katika ikama, lakini vilevile wahakikishe kwamba lengo la uhamisho huo lina manufaa kwa umma na ni katika kuboresha ikama katika Halmashauri zetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Mwassa, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kutokupandisha madaraja kwa wakati, kutolipa na stahili za wafanyakazi kwa wakati na kufuta posho mbalimbali kumefanya ufanisi wa wafanyakazi kushuka. Je, Serikali ina mpango gani katika hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 13 Juni, 2016, tulitoa Waraka wa Utumishi kupitia kwa Katibu Mkuu tukitoa maelekezo mbalimbali. Lengo kubwa la Waraka huo tulikuwa na mazoezi mawili; zoezi la kwanza ni kupitia upya muundo wetu wa Serikali pamoja taasisi zetu kuhakikisha kwamba tuna muundo wenye ufanisi lakini zaidi kuhakikisha kwamba tuna muundo ambao unahimilika. Kama mnavyofahamu tumepunguza idadi ya Wizara kutoka 26 mpaka sasa tunazo 18 au 19.

Kwa hiyo, ni lazima pia na ni dhahiri kwamba baadhi ya taasisi ambazo zitakuwa na muingiliano wa majukumu nyingine itabidi ziweze kuunganishwa, lakini vilevile baadhi ya Idara na baadhi ya Vitengo vingine pia itabidi viweze kuunganishwa kuhakikisha kuwa tunaenda na wakati na tunaendana na mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutokana na Waraka huo huo tuliahirisha zoezi la kupandisha madaraja pamoja na kupandisha watu vyeo. Napenda kumtoa hofu Mheshimiwa Mbunge kuanzia mwaka ujao wa fedha tutapandisha madaraja zaidi ya watumishi 193,166 na hakuna atakayepoteza haki yake.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza, Mheshimiwa Ikupe Alex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali na vigezo ambavyo vimetolewa vya upangaji na uhamishaji watumishi wa umma, je, Serikali haioni kuwa ulemavu nao uwe ni miongoni mwa vigezo ambavyo vimetolewa ili mtu mwenye ulemavu awe *comfortable* na hatimaye aweze kutimiza wajibu wake ipasavyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru kwa swali zuri au kwa ushauri. Hili ni eneo ambalo tutakwenda kuliangalia, tumekuwa tukiangalia sababu za kiafya, wengine kuwafuata wenzi wao, niseme na lenyewe tatalifanyia kazi ili kuona ni namna gani na hii pia inaweza kuwa ni moja ya kigezo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Devotha Minja.

Na. 222

### **Uvunjifu wa Haki za Wafungwa Magerezani Nchini**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA (K.n.y. MHE. ZUBEDA H. SAKURU)** aliuliza:-

Magereza mengi nchini hayapo katika viwango na ubora unaotakiwa na hivyo kuvunja haki za wafungwa.

Je, Serikali ina mkakati gani katika kufanya matengenezo na kulinda haki za wafungwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza limekuwa likitekeleza na kusimamia haki za wafungwa magerezani kwa kuzingatia Sheria ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967 (*The Prisons Act. No. 34 of 1967 CAP. 58 R.E 2002*) pamoja na sheria nyingine na Kanuni za Uendeshaji wa Magereza za mwaka 1968 (*The Prisons (Prison Management) Regulations of 1968 G.N. 19 of 23/01/1968*) na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, haki za wafungwa zinazotekelezwa na kusimamiwa magerezani kwa mujibu wa Sheria ya Magereza na Kanuni zake nilizoitaja au msingi mwingine, chimbuko lake ni Mkataba wa Kimataifa unaohusu Taratibu na Haki za Wafungwa na Mahabusu. Haki hizo zimeainishwa wazi sehemu ya VII na IX ya Sheria ya Magereza na Kanuni za Uendeshaji wa Magereza kama ifuatavyo:-

(i) Haki ya kutenganishwa ambapo wafungwa hutenganishwa kutokana na umri wao, jinsia, aina ya kosa, afya na tabia.

(ii) Haki ya kupatiwa chakula na mahitaji mengine. Mfungwa hupewa chakula kama ilivyoainishwa na Kanuni za Uendeshaji wa Magereza niliyoitaja.

(iii) Haki ya kuwa na uhuru wa kupata mawasiliano na kutembelewa na ndugu na jamaa zake. Mawasiliano haya ni pamoja na kupokea na kuandika barua, kusoma magazeti na kusikiliza taarifa mbalimbali kutoka katika vyombo vya habari.

(iv) Huduma za afya. Huduma hizi hutolewa kwa mfungwa pindi anapoumwa wakati wote awapo gerezani.

(v) Haki ya kupatiwa malazi safi na ya kutosha ambapo mfungwa mmoja anahitaji eneo la mita za mraba 2.8.

(vi) Haki ya kukata rufaa pale anapoona hakutendewa haki katika hukumu iliyotolewa na Mahakama dhidi yake.

(vii) Haki ya kucheza michezo. Mfungwa anayo haki ya kushiriki na kucheza michezo ya aina mbalimbali na hii inafanyika magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, zipo changamoto kwa Jeshi la Magereza zinazojitokeza katika kutekeleza baadhi ya haki hizo kutokana na msongamano wa wafungwa katika baadhi ya magereza na kutokana na hali halisi katika baadhi ya maeneo hayo niliyoyataja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja, swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Magereza mengi nchini yanaendeshwa kinyume kabisa na Kanuni Namba 10 ya Umoja wa Mataifa ambayo inazungumzia namna ya kuwahifadhi wafungwa kwamba ni lazima wakidhi vigezo ikiwemo afya, hali ya hewa, joto na nafasi ya kutosha. Magereza mengi nchini likiwemo Gereza la Songea ni mojawapo ya magereza kongwe nchini ambalo lilijengwa tangu mwaka 1948. Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba gereza hili nalo linakidhi vigezo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tangu Rais aseme maneno ka-ta yameleta athari kwa magereza mengi nchini ikiwemo magereza 14 ya Mkoa wa Morogoro ambayo hivi sasa yako kwenye giza tororo. Serikali haioni kama magereza haya kuendelea kuwa na giza ni kinyume kabisa na haki za Umoja wa Kimataifa na pia inasababisha Askari Magereza kushindwa kufanya kazi zao vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja, nimpongeze kwa kuonyesha *concern* ya msongamano wa wafungwa kwenye magereza na ameuliza Serikali tuna mkakati gani. Moja ya mkakati wa muda mrefu tunaofanya ni wa kuhahakisha kwamba tunajenga magereza hasa kwenye maeneo ambayo ni ya kilimo yawe na ukubwa wa kutosha na magereza ya mijini yawe kwa ajili ya mahabusu ambao wanahitajika kuwa karibu na mahakama kwa ajili ya usikilizaji wa kesi zao. Kwa hawa ambao walishahukumiwa wawe katika magereza ambako kazi ya kuwarekebisha inaweza ikafanyika huku kukiwa na kazi ya uzalishaji inayoendelea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la umeme kukatwa, jambo hilo lilishashughulikiwa kwa sababu tayari Hazina ilishatoa fedha kwa ajili ya mafungu yetu ya Polisi, Magereza pamoja na maeneo mengine. Mimi niwasisitizie Waheshimiwa Wabunge, nia na maelekezo aliyoyotoa Mheshimiwa Rais yanarekebisha kwa kiwango kikubwa Maafisa Masuuli wanapopewa fedha zilizokuwa zimeelekezwa kwa ajili ya *utilities* waweze kutumia katika maeneo yale ambayo yalikusudiwa fedha hizo ziweze kutumika. Kwa maana hiyo, badiliko hili linaweza likaathiri katika kipindi ambacho tu madeni yalikuwa yamelimbikizwa lakini itajenga nidhamu ya kudumu ya Maafisa Masuuli kuweza kuelekeza fedha zilipokuwa zimeelekezwa ili kupata jawabu la kudumu la matumizi bora ya fedha zinazotolewa na Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kakoso swali fupi.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali fupi la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa magereza mengi nchini yamekuwa chakavu likiwemo Gereza la Kalilamkurukuru lililopo Wilaya ya Tanganyika. Nini mkakati

wa Serikali kuimarisha magereza haya kwa kuyafanyia ukarabati sambasamba na nyumba za askari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Kakoso kwa swali lake zuri la nyongeza. Niseme tu kwamba tuna mikakati ya aina mbili, kwa upande wa nyumba za askari kama nilivyoelezea wakati wa bajeti tunaenda hatua kwa hatua, tuna miradi midogo na mikubwa ambayo tunaitekeleza. Kwenye ukarabati sambasamba na upande wa ujenzi wa nyumba tumekubaliana kutumia bajeti inayotengwa lakini pamoja na nguvukazi tunayoipata kutokana na wajuzi tulionao kwa upande wa askari, lakini wajuzi tulionao kwa wale walioko magerezani ili tuunganishe nguvu zote hizo na bajeti inayopatikana tuweze kufanya marekebisho pamoja na ujenzi wa makazi mapya pamoja na mabweni kwa ajili ya wafungwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magige swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kumekuwa na tabia mbaya kwa baadhi ya askari kudhalilisha raia na hata kuwatolea kauli mbaya ikiwemo hata sisi Wabunge tumekuwa tukikutana na kauli mbaya kutoka kwa baadhi ya askari lakini inapokuja kwenye kutetea maslahi yao sisi ndiyo tumekuwa wa kwanza kuwatetea. Je, Serikali inatoa kauli gani? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja, askari wetu wa Jeshi la Polisi pamoja na askari wengine ni Watanzania na wanafanya kazi kwa gharama za maisha yao. Kwa hiyo, tuna wajibu wa kutimiza kama Taifa kwa kutambua kwamba askari wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria na hakuna haki isiyo na wajibu. Sisi



kama Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na taasisi zingine tuna utaratibu wa kuchukua hatua punde inapotokea askari amefanya kazi kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna wajibu ambao Watanzania, wananchi kwa ujumla wanatakiwa watimize wanapokuwa wamekutana na askari wetu. Kwa mfano, afadhali sisi ni viongozi, wengi wetu tunatoa uongozi tunapokutana na askari lakini kuna watu wengine ambao hawatoi heshima inayostahili kwa vyombo vyetu vya dola. Sasa vyombo vyetu vya dola vimepitia mafunzo na mimi kama kiongozi wao nisingependa kuona Jeshi la Polisi linafanana na *green guard, blue guard* au *red brigade*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Watanzania watambue kwamba vyombo vyetu vya dola vina heshima, vinafanya kazi kubwa na vinastahili kupewa heshima kama vyombo vya dola. Ukitaka kupambana na vyombo vya dola wana sehemu ambayo wanaruhusiwa kutumia nguvu wanapoona kile kinachofanywa na raia kinaweza kikahatarisha ama kikaleta athari iliyo kubwa zaidi. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge tunakutana na watu wetu, tuendeleo kutoa elimu hiyo ili vyombo vya dola katika nchi yetu kama ilivyo katika nchi zingine viweze kupewa heshima vinavyostahili.

**NAIBU SPIKA:** Swali fupi la mwisho Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya haki za wafungwa zinazovunjwa ni pamoja na makazi duni sambamba na kukosekana kabisa kwa rufaa za hukumu jambo ambalo linafanywa kwa makusudi na baadhi ya maafisa husika na *Case Flow Management Committees* haziendi kwa wakati. Swali, Serikali ina mkakati gani wa ziada kukamilisha taratibu hizi ili wafungwa wapate haki zao inavyostahili? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Masoud kwa swali hilo. Niseme tu kama nilivyotaja baadhi ya haki, zile nilizotaja ni baadhi tu, lakini kwa upana wake kuna vitu vingine vingi zaidi na kama Serikali tumejipanga na hivi vinahusisha zaidi ya Wizara moja. Utaona Mheshimiwa Rais anapoweka nguvu upande wa mahakama anamaanisha kesi zisikae sana kwa sababu haki ikicheleweshwa inakuwa haki iliyokataliwa, unaona jambo hilo linavyofanyika. Anavyoiwezesha magereza kupata magari ya kubebea mahabusu waweze kupelekwa kusikilizwa kesi zao anawezesha *connection* kati ya mahakama, magereza pamoja na polisi waweze kufanya kazi hizo ambazo zote hizo zikipunguza mahabusu waliokuwa magerezani *automatically* inakuwa zimepunguza msongamano kwenye magereza hayo na kuwafanya wapate haki hiyo mojawapo aliyoitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu maswali yenu yote mliyouliza yale ambayo yana mlengo wa kiushauri kama Serikali tumepokea na tutaenda kuyafanyia kazi ili kuweza kuleta ustawi katika maeneo haya mliyoyataja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Omary Mgumba.

Na. 223

### **Mradi wa Maji - Vijiji vya Jimbo la Malinyi**

**MHE. OMARY T. MGUMBA (K.n.y. MHE. DKT. HADJI H. MPONDA)** aliuliza:-

Vijiji vya Ngoheranga na Tanga katika miradi ya maji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia (*Phase II World Bank Project*), vimepangiwa kufanyiwa upembuzi yakinifu, usanifu wa kina,

uchimbaji wa visima na ujenzi wa miundombinu ya maji; zoezi hili limeishia tu kwa uchimbaji wa visima virefu nane na mradi kusitishwa.

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha utekelezaji wa miundombinu ya usambazaji wa maji ya bomba kama ilivyo katika vijiji vingine vinavyofadhiliwa na Benki ya Dunia?

(b) Je, ni lini Serikali itapelekea maji katika vijiji vilivyosahaulika vya Mtimbira, Majiji, Kiswago na Ihowanja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali Mheshimiwa Dkt. Hussein Mponda, Mbunge wa Malinyi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Ngoheranga na Tanga ni kati ya vijiji kumi ambavyo vilifanyiwa usanifu mwaka 2008 na mwaka 2010 vilichimbwa visima vitatu ili vitumike kwa ajili ya usambazaji wa maji ya bomba. Kati ya visima hivyo visima viwili vilikosa maji kabisa na kitongoji kimoja cha Mkanga kilipata maji kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 wataalam wa Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge walishauri vichimbwe visima virefu na kufungwa pampu za mkono kwa kila kitongoji ikiwa ni mbadala wa maji ya bomba. Ushauri huu ulizingatiwa na visima 13 vilichimbwa ambapo visima vinane vilipata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakamilisha uwekaji wa miundombinu ya usambazaji wa maji ya bomba katika visima vinane vilivyopata maji kupitia Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo imeanza kutekelezwa mwezi Julai, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vijiji vya Mtimbira, Majiji, Kiswago na Ihowanja havijasahaulika kwani Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya maji katika vijiji hivyo kupitia Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Halmashauri inaendelea kukamilisha taratibu za utekelezaji wa miradi katika vijiji hivyo ili wananchi waweze kunufuka na huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Mgumba, swali la nyongeza.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kuna mradi mwingine unaofadhiliwa na Benki ya Dunia katika Mji Mdogo wa Malinyi unaosuasua toka mwaka 2013. Kwa sasa mabomba ya usambaji maji ya mradi huo yamekwama katika Bandari ya Dar es Salaam kwa sababu ya tozo ya *storage*. Halmashauri tumeomba kuondolewa kwa tozo hiyo lakini mpaka sasa hatujafanikiwa. Je, Serikali inatusaidiaje katika ombi hilo ili kukamilisha mradi huu ili wananchi wapate maji safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa matatizo ya maji yanayowakabili wananchi wa Malinyi yanafanana na matatizo yanayotukabili wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki; na kwa kuwa vijiji vya Mtego wa Simba na Newland vilikuwa ni vitongoji wakati wa mradi wa maji Fulwe - Mikese unafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwaka 2006; na kwa kuwa mradi huo sasa unatekelezwa tangu mwaka 2016 na vitongoji hivi viwili vya Newland na Mtego wa Simba sasa ni vijiji kamili.

Je, Serikali inavisaidiaje vijiji hivi vya Mtego wa Simba na Newland kupata maji safi na salama ukizingatia vilikuwa ni sehemu ya mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa Malinyi, kwa bahati nzuri nimeshatembelea kule na niliyakuta mabomba yapo na mkandarasi alikuwa anaendelea kufanya kazi. Kama kuna mabomba ambayo yamesalia, yako bandarini na yanaendelea kuongeza *storage*, kwangu hii ni taarifa mpya lakini hili ni suala la kiutawala, tupate taarifa ni kwa nini mabomba hayo yamekwama, tutasaidiana ili yaweze kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusu kupeleka maji Mtego wa Simba na Newland. Tunaendelea na Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Kama alivyosema mwenyewe kwamba kuna mradi unaendelea tutahakikisha kwamba mradi huu unakamilika ili na hayo maeneo mawili yaweze kupata maji ama ya mabomba au kwa kutumia visima ili mradi wananchi hao wapate maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Willy Qulwi Qambalo, swali la nyongeza.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mradi wa maji wa kijiji cha Getamok katika Wilaya ya Karatu uliojengwa kwa zaidi ya gharama ya shilingi milioni 600 chini ya Programu ya Kwanza ya *WSDP* hivi sasa haufanyi kazi kwa sababu ya kujengwa chini ya kiwango. Mabomba yaliyofungwa kwenye mradi huo yanapasuka kila kukicha na hata matenki yanavuja. Halmashauri ya Wilaya imejaribu kurejesha huduma kwa kutumia vyanzo vyake lakini imeshindikana kwa sababu fedha nyingi zinahitajika.

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi wa kijiji hicho kupata huduma hiyo ya maji safi na salama na pia wale waliofanya ujenzi huo chini ya kiwango Serikali itawachukulia hatua gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Qulwi ni swali moja tu ndiyo litajibiwa hapo. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali moja kati ya hayo kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miradi mingi katika nchi yetu ambayo imepata shida hiyo kwamba kiwango cha utendaji kilikuwa chini aidha mabomba yaliyonunuliwa hayakuwa yamenunuliwa katika viwango vinavyotakiwa. Kwa sasa tunatakiwa ku-*review* ili tuweze kununua mabomba ambayo ni bora sambamba na kuchukulia hatua wale ambao wamehusika kutufikisha hapo tulipo. Sheria na taratibu tunazo, tutumie Halmashauri na kama utaona kwamba mambo hayaendi, naomba tuwasiliane. Kupitia kwenye Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara ya Maji na Umwagiliaji tutaingilia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, miradi hii ya *World Bank* katika Jimbo langu la Mbagala ilikuwepo Kijichi, Kiwika, Kizinga na Bugdadi ambapo visima vimechimbwa, maji yamepatikana lakini mpaka sasa hivi miundombinu ile haijasambazwa, wananchi bado wana kero kubwa. Je, ni lini Serikali sasa itasambaza miundombinu ile ili wananchi waweze kupata maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni hatua nzuri na ndiyo tunavyokwenda, tunachimba tunapata maji, tunafanya *test*, tunaona kwamba maji haya yanafaa kwa matumizi ya binadamu. Baada ya hapo tunaweka bajeti kwa ajili ya kuweka sasa miundombinu ya kusambaza na kuhifadhi maji ikiwemo na kujenga matanki. Kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na juzi Mheshimiwa Mbunge umepitisha

bajeti basi naomba kwa kutumia Halmashauri yako na fedha mnapanga wenyewe mhakikishe kwamba mnaweka sasa miundombinu ili wananchi waendeleo kupata maji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 224

### **Kukamilika kwa Ujenzi wa Bwawa la Sola – Maswa**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO** aliuliza:-

Naibu Waziri wa Maji alipotembelea Mji wa Maswa alipata nafasi ya kutembelea bwawa lililobomoka la Sola na kuahidi kutoa fedha ya ukarabati wa bwawa hilo kiasi cha shilingi milioni 900.

(a) Je, ni lini fedha hizo zitatolewa ili kukamilisha ujenzi wa bwawa hilo ambalo ni muhimu kwa wakazi wa Mji wa Maswa?

(b) Kuna mabwawa 35 katika Wilaya ya Maswa, je, ni lini Serikali itatoa kiasi cha shilingi bilioni 1.9 ambazo zilikadiriwa kwa ajili ya kukarabatiwa mabwawa hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la *New Sola* lina uwezo wa kuhifadhi maji meta za ujazo 4,200,000 na maji hayo ndiyo yanayotumika kuhudumia Mji wa Maswa na vijiji

11 vinavyozunguka mji. Bwawa lililobomoka ambalo ni la *Old Sola* liko kwenye dakio lilelile la bwawa la *New Sola* na liko upande wa juu (*upstream*). Kwa hivyo, ukarabati wake utapunguza maji katika bwawa la *New Sola* ambalo tayari lina miundombinu ya kusambaza maji. Wizara itafanya uchunguzi zaidi kuhusu faida za ukarabati wa Bwawa la *Old Sola*.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mabwawa manne na malambo 31 yaliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa. Aidha, mpango mkakati wamiaka mitano umeandaliwa kwa ajili ya kufanya ukarabati wa mabwawa ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa vyanzo vya maji katika Halmashauri zote nchini. Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini imeanza zoezi la kuainisha mabwawa (*inventory*) ambayo yatakidhi viwango vya kiufundi, hatimaye kufanyiwa tathmini ili kujua idadi na gharama halisi ya ukarabati wa mabwawa hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Waziri maswali ya kwamba tunatambua Bwawa la *New Sola* yaani Bwawa la Zanzui linapokea maji kutoka mito mitatu, Mto Mwashegeshi, Mto Sola na Mto Mwabayanda na bwawa hili lilikuwepo wakati Bwawa la *Old Sola* likiwepo na lilikuwa linatunza maji ya ziada. Je, hamuoni kwamba kuna umuhimu wa kulijenga hili Bwawa la *Old Sola* ili kuhifadhi maji na kukabiliana na ukame wa maji katika Wilaya yetu ya Maswa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nimejibiwa kama Mbunge wa nchi nzima, mimi ni Mbunge wa Maswa, mabwawa 35 yalishafanyiwa upembuzi yakinifu, leo mnasema mnaangalia *inventory* ya nchi nzima halafu mtafanya ukarabati. Mimi naomba kwa ajili ya Wana-Maswa, ni lini mtawajali Wana-Maswa ili muweze kuwajengea mabwawa haya na vijiji vya Maswa viweze kupata maji ya



kutosha? Kwa sababu katika Mradi wa Ziwa Victoria tuko *phase* ya pili, tutachelewa kupata maji. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kwa jinsi ambavyo anawapenda wananchi wake kuhakikisha kwambwanapata maji safi na salama. Pia nishukuru kwamba nilivyofanya ziara Maswa tulikuwa wote, tulitembea mpaka tukaenda mabwawa yote mawili. Mheshimiwa Mbunge tunafuata wataalam wanatushauri nini na bado tunaendelea kuongea nao kwamba kwa nini tusikarabati *Old Sola* ili liweze kutunza maji wakati haya ya hili bwawa lililopo yakiisha tunaweza tukatumia lile. Wamenambia kwamba hiyo inawezekana lakini kama lile likaweka maji bila kutumika chochote kinaweza kikatoka, kama ilivyotokea kwamba lilibomoka, linaweza likaja kuathiri na hili bwawa ambalo tayari limeshawekewa miundombinu. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge siyo kwamba tumeishia hapo, bado wataalam wanajaribu kufanya uchunguzi kuona ni namna gani watafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukija kwa upande wa swali la pili, ujenzi wa mabwawa hayo, ni kwamba ndani ya Bunge hili tulishatoa maelekezo kwenye Halmashauri nchi nzima kwamba kila Halmashauri iainishe mabwawa. Pia tumeelekeza kwamba Halmashauri zenyewe zinatakiwa kutenga fedha na kuhakikisha kila mwaka walau wanajenga bwawa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia hivi kwa ujumla kwa sababu sisi Wizara tunafanya kazi ya maji kwa nchi nzima, hatufanyi kwa Halmashauri moja. Kwa hiyo, pamoja na Halmashauri yake na Halmashauri nyingine zilizopo hapa nchini zinatakiwa kutekeleza hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martin Msuha, swali la nyongeza.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maji na umwagiliaji nchini imetekelezwa chini ya kiwango ukiwemo mradi wa maji unaotekelezwa katika Kata ya Mkako, Wilayani Mbinga. Mradi huu wa Mkako ulikuwa ukabidhiwe katika Mbio za Mwenge zilizofanyika wiki iliyopita, wananchi waliukataa kwa sababu hautoi maji kabisa. Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam Wilayani Mbinga kukagua Mradi wa Mkako pamoja na miradi mingine ya Kigonsera, Litoho na ya kijiji cha Kiongo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, amesema kwamba miradi mingi ya maji imejengwa chini ya kiwango. Sawa inawezekana ni hilo, lakini sisi taarifa tuliyonayo ni kwamba miradi mingi ilibuniwa lakini baada ya kujengwa vile vyanzo vya maji vimekosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inawezekana ni kwa ajili ya kukosa maji au ilikuwa vimejengwa vibaya, hilo linahitaji utafiti ili tuweze kulidhihirisha na tuweze kulitolea majibu katika Bunge hili.

Hata hivyo, kama kweli mradi umejengwa chini ya kiwango, basi Halmashauri husika inatakiwa ilione hili, iweke wataalam walifanyie uchunguzi kuona tatizo lilikuwa liko wapi. Wakiona kuna tatizo sheria stahiki zitachukuliwa ili tuweze kuhakikisha kwamba mradi huo tunauboresha wananchi wapate maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge Bukoba Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 225

## **Baadhi ya Vijiji Kukosa Umeme – Bukoba Mjini**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE** aliuliza:-

Mji wa Manispaa ya Bukoba una vijiji ambavyo havina umeme kabisa na havikuungizwa katika mpango wa *REA* wa kusambaza umeme.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia umeme vijiji vya kata za Nyanga, Ijuganyondo na Kahororo ambavyo mazingira na hali ya kiuchumi haitofautiani na vijiji vilivyosambaziwa umeme katika wilaya nyingine vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu umeanza rasmi nchi nzima mwezi Machi, 2017. Mradi huu utajumuisha vipengele vya mradi vitatu vya *Densification*, *Grid Extension* na *Off-Grid Renewable*. Mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vijiji vyote nchi nzima, vitongoji vyote, taasisi zote za umma na maeneo yote ya pembezoni, ikiwa ni pamoja na visiwa. Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu utakamilika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* inaendelea na usambazaji wa umeme katika maeneo ya mijini ambayo hayajapata umeme, vikiwemo vijiji vya Kata za Ijuganyondo, Kahororo, Nyanga pamoja na Jimbo zima la Bukoba Mjini.

Kazi hii inafanyika mwaka huu wa fedha 2016/2017 kwa gharama ya shilingi bilioni 22.96.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ikiwemo kata ya Nyanga na vijiji vya Hyolo, Kyakailabwa pamoja na Vijiji vingine vya Rubumba, vitapatiwa umeme kupitia umeme wa *Urban Electrification Program* chini ya *TANESCO*. Mradi huu unatarajiwa pia kuanza mwaka 2018. Upembuzi yakinifu wa mradi huo umeshakamilika. Mradi utafikisha umeme kwa wateja wote wa awali 469 na utagharimu shilingi bilioni 782.6.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, swali la nyongeza.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba mojawapo ya faida zilizomo katika mradi wa *REA* ambayo kawaida inaleta mvuto kwenye mradi huu ni pamoja na *complementary* au unafuu wa bei ambao wanapewa watu wanaosambaziwa umeme huo. Kwa mazoea ambayo yamezoeleka kwa umeme ambao unasambazwa na *TANESCO* ni kwamba bei za *TANESCO* zinakuwa kubwa kuliko zile bei au gharama za *REA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba hizi fedha zilizotengwa kwa ajili ya *TANESCO* na kwa maeneo ambayo ameyazungumza, ikiwemo na vijiji vya Ijuganyundo B ambavyo havina umeme kabisa, maeneo ya Makongo kule Kahororo na maeneo ya Chaya kule Busimbe, hizi gharama pia za *TANESCO* zitakuwa *complimented* au itakuwa ni gharama zilezile za *TANESCO* ambazo zimekuwa kubwa na watu wa maeneo haya ambao hawana uwezo wasiweze kupata umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili,...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lwakatare, katika hilo la kwanza umeshauliza maswali mawili tayari. Sasa labda ufute mojawapo halafu ndiyo uulize la pili ama umruhusu Waziri ajibu hayo mawili uliyouliza kwenye swali lako la kwanza.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba tu atajibu mojawapo atakaloliona linafaa kwenye...

**NAIBU SPIKA:** Sasa muda wetu basi haututoshi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba baadhi ya vijiji ambavyo vinaonekana viko ndani ya mji vinapelekewa umeme kupitia Shirika la Umeme *TANESCO* na ni kweli kabisa bei ni tofuati, bei za *TANESCO* kwa wateja wa awali kabisa ni shilingi 177,000 na kwa upande wa *REA* ni shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Lwakatare kwa jinsi anavyofuatilia maslahi ya wananchi wa Bukoba Mjini, ni mdau mzuri, lakini tunamhakikishia kwamba tutafanya upembuzi kwa ukina kabisa tuangalie kama vijiji vina sifa ya kupelekewa umeme kwa mradi wa *REA* tutafanya hivyo, tutakaa naye pamoja ili ikibainika basi wapelekewe kwa utaratibu wa *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie pia Mheshimiwa Muganyizi Lwakatare kwamba vijiji vyote ambavyo amevitaja vikiwemo vya Kashai, Mafumbo Tweyambe, Turabirere, Kahororo pamoja na visiwa vyake vya Nyabisaka pamoja na Msira vitapata umeme kupitia Mradi wa *REA*. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui kama unaiona idadi ya Wabunge waliosimama kwenye swali hili. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, swali kwa kifupi.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mwezi mmoja uliopita Wizara ilikuwa

inazindua umeme wa *REA* Awamu ya Tatu katika maeneo mbalimbali lakini baadaye wamesimama. Ni lini wanafanya uzinduzi huo katika Mkoa wa Geita na hasa Jimbo la Geita Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni kweli tulianza kuzindua mikoa kumi kwa Tanzania Bara na tulibakiza mikoa takribani 15. Nimhakikishie Mheshimiwa Kanyasu kwamba tumemaliza taratibu zote za kuwapata wakandarasi. Nitumie nafasi hii kwa heshima ya Bunge lako Tukufu kuwaambia Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi kwa ujumla, kesho tarehe 18 Mei, saa 08.00 mchana hapa Mjini Dodoma, kupitia Ukumbi wa Mikutano wa Hazina, wakandarasi wote katika mikoa ya nchi nzima watakabidhiwa katika mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia niwakaribishe Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa na nafasi ya kuhudhuria katika ukabidhiwaji wa mikataba hiyo na majukumu yale ili muweze kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo tutakwenda kuwatambulisha wakandarasi wote mkoa kwa mkoa ili Waheshimiwa Wabunge muweze kufuatilia uwajibikaji wao na orodha pia mtakabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nichukue nafasi hii pia kuwataka wakandarasi wote watakaokabidhiwa mikataba yao kesho, waende katika maeneo yao ya kazi na waanze sasa kutekeleza mradi wa *REA* kwa nchi nzima, kijiji kwa kijiji, kitongoji kwa kitongoji na bila kuruka kijiji wala tarafa.

Nichukue nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo umeme haubagui itikadi, umeme pia wa *REA* hautabagua aina ya nyumba, iwe nyumba ya tembe au vinginevyo, kila aina ya nyumba watapatiwa umeme kupitia mradi huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pamoja na majibu hayo ya kukaribishwa Hazina kesho bado mmesimama? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waitara swali fupi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nimuulize swali dogo Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo anafanya...

**NAIBU SPIKA:** Sasa usianze na pongezi Mheshimiwa, wewe uliza swali, maana watu waliosimama walikuwa wengi na wenyewe wanataka nafasi. Uliza swali moja kwa moja.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Ukonga, Kata za Msongola, Buyuni, Zingiziwa, Majohe, Pugu, *Pugu Station* na Chanika hazina umeme na Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu. Kwa sababu kuna mkanganyiko kule Dar es Salaam kwamba ni mjini siyo vijijini, je, *REA* inaenda maeneo hayo au haiendi? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, yako maeneo yako mjini, lakini kwa Mheshimiwa Mbunge wa Ukonga tumeshakaa naye. Maeneo anayoyataja ya Majohe, Chanika, Zingiziwa mpaka kwenye gereza lako kijijini kule, yale ni maeneo ya vijijini yatapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* na tumeshaanza. Hata hivyo shule yake aliyosema Mheshimiwa ya Bombambili tumeshaifanyia kazi na yeye ni shahidi. Kwa hiyo, maeneo hayo yatapelekwa umeme kwa kupitia mradi wa *REA*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba umeme wa *REA* ni wa vijijini, lakini yako maeneo ya mjini ambayo yana maeneo mengi na makubwa ya vijijini. Nashukuru kwamba *REA* wameweza kutupatia umeme katika mitaa michache kama ya Nyabisare pamoja na kule Bukanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, kwa kuwa, maeneo mengi ya taasisi yako kwenye hizo kata za pembezoni, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba *REA* wanaweza kutupatia umeme katika maeneo yote hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa yako maeneo, najua Tarime mko wawili na kuna Musoma na Tarime lakini ki-*TANESCO* ni Tarime, hakuna shida Mheshimiwa, nimeshakuona Mheshimiwa Esther Matiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba, ukweli yako maeneo ambayo yako pembezoni ingawaje yanasemeka yako mjini. Tumeshakaa na Mheshimiwa Manyinyi, yako maeneo na hasa kwa taasisi za umma, taasisi zote za umma zitapelekewa umeme kupitia mradi wa *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini viko vijiji ambavyo itabidi tviangalie, vile vijiji ambavyo vinaonekana viko mjini vitapelekewa umeme kupitia miradi ya *TANESCO* lakini vile vya vijijini kama ambavyo amesema Nyabisare na vingine, tutachambua ili kuona ni vijiji gani vipelekewe kwa Mradi wa *REA*. Vijiji vyote vya Miradi ya *REA* tumeshakabidhiwa, kwa hiyo, kwa Mheshimiwa Mbunge ambaye anaona kuna



sehemu kuna utata ni vema tukae ili isionekane kijiji fulani kinarukwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 226

### **Utekelezaji wa Mradi wa REA**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliluliza:-

Serikali inapeleka umeme vijijini kupitia mpango wa REA lakini kuna maeneo mengi ambayo hayajafikiwa na huduma hiyo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye kijiji cha Mlalo, Bagamoyo, Mngaza na Kieti kwenye kata ya Vugiri?

(b) Je, ni lini Serikali itafikisha umeme kwenye kata mpya ya Mpale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Ngonyani, almaarufu Maji Marefu, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi Kabambe wa REA katika nchi nzima kama nilivyosema umeanza tangu mwezi Machi, 2017. Mradi huu utajumuisha vipengele vya mradi vitatu katika mikoa yote, *Grid Densification*, *Grid Extension* na *Off-Grid Renewable*. Katika eneo la Mheshimiwa vijiji vya Bagamoyo, Kieti, Mlalo na

Mganza katika Kata ya Buhuli vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa REA Awamu ya Tatu utakaokamilika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme maeneo hayo itajumuisha ujenzi wa njia ya msongo wa umeme wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 6.6; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 19; ufungaji wa transfoma saba pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 350. Gharama ya kazi hiyo ni shilingi bilioni 940.9

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Ngonyani, swali la nyongeza.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza kufuatana na Wizara hii kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, REA ya Awamu ya Pili ilikuwa ina sehemu ambayo imepima lakini sehemu hizo mpaka leo hii bado hazijapata umeme. Mfano ni katika kata ya Magoma katika kijiji cha Makangala na Mwanahauya na Pemba na katika kata ya Kerenge katika vitongoji vya Ntakae, Mianzini, Kwaduli, Migombani, Mfunte na Kiangaangazi. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuhakikisha kwamba vijiji hivi na ile vya Kata mpya ya Mpale vinapata umeme kwa haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ngonyani kwa jinsi ambavyo anashughulikia maendeleo ya umeme kwa jimbo lake, hongera sana Mheshimiwa Ngonyani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuonesha tuna mkakati gani kwanza kabisa upatikanaji wa fedha ya mradi huu

unakwenda vizuri na ni mkakati mzuri. Nimhakikishie Mheshimiwa Ngonyani vijiji vyake vitapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kwamba ana wasiwasi na Kata ambazo ametaja za Magoma, Kelege pamoja na Mazizini lakini yako maeneo ya Foroforo pamoja na Majimoto Mheshimiwa Ngonyani atapata umeme kupitia mradi huu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Manjelwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Korogwe Vijijini linafanana sana na Jiji la Mbeya ambalo linapanuka kwa kasi, jiji hili kwenye kata za pembezoni ambazo ni Tangano, Iduda, Itezi, Iganjo, Nsomwa, Sanga, Mwasekwa na Msalaga hazina kabisa umeme na ni kwa muda mrefu sana. Kata hizi mazingira yake yamekaa kwa mfumo wa *REA* na tunashukuru kwamba *REA* Awamu ya Tatu ilishazinduliwa katika Mkoa wa Mbeya. Swali langu ni kwamba Serikali ina mkakati gani wa kuvipatia umeme vijiji hivi ambavyo kwa *TANESCO* inaelekea imeshindikana? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa kwamba hata *TANESCO* bado inapeleka umeme katika maeneo mbalimbali kufuatana na bajeti zake. Tumeshakaa na Mheshimiwa Mbunge na ni kweli kabisa yako maeneo yenye utata kidogo kama eneo la Uyole.

Hata hivyo, vijiji anavyotaja vya Idunda, Kasilanda pamoja na vingine baadhi yake vipo kwenye miradi ya *REA*. Kwa hiyo, tutakaa na Mheshimiwa Mbunge tuone vijiji

vinavyoingia mijini vitabaki *TANESCO* na vile ambavyo viko kwenye vijiji vitapelekewa umeme kupitia miradi ya *REA*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Bagamoyo, vijiji vya Kondo na Kongo vilikuwa kwenye *REA* Awamu ya Pili lakini miradi hii haikuteklezwa na katika *REA* Awamu ya Tatu miradi ya vijiji hivi haimo. Nilishamsikia Mheshimiwa Naibu Waziri akitamka hapa Bungeni kwamba miradi yote ile ambayo haikuteklezwa kwenye Awamu ya Pili ndiyo itapata kipaumbele katika Awamu ya Tatu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaambiaje wananchi wa vijiji vya Kongo na Kondo waliokwemo kwenye Awamu ya Pili lakini wamefutwa kwenye Awamu ya Tatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nipende kusema viko vijiji kwa nchi mzima ambavyo havikuteklezwa katika *scope* ya *REA* Awamu ya Pili lakini vilikuwa ndani ya mradi. Vijiji vyote ambavyo vilikuwa chini ya *REA* Awamu ya Pili vitaendelea kutekelezwa katika Awamu ya Tatu ya *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kawambwa kwamba vile vijiji vyake vya Kondo na Kongo na vingine, viko kama vijiji vinane hivi viko katika mradi wa *REA* Awamu ya Tatu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Kawambwa aamini tu kwamba vijiji hivyo vitapatiwa umeme katika mradi wa *REA* Awamu ya Tatu ambao umeshaanza na tayari katika Mkoa wake wa Pwani tumefanya uzinduzi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa kama kuna shida tutakaa lakini tumhakikishie vijiji vyake vitapata umeme kupitia mradi wa *REA*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Upendo Peneza, swali fupi la nyongeza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nilikuwa nimeanza kukata tamaa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mji wa Geita tuna shida sana ya umeme na asilimia 70 ya vijiji vinavyozunguka Mji wa Geita viko katika giza. Ni lini Serikali itapeleka umeme katika kata za Nyanguku, Ihanamilo, Shiloleli, Bulela na Bugwagogo ili kuweza kusaidia katika huduma za jamii ambazo ziko katika maeneo hayo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vipo vijiji ambavyo havijapata umeme kwa Mji wa Geita na ametaja vitatu lakini viko zaidi ya ishirini. Nimhakikishie Mheshimiwa Peneza vijiji ambavyo ametaja vya Nyanguku na vingine baadhi yake viko katika mradi *REA* lakini viko katika mradi wa *TANESCO*. Bahati nzuri sana nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mkoa wa Geita na mikoa ya jirani iliyokuwa inapata umeme wa *low voltage* sasa tunakamilisha ujenzi wa mradi wa kusafirisha umeme mkubwa unaotoka Mbeya kwenda Sumbawanga mpaka Nyakanazi na baadaye utatoka Nyakanazi mpaka Bulyankulu na baadaye Geita. Kwa hiyo, wananchi watapata umeme wa kilovoti 400 lakini tutaanza na kilovoti 220.

Kwa hiyo, napenda nimjulishe Mheshimiwa Upendo Pendeza kwamba vijiji hivyo vitapata umeme kupitia miradi ya *REA* na baadhi yake vitaendelea kupata umeme kupitia miradi ya *TANESCO*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Adadi Rajab, swali fupi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uzinduzi wa *REA* Awamu ya Tatu Mkoani Tanga, Naibu Waziri alikuja na mimi nilihudhuria. Tulipata orodha ya vijiji na Muheza tulipewa vijiji 44 kwenye *REA* Awamu ya Tatu. Baadaye orodha hiyo ilipunguzwa vijiji saba vikakosekana ambavyo ni Kwakopwe, Kibaoni, Magoda, Mbambara, Kitopeni, Masimbani na Msowero. Nataka kufahamu hatma ya vijiji hivyo kama vitarudishwa ili waweze kupata umeme kwa sababu wameshaanza kufanya matayarisho ya kuanza kufunga nyaya? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wakati tunazindua katika Mkoa wa Tanga na tulifanya uzinduzi katika maeneo ambayo ameyasema na katika utafiti ikaonekana viko vijiji saba au vinane hivi ambavyo vitaingia kwenye *densification stage* ya pili.

Mheshimiwa Adadi Rajab vijiji saba vitaendelea kupatiwa umeme, kilichofanyika *densification* inaanza kwanza kwa miezi kumi na tano. Baada ya miezi kumi na tano tutaendelea na miezi mingine kumi na mitano mpaka tukapofikia hatua ya kukamilisha vitongoji vyote.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Adadi Rajab vijiji vyake saba si kwamba vimeondolewa bali vimepelekwa mbele ili baada ya miezi kumi tano na vyenyewe vitaanza kupelekwa umeme kwa utaratibu huu wa *REA*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Adadi awape faraja wananchi wake wa Muheza kwamba bado watapelekwa umeme kupitia mradi huu.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, saa aulize swali lake.

Na. 227

**Ahadi ya Kujenga Barabara ya Kirando - Kazovu - Korongwe**

**MHE. ALLY K. MOHAMED** aliuliza:-

Kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa alipokuwa Waziri wa Ujenzi na sasa ahadi aliyoitoa akiwa Rais wakati wa kampeni zake za uchaguzi kwamba barabara ya Kirando – Kazovu –Korongwe yenye urefu wa kilometa 35.6 ingejengwa kwa sababu Halmashauri haina uwezo wa kujenga.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo ili iwasaidie wananchi wa vijiji vya Katete, Chongo, Isaba na Kazovu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kirando - Kazovu - Korongwe (kilometa 35.6) inahudumiwa na Halmashauri ya Wiaya ya Nkasi na haijawahi kuhudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Hata hivyo, Serikali kupitia *TANROADS* Mkoa wa Rukwa ilifanya tathmini ya awali ya barabara hii ili kuweza kujua hatua za kuchukua kwa nia ya kuifungua. Katika tathmini hiyo zilionekana changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na barabara kupita kwenye milima, mabonde, mbunga, mapori na milima yenye miamba. Barabara hii inahitaji

kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili iweze kujengwa kikamilifu. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha ili kukamilisha kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuiwezesha barabara hii kupitika, katika mwaka wa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017, kiasi cha shilingi 705,000,000 zimetengwa zikiwa ni fedha za maendeleo kutoka Umoja wa Ulaya (EU) kwa ajili ya kuanza kujenga kilometa 15 za mwanzo za barabara hii kwa kiwango cha changarawe. Zabuni kwa ajili ya matengenezo ilitangazwa tarehe 15/02/2017 na kufunguliwa tarehe 07/03/2017 ambapo mkataba wa kazi ya matengenezo unatarajiwa kusainiwa tarehe 18/05/2017 yaani kesho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa mara ya kwanza wananchi wa Kazovu, Isaba, Chongo na Katete wataona hata bajaji na gari. Nilipoingia Bungeni mwaka 2010 kilio changu cha kwanza ilikuwa ni barabara lakini awamu ya sasa ni awamu ya chapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali dogo, Mheshimiwa Naibu Waziri juzi umetuma wakandarasi wako kuangalia kipande kilichosalia cha kutoka Kazovu kwenda Korongwe, lini sasa Serikali yako itasaidia kipande hicho kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi haina fedha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Wazi wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Keissy kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutafuta barabara hii ijengwe na hatimaye sasa amepata majibu.



Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa na mimi napokea salamu hizo za pongezi kwa niaba ya Serikali kwamba tumedhamiria barabara hii ikamilike. Ndiyo maana nimepeleka wataalam wangu kwenda kuiangalia kazi hiyo ili hatimaye tuangalie namna gani tunafanya na kama tulivyojibu katika swali la msingi kwamba sasa tunatafuta fedha kwa ajili ya kuishughulikia barabara hii tukianza na *feasibility study and detail design*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha, tutamalizia swali la mwisho, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge sasa aulize swali lake.

Na. 228

### **Kuboresha Chuo cha Maendeleo ya Jamii (FDC)**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakiboresha Chuo cha Maendeleo ya Jamii yaani *FDC* Sikonge ili kilingane na Vyuo vya *VETA* kwa kuogeza idadi ya walimu na mafunzo yanayotolewa?

**NAIBU WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) kuhamishiwa katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mwaka 2016/2017 Wizara imeanza kufanya tathmini kwa vyuo vyote ili kujua mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza azma hiyo, katika bajeti ya maendeleo kwa mwaka fedha 2017/2018

zimetengwa kiasi cha shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kukarabati majengo na miundombinu ya baadhi ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Wizara pia katika bajeti ya maendeleo ya mwaka 2017/2018 imetenga shilingi bilioni 10 kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi (ESPJ) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na ambao utadumu kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2017 imepanga kuviboresha kwa awamu vyuo hivyo 55 vya Maendeleo ya Wananchi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Sikonge kitatembelewa ili kuona uwezekano wa kukiboresha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha FDC Sikonge kinatakiwa kutoa mafunzo katika fani za useremala, uashi, ucholemeaji, ushonaji na ufundi umeme. Kutokana na upungufu wa walimu uliopo na uchakavu wa majengo, chuo kwa sasa kinatoa mafunzo kwenye fani ya umeme peke yake. Maswali yangu mawili, je, Serikali aione kuwa chuo hiki kinahitaji jicho la kimkakati ili kukiokoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika jibu la msingi ameahidi kwamba Chuo hiki kitatembelewa, kitatembelewa lini na nani? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua umuhimu wa kuviimarisha vyuo hivi ili kuweza kuchukua wanafunzi wengi zaidi na kutoa mafunzo yaliyo bora zaidi kulingana na uhitaji wa soko, lakini vilevile kuhakikisha kwamba wananchi wengi zaidi wanaweza kujiajiri wenyewe. Kwa upungufu alioainisha Mheshimiwa Mbunge tutatembelea chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake Waheshimiwa Wabunge ili tu-save muda, kimsingi mkakati

ni kutembelea vyuo vyote vya *FDCs* ili kuona namna bora zaidi ya kuviendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la kwenda Sikonge nitakufahamisha Mheshimiwa, kimsingi tutaenda na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ni muhimu kuwepo, tutakujulisha twende wote ikiwezekana katika kipindi hiki cha bajeti katika *weekend* mojawapo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu, tutaleta matangazo yaliyopo Mezani.

Tangazo la kwanza ni la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wapo wageni wa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles Mwijage kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji wakiongozwa na Dkt. Adelherm Meru ambaye ni Katibu Mkuu (Viwanda), Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Katibu Mkuu (Biashara na Uwekezaji). Yupo pia Injiniya Joseph Malongo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu. Pia wamo Wenyeviti saba wa Bodi za Taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara hiyo. Wengine ni Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Taasisi, Vitengo na Maafisa mbalimbali waliopo chini ya Wizara hiyo. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Pia tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji ambao ni Madiwani saba kutoka Halmashuri ya Wilaya ya Kondoa wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashuri ya Kondoa ambaye ni Bi. Hija Suru, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Yapo pia matangazo ya kazi, tangazo la kwanza linatoka kwa *Engineer* Atashasta Nditiye ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili

na Utalii, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hii kuwa leo tarehe 17/5/2017, saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi Na. 227, Jengo la Utawala. Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati hii mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hii kuwa leo tarehe 17 Mei, 2017, saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo na kitafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa B. Wajumbe wa Kamati mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo tuliyonayo tutaendelea, Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA- KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutokana na mzigo nilionao naomba taarifa zangu zote ziingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge zikihusisha maelezo, majarida na picha zitakazooneshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuanzia tarehe 29 hadi 30 Machi, 2017 naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya, upendo, baraka, ulinzi na usalama na kutuwezesha kumudu majukumu, dhamana na wajibu wetu kwa Taifa na jamii nzima kwa ujumla. Naomba kazi njema ya mikono yetu ziendelee kumpendeza na hivyo kupata kibali chake daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi thabiti na maamuzi makini yanayotia chachu, ari na kasi ya utekelezaji wa mipango yenye tija na manufaa mapana kwa Taifa. Hatua hizo zimetoa msukumo wa kipekee katika kuimarisha uwajibikaji wa umma wa Watanzania katika kuchochea maendeleo na vita dhidi ya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge) na Waziri Mkuu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuongoza vema shughuli za Serikali Bungeni na kusimamia vema shughuli za Serikali Bungeni. Pia ninampongeza kwa hotuba yake yenye kutoa dira makini ya malengo, mipango na mwelekeo wa utendaji wa Serikali hususan katika kutekeleza mipango na programu za Serikali ya Awamu ya Tano kwa mwaka 2017/2018. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wamewasilisha hotuba za bajeti za mwaka 2017/2018 na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza vema Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Serikali ya Awamu ya Tano ya uongozi wa nchi yetu. Nashukuru kwa ushirikiano ambao Wizara na wadau wake wameendelea kutupata kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kushika dhamana ya kusimamia na kuendeleza sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji nchini. Na mimi napenda kumhakikishia kuwa nitaendelea kujibidiisha kutekeleza jukumu hilo ili kukidhi matarajio ya Watanzania walio wengi kwa kuifanya Tanzania ya kesho kuwa ya matumaini makubwa zaidi kupitia maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa namna ambavyo wameipokea, kuichambua na kushauri juu ya mambo ya msingi ya bajeti ya mwaka 2017/2018 katika kuendeleza sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji. Napenda kukuhakikishia ushauri na maelekezo ya Kamati tunayathamini na tumeyazingatia katika kuandaa na kuboresha hotuba ninayoiwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze wote waliopata uteuzi na kwa majukumu yao. Napenda kutambua na kushukuru mchango wa wadau wote ambao wanasimamia sekta hii. Kipekee kwa ajili ya muda napenda nichukue fursa hii kuwapa pole wale wote ambao wameondokewa na wenza wao na zaidi wale malaika wetu wa shule ya Lucky Vincent ambao walipoteza maisha yao katika ajali kule Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pole kwa mara ya pili kwa wananchi wa Jimbo langu ambao wamekuwa wakisumbuliwa na matatizo ya mvua. Nitumie nafasi hii kuwapa moyo kwamba nipo pamoja nanyi na Wizara ya Ujenzi imeshaahidi namna gani ya kurekebisha adha katika utekelezaji wa Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mchango na

mwelekeo wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji katika kuleta mageuzi ya uchumi; Serikali ya Awamu ya Tano inaingia katika mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016/2017 – 2020/2021 unaojikita katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Lengo kuu la Mpango huo ni kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati inayoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri Tanzania kama zilivyo nchi nyingine duniani inahitaji uchumi wa viwanda ili kuleta mageuzi ya haraka na kujenga msingi imara wa uchumi. Uamuzi wa Serikali wa kujenga uchumi wa viwanda unalenga kuleta maendeleo jumuishi na endelevu kwa kutumia ipasavyo rasilimali zilizopo na hivyo kuchangia katika kukuza pato la Taifa, kutoa nafasi nyingi na endelevu za ajira, kuzalisha na kukuza teknolojia zinazohitajika na kuwa chachu ya maendeleo ya sekta zinazohusiana na kuzalisha bidhaa bora kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa uchumi wa viwanda unahitaji umadhubuti na nguvu za ziada katika kusimamia na kutekeleza kwa vitendo uvutiaji wa wawekezaji, ujenzi wa viwanda, kulea na kulinda viwanda vya ndani na pia kupambana na nguvu za ushindani usio haki katika soko. Mfumo wa mahusiano ya kiuchumi kati ya mataifa makubwa na madogo duniani hauna urafiki wa kuachia nchi maskini zijitawale kiuchumi. Kwa hiyo, Wizara inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kila Mtanzania kwa nafasi yake awe na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya soko, kufichua na kudhibiti mbinu chafu za soko, kuwa tayari kuwekeza na pia kutoa kipaumbele katika kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya sekta binafsi na uwekezaji ndio msingi wa mipango mikuu ya maendeleo ya nchi yetu. Sera, mipango na mikakati mbalimbali ambayo Serikali imekuwa inaandaa, kuboresha na kutekeleza siku zote

ina lengo la kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi iendelee kuwa muhimili wa uchumi na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya viwanda. Jukumu kubwa la Serikali katika mipango hiyo ni kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi itimize wajibu wake wa kuwekeza na kuzalisha bidhaa na kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina thamini jitihada za sekta binafsi zinavyoshiriki katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji, kushirikiana na sekta za umma na kuendesha shughuli za uzalishaji katika kipindi cha mwaka 2016/2017. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania ilifanikiwa kusajili jumla ya miradi 242 ya sekta mbalimbali ambayo ilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,079 inayotarajiwa kutoa ajira mpya zipatazo 17,385. Kati ya miradi hiyo, miradi ya viwanda ni 170 ambapo miradi 54 ipo katika hatua ya awali ya ujenzi na miradi 17 imeanza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa viwanda vidogo, *SIDO* imeweza kusajili viwanda vidogo 1,843 katika Mikoa mbalimbali nchini. Serikali itaendelea kushirikiana kikamilifu na sekta binafsi katika maandalizi na maboresho ya sera, mikakati na sheria mbalimbali kwa kuhusisha wadau wa kissekta wakiwemo *Tanzania Private Sector Foundation*, *TCCIA*, *CTI* na *TAFOPA* kwa kutaja baadhi, wengi wao wapo ukumbini wakifuatilia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji; sekta ya viwanda. Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2016, shughuli za uzalishaji viwandani zilikuwa kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2015. Ongezeko la ukuaji huo ulitokana na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za vyakula, vinywaji na bidhaa za tumbaku. Ukuaji huo ni juu ya wastani wa ukuaji wa pato la Taifa kwa asilimia 7.8 kwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa ulikuwa kwa asilimia 5.1 ukilinganishwa na asilimia 5.2 katika mwaka 2015. Kwa



mwaka 2016, sekta ya viwanda imetoa ajira 146,892 ikilinganishwa na ajira 139,895 zilizotolewa mwaka 2015. Ongezeko hilo la asilimia 7.1 kwa mwaka lilitokana na ajira mpya viwandani kufuatia uwekezaji katika upanuzi na uanzishaji wa viwanda vipya nchini. (Rejea jedwali Na.2(a), 2(b), 2(c), 2(d) na 2(e).

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo nchini ni sekta muhimu katika kutengeneza ajira, kukuza kipato na kuondoa umaskini. Sekta hiyo ina jumla ya jasiriamali milioni 3.1 ambazo zimeajiri asilimia 23.4 ya nguvu kazi ya Taifa na imechangia asilimia 23 katika pato la Taifa. Aidha, kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 iliyozinduliwa mwezi Oktoba, 2016 Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda 49,243 ambapo asilimia 85.13 ni viwanda vidogo sana, asilimia 14.02 ni viwanda vidogo, asilimia 0.35 ni viwanda vya kati na asilimia 0.5 ni viwanda vikubwa. Hivyo, viwanda vidogo ni muhimu sana katika maendeleo ya uchumi wetu kwani huchukua jumla ya asilimia 99.15 ya viwanda vyote nchini. (Rejea jedwali Na. 7(a)).

Mheshimiwa Spika, taswira ya takwimu hizo inaonesha kuwa maendeleo ya viwanda Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine yatatokana na kuweka nguvu katika sekta za viwanda vidogo, viwanda vidogo sana na vya kati. Hali hiyo siyo ya kushangaza kwa kuwa taswira kama hiyo inajitokeza pia katika nchi karibu zote duniani. Kwa mfano, Japan ni asilimia 99, Kenya asilimia 98, Indonesia asilimia 99.9, Canada asilimia 98 na Ujerumani asilimia 99. Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuviwezesha viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati kukua na kufanya kazi kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya sekta ya viwanda vidogo ni kuwa uanzishwaji wake hauhitaji elimu na mtaji mkubwa na hivyo vinaweza kuanzishwa katika eneo lolote la nchi yetu. Sekta hiyo inatoa mwanya mkubwa kwa vijana na akina mama kuanzisha viwanda na kujiajiri ambapo wasingepata fursa hizo sehemu nyingine. Viwanda vidogo huongeza thamani ya mazao, hali ambayo humpatia kipato

zaidi mzalishaji na kupunguza hasara baada ya mavuno. Sekta ya viwanda vidogo husaidia kusambaa kwa viwanda nchi nzima hali ambayo pamoja na faida nyingine, hupunguza wimbi la wananchi kutoka vijijini kuhamia mijini. Pia viwanda vidogo ni shule, kwanza mtu anaanza na kiwanda kidogo, kiwanda cha kati mpaka kiwanda kikubwa. Aidha, ujenzi wa viwanda kwa kutumia mfumo huu ndiyo kujenga sekta ya viwanda iliyoendelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya biashara na masoko; Serikali imeendelea na jitihada za kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuchangia ipasavyo katika uwekezaji nchini. Kutokana na jitihada hizo, sekta ya uwekezaji imeendelea kukua ikilinganishwa na nchi nyingi za Afrika Mashariki. Ripoti mbalimbali za uwekezaji duniani zinaonesha Tanzania imeongoza kwa kuvutia uwekezaji kwa mwaka 2016 katika Afrika Mashariki. Kwa mfano, Ripoti ya Uwekezaji ya Dunia (*World Investment Report*) ya mwaka 2016 inayotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (*UNCTAD*) inaonesha kuwa Tanzania imevutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,532, ikilinganishwa na Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ripoti ya Shirika la *Quantum Global* inayotafiti hali ya uwekezaji katika nchi 54 za Afrika imeiweka Tanzania katika namba 8 kutoka nafasi ya 19 mwaka 2015, ikiwa ni nchi pekee katika Afrika Mashariki kuwa katika nafasi kumi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2017, jumla ya shilingi 11.98 zilikuwa zimekusanywa ikilinganishwa na shilingi 8.9 zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Aidha, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 39.39 asilimia 48 inayojumuisha shilingi bilioni 31.6 na matumizi ya kawaida shilingi bilioni 7.76 za matumizi ya maendeleo fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo; sekta ya viwanda, Kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara kwa

kushirikiana na Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendesha kampeni za kuhamasisha Watanzania na taasisi mbalimbali kuchangamkia ujenzi wa uchumi wa viwanda. Elimu iliyotolewa na uhamasishaji huo inahusisha pia kutenga maeneo ya kujenga viwanda na kufanyia biashara, kuwahimiza na kuvutia wawekezaji na kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Shirikisho la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*Tanzania Social Security Association - TSSA*) pamoja na Mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF, PPF, LAPF, GEPF, PSPF* na *NHIF* imehamasika kuwekeza katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ikiwemo miradi ya kilimo cha miwa ya uzalishaji wa sukari Mkulazi, kutengeneza viatu vya ngozi, Kiwanda cha Chai Mponde, Kiwanda cha Mvinyo Dodoma na ujenzi wa kinu cha kuyeyusha chuma kitakachojengwa kule Kilimanjaro *machine tools* kwa kutaja baadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhamasisha hamasa ya uzalishaji na utumiaji wa bidhaa zinazotengenezwa nchini, Wizara imeendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda nchini. Kwa kushirikiana na Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (*CTI*), Wizara ilishiriki katika utoaji wa Tuzo za Mzalishaji Bora wa mwaka (*Presidential Manufacturers of the Year Awards*). Vilevile kwa kushirikiana na *Tanzania Private Sector Foundation*, tuliandaa kampeni kwanza ya kuhamasisha ununuzi wa bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *TanTrade* iliandaa maonesho ya kwanza ya viwanda Tanzania yaliyofanyika katika uwanja wa maonyesho ya Mwalimu Jusius Nyerere, barabara ya Kilwa Dar es Salaam tarehe 7-11 Disemba. Maonesho hayo yalishirikisha jumla ya viwanda vidogo 340, viwanda vikubwa na kati 80, taasisi za fedha tatu na taasisi 16 za Serikali zikiwemo Wizara na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamasishaji umefanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mikoa na Wilaya

kutenga maeneo ya uwekezaji wa viwanda kwa mahitaji ya sasa na baadae.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya viwanda; tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani hadi kufikia mwezi Machi, 2017, miradi ya viwanda vikubwa 393 yenye jumla ya mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 2,362.59 (shilingi trilioni 5.198 za Kitanzania) inayotarajiwa kutoa ajira 38,862 imesajiliwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na mingine katika hatua za mwisho za kuanza uzalishaji (Rejea jedwali langu Na. 7(b)).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya kimkakati; katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia *NDC* imewezesha kufikia makubaliano ya mfumo wa uziano ya umeme kati ya *TANESCO* na kampuni ya ubia ya Kichina. Mfumo uliokubalika ni mwekezaji kujenga mtambo wa kufua umeme, kumiliki na kuendesha (*build, own and operate*). Kamati ya Taifa ya Uwekezaji imepitia kwa mara nyingine vivutio vilivyoombwa na mwekezaji kwa maslahi mapana zaidi kwa Taifa. Aidha, mwekezaji amekwisha wasilisha nchini fedha za fidia na ameihakikishia Wizara kuwa yupo tayari kulipa fidia kwa watu watakaopisha mradi pindi apatapo Tangazo la Serikali (*Government Notice - GN*) kuhusu vivutio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uendelezaji wa eneo la viwanda *TAMCO*; eneo la viwanda la *TAMCO* Kibaha lenye ukubwa wa ekari 232 utahusisha sekta za uunganishaji magari, viwanda vya nguo na mavazi na viwanda vya dawa za binadamu limeshafunguliwa. Katika eneo hilo ndiko tunaunganisha matrekta 2,400 chini ya kampuni ya *URSUS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa magadi soda; utafiti wa magadi soda unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha Kutengeneza Matairi Arusha; katika mwaka 2016/2017, Wizara imefanya utafiti uliolenga kuangalia namna bora ya kufufua kiwanda cha matairi Arusha. Taarifa ya awali imebaini mambo makuu manne yaliyotakiwa kuzingatiwa katika

kukiendeleza kiwanda hiko ikiwemo kutafuta mitambo ya kisasa itakayofanya kazi kwa ufanisi na kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi za mazingira. Pia kiwanda kiendeshwe na sekta binafsi Serikali ikiwa mbia kwa hisa zilizozingana na rasilimali za kiwanda zilizopo. Kwa sasa taarifa hiyo inachambuliwa kuwezesha Serikali kufanya maamuzi ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uanzishaji wa Kanda Maalum za kiuendeshaji (*Bagamoyo Special Economic Zone*); Mradi wa Bagamoyo *Special Economic Zone* Awamu ya kwanza utaendelezwa kwa ubia kati ya Kampuni ya *Merchants Port Holdings Company Limited* ya China na Mfuko wa Hifadhi ya Hazina wa Serikali ya Oman. Awamu hiyo itahusisha ujenzi wa Bandari (*Sea Port*) kwenye eneo la hekta 800 na uendelezaji wa Eneo Maalum la Viwanda (*Portside Industrial City*) kwenye eneo la hekta 2,200 na ujenzi wa miundombinu wezeshi; barabara, reli, umeme, maji na gesi ili kuunganisha eneo la mradi na maeneo mengine ya nchi. Eneo linalobakia la hekta 6,800 litaendelezwa katika awamu ya pili itakayokwenda sambamba na awamu ya kwanza kwa kuzingatia mpango kabambe wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza kasi ya ulipaji wa fidia kwa watu ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kupisha mradi wa *Bagamoyo Special Economic Zone*, tarehe 7 Disemba, 2016 Serikali iliamua sekta binafsi ipewe nafasi kubwa ya kutekeleza mradi huo ikiwepo kulipa fidia. Niliambie Bunge lako Tukufu kwamba hawa wabia tuliowapata wapo tayari kuanza na kulipa fidia za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuendeleza mradi wa *Kurasini Logistic Centre*; eneo la Kurasini lina ukubwa wa hekta 62, ambapo kiasi cha fidia kilicholipwa ni Shilingi bilioni 101 kwa kaya 1,019. Eneo hilo limetangazwa kwa wawekezaji tarehe 20 Disemba na tayari makampuni matatu yameonesha nia ya kuendeleza. Taratibu za kumpata mwekezaji zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Morogoro Star City*;

tumebaini eneo la *Morogoro Star City* lenye ekari 10,661 wawekezaji kutoka Singapore wanajasilia eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mapya ya *special economic zone*; katika mwaka 2016/2017 Wizara imesajili na kuidhinisha kampuni mpya nane maeneo maalum ya uwekezaji (*Special Economic Zone*) nane zimeanzishwa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya ufundi stadi; katika juhudi za Serikali kuongeza ajira nchini, Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi na Ajira) kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi ilibuni na kuanzisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa vijana juu ya stadi za uzalishaji viwandani kwa kushirikiana na wenye viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vilivyoanzishwa katika kipindi cha mwaka mmoja; uwekezaji katika uzalishaji wa chuma na bidhaa za chuma umeendelea kuongezeka ambapo mwaka 2016/2017 viwanda vipya vitatu vimeanzishwa. Viwanda hivyo ni kiwanda cha *Kilwa Steel* ambacho kimewekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 41 kitazalisha tani laki tano kwa mwaka; Kiwanda cha *Lodhia Steel Industry* ambacho nacho kimewekeza Dola za Kimarekani 9.35 na kitatoa ajira 200. Kiwanda cha *Lake Steel and Allied Products Ltd* ambacho kimewekeza Dola za Kimarekani 13 na kitazalisha tani 168,000 za chuma kwa mwaka na kitaajiri watu 120. Uwekezaji umeongeza idadi ya sasa ya viwanda vya chuma kuwa 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya saruji; uzalishaji wa saruji nchini umeongezeka kutokana na upanuzi wa Kiwanda cha *Tanga Cement* kutoka tani 750,000 hadi tani 1,250,000 kwa mwaka na upanuzi wa Kiwanda cha *Mbeya Cement* ambacho kimeongeza uwezo kutoka tani 400,000 mpaka tani 1,100,000, hivyo, uwezo uliosimikwa kwa viwanda vyote 11 vya Tanzania (tuna viwanda 11 sasa vya kuzalisha saruji) ni tani milioni 10.8 kwa mwaka, mahitaji ya soko letu la ndani ni tani milioni 4.8. Aidha, kiwango cha juu cha

uzalishaji kilichowahi kufikiwa ni tani milioni 7.1 kilichofikiwa baada ya Kiwanda cha Dangote kuingia kwenye shughuli. Waheshimiwa Wabunge, mnajionea wenyewe, kuingiza kwa viwanda hivi vyote kumepelekea bei ya saruji mtaani kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi zimefanyika na kuweza kupata wawekezaji wapya. Pamoja na uwezo uliosimikwa wa *metric tonne* milioni 10.8, juhudi zilizofanyika tumeweza kupata kampuni ya Motisun itakayowekeza kiwanda cha saruji pale Chalinze na kitatengeneza saruji Chapa Mamba lakini Kampuni ya *Hengya Cement* itawekeza na kuzalisha tani milioni saba zitakazotuwezesha Tanzania kuzalisha saruji kwa ajili ya matumizi ya nchi hii na kuuza nje ya nchi. Wawekezaji wa Kiwanda cha Hengya wako hapo jukwaani wamekuja kushuhudia namna Serikali yao inavyotambua sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya vigae; kutokana na kutokuwa na viwanda vya vigae, nchi imekuwa ikitumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa hizo kutoka nje. Kwa mfano, mwaka 2015 nchi ilitumia Dola za Kimarekani milioni 90.61 kuagiza vigae nje. Juhudi za kuhamasisha uwekezaji zimeweza kupatikana uwekezaji mkubwa wa viwanda viwili ambavyo ni Kiwanda *Goodwill Ceramic Limited* kilichopo Mkuranga na Kiwanda cha *Twyford* kilichopo Chalinze, hili ndilo jalada katika kitabu chenu nilichowapatia. Kiwanda cha *Goodwill Ceramic* kimeshaanza na kinatarajia kuzalisha mpaka mita za mraba milioni 20 kwa mwaka na kitatoa ajira 4,500. Kiwanda cha *Twyford* kina uwezo wa kuzalisha mita za mraba milioni 12.5 kwa mwaka na kitatoa ajira 6,000. Viwanda vyote hivi viwili vinategemea malighafi za ndani kwa kiasi cha asilimia 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya nguo na mavazi; katika mwaka 2016/2017, Wizara imeanza utekelezaji wa mkakati wa kuendeleza sekta ya nguo na mavazi (*Cotton to Clothing Strategy*) ya mwaka 2016-2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya ngozi

na bidhaa za ngozi; kwa mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuhamasisha usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi ambapo Kiwanda cha Viatu - Bora, kimesimika mitambo yenye uwezo wa kuzalisha jozi za viatu vya ngozi 25,000 kwa mwaka maalum kwa ajili ya usalama viwandani. Pia kiwanda hicho kimekamilisha kufunga mitambo mitatu yenye uwezo wa kuzalisha viatu jozi 500,000 kwa mwaka kwa kutumia teknolojia ya *PVC* na raba jozi laki tano. Hiki ndicho kiwanda kilichokuwa kinaleta mgogoro miongoni mwa viwanda vilivyobinafsishwa. Kimeanza kazi, nina imani na wengine watafuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya kusindika nyama na maziwa; juhudi za kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya nyama umewezeshwa kupatikana eneo la ekari 6,000 kwa ajili ya kuanzisha Kiwanda cha Nyama cha *Nguru Hills* Wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro. Zaidi pacha wangu, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi atalizungumzia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya chakula na mbogamboga; hapa tunacho Kiwanda cha Sayona ambacho kitakuwa mkombozi kwa kuchakata matunda, lakini vilevile tunacho kiwanda cha Mheshimiwa Bakhresa ambacho kinakusanya matunda na kuyachakata. Kipekee, kuna Kiwanda cha *Elven Agri Company Limited* kitakachotumia teknolojia ya kukausha matunda na mahsusi kikilenga matunda yanayozalishwa kwa kutumia kilimo hai (*organic fruits*). Kina uwezo wa kukausha matunda tani 2,500 na kusindika tani 1,500 za nyanya kwa mwaka. Kiwanda kitatoa ajira za moja kwa moja 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *Vegeta Padravka Limited* kilichopo Bagamoyo nilikifungua mimi hicho – Mkoa wa Pwani, kimewekeza katika ukaushaji wa mbogamboga kwa ajili ya kutengeneza vionjo vya chakula (*food seasoning*). Kiwanda cha kutengeneza makaroni (*pasta*) cha aina yake kimeanzishwa sehemu ya Vingunguti kwa mtaji wa dola milioni 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda sio rafiki, viwanda



vya mafuta ya kula; Tanzania ina fursa ya kuzalisha mafuta ya kula kwa ajili ya matumizi ya ndani na ziada kuuzwa nje ya nchi. Uzalishaji wa mafuta ya kula kwa sasa ni tani 180,000 wakati mahitaji yanakadiriwa kuwa tani 400,000 kwa mwaka. Aidha, asilimia 55 ya mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni mafuta ya mawese (*crude palm oil*).

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya sukari; kama kila mtu anavyojua, tuna tatizo la upatikanaji wa sukari. Katika kueneza jitihada hizo, kama nilivyoeleza kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii watazalisha tani 200,000 kwa kutumia njia Mkulazi ambazo zitatuzesha kutengeneza 100,000.

Kiwanda *Kagera Sugar Estate* kinapanua uwezo wa uzalishaji na kitaongeza ajira kutoka 2,500 za sasa hadi 3,000. Aidha, kila Aprili 2017, Kampuni ya *Mkulazi Holdings*, kama nilivyoeleza, itazalisha tani 200,000 na kutengeneza ajira 100,000. Kiwanda cha Sukari Mbigiri - Morogoro, pacha wangu, Mheshimiwa Mwigulu atakuja kueleza na chenyewe kinarudia kwenye kazi, kitazalisha tani 30,000 kwa mwaka (Rejea jedwali Na. 9 kwa biashara ya sukari).

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya vifungashio; Wizara inaendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya vifungashio kwa kutambua mahitaji yake kwa soko la ndani. Kiwanda cha *La Kairo Polybag*, ambacho ni cha Mheshimiwa Mbunge na chenyewe kimeshaingia kazini, kimewekezwa kwa kutumia bilioni nne. Kiwanda cha *Global Packaging* kilichotumia bilioni 10 na chenyewe kimeanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya mbolea; Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara zingine kufanikisha miradi ya viwanda vya mbolea kwa kutumia gesi asilia kupitia miradi miwili ya *Ferrostaal Consortium Limited* na *Helm*. Kampuni ya *Ferrostaal Consortium* kwa kushirikiana na *TPDC* wapo kwenye majadiliano ili waweze kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya dawa za binadamu; kwa mwaka 2016/2017 Serikali imefanya uhamasishaji mkubwa kwenye sekta ya dawa za binadamu

ili kuvutia ujenzi wa viwanda vipya na kufufua vilivyofungwa. Uhamasishaji huo umefanikisha ushirikiano mkubwa kati ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto chini ya usimamizi mahiri wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msimamizi wa viwanda vya sekta ya madawa ni Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi hizo miradi mbalimbali imeanza kutekelezwa; mradi wa kutengeneza vifaa tiba vitokanavyo na pamba (*medical textile*) utakaojengwa Mkoa wa Simiyu wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 36.5 unatarajiwa kuanza hivi karibuni. Kiwanda hicho kitatumia tano 50,000 za pamba kwa mwaka na kutoa ajira 1,600 za moja kwa moja na ajira 5,000 zisizokuwa za moja kwa moja. Mradi wa *Zinga Pharmaceutical* unaoanzishwa na Watanzania katika eneo la Zinga, Bagamoyo utazalisha vidonge bilioni moja, *capsules* milioni 175, dawa za maji (*syrups*) chupa milioni 15 na dawa ya kupunguza makali ya UKIMWI vidonge milioni 200 kwa mwaka. Mradi utatekelezwa kwa kutumia shilingi bilioni 70 na utatoa ajira kwa watu 210.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine ni pamoja na mradi wa kutengeneza sindano (*syringes*) ambao ni milioni 80 kwa mwaka na kutoa ajira 150, pamoja na huo ni mradi wa *Pharmaceutical Park* utakaotengeneza *Intravenous Fluids* chupa 10,000 kwa mwaka utakaojengwa katika eneo la viwanda la *TAMCO* kwa mtaji wa shilingi milioni 102.732 na kutoa ajira 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya sabuni; Kiwanda cha *KEDS Tanzania* cha kuzalisha sabuni ya unga kinajengwa katika eneo la viwanda *TAMCO*, Kibaha. Kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka kitawekeza Dola za Kimarekani milioni 11.5 sawa na shilingi bilioni 25 za Kitanzania. Kiwanda kitakapokamilika kitatoa ajira za moja kwa moja 700, na hiki niliweka jiwe la msingi mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya kutengeneza sigara; kiwanda kitafunguliwa Morogoro mwezi wa saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa na visivyofanya kazi; katika mwaka 2016/2017, ufuatiliaji ulifanyika ambapo jumla ya viwanda 30 vilifanyiwa ufuatiliaji na Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Taarifa zaidi nitaeleza huko mbele, mojawapo ni Kiwanda cha *Morogoro Canvas*, wakati wowote kitaanza kazi, Kiwanda cha *MOPROCO* nina uhakika kinaanza mwezi wa sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Korosho Nachingwea kilingia makubaliano ya awali na kampuni ya *Sunshine Industry* ya China mwezi Machi, 2017 ya kufufua kiwanda hicho kwa utaratibu wa kujenga, kumiliki na kuendesha. Usimikaji wa mitambo unaendelea na uzalishaji unatarajiwa kuanza Septemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kujenga kongano za viwanda (*industrial clusters*); hadi kufikia mwezi Aprili 2017, Wizara imewezesha kuzalisha makongano ya uzalishaji ambayo ni kongano la mafuta ya alizeti katika eneo la Chamwino Dodoma, kongano la useketaji nguo kwa kutumia mashine za mikono (*handlooms*) Tabora, Arusha na Dar es Salaam na kongano la ngozi na bidhaa za ngozi katika eneo la viwanda la Zuzu Magharibi, Dodoma. Kongano hizo zitawezesha wazalishaji wadogo kuongeza uwezo wa uzalishaji, ubora wa bidhaa zitakazozalishwa na ufanisi katika uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilishiriki kikamilifu katika kuandaa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda kwa Nchi za *SADC*, 2015 - 2030. Mpango Kazi wa kutekeleza Mkakati huo ulipitishwa na Wakuu wa nchi za *SADC* tarehe 18 Machi, 2017 huko Swaziland.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya makaa ya mawe; katika mwaka wa fedha tunaomaliza, Serikali imefanya maamuzi ambapo tumeanza kuchochea utumiaji

wa makaa ya hapa nchini. Kampuni ya *TANCOAL, Magamba Coal, Kabulo Ridge, Katewaka Coal Mine*, zinazalisha makaa ya mawe na Tanzania itakuwa inatoa makaa ya mawe kwa nchi zilizotuzunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa KAIZEN umeendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo, sera ya maendeleo ya viwanda vidogo na biashara ndogo; kutokana na ushirikiano mzuri wa Serikali na Shirika la Kazi Duniani, *International Fund for Agriculture Development (IFAD)* na *Financial Sector Deepening Trust* Wizara imekamilisha kutathmini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003 ili kutambua mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhamasishaji Halmashauri kutenga maeneo; katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuhamasisha na kufuatilia utengaji wa maeneo kwa ajili ya viwanda vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa *NEDF*; Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara wa nchi (*National Entrepreneurship Development Fund*) ulianzishwa mwaka 1994 na nitasambaza taarifa ya utekelezaji wake, kwa mwaka huu mfuko huo umeweza kusambaza shilingi bilioni 3.92.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya biashara; katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Wizara imeratibu na kufuatilia majadiliano mbalimbali ya biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine. Kuanzia Ibara ya 78 inaonesha safari za kimataifa na uhamasishaji uliofanyika tukiwa tunawashawishi wawekezaji waje nchini kwetu, mpaka Ibara ya 76.

Aidha katika Ibara ya 78, Wizara imeshiriki kikamilifu katika mkutano wa dharura wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) uliofanyika mwezi Machi, 2017 Mjini Lozitha, Swaziland.

Kupitia mkutano huo, Tanzania imefanikiwa kupata upendeleo maalum (*dispensation*) wa kuendelea kutoza ushuru wa asilimia 25 kwa sukari inayotumika kwa matumizi ya nyumbani kutoka nchi za SADC.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya biashara ya Kimataifa ni kama nilivyoeleza, tumeendelea na jitihada za kuhamasisha nchi ziweze kushiriki lakini muhimu kuzungumza, katika kupambana na bidhaa zinazotoka nje ya nchi na kuuzwa nchini chini ya bei halisi ya soko, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeratibu zoezi la kuandika upya Sheria ya *Anti-dumping and Countervailing Measures*, sheria hiyo inalenga kuzuia uingizaji wa bidhaa nchini zinazouzwa chini ya bei halisi ya bidhaa hizo (*dumping price*) ili kuhakikisha kunakuwepo na ushindani wa haki kwenye soko. Kutokana na umuhimu wake, tunatarajia sheria hiyo ianze kutumika rasmi katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya masoko ina jukumu la kuvipatia viwanda malighafi, kuvilinda, kuuza bidhaa, kumlinda mlaji na kuhakikisha ubora na ushindani ulio haki. Katika kujenga uchumi wa viwanda, Wizara imesimamia majukumu chini ya sekta hiyo kwa lengo la kuongeza tija katika sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa ubora na viwango ni kazi ya TBS, tumeifanya vizuri, bei za mazao ya soko tumeendelea kuyadhibiti kama inavyozungumzwa kwenye Ibara ya 95. Kuimarisha biashara za mipakani, Ibara za 97 na 98, tumeanzisha *One Stop Border Posts* kwenye mipaka yetu, inajieleza kwenye kitabu changu.

Mheshimiwa Naiu Spika, kuhusu sekta ya uwekezaji, kuhamasisha uwekezaji wa ndani. Mnamo mwezi Septemba, 2016, Wizara ilishiriki katika Kongamano la Uwekezaji Mkoani Morogoro lililolenga kuhamasisha uwekezaji katika Mkoa wa Morogoro. Tumehamasisha na nitatoa mwongozo namna Mikoa mingine itakavyoweza kuiga Morogoro, Pwani na Simiyu kuweza kueneza sera ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa mazingira ya kufanya shughuli; ili nchi ivutie na kukuza uwekezaji wa ndani na kuvutia wawekezaji kutoka nje, yapo mambo manne muhimu ya kufanya; kwanza, ni lazima nchi iwe na amani na utulivu; pili, lazima mwenendo wa uchumi wa nchi uwe na utulivu; tatu, uimara na uendelevu yaani kuwe na *macroeconomic stability and sustainability*; nne, ni lazima nchi iwe na miundombinu na huduma nzuri za kuwezesha ufanyaji wa shughuli za uchumi na tano, ni kuweka mazingira ya kiseru, kisheria, kikanuni na kiutendaji ambayo ni wezeshi kwa ajili ya kuendesha shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 105 tunakwenda kwenye uratibu na urahisi wa kufanya biashara, nimetengeneza Mkakati wa *Ease of Doing Business*, mnaweza kuusoma Ibara ya 106 unajieleza wenyewe, kwa faida ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa taasisi chini ya Wizara, tuna Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (*TIRDO*); kazi za *TIRDO* nzuri kuliko yote niliyoeleza katika Ibara ya 109 na 110 ni kufanya utafiti wa kutumia makaa ya mawe ambayo yataondoa utumiaji wa makaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (*TEMDO*); Waheshimiwa Wabunge msome kitabu changu ukurasa wa 295 na kuendelea mvione vile viwanda vilivyotengenezwa na *TEMDO* ambavyo jamaa mmoja huwa anaviita viwanda vya mfukoni. Kuna kiwanda na bei yake na matumizi yake na kinakuonesha namna unavyoweza kuwapelekea wapiga kura wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya mbolea; Kampuni ya mbolea kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi imeendelea kuratibu uingizaji wa mbolea nchini. Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*) limeendelea kutoa elimu ya uenezaji wa teknolojia, uanzishaji wa miradi ya viwanda vidogo, mafunzo, ushauri, huduma za masoko, huduma za fedha; hizo zote ni kazi za *SIDO* na viatamizi kuwalea wajasiriamali wadogo. Napenda niseme,

mwakilishi wangu Mkoani ni *SIDO*, anayetaka viwanda tuanzie *SIDO*. Huwezi kuanzia darasa la saba, anza darasa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Viwango Tanzania limeendelea na udhibiti wa ubora wa bidhaa kutoka nje ya nchi kwa kufanya ukaguzi wa bidhaa hizo katika nchi zinakotoka. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, jumla ya vyeti vya ubora (*Certificate of Conformity*) 23,606 vimetolewa, sawa na asilimia 73, na nipende kusema – ninaweza nikakosa muda huko mbele, tufikapo Julai, tarehe 01, bidhaa zisizokidhi viwango zikipita mtakuwa hamnitakii mema lakini na waliopo chini yangu tukae mkao tayari wa kuondoka kama bidhaa zisizokidhi viwango zitakuja kuumiza viwanda vyetu. Pia Tume ya Ushindani, nimeielezea katika Ibara ya 130.

Kuhusu Wakala wa Usajili wa Biashara nchini, nimeielezea katika Ibara ya 132, kubwa zaidi, kwa faida ya muda, kwa mamlaka niliyopewa na Mheshimiwa Rais sasa usajili wa leseni daraja "A" utafanyika katika Kanda badala ya kufanyika Dar es Salaam tu. Kwa hiyo, tunapeleka madaraka Mikoani, ni mamlaka niliyopewa, ndiyo kazi ambayo nimeifanya katika mwaka uliopita. Kupeleka huduma karibu na wananchi, ndiyo nimezungumza ya *BRELA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Vipimo ndiyo amesaidia mambo ya lumbesa, lakini wakulima wa korosho wanatambua kazi yake aliyofanya na wakulima wa pamba, ndiyo amechochea kwa kiasi kikubwa bei nzuri walizozipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania; kituo hiki kimeboreshwa kama ninavyoeleza katika Ibara ya 142 na kuendelea, tukiwa tunaboresha *One Stop Centre* kama tulivyoshauriwa na kuelekezwa na Kamati ya Bunge inayonisimamia. Kimsingi watu wa *NEMC*, watu wa *TBS* wanakuwepo wakati wote pale ili kuweza kutoa ushauri kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya uwekezaji mahiri; nimeielezea ibara ya 145, uhamasishaji wa uwekezaji katika

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ibara ya 146, uendeshaji wa ofisi na mambo mtambuka. Kwa faida ya muda, Ibara ya 148 nazungumzia mambo mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018, Sekta ya Viwanda ina malengo yafuatayo:-

(a) Kuendeleza jitihada za kuhamasisha sekta binafsi kuendeleza viwanda vilivyopo na kuanzisha viwanda vipya.

(b) Kuendeleza viwanda mama na miradi ya kimkakati.

(c) Kuendeleza jitihada za kubainisha na kutenga maeneo ya ujenzi wa viwanda.

(d) Kujenga mfumo wa taarifa za sekta mbalimbali za viwanda nchini.

(e) Kufanya tathmini ya mahitaji ya ujuzi maalum wa viwanda na kuziendeleza.

(f) Kujenga uwezo wa taasisi za utafiti zilizo chini ya Wizara.

(g) Kushirikiana na Msajili wa Hazina na Wizara za kisekta.

(h) Kushirikiana na Wakuu wa Mikoa kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi ipasavyo. Rejea ukurasa wa 107 hadi 109 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda vidogo, nimeeleza katika ukurasa wa 109 hadi 110. Sekta ya Biashara nimeeleza zaidi, rejea ukurasa wa 111 hadi 114.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018, sekta ya masoko itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na



uwekezaji. Nirudie tena; ni jukumu langu kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

(b) Kuwaunganisha wazalishaji na masoko.

(c) Kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

(d) Kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vituo maalum vya kuuzia mazao ili kupambana na lumbesa. Rejea ukurasa wa 114 mpaka 116 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uwekezaji; katika mwaka 2017/2018, idara ya uwekezaji itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea na kuratibu na utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996;

(b) Kukamilisha mapitio ya Sera, Mkakati na Sheria ya Uwekezaji;

(c) Kufuatilia miradi ya uwekezaji nchini; na

(d) Kuratibu kwa karibu uwekezaji katika sekta maalum. Rejea ukurasa wa 116 mpaka 117 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi chini ya Wizara; kama ulivyoeleza, ninazo taasisi 19 na Wakurugenzi wake wako pale ukurasa wa 117 mpaka 133 wa hotuba yangu nimeeleza kazi watakazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2017/2018; Mapato ya Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 20 kutokana na ada za leseni, uzaji wa nyaraka za zabuni za Serikali na kutoza faini wale watakaokiuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya jumla ya fedha;

kwa mwaka 2017/2018 Wizara imetengewa kwa Fungu 44 na Fungu 60 jumla ya shilingi 122,215,109,750 kwa Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha, hizo Matumizi ya Kawaida ni shilingi 42,024,732,750 na Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 80,190,377,000. Kwa faida ya muda, nimenyambua kazi inavyoendelea, hizo pesa zitakavyokwenda.

Kwa faida ya muda nimenyambua kazi zinazoendelea na hizo fedha jinsi zitakavyokwenda kwa hiyo niende kwenye hitimisho. Wajenzi wa nchi ni wananchi. Hivyo, napenda kuwashukuru kwa dhati Watanzania wote kwa uzalendo wenu wa kuitendea haki na kuipigania kwa kauli na vitendo ajenda ya kitaifa ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Ndiyo, tumepiga hatua kwenda mbele, lakini inatubidi kuongeza nguvu, mbinu na maarifa zaidi ili vita hiyo iwe na medani zinazokidhi aina na namna ya mapambano ya kiushindani yaliyopo na yajayo. Siri ya wazi ya ushindi ni uwajibikaji wa kila mmoja wetu na kuwepo ushirikiano usio na shaka na endelevu wa wadau wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa upande wake itaendeleza na kuboresha ulinzi kwa sekta, kuweka mazingira ya uwekezaji, uendelezaji, ujenzi na uboreshaji wa viwanda, biashara na masoko ili wadau wote waweze kutumia ipasavyo fursa zilizopo na zijazo. Naomba Watanzania wote na wote wenye mapenzi mema kwa nchi yetu muendeleo kutuamini na kutupa ushirikiano unaohitajika. Tunaamini tuko katika njia na mwelekeo sahihi, sasa tusonge mbele pamoja kwa nia na ari moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(Makofi)

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono,

**HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA  
UWEKEZAJI MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018 -  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuanzia tarehe 29 hadi 30 Machi, 2017, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka 2017/2018.

**2. Mheshimiwa Spika,** napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya, upendo, baraka, ulinzi na usalama unaotuwzesha kumudu majukumu, dhamana na wajibu wetu kwa Taifa na jamii nzima ya Watanzania. Naomba kazi njema za mikono yetu ziendeele kumpendeza na hivyo kupata kibali chake daima.

**3. Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi thabiti na maamuzi makini yanayotia chachu, ari na kasi ya utekelezaji wa mipango yenye tija na manufaa mapana kwa Taifa. Hatua hizo zimetoa msukumo wa kipekee katika kuimarisha uwajibikaji wa umma wa Watanzania katika kuchochea maendeleo na vita dhidi ya umaskini.

**4. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuwa nguzo imara ya kuelekeza na kusimamia masuala yanayoimarisha ushirikiano wa masuala ya kisekta kwa Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT)

**5. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuongoza vyema shughuli za Serikali Bungeni na kusimamia vyema shughuli za Serikali bungeni. Pia, ninampongeza kwa hotuba yake yenye kutoa dira makini ya malengo, mipango na mwelekeo wa utendaji wa Serikali hususan katika kutekeleza mipango na programu za Serikali ya Awamu ya Tano kwa mwaka 2017/2018. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wamewasilisha Hotuba za Bajeti za mwaka 2017/2018 na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

**6. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge la Kumi na Moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Tano ya Uongozi wa nchi yetu. Tunashukuru kwa ushirikiano ambao Wizara na wadau wake wameendelea kuupata kutoka kwa wenyeviti wa kamati za kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**7. Mheshimiwa Spika**, namshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniadini kushika dhamana ya kusimamia na kuendeleza sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji nchini. Nami napenda kumhakikishia kuwa nitaendelea kujibidiisha kutekeleza jukumu hilo ili kukidhi matarajio ya Watanzania walio wengi kwa kuifanya Tanzania ya kesho kuwa ya matumaini makubwa zaidi kupitia maendeleo ya viwanda.

**8. Mheshimiwa Spika**, vilevile, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Stanslaus

Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki (CCM) na waheshimiwa wajumbe wote kwa namna ambavyo wameipokea, kuichambua na kushauri juu ya mambo ya msingi ya Bajeti ya Mwaka 2017/2018, katika kuendeleza sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji. Napenda kukuhakikishia Mheshimiwa Spika, ushauri na maelekezo ya Kamati, tunayathamini na tumeyazingatia katika kuandaa na kuboresha Hotuba ninayoiwasilisha.

**9. Mheshimiwa Spika,** napenda kuwapongeza Mheshimiwa Alhaji Abdallah Majura Bulembo (Mb.), Mheshimiwa Anne Killango Malecela (Mb.); Mheshimiwa Juma Ali Juma (Mb.); Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.); Mheshimiwa Salma Rashidi Kikwete (Mb.); na Mheshimiwa Mch. Dkt. Gertrude Pangalile Rwakatare (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge. Vilevile, nawapongeza wabunge wateule wa Bunge la Afrika Mashariki kwa ushindi wao. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Tunawakaribisha kuungana nasi katika shughuli hii muhimu ya kujenga Tanzania ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

**10. Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wao katika Bunge hili tukufu. Aidha, naishukuru sana familia yangu hususan mke wangu, watoto, ndugu na jamaa kwa sala zao na kwa ushirikiano wao mzuri unaonipa nguvu na hamasa katika kuwatumikia Watanzania wenzangu.

**11. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa uchumi wa nchi yetu na hususan maendeleo ya sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo, biashara ndogo na uwekezaji unategemea sana ushirikiano wa wananchi na wadau wote ndani na nje ya nchi. Hivyo, napenda kutambua na kushukuru taasisi za sekta binafsi za ndani na nje ya nchi, waandishi na

wamiliki wa vyombo vya habari, Washirika wa Maendeleo na Watanzania wote kwa ujumla. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara kwa wakati.

**12. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii ya bajeti ninayoiwasilisha ni matokeo ya kazi nzuri na makini ya ushirikiano wa Menejimenti ya Wizara na taasisi zake. Hivyo, niruhusu niwapongeze Dkt. Adelhelm J. Meru, Katibu Mkuu – Viwanda; Prof. Adolf F. Mkenda, Katibu Mkuu-Biashara na Uwekezaji; Mhandisi Joseph K. Malongo, Naibu Katibu Mkuu; wenyeviti wa bodi, wakuu wa idara na vitengo; taasisi na watumishi wote wa Wizara. Nina imani kubwa kuwa ari hiyo itaendelea kuimarishwa kwa kutumia ipasavyo fursa, utaalum na ujuzi walionao katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kisekta (*Jedwali Na. 1*).

**13. Mheshimiwa Spika**, naomba kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mhe. Hafidh Ally Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Dimani (CCM) na Mhe. Dkt. Elly Marko Macha, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Aidha, nawapa pole ndugu, jamaa marafiki na wananchi wote waliokumbwa na kadhia ya tetemeko la ardhi, maafa ya mvua, ukame na ajali zilizotokea ambazo zimesababisha majeruhi, ulemavu, vifo na uharibifu mkubwa wa mali. Tunaomba Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa faraja timilifu.

**14. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nieleze majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

## **2.0 MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**

**15. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambayo imeundwa kwa Tamko la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili, 2016 ina majukumu yafuatayo:-

(a) Kuandaa, kuratibu na kupitia Sera na mikakati ya sekta

ya Viwanda, Biashara, Uwekezaji, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo;

(b) Kufuatilia na Kuperemba (M&E) utendaji katika viwanda, biashara, uwekezaji, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na taasisi zinazowezesha maendeleo ya viwanda, biashara na uwekezaji;

(c) Kubuni na kuandaa programu za kuendeleza sekta za viwanda, biashara, uwekezaji, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na taasisi zinazowezesha maendeleo ya viwanda, biashara na uwekezaji;

(d) Kukusanya, kuchambua, kusambaza na kutathmini taarifa za sekta za viwanda, biashara, uwekezaji, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo;

(e) Kukuza na kuhamasisha biashara ya ndani na nje na kuboresha upatikanaji wa huduma za kuendeleza biashara;

(f) Kuimarisha ufanisi wa utendaji wa wafanyakazi wa Wizara na taasisi zake;

(g) Kusimamia utekelezaji wa sheria zinazosimamia viwanda, biashara na uwekezaji;

(h) Kuimarisha utafiti wa maendeleo ya Sekta ya Viwanda;

(i) Kusimamia utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara;

(j) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa sekta binafsi;

(k) Kutafuta fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania; na

(l) Kuratibu na kutoa mwongozo juu ya maendeleo ya uwekezaji na uboreshaji wa mazingira ya biashara.

**16. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nieleze Mchango na Mwelekeo wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika mwaka 2016/2017.

### **3.1 MCHANGO NA MWELEKEO WA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI KATIKA KULETA MAGEUZI YA UCHUMI**

### **3.2 DHIMA YA MAGEUZI YA UCHUMI WA VIWANDA**

**17. *Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Awamu ya Tano inaingia katika mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016/2017 – 2020/2021 unaojikita katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Lengo kuu la Mpango huo ni kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati inayoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Ni dhahiri, Tanzania kama zilivyo nchi nyingine duniani inahitaji uchumi wa viwanda ili kuleta mageuzi ya haraka na kujenga msingi imara wa uchumi. Uamuzi wa Serikali wa kujenga uchumi wa viwanda unalenga kuleta maendeleo jumuishi na endelevu kwa kutumia ipasavyo rasilimali zilizopo na hivyo kuchangia katika kukuza Pato la Taifa, kutoa nafasi nyingi na endelevu za ajira, kuzalisha na kukuza teknolojia zinazohitajika na kuwa chachu ya maendeleo ya sekta zinazohusiana na kuzalisha bidhaa bora kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

**18. *Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa uchumi wa viwanda unahitaji umadhubuti na nguvu za ziada katika kusimamia na kutekeleza kwa vitendo uvutiaji wa wawekezaji, ujenzi wa viwanda, kulea na kulinda viwanda vya ndani na pia kupambana na nguvu za ushindani usio haki katika soko. Mfumo wa mahusiano ya kiuchumi kati ya mataifa makubwa na madogo duniani hauna urafiki wa kuachia nchi maskini zijitawale kiuchumi. Kwa hiyo, Wizara inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kila Mtanzania kwa nafasi yake awe na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya soko, kufichua na kudhibiti mbinu chafu za soko, kuwa tayari kuwekeza na pia kutoa kipaumbele katika kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini.

### **3.3 SEKTA BINAFSI KATIKA UJENZI WA UCHUMI WA VIWANDA**

**19. *Mheshimiwa Spika***, kimsingi, sekta binafsi



inajumuisha shughuli zote za uzalishaji kiuchumi zinazoendeshwa na watu binafsi, makampuni, taasisi pamoja na shughuli zinazohusisha ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi (*Joint Ventures*). Kwa maana nyingine, sekta binafsi inajumuisha jasiriamali ndogo sana, ndogo na za kati (*Micro, Small and Medium Enterprises - MSMEs*) ambazo uzoefu duniani unaonesha ndizo zenye mchango mkubwa kwa maendeleo ya jamii. Katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, sekta binafsi inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kutumia fursa zilizopo na zinazojitokeza katika uwekezaji, biashara na masoko. Pia, ina jukumu la kutoa ushirikiano unaohitajika (*Public-Private Dialogue*) katika jitihada zinazofanywa na Serikali za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kupambana na mbinu chafu na zisizo haki katika soko zinazopunguza ushindani na kuboresha mbinu za uzalishaji kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kukidhi matakwa ya kuchochea maendeleo kwa wote. Hivyo, Serikali inategemea ushirikiano wa dhati kwa sekta binafsi kuunga mkono ipasavyo sera, programu, mikakati, sheria na kanuni zinazopigania, kutetea na kulinda maslahi ya Taifa.

**20. *Mheshimiwa Spika***, maendeleo ya sekta binafsi na uwekezaji ndio msingi wa mipango mikuu ya maendeleo ya nchi yetu. Sera, mipango na mikakati mbalimbali ambayo Serikali imekuwa inaandaa, kuboresha na kutekeleza siku zote ina lengo la kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi iendelee kuwa mhimili wa uchumi na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya viwanda. Lengo ni kufikia Dira ya Maendeleo (2025) kwa kuweka misingi ya uchumi wa soko huria ili kuwa na uchumi wenye ushindani (*competitive economy*). Jukumu kubwa la Serikali katika mipango hiyo ni kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi itimize wajibu wake wa kuwekeza na kuzalisha bidhaa na kutoa huduma.

**21. *Mheshimiwa Spika***, Serikali inathamini jitihada za sekta binafsi zinavyoshiriki katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji, kushirikiana na sekta za umma na kuendesha shughuli za uzalishaji. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania ilifanikiwa kusajili jumla ya miradi 242 ya sekta mbalimbali ambayo

ilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,079; na inayotarajiwa kutoa ajira mpya zipatazo 17,385. Kati ya miradi hiyo, miradi ya viwanda ni 170 ambapo miradi 54 ipo katika hatua ya ujenzi na miradi 17 imeanza uzalishaji. Kwa upande wa viwanda vidogo, SIDO imeweza kusajili viwanda vidogo 1,843 katika mikoa mbalimbali nchini. Serikali itaendelea kushirikiana kikamilifu na sekta binafsi katika maandalizi na maboresho ya sera, mikakati na sheria mbalimbali kwa kuhusisha wadau wa kisekta wakiwemo TPSF, TCCIA, CTI na TAFOPA kwa kutaja baadhi.

### **3.4 MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**

#### **3.3.1 Sekta ya Viwanda**

**22. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2016, shughuli za uzalishaji viwandani zilikuwa kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2015. Ukuaji huo ulitokana na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za vyakula, vinywaji na bidhaa za tumbaku. Ukuaji wa Sekta ya Viwanda wa asilimia 7.8 ni juu ya wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2016. Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 5.1 ukilinganishwa na asilimia 5.2 katika mwaka 2015. Kwa mwaka 2016, Sekta ya Viwanda imetoa ajira 146,892 ikilinganishwa na ajira 139,895 zilizotolewa mwaka 2015. Ongezeko hilo la asilimia 7.1 kwa mwaka lilitokana na ajira mpya viwandani kufuatia uwekezaji katika upanuzi na uanzishaji wa viwanda vipya nchini (*Jedwali Na.2a, 2b, 2c, 2d, 2e, 2f na 2g*).

#### **3.3.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

**23. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo nchini ni sekta muhimu katika kutengeneza ajira, kukuza kipato na kuondoa umasikini. Sekta hiyo ina jumla ya jasiriamali milioni 3.1 ambazo zimeajiri asilimia 23.4 ya nguvu kazi ya Taifa na imechangia asilimia 27 katika Pato la Taifa. Aidha, kulingana na takwimu za Sensa ya Viwanda ya mwaka 2013 iliyozinduliwa mwaka 2016, Tanzania ina jumla

ya viwanda 49,243 ambapo asilimia 85.13 ni viwanda vidogo sana, asilimia 14.02 ni viwanda vidogo, asilimia 0.35 ni viwanda vya kati na asilimia 0.5 ni viwanda vikubwa. Takwimu hizo zinadhihirisha kuwa asilimia 99.5 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati (*Jedwali Na.3a*).

**24. Mheshimiwa Spika**, taswira ya takwimu hizo inaonesha wazi kuwa maendeleo ya viwanda Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine yatatokana na kuweka nguvu katika sekta za viwanda vidogo, viwanda vidogo sana na vya kati. Hali hiyo siyo ya kushangaza kwa kuwa taswira kama hiyo inajitokeza pia katika nchi karibu zote duniani. Kwa mfano, Japan, viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati vinachukua takribani asilimia 99 ya Sekta ya Viwanda; Kenya asilimia 98; Malaysia asilimia 97.3; Indonesia asilimia 99.9; Canada asilimia 98 na Ujerumani asilimia 99. Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuviwezesha viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati kukua na kufanya kazi kwa tija zaidi.

**25. Mheshimiwa Spika**, faida ya Sekta ya Viwanda Vidogo ni kuwa uanzishwaji wake hauhitaji elimu kubwa na mtaji mkubwa na hivyo vinaweza kuanzishwa katika eneo lolote la nchi yetu. Sekta hiyo inatoa mwanya mkubwa kwa vijana na wanawake kuanzisha viwanda na kujajiri ambapo wasingepata fursa katika sekta nyingine zinazotoa ajira. Viwanda vidogo huongeza thamani ya mazao, hali ambayo humpatia kipato zaidi mzalishaji na kupunguza hasara baada ya mavuno. Sekta ya Viwanda Vidogo ni msingi muhimu wa kuwandaa Watanzania kuwa wamiliki wa viwanda vya kati na viwanda vikubwa hapo baadaye. Viwanda vidogo ni darasa kwani wale wanaoanza na viwanda vidogo sana huhitimu na kujenga viwanda vidogo, vya kati na hatimaye viwanda vikubwa. Sekta ya Viwanda Vidogo husaidia kusambaa kwa viwanda nchi nzima hali ambayo pamoja na faida nyingine, hupunguza wimbi la wananchi kutoka vijijini kuhamia mijini. Aidha, ujenzi wa viwanda kwa kutumia mfumo huo ndio hujenga Sekta ya Viwanda endelevu.

### 3.3.3 Sekta ya Biashara na Masoko

26. *Mheshimiwa Spika*, shughuli za biashara za jumla na rejareja, ukarabati wa magari na pikipiki na vifaa vingine vya nyumbani kwa mwaka 2016 zilikuwa kwa kasi ya asilimia 6.7 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.8 mwaka 2015. Kasi ya ukuaji wa shughuli hizo ulipungua kwa asilimia 1.1 kutokana na kushuka kwa mauzo ya bidhaa zilizoingizwa nchini katika mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka 2015. (*Jedwali Na. 3b*).

### 3.3.4 Sekta ya Uwekezaji

27. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea na jitihada za kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuchangia ipasavyo katika uwekezaji nchini. Kutokana na jitihada hizo, Sekta ya Uwekezaji imeendelea kukua ikilinganishwa na nchi nyingi za Afrika Mashariki. Ripoti mbalimbali za uwekezaji duniani zinaonesha Tanzania imeongoza kwa kuvutia uwekezaji kwa mwaka 2016 katika Afrika Mashariki. Kwa mfano, Ripoti ya Uwekezaji ya Dunia (World Investment Report) ya mwaka 2016 inayotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) inaonesha kuwa Tanzania imevutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,532 mwaka 2015, ikifuatiwa na Kenya Dola za Kimarekani 1,437 na Uganda Dola za Kimarekani 1,057. Vile vile, ripoti ya Shirika la *Quantum Global* inayotafiti hali ya uwekezaji katika nchi 54 za Afrika imeiweka Tanzania katika namba nane kutoka nafasi ya 19 mwaka 2015, ikiwa ni nchi pekee katika Afrika Mashariki kuwa katika nafasi kumi za juu. Ripoti hiyo inaangalia vigezo sita vikiwemo ukuaji wa uchumi, mzunguko wa fedha, ubadilishaji wa fedha, mazingira ya biashara, wingi wa watu na matumizi ya teknolojia na ubunifu.

28. *Mheshimiwa Spika*, takwimu hizo za nafasi nzuri ya nchi yetu kwenye uwekezaji zinaonekana pia katika viwango vya uwekezaji nchini. Kwa mfano, takwimu za Benki ya Dunia zinaonesha uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa umekua kutoka asilimia 14.8 mwaka 1997 mpaka asilimia 31.3

mwaka 2015. Hivyo ni viwango vikubwa ikilinganishwa na wastani wa nchi za Afrika wa asilimia 21 – 22 na nchi zilizoendelea wa asilimia 23 - 25. Kwa kuwa uchumi wetu umekuwa ukikua, hiyo inaonesha bado kuna uwezekano mkubwa wa kuongeza kiwango cha uwekezaji nchini.

**29. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa nitoe taarifa ya Utekelezaji wa Mipango na Bajeti kwa mwaka 2016/2017.

#### **4.0 UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/2017**

**30. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imetekeleza mipango iliyoanishwa katika Ilani ya CCM ya 2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Mwaka 2016/2017 – 2020/2021, ambayo imefafanuliwa kissekta katika Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano na Mpango Kazi wa 2016/2017. Aidha, Wizara imezingatia ahadi na maagizo ya viongozi wakuu wa Serikali, sera na mikakati mbalimbali ya kissekta, kitaifa na kimataifa. Mipango hiyo inatoa mwelekeo wa kissekta na kuwa mwongozo wa utekelezaji wa sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji.

#### **4.1 MALENGO YA MWAKA 2016/2017**

**31. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika kipindi cha mwaka 2016/2017, iliweka msukumo mkubwa katika kuimarisha uzalishaji na tija katika viwanda vilivyopo; kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya na kuhamasisha mauzo ndani na nje ya nchi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa Tanzania. Pia, kushirikiana na sekta binafsi katika uanzishaji na kuendeleza viwanda vya msingi na vya kimkakati kupitia taasisi zake za NDC na EPZA na kuendeleza na kuimarisha taasisi za utafiti na maendeleo ya viwanda. Vilevile, kuboresha mazingira ya kufanya biashara, uwekezaji na uzalishaji; na kuendeleza taaluma na weledi wa watumishi wake ili kutoa huduma bora zaidi kwa wadau.

Madhumuni ya hatua zote hizo ilikuwa ni kuchangia katika uboreshaji wa uchumi ili kujenga Taifa linalojitegemea na litakaloongozwa na uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

#### 4.1.1 Maduhuli ya Serikali

32. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi **20,000,000,000** kutokana na ada za leseni, uuzaji wa nyaraka za zabuni, faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni pamoja na makusanyo mengine. Hadi kufikia Aprili, 2017, jumla ya Shilingi **11,298,764,130.71** zilikuwa zimekusanywa ikilinganishwa na Shilingi **8,910,207,736.69** zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2015/2016, sawa na ongezeko la Shilingi **2,388,556,394.02**. Ongezeko hilo linatokana na matokeo chanya ya uboreshaji wa mazingira ya biashara.

#### 4.1.2 Matumizi

33. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilitengewa Shilingi **81,871,992,000** za matumizi. Kati yahizo, Shilingi **41,871,992,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **40,000,000,000** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, Shilingi **5,304,997,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **36,566,995,000** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, katika Shilingi **5,304,997,000** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi **4,652,877,000** zilikuwa kwa ajili ya Wizara na Shilingi **625,120,000** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara.

34. *Mheshimiwa Spika*, bajeti yote ya maendeleo ya Shilingi **40,000,000,000** ilikuwa ni ya fedha za ndani. Katika matumizi ya fedha za maendeleo, vipaumbele vilivyozingatiwa kwa fedha za ndani ni pamoja na kuendeleza Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga shilingi **10,000,000,000 (25%)**, Kuwezesha taasisi chini ya Wizara kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama ile inayosimamiwa na NDC- *Industrial Park*

(TAMCO, Kibaha) shilingi **9,000,000,000 (23%)**; Mashirika ya tafiti za viwanda ya TIRDO, TEMDO na CAMARTEC Shilingi **1,500,000,000 (4%)**; Kuchangia (*counter part funds*) katika utekelezaji wa miradi ya MUVI, *Gender Mainstreaming, Support for Trade Mainstreaming*, ASDP, UNIDO, WRRB, NEDF, BEST na KAIZEN Shilingi **11,300,000,000 (28%)**; *Lake Natron/Engaruka Soda Ash Project*, Kiwanda cha Matairi Arusha Shilingi **1,850,000,000 (5%)**; na kuendeleza biashara katika maeneo ya CBE, COSOTA, TANTRADE na SIDO Shilingi **6,350,000,000 (16%)**.

#### **4.1.3 Fedha Zilizopokelewa kutoka Hazina**

**35. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 39,393,067,796.49 sawa na asilimia 48 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka 2016/2017. Kati ya fedha hizo, Shilingi 31,630,307,171.49 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 7,762,760,625.00 ni za Matumizi ya Maendeleo (fedha za ndani). Aidha, kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 31,630,307,171.49 zilizopokelewa kutoka Hazina, Shilingi 26,429,483,302.00 ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na Shilingi 5,200,823,869.49 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Kwa upande wa fedha za maendeleo, Shilingi 7,566,620,625.00 sawa na asilimia 18.92 ya fedha za ndani na Shilingi 196,140,000 ni fedha za nje zilizopokelewa kutoka Hazina. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa kutoka Hazina ni kama ilivyoainishwa katika *Jedwali Na.4*.

## **4.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO**

### **4.2.1 Sekta ya Viwanda**

#### **a) Kuhamasisha Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

##### **(i) Ushirikiano wa Wizara na OR-TAMISEMI**

**36. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendesha kampeni za kuhamasisha

Watanzania na taasisi mbalimbali kuchangamkia ujenzi wa uchumi wa viwanda. Zoezi hilo limehusisha kutenga maeneo ya kujenga viwanda na kufanyia biashara, kuwahimiza na kuelimisha wananchi juu ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, kuvutia wawekezaji na kuboresha mazingira ya uwekezaji.

**(ii) Ushiriki wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

**37. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza kasi ya uwekezaji wa ndani, Shirikisho la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*Tanzania Social Security Association - TSSA*) pamoja na Mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF, PPF, LAPF, GEPF, PSPF na NHIF imehamasika kuwekeza katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo hadi Aprili, 2017 miradi 25 ya kuwekeza imebainishwa. Baadhi ya miradi hiyo ni mradi utakaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya mifuko ya PPF na NSSF ya kuendeleza eneo la Mkulazi kwa ajili ya kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari; PPF imeingia mkataba na Gereza la Karanga kwa ajili ya kutengeneza viatu; LAPF inafanya majadiliano ili kuwekeza kwenye Kiwanda cha Chai Mponde; GEPF imesaini makubaliano ya kuwekeza katika Kiwanda cha Mvinyo Dodoma pamoja na kuwekeza katika ujenzi wa kinu cha kuyeyusha chuma katika Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools Corporation* (KMTC), Moshi. Vilevile, TSSA imeanza majadiliano na Kiwanda cha Urafiki kwa ajili ya kuzalisha mavazi. (*Jedwali Na.5*)

**(iii) Ushirikiano na Sekta Binafsi**

**38. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda nchini. Kupitia Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI), Wizara ilishiriki katika utoaji wa Tuzo za Mzalishaji Bora wa mwaka (*11th Presidential Manufacturers of the Year Awards*) ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Wizara iliandaa kampeni ya kuhamasisha ununuzi wa bidhaa za ndani ijulikanayo kama *Top 50 Tanzania Brands*. Mpango huo ulibuniwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja



na TPSF ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa nchini zinafikia viwango vya kitaifa na vile vya kimataifa na hivyo kuongeza ushindani kwenye soko.

**39. Mheshimiwa Spika**, baadhi ya washindi wa tuzo hizo ni *Kilimanjaro Lager, Konyagi, Superdoll, Twiga Cement, Azam Embe, Azania Wheat Flower, Sundrop Cooking Oil, Whitedent* na *Grand Malt*. Baadhi ya washindi kwenye kundi la wajasiriamali wadogo na wa kati ni *Alaska Rice, Asali ya Bibi, Chocolate Mama, Nelwa's Delight Ice Cream* na *Nuya's Essence*. Aidha, Mkurugenzi wa *Nuya's essence*, Bi. Hellen Dausen alitambuliwa na jarida maarufu la *Africa's Most Promising Entrepreneurs* (Forbes Africa's Under 30 for 2016). Washindi wa tuzo hizo mbili za CTI na TPSF wameoneshwa kwenye **Jedwali Na.6a** na **6b**.

#### **(iv) Kutenga Maeneo ya Viwanda katika Mikoa**

**40. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia mikoa na wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Lengo la mpango huo ni kuwa na maeneo ya kutosha kujenga viwanda sasa na baadae. Hadi Aprili, 2017 mikoa 13 imetoa taarifa ya utengaji wa maeneo hayo na kuwasilisha taarifa zao ambapo mkoa wa Kigoma umetenga ekari 451.46; Kilimanjaro ekari 53,033.16; Simiyu ekari 807.06; Shinyanga ekari 33,637.63; Tanga ekari 33,788.62; Mbeya ekari 6,618.83; Pwani ekari 63,065.2; Dodoma ekari 54,614.16; Singida ekari 15,442; Mwanza ekari 11,204.3; Njombe ekari 15,662.29; Lindi ekari 8,790.52; na Geita ekari 472 na viwanja 144.

**41. Mheshimiwa Spika**, pamoja na maeneo ya uwekezaji yaliyotengwa na Serikali chini ya mpango wa SEZ katika maeneo ya Kigoma (KISEZ) hekta 3,000; Bunda (Bunda SEZ) hekta 1,360; Ruvuma-SEZ hekta 2,033; Manyoni-SEZ hekta 1,909, kwa mwaka 2016/2017, eneo lenye ukubwa wa hekta 63,000 lililopo Mkulazi- Morogoro limekabidhiwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PPF kwa ajili ya kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari chini ya *Mkulazi Holdings Co. Ltd*

iliyoundwa kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza mradi huo. Upatikanaji wa maeneo hayo unatoa nafasi kwa Serikali na sekta binafsi kuyaendeleza kwa kuyawekea miundombinu ya msingi ili kuvutia wawekezaji na kuongeza idadi ya viwanda nchini. Serikali itaendelea kukamilisha malipo ya fidia kwa maeneo yaliyobaki na kuyawekea miundombinu wezeshi.

## **b)       Sensa ya Viwanda**

**42.       Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na UNIDO, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilikamilisha Ripoti ya Sensa ya Viwanda ya mwaka 2013 na kuzinduliwa rasmi mwezi Oktoba 2016. Ripoti hiyo inaonesha kuwa, Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda 49,243 (**Jedwali Na. 7a**), ambapo asilimia 85.13 ni viwanda vidogo sana, asilimia 14.02 ni viwanda vidogo, asilimia 0.35 ni viwanda vya kati na asilimia 0.5 ni viwanda vikubwa. Takwimu hizo zinadhihirisha kuwa, asilimia 99.15 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo sana na viwanda vidogo. Aidha, juhudi za Serikali za kuhamasisha uwekezaji katika kukuza uchumi kupitia viwanda umewezesha kuongeza uwekezaji katika viwanda.

## **c)       Miradi ya Viwanda**

**43.       Mheshimiwa Spika**, tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani hadi kufikia mwezi Machi, 2017, miradi ya viwanda vikubwa 393 yenye jumla ya mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 2,362.59 (Shilingi trilioni 5.198) inayotarajiwa kutoa ajira 38,862 imesajiliwa. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na mingine katika hatua za mwisho za kuanza uzalishaji. Kati ya miradi hiyo, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesajili miradi 224 (**Jedwali Na. 7b**); Mamlaka ya EPZ imesajili miradi 41 (**Jedwali Na. 7c**) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imesajili miradi 128 (**Jedwali Na. 7d**). Aidha, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) limeratibu uanzishwaji wa viwanda vidogo 1,843.

**d) Viwanda Vilivyoanzishwa**

**44. Mheshimiwa Spika**, kwa muhtasari naomba niwapitishe katika baadhi ya viwanda ambavyo vimeanzishwa kwa kipindi cha mwaka 2016/2017.

**(i) Viwanda vya Kuzalisha Chuma na Bidhaa za Chuma**

**45. Mheshimiwa Spika**, kwa sasa Tanzania kuna jumla ya viwanda 22 vya chuma na bidhaa za chuma. Viwanda hivyo vimeendelea kuongeza uzalishaji mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2015, viwanda hivyo vilizalisha tani 62,612 na mwaka 2016 tani 65,686 (**Jedwali Na.3a**). Uwekezaji katika uzalishaji wa chuma na bidhaa za chuma umeendelea kuongezeka ambapo viwanda vitatu tayari vimefanya uwekezaji katika Mkoa wa Pwani. Kiwanda cha *Kiluwa Steel* kilichopo Mlandizi mkoani Pwani kimewekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 41 sawa na Shilingi bilioni 90.2 na kina uwezo wa kuzalisha tani 500,000 kwa mwaka na kutoa ajira 800. Kiwanda hicho kimeanza uzalishaji. Kiwanda cha *Lodhia Steel Industry* kilichopo Mkuranga kimewekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 9.35 sawa na Shilingi bilioni 20.57 na kinatarajia kutoa ajira 300. Aidha, kiwanda cha tatu ni *Lake Steel and Allied Products Ltd* kinachojengwa Kibaha, Pwani. Kiwanda hicho kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 13 sawa na Shilingi bilioni 28.6 na kitazalisha tani 168,000 za chuma kwa mwaka na kitaajiri wafanyakazi 120. Ujenzi wake upo katika hatua ya msingi.

**(ii) Viwanda vya Saruji**

**46. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu kwa sasa ina viwanda 11 vya kuzalisha saruji vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani milioni 10.8 kwa mwaka ilihali mahitaji ya soko la ndani ni tani milioni 4.8. Kiasi cha juu cha uzalishaji kilichowahi kufikiwa na viwanda vyetu ni tani milioni 7.1 kwa mwaka. Ongezeko la uwezo wa uzalishaji na kiasi kilichozalishwa kwa mwaka 2016/2017 limechangiwa kwa kiasi kikubwa na kukamilika kwa ujenzi wa Kiwanda cha *Dangote* chenye uwezo wa kuzalisha tani milioni 3 kwa mwaka kilichowekeza

Dola za Kimarekani milioni 568.1 sawa na Shilingi trilioni 1.25 na kutoa ajira 1,150; upanuzi wa *Tanga Cement Co. Ltd* kwa tani 500,000 kutoka tani tani 750,000 hadi tani 1,250,000 kwa mwaka uliogharimu Dola za Kimarekani milioni 152 sawa na Shilingi bilioni 334.4 na upanuzi wa *Mbeya Cement Co. Ltd* kwa tani 710,000 kutoka tani 400,000 hadi tani 1,100,000 uliogharimu Euro milioni 50 sawa na Shilingi bilioni milioni 154. Ongezeko hilo la uzalishaji limeongeza ajira 1,185 za moja kwa moja na 3,167 zisizo za moja kwa moja. Aidha, Sekta ya Saruji kwa kiasi kikubwa imechangamsha sekta nyingine za uchumi ikiwa ni pamoja na ujenzi, usafirishaji, uchimbaji wa madini na nishati kwa kutaja baadhi.

**47. Mheshimiwa Spika**, juhudi zimefanyika na kuweza kupata wawekezaji zaidi katika Sekta ya Saruji. Kampuni ya *Motisun* itawekeza kiwanda cha saruji Chapa Mamba chenye uwezo wa kuzalisha tani milioni moja kwa mwaka na kitajengwa mkoani Pwani. Kampuni ya *Hengya Cement Co. Ltd* imekamilisha taratibu zote za uwekezaji katika uzalishaji wa saruji mkoani Tanga. Kiwanda hicho ambacho kitazalisha saruji kwa kulenga soko la ndani na kimataifa uwekezaji wake ni Dola za Kimarekani bilioni 2.35 sawa na Shilingi trilioni 5.17 na utafanyika kwa awamu mbili hadi kufikia uwezo wa kuzalisha jumla ya tani milioni 7 za saruji kwa mwaka. Mradi huo mkubwa utakapokamilika unategemewa kutoa ajira za moja kwa moja 8,000 (**Jedwali Na.8**). Mafanikio katika uwekezaji wa Sekta ya Saruji ndio umesababisha kushuka kwa bei ya saruji nchini.

**(iii) Viwanda vya Vigae(tiles)**

**48. Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi, nchi yetu haikuwa na viwanda vya vigae. Kutokuwepo kwa viwanda hivyo kulisababisha nchi kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, mwaka 2015 nchi ilitumia Dola za Kimarekani milioni 90.61. Juhudi za kuhamasisha uwekezaji nchini zimezaa matunda na kuwezesha viwanda viwili vikubwa vya kuzalisha bidhaa hizo kuanzishwa. Viwanda hivyo ni Kiwanda cha Vigae cha *Goodwill Ceramic Ltd* kilichopo Kijiji cha Mkiu Wilaya ya

Mkuranga Mkoa wa Pwani. Uwekezaji katika kiwanda hicho umegharimu Dola za Kimarekani milioni 50 sawa na Shilingi bilioni 110. Kiwanda hicho kilichowekwa jiwe la msingi na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania tarehe 2 Machi, 2017 kimeanza uzalishaji. Kiwanda hicho kitazalisha vigae mita za mraba milioni 20 kwa mwaka na kitatoa ajira 4,500.

**49.** *Mheshimiwa Spika* kiwanda cha pili ni *Twyford* kilichopo Chalinze kilichowekwa jiwe la msingi na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji tarehe 22 Januari, 2017, kinategemewa kukamilika na kuanza uzalishaji mwezi, Agosti 2017. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha vigae mita za mraba milioni 12.5 kwa mwaka na kutoa ajira 6,000 kati ya hizo 2,000 za moja kwa moja na 4,000 zisizo za moja kwa moja. Viwanda vyote viwili vinategemea malighafi za ndani kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 95. Sekta zitakazofaidika ni pamoja na madini ujenzi, usafirishaji, makaa ya mawe na gesi asilia.

**(iv) Viwanda vya Nguo na Mavazi**

**50.** *Mheshimiwa Spika*, katika kuendeleza Sekta ya Nguo nchini, Wizara kupitia Mradi wa *Supporting Indian Trade and Investment for Africa (SITA)* iliandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Nguo na Mavazi (*Cotton to Clothing Strategy-C2C*), 2016-2020, uliozinduliwa Mei 2016. Mkakati huo unatoa mwongozo wa kuendeleza mnyororo wa uongezaji thamani kuanzia pamba hadi mavazi kwa kubainisha hatua za kuchukuliwa kutatua changamoto zinazokwamisha uwekezaji na uendelezaji viwanda. Wizara imekuwa ikikutana na wazalishaji na kujadiliana jinsi ya kutatua kero zinazowakabili. Mawasiliano yamefanyika na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kushughulikia kero ya *under invoicing and under-declaration* hususan kwa bidhaa kutoka nje; Shirika la Viwango Tanzania limeelekezwa kudhibiti bidhaa zisizo na ubora zisiingie sokoni na Tume ya Ushindani Tanzania imeelekezwa kudhibiti bidhaa bandia.

**51.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia NDC imefanya

majadiliano na *Gatsby Africa* kwa kushirikisha Kitengo cha Nguo na Mavazi (Textile Development Unit -TDU) ili kuandaa Mpango Kabambe (*Master Plan*) kwenye eneo la ekari 95 maalum kwa viwanda vya nguo TAMCO Kibaha. Wizara imefanya majadiliano na kuzishawishi taasisi za Serikali hususan majeshi na hospitali ili wanunue nguo na mavazi yanayozalishwa na viwanda vya ndani. Aidha, mafunzo ya useketaji nguo (weaving) kwa kutumia mashine za mikono (*Handlooms*) yalitolewa kwa waseketaji 89 katika Chuo cha VETA Tabora. Wahitimu hao wameweza kujajiri na wanaendesha shughuli zao katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Morogoro. Pamoja na kufanya shughuli zao, wahitimu hao wanatoa mafunzo kwa waseketaji wengine.

**52. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wataalam chini ya Mradi wa SITA ilitoa mafunzo kwa wazalishaji (artisans) 30 kuhusu usanifu wa mavazi, mbinu za useketaji bora kwa kutumia mashine za mikono na uwekaji rangi (tie & dye). Pia, taasisi za VETA na Kampuni za: *Shime Sanaa Machinga Complex Tie & Dye* na *Hand Made in Tanzania* kila moja ilitoa mwakilishi mmoja ambao waliwezesha kupata mafunzo ya utumiaji rangi za asili (natural die) huko Hyderabad, India. Vilevile, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia msaada wa *Gatsby Africa*, kimeendelea kutoa mafunzo ya Shahada ya Teknolojia ya Nguo (*Textile Degree*) ambapo, mwaka 2016/2017 Chuo kilitoa wahitimu 44 ikilinganishwa na wahitimu 13 kwa mwaka 2015/2016. Lengo ni kuhakikisha kuwa kuna wataalam wa kutosha wa fani ya ubunifu na uzalishaji mavazi nchini.

**(v) Viwanda vya Ngozi na Bidhaa za Ngozi**

**53. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Ngozi ni mojawapo ya sekta zenye mnyororo mrefu wa uongezaji thamani na hivyokuwa na uwezo wa kutoa ajira nyingi. Kwa mwaka 2016/2017, Wizara imefanya kazi kwa karibu na wadau wa Sekta ya Ngozi kwa lengo la kuongeza thamani ngozi ya hapa nchini. Mawasiliano yenye matumaini yamefanyika na wawekezaji wa viwanda vya Mwanza na *Morogoro Tanneries*

ili kuongeza uwezo wa kusindika ngozi kutoka hatua ya mwanzo hadi ya mwisho (wetblue, crust to finished). Kiwanda cha Viatu cha Bora kimesimika mtambo wenye uwezo wa kuzalisha jozi za viatu vya ngozi 25,000 kwa mwaka maalum kwa ajili ya matumizi ya usalama na viwandani. Pia, kiwanda hicho kimekamilisha kufunga mitambo mitatu yenye uwezo wa kuzalisha viatu jozi 500,000 kwa kutumia teknolojia ya PVC; viatu aina ya raba jozi 500,000 kwa ajili ya michezo na hospitali na viatu vya *Canvas* jozi 500,000 kwa mwaka.

**54. Mheshimiwa Spika**, kiwanda cha kutengeneza viatu vya ngozi kinachomilikiwa na Jeshi la Magereza kilichopo Karanga Moshi kinaendesha mradi kabambe wa kuongeza uwezo wa uzalishaji. Lengo ni kutumia kiwanda hicho kuzalisha ikiwa ni pamoja na bidhaa nyingine kama soli za viatu kwa ajili ya viwanda vingine. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PPF upo tayari kuwekeza Shilingi bilioni 56.64 katika mradi huo hali itakayoongeza ajira za moja kwa moja 707. Kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), mafunzo maalum ya kuchuna na kusindika ngozi yamekuwa yakiendeshwa sehemu mbalimbali za nchi. Kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi na Ajira), Chuo cha Teknolojia ya Ngozi cha Mwanza (DIT Kampasi ya Mwanza) kilitoa Mafunzo ya Stadi za Kutengeneza Viatu vya Ngozi yanayohusisha usanifu, ukataji ngozi na utengenezaji viatu vya ngozi kwa vijana 100 kutoka mikoa 11 ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kagera, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza na Tanga na mafunzo ya kutengeneza mipira ya miguu kwa vijana 25 kutoka mikoa sita ya Kagera, Mara, Morogoro, Mwanza, Pwani na Shinyanga. Aidha, mkufunzi mmoja kutoka Chuo hicho amepata mafunzo huko Uturuki ya *Eco-friendly leather production technologies, waste management in leather production* chini ya ufadhili wa UNIDO. Pia, kwa mwaka 2016/2017, sekta binafsi imejasiria uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati vya bidhaa za ngozi.

#### **(vi) Viwanda vya Kusindika Nyama**

**55. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Usindikaji wa Nyama ni

sekta muhimu katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Juhudi zimefanyika katika kuhamasisha uwekezaji katika sekta hiyo ambapo eneo la ekari 6,000 limepatikana kwa ajili ya kuanzisha Kiwanda cha Nyama cha *Nguru Hills Ranch* eneo la Makunganya Wilaya ya Mvomero Mkoa wa Morogoro. Kiwanda kimeanzishwa kwa ubia kati ya Kampuni ya *Zubair Corporation* ya Muscat, Oman na *Busara LLC*. Mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 13.741 sawa na Shilingi bilioni 30.23 zimekwishawekezwa. Kampuni ipo katika mazungumzo na wadau wengine ili kupata Shilingi bilioni 3.892 za kukamilisha mradi huo. Kiwanda hicho ambacho kimesajiliwa na Mamlaka ya EPZ kitasindika nyama ya ng'ombe na mbuzi kwa ajili ya soko la nje na kitakuwa na uwezo wa kusindika ng'ombe 50,000 na mbuzi 60,000 kwa mwaka, kutoa ajira za moja kwa moja 350 na kutoa fursa ya ajira zisizo za moja kwa moja ikiwemo kilimo cha nafaka na majani maalum kwa ajili ya kulishia mifugo.

**56. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Nyama cha *Meat King Limited* kilichopo eneo la Moshono, Mkoa wa Arusha kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 2.5 sawa na Shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya kuongeza uwezo wa uzalishaji wa kiwanda hicho kinachosindika nyama ya ng'ombe, kuku na kondoo. Kiwanda hicho kinatoa ajira 45 za moja kwa moja na 500 zisizo za moja kwa moja. Kiwanda kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kusindika kilo 900,000 za nyama kwa mwaka na kinalenga kuuza bidhaa zake katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Aidha, kufuatia kufungwa kwa kiwanda cha Nyama cha Manyara, Wizara inawasiliana na wadau ili kuona uwezekano wa kurudisha katika uzalishaji kiwanda hicho ili kuweza kusaidia kununua mifugo ya wananchi.

#### **(vii) Viwanda vya Chakula, Mbogamboga na Matunda**

**57. Mheshimiwa Spika,** tatizo la kuharibika kwa matunda yanayolimwa nchini limeanza kupatiwa ufumbuzi baada ya wawekezaji watatu kupatikana na kuanza ujenzi wa viwanda katika maeneo ya Mboga - Chalinze na Mapinga-Bagamoyo Mkoa wa Pwani. Kiwanda cha *Sayona Fruits Limited* kinachojengwa eneo la Mboga- Chalinze



kitasindika matunda mbalimbali ikiwa ni pamoja na nyanya. Mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 55.17 sawa na Shilingi bilioni 121.374 umewekezwa na kinatarajia kuzalisha lita milioni 91.65 za juisi kwa mwaka. Kiwanda hicho kinatarajiwa kutoa ajira za moja kwa moja 825 na zisizo za moja kwa moja 30,000. Aidha, Kiwanda cha Bakhresa Food Product Ltd kinachosindika matunda katika eneo la Mkuranga - Pwani, kilifanya upanuzi na kuzinduliwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 6 Oktoba, 2016. Upanuzi huo uliongeza uwezo wa usindikaji matunda tani 37,500 hadi tani 75,000 kwa mwaka. Upanuzi huo uligharimu mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 7.0 sawa na Shilingi bilioni 15.4 na kuongeza ajira za moja kwa moja 150 kutoka 150 hadi 300.

**58. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha *Elven Agri Company Limited* kinachotumia teknolojia ya kukausha matunda na mahsusi kikilenga matunda yaliyozalishwa kwa kutumia kilimo hai (organic fruits) kitakuwa na uwezo wa kukausha matunda tani 2,500 na kusindika tani 1,000 za nyanya kwa mwaka. Kiwanda kitatoa ajira za moja kwa moja 300 bila kuhusisha ajira kwa wakulima watakaozalisha matunda kwa kiwanda hicho. Bidhaa zitakazozalishwa na kiwanda hicho zitauzwa katika masoko ya nje. Kiwanda cha *Vegeta Padravka Limited* kilichopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani kimewekeza katika ukaushaji wa mbogamboga kwa ajili ya kutengeneza vionjo vya chakula (*food seasoning*). Uzinduzi wa kiwanda hicho ulifanyika mwezi Machi, 2017 na kinatarajia kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 4.5 sawa na Shilingi bilioni 9.9 na kinatarajiwa kutoa ajira 63 za moja kwa moja. Aidha, kiwanda kitashirikisha wananchi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ili washiriki katika kilimo cha mbogamboga kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya malighafi kwa kiwanda.

**59. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha Kutengeneza Makaroni (pasta) cha aina yake kimeanzishwa hapa nchini katika eneo la Vingunguti, Dar es Salaam kwa ajili ya kuzalisha makaroni (pasta) kwa kutumia malighafi ya 'Semolina'. Dola za Kimarekani milioni 16 sawa na Shilingi bilioni 35.2

zimewekezwa. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 29,200 kwa mwaka. Kwa vile malighafi inayotumiwa na kiwanda hicho kwa sasa inatoka nje ya nchi, mwekezaji amewekeza Dola za Kimarekani milioni 2.5 sawa na Shilingi bilioni 5.5 katika mtambo wa kuongeza thamani (milling plant) wenye uwezo wa kusaga tani 50,000 za *Semolina* kwa mwaka. Kiwanda hicho kipo mbioni kukamilika.

**60. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya *Jambo Group Ltd* imeanzisha kiwanda cha *Jambo Food Products Company Ltd* katika Mkoa wa Shinyanga cha kuzalisha maji, juisi na soda. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha lita za ujazo milioni 1.95 kwa mwaka na kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 35 sawa na Shilingi bilioni 77. Ajira 500 za moja kwa moja na 1,500 zisizo za moja kwa moja zitatengenezwa. Kampuni inatarajia kuongeza uwekezaji wa Dola za Kimarekani milioni 40 sawa na Shilingi bilioni 88 ifikapo Desemba 2017 ili kuongeza uzalishaji zaidi.

#### **(viii) Viwanda vya Maziwa**

**61. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya *Watercom Ltd* imejenga Kiwanda cha Kusindika Maziwa eneo la Kigamboni, Mkoa wa Dar-es- Salaam ambacho kitatumia teknolojia ya *Ultra Heat Treatment* (UHT) ambayo huzalisha maziwa yenye ubora wa hali ya juu. Kiwanda hicho kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 20 sawa na Shilingi bilioni 44 na kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 67.5 za maziwa kwa mwaka na kutoa ajira 500. Kampuni hiyo pia imeanzisha Kiwanda cha *Watercom Ltd* kwa ajili ya kuzalisha maji ya kunywa aina ya Afya. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 125 za maji kwa mwaka, kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 25 sawa na Shilingi bilioni 55 na kinatoa ajira 1,270. Kampuni ya *Watercom Ltd* pia iko mbioni kuanzisha kiwanda cha kutengeneza juisi na vinywaji baridi kitakachowekeza Dola za Kimarekani milioni 40 sawa na Shilingi bilioni 88 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 275 za vinywaji kwa mwaka na kutoa ajira 3,500.

**(ix) Viwanda vya Mafuta ya Kula**

**62.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania ina fursa ya kuzalisha mafuta ya kula kwa ajili ya matumizi ya ndani na ziada kuuzwa nje ya nchi. Uzalishaji wa mafuta ya kula kwa sasa ni tani 180,000 wakati mahitaji yanakadiriwa kuwa tani 400,000 kwa mwaka. Hivyo, asilimia 55 ya mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni mafuta ya mawese (*palm oil*) yanayoagizwa kutoka nje ya nchi. Inakadiriwa kuwa mafuta ya alizeti yanayozalishwa yanatosheleza mahitaji ya ndani kwa asilimia 40 tu. Changamoto kubwa katika uzalishaji wa mafuta ya alizeti nchini inatokana na upungufu wa mbegu zenye ubora stahiki wa kutoa mafuta kwa wingi. Kutokana na hali hiyo, Serikali kwa kushirikisha wadau katika Sekta ya Mafuta ya Kula iliandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ndogo ya Alizeti uliozinduliwa mwezi Mei, 2016.

**63.** *Mheshimiwa Spika*, tangu kuzinduliwa kwa Mkakati wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Alizeti, yafuatayo yamekwishafanyika:

a) Ekari 75 za ardhi kwa ajili ya kujenga Kongano la Mafuta ya Alizeti katika eneo la Chamwino, Dodoma limepatikana. Barabara ya urefu wa Kilometa moja kutoka barabara kuu ya Dar es Salaam - Dodoma hadi eneo la mradi na barabara za ndani zenye urefu wa jumla ya Kilometa tano zimejengwa kwa kiwango cha changarawe;

b) Kwa lengo la kupata malighafi ya uhakika katika kongano hilo, eneo la ekari 15,000 limebainishwa na kuunganishwa na wakulima 370;

c) Wazalishaji wa mafuta ya alizeti 31 wamepewa mafunzo ya viwango vya ubora unaokidhi matakwa ya soko la ndani, kikanda na kimataifa;

d) Kupitia Mradi wa SITA, mkutano kati ya wazalishaji wa mafuta ya alizeti wa Tanzania na India ulifanyika Dodoma tarehe 27 Julai, 2016 kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji na uhaulishaji wa teknolojia;

e) Kuanzishwa kwa Jukwaa la Wadau wa Alizeti (*Sunflower Round Table*) chini ya Mradi wa SITA na usimamizi wa Chama cha Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti Tanzania (Tanzania Sunflower Processors Association-TASUPA). Jukwaa hilo limezindua miradi miwili ya:

i) Kilimo cha kuzalisha aina nne (4) ya mbegu bora (certified seeds) za Alizeti;

ii) Kuendeleza Kongano za Wasindikaji Mafuta ya Alizeti zikiwepo za Dodoma, Singida na Kondo; na

f) TASUPA imeingia makubaliano na Benki ya Dunia ya kuendeleza miundombinu katika Kongano za Kusindika Alizeti zitakazojengwa.

#### **(x) Viwanda vya Sukari**

**64. *Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa sukari ya majumbani na ya viwandani kutokana na kuwa na mahitaji makubwa kuliko uwezo wa uzalishaji wa ndani. Utafiti uliofanywa na Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) kwa kutumia Kampuni ya *LMC International*, ulibaini mahitaji ya sukari kwa mwaka 2016/2017 ni wastani wa tani 590,000 ambapo kati ya hizo, tani 455,000 ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na tani 135,000 kwa matumizi ya viwandani. Malengo ya uzalishaji kwa msimu wa 2016/2017 yalikuwa tani 329,169 ambapo kufikia tarehe 19 Aprili, 2017 msimu wa uzalishaji ulipofungwa, jumla ya tani 330,843.48 zilikuwa zimezalishwa. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 100.51 ya malengo ya uzalishaji.

**65. *Mheshimiwa Spika***, katika kutatua changamoto ya uhaba wa sukari nchini, Serikali ilianisha maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya upandaji miwa katika mabonde mbalimbali nchini pamoja na kuvutia uwekezaji wa viwanda vipya na kuongeza uwezo wa uzalishaji wa viwanda vilivyopo. Kiwanda cha *Kagera Sugar Estate Ltd* kinapanua uwezo wa uzalishaji kufuatia makubaliano na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PSPF ya kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 20 sawa na

Shilingi bilioni 44. Upanuzi huo utaongeza ajira 1,000 kutoka 2,500 za sasa hadi 3,500. Aidha, hadi kufikia Aprili 2017, Kampuni ya *Mkulazi Holdings* ambayo ni ya ubia kati ya Mifuko ya Jamii ya NSSF na PPF itawekeza katika kilimo cha miwa na ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza sukari ya majumbani katika eneo la Mkulazi Morogoro. Kiwanda hicho kitazalisha tani 200,000 za sukari kwa mwaka na kutengeneza ajira zipatazo 100,000. Aidha, Jeshi la Magereza limeingia ubia na Mifuko ya Jamii ya NSSF na PPF ili kufufua na kuendeleza mashamba na Kiwanda cha Sukari Mbigiri Morogoro chenye uwezo wa kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka (*Jedwali Na.9*).

#### **(xi) Viwanda vya Vifungashio**

**66. Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mahitaji ya vifungashio kwa soko la ndani na nchi jirani viwanda vya kuzalisha vifungashio vimejengwa kwa mafanikio. Kiwanda cha *Lakairo Polybag* kilichojengwa Mwanza kwa gharama ya Shilingi bilioni 4 chenye uwezo wa kuzalisha magunia ya sandarusi (polypropylene bags) milioni 10 kwa mwaka na kinaajiri watu 85. Kiwanda cha *Global Packaging* kilichopo Kibaha kilichowekeza Shilingi bilioni 8 kina uwezo wa kuzalisha magunia ya sandarusi milioni 11.75 kwa mwaka na kinaajiri watu 110. Wizara inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika eneo hilo ili kukidhi mahitaji ya vifungashio kwa mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani.

#### **(xii) Viwanda vya Mbolea**

**67. Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya *Ferrostaal Consortium Ltd* kwa ushirikiano na TPDC itawekeza Dola za Kimarekani bilioni 1.982 sawa na Shilingi trilioni 4.360 kwa ajili ya kujenga kiwanda cha mbolea katika eneo la Kilwa Masoko, Lindi, chenye uwezo wa kuzalisha tani milioni 1.3 za mbolea kwa mwaka. Kampuni ya *Helm* itawekeza Dola za Kimarekani bilioni 1.2 sawa na Shilingi trilioni 2.640 ili kujenga kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha tani milioni 1.365 za mbolea kwa mwaka katika eneo la Msanga Mkuu, Mtwara Mikindani. Majadiliano ya kufanikisha uanzishwaji wa miradi

hiyo yanaendelea. Wizara imeshiriki katika kufanikisha miradi hiyo kwa kufuatilia ukamilishaji wa majadiliano hasa uamuzi juu ya bei ya gesi itakayotumika kutengenezea mbolea.

### **(xiii) Viwanda vya Dawa za Binadamu**

**68.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2016/2017, Serikali imefanya uhamasishaji mkubwa kuvutia uwekezaji kwenye Sekta ya Dawa za Binadamu. Lengo ni kuhakikisha viwanda vipya vinajengwa na kufufua vilivyofungwa ikizingatiwa kuwa takriban asilimia 90 ya dawa muhimu (Essential Drugs) zinazotumika nchini huagizwa kutoka nje. Juhudi za uhamasishaji wa uwekezaji katika sekta hii zimeendeshwa kwa ushirikiano mkubwa kati ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto chini ya usimamizi mahiri wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**69.** *Mheshimiwa Spika*, mradi wa kutengeneza vifaa tiba vitokanavyo na pamba (medical textile) utakaojengwa Mkoa wa Simiyu ulibuniwa na kamati maalum inayohusisha wataalamu kutoka taasisi za MSD, NHIF, TIRDO, TIB na TFDA. Mradi huo utakaojengwa na NHIF utakuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 36.5 sawa na Shilingi bilioni 80.3. Tani 50,000 za pamba zitatumika kwa mwaka na kutoa ajira 1,600 za moja kwa moja na 5,000 zisizo za moja kwa moja. Mradi wa *Zinga Pharmaceutical Ltd* unaoanzishwa na Watanzania katika eneo la Zinga, Bagamoyo utazalisha vidonge bilioni 1.0, capsules milioni 175, dawa za maji (syrups/suspensions) chupa milioni 15 na dawa ya kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI (ARVs) vidonge milioni 200 kwa uzalishaji wa masaa nane (single shift) kwa mwaka. Mradi utawekeza Shilingi bilioni 70 na kutoa ajira 210 za moja kwa moja. Aidha, mradi utaongeza uzalishaji hadi kufikia *shift* tatu baadae.

**70.** *Mheshimiwa Spika*, Miradi mingine ni pamoja na mradi wa kutengeneza sindano (syringes) milioni 80 kwa mwaka na kutoa ajira 150 za moja kwa moja unaotekelezwa na Kampuni ya *El-Dawlia Ltd* ya Misri katika Eneo la Viwanda

la TAMCO. Mradi wa *Pharmaceutical Park* utakaotengeneza *Intravenous (IV) Fluids* chupa 10,000 kwa mwaka utajengwa katika Eneo la Viwanda TAMCO kwa mtaji wa Shilingi milioni 102.732 na kutoa ajira 80. Pia, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PSPF kwa kushirikiana na mwekezaji, Kampuni ya *Pharmaceutical Investment Ltd* (PIL) wanakamilisha taratibu za kufufua Kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd* (TPI) cha kutengeneza dawa za binadamu na za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI. Miradi hiyo ikikamilika itapunguza kwa kiasi kikubwa uagizaji wa dawa kutoka nje.

#### **(xiv) Viwanda vya Sabuni**

**71.** *Mheshimiwa Spika*, Kiwanda cha *KEDS Tanzania Ltd* cha kuzalisha sabuni ya unga kinajengwa katika Eneo la Viwanda TAMCO, Kibaha. Kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka kitawekeza Dola za Kimarekani milioni 11.5 sawa na Shilingi bilioni 25.3. Aidha, kiwanda hicho kitakapokamilika kitatoa ajira za moja kwa moja 700 na 1,500 zisizo za moja kwa moja. Ujenzi wa kiwanda ulianza mwezi Februari, 2017 na uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2017.

#### **(xv) Viwanda vya Kutengeneza Sigara**

**72.** *Mheshimiwa Spika*, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa na kiwanda kimoja cha kutengeneza sigara cha *Tanzania Cigarette Co. Ltd (TCC)*. Kiwanda hicho kimekuwa kikitumia tumbaku inayozalishwa na kusindikwa nchini na nyingine imekuwa ikiuzwa nje ya nchi baada ya kusindikwa. Tumbaku inayouzwa nje huwa imeongezwa thamani kiasi kidogo na sehemu kubwa huongezwa thamani huko inakouzwa. Hivyo, uuzaji huo hufanya ajira ambazo zingekuwa za Watanzania kutengenezwa inakouzwa tumbaku hiyo. Kufuatia juhudi za kuvutia uwekezaji zinazofanyika nchini, Kiwanda cha *Philip Morris Tanzania Ltd* ambacho ni Kampuni Mshirika (affiliate company) ya Kampuni ya *Philip Morris International* (PMI) inajenga kiwanda cha kutengeneza sigara za aina mbalimbali katika eneo la Kingolwira, Morogoro. Kiwanda hicho kitawekeza Shilingi

bilioni 61.7 na kusindika tani 500 za tumbaku kwa mwaka kwa kuanzia na kutoa ajira za moja kwa moja 100 na zisizo za moja kwa moja 2,000. Uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Julai 2017 ambapo sigara zitakazozalishwa zitauzwa katika soko la ndani na nje.

#### **(xvi) Viwanda Vinginevyo**

**73. Mheshimiwa Spika**, mbali ya makundi ya viwanda yaliyotajwa hapo juu, kwa mwaka wa 2016/2017 tumepata mafanikio makubwa katika kuanzisha viwanda vidogo na viwanda vya kati. Viwanda vya kundi hili vimeanzishwa na wajasiriamali wanaosindika chakula, mafuta ya kula, viungo, asali na mvinyo. Kundi hilo linahusisha pia viwanda vya kusaga nafaka, useketaji wa nguo, ushonaji, useremala, uhomeaji vyuma, utengenezaji samani na utengenezaji wa mashine ndogondogo kwa kutaja baadhi. Faida ya viwanda hivyo ikilinganishwa na makundi ya viwanda vilivyotajwa hapo juu ni kuwa vimesambaa nchi nzima.

#### **e) Viwanda Vilivyobinafsishwa Visivyofanya kazi**

**74. Mheshimiwa Spika**, moja ya majukumu ya Wizara, ni kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi. Jukumu hilo tunalitekeleza kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Mikoa. Katika mwaka 2016/2017, ufuatiliaji ulifanyika ambapo jumla ya viwanda 30 vilifanyiwa ufuatiliaji na Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kati ya hivyo, viwanda 18 vinafanya kazi vizuri, vitatu (3) vinafanyakazi kwa kusuasua na tisa (9) vimefungwa. Ufuatiliaji huo unafanya jumla ya viwanda vilivyofuatiwa katika kipindi cha 2015/2016 na 2016/2017 kuwa 110. Baadhi ya viwanda vilivyofungwa wakati wa ufuatiliaji wa mwaka 2015/2016 vilitembelewa tena mwaka 2016/2017 ili kujua maendeleo ya viwanda hivyo na hatua zilizochukuliwa na wamiliki baada ya kupata maelekezo ya Serikali (*Jedwali Na. 10a*).

**75. Mheshimiwa Spika**, juhudi mbalimbali zimefanyika kushawishwamilikiwaviwandavilivyofungwailiwavifufue.Matokeo



ya juhudi hizo ni pamoja na majadiliano ya kukifufua Kiwanda cha *Morogoro Canvas Mills Ltd* (MCM) ambayo yamefikia hatua nzuri. Kiwanda cha MOPROCO kilichoko Morogoro kimekarabatiwa ikiwa ni pamoja na kufungwa mitambo yenye teknolojia mpya yenye uwezo wa kusindika mbegu za mafuta na pia kusindika mashudu baada ya kukamuliwa na wakamuaji wadogo. Uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2017. Kiwanda cha Korosho Nachingwea kililingia Makubaliano ya Awali (MoU) na Kampuni ya *Sunshine Industry* ya China mwezi Machi, 2017 ya kufufua Kiwanda hicho kwa utaratibu wa Kujenga, Kumiliki, Kuendesha na Kuhamisha (*Build, Own, Operate and Transfer-BOOT*). Usimikaji mitambo unaendelea na uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2017. Kampuni hiyo pia ilitumia utaratibu huo kufufua Kiwanda cha Korosho cha Mtama ambacho sasa kinafanya kazi vizuri. Kwa viwanda vilivyofanyiwa ufuatiliaji mwaka 2015/2016 na kubainika vimefungwa, uchambuzi wa kina wa Mikataba ya Mauzo ulifanyika chini ya usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuwezesha hatua stahiki kuchukuliwa. Msajili wa Hazina alikwishatoa kusudio la kutwaa viwanda vinane (8) kutokana na wamiliki wa viwanda hivyo kubainika wamevunja Mikataba ya Mauzo. Kufuatia kusudio hilo, Kiwanda cha Chai cha Mponde kilitwaliwa tarehe 26 Januari 2016 na juhudi za kumpata mwekezaji wa kukifufua na kukiendeleza zinaendelea. Pia, Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga kilichobinafsishwa kwa Kampuni ya *Triple S*, ikashindwa kukifufua, kilitwaliwa tarehe 15 Machi, 2017. Juhudi za kumpata mwekezaji wa kukifufua zinaendelea.

**76. Mheshimiwa Spika,** utwaaji na uendelezaji wa viwanda vilivyobinafsishwa unakabiliwa na changamoto kutokana na madeni makubwa ya mabenki kufuatia mikopo inayochukuliwa na mwekezaji pindi anapokabidhiwa kiwanda. Uchukuaji wa mikopo huenda sambamba na Hati Miliki ya kiwanda kushikiliwa na benki iliyotoa mkopo na hivyo kuwa vigumu mwekezaji anayepatikana kukabidhiwa mali husika bila Hati Miliki. Pia, viwanda hivyo vinakabiliwa na migogoro inayozuia uendelezaji wa kiwanda baada ya kutwaliwa. Hizo ni baadhi ya changamoto zinazokabili

ufufuaji wa Kiwanda cha Chai Mponde. Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutatua changamoto husika ili kuwezesha Kiwanda cha Mponde kuanza uzalishaji.

**77.** *Mheshimiwa Spika*, kwa kupitia Msajili wa Hazina, TIRDO imefanya ukaguzi wa kitaalam (technical audit) wa viwanda vilivyobinafsishwa na kusimama uzalishaji, vikiwemo Kiwanda cha Chai Mponde na Kiwanda cha Ngozi Mwanza. Uainishaji huo umesaidia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kutoa maamuzi ya ufufuaji wa baadhi ya viwanda hivyo. Aidha, TIRDO imekwishatoa ushauri wa kitalaam kwa mifuko hiyo ya jamii katika uanzishwaji wa viwanda vya ngozi, dawa na usindikaji wa chakula.

#### **f) Mazingira na Viwanda**

**78.** *Mheshimiwa Spika*, Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (*Sustainable Industrial Development Policy-SIDP*), 1996-2020 inatilia mkazo juu ya uzalishaji wenye tija unaozingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Tathmini ya utekelezaji wa Sera hiyo sambamba na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (*Environmental Management Act-EMA Act*) 2004 na Kanuni zake, unafanywa kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais; Mazingira, Baraza la Taifa la Mazingira (*NEMC*) na Mamlaka ya Usalama Mahali pa Kazi (*OSHA*). Tathmini hiyo inahusisha athari za miradi (*Environmental Impact Assessment- EIA*) na uzalishaji viwandani (*Environmental Audit-EA*) kwa mazingira. Tathmini ya EIA hufanyika kabla ya mradi kuanza ujenzi ili kuhakikisha kuwa miradi ya uzalishaji inaanzishwa kwa misingi ya Sera na Sheria husika na viwanda kubainisha kama vinazalisha kwa kuzingatia matakwa ya uhifadhi na utunzaji mazingira kwa mujibu wa Sera na Sheria hizo. Kwa mwaka 2016/2017; jumla ya miradi 120 ilijisajili kufanya EIA ambapo 38 ilipata Vyeti vya EIA. Aidha, viwanda 59 vilijisajili kufanya EA na 30 vilifanikiwa kupata Vyeti vya EA.

#### **g) Kujenga Kongano za Viwanda (Industrial Clusters)**

**79.** *Mheshimiwa Spika*, uzalishaji katika makongano

husaidia sana wazalishaji wadogo kushirikiana huduma na vifaa ambavyo hawana uwezo wa kuvinunua ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kuboresha uzalishaji, upatikanaji wa malighafi, masoko na ushauri. Hadi kufikia mwezi Aprili 2017, juhudi mbalimbali zilifanyika za kuanzisha makongano ya uzalishaji yafuatayo:

(i) Kongano la Mafuta ya Alizeti katika eneo la Chamwino Dodoma;

(ii) Kongano la Useketaji Nguo kwa kutumia mashine za mikono (handlooms) Tabora, Arusha na Dar es Salaam; na

(iii) Kongano la Ngozi na Bidhaa za Ngozi katika eneo la Viwanda la Zuzu Magharibi, Dodoma. Kongano hizo zitawezesha wazalishaji wadogo kuongeza uwezo wa uzalishaji, ubora wa bidhaa zitakazozalishwa na ufanisi katika uzalishaji.

## **h) Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda SADC**

**80.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilishiriki kikamilifu katika kuandaa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda kwa Nchi za SADC, 2015- 2030. Mpango Kazi wa kutekeleza Mkakati huo ulipitishwa na Wakuu wa Nchi za SADC tarehe 18 Machi, 2017 huko nchini Swaziland. Sekta za kipaumbele ni usindikaji wa mazao ya kilimo, uchenjuaji madini (mineral beneficiation) na dawa za binadamu. Katika kutekeleza Mpango Kazi husika, wafadhili mbalimbali wamejitokeza kusaidia nchi wanachama wa SADC kushiriki kikamilifu katika mnyororo wa kikanda wa uongezaji thamani (*regional value chain*) ili kufikia uchumi wa viwanda na kuongeza kasi ya maendeleo ya wananchi wake. Hivyo, Wizara imepokea ufadhili kutoka Jumuiya ya Ulaya (EU) kupitia Programu ya EDF11 kurejea Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (SIDP), 1996-2020. Maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kurejea SIDP yameanza. Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya SADC inaandaa miradi katika Sekta ya Dawa za Binadamu na usindikaji mazao ya kilimo kwa ajili ya kupata ufadhili wa

kuitekeleza. Miradi hiyo ikikamilika itawasilishwa Sekretariati ya SADC ili kuwasilishwa kwa wafadhili.

**i) Matumizi ya Makaa ya Mawe Viwandani**

**81.** *Mheshimiwa Spika*, nishati ni nyenzo muhimu kwa uzalishaji viwandani na ina mchango mkubwa katika kupunguza gharama za uzalishaji inapokatikana kwa uhakika na kwa bei nafuu. Makaa ya mawe ni moja ya vyanzo vya kutoa nishati kwa viwanda na kwa gharama nafuu ikilinganishwa na vyanzo vingine. Nchi yetu kwa sasa ina machimbo manne ya makaa ya mawe ambayo ni *TANCOAL Energy Limited* iliyoko Ngaka, Mbinga Mashariki; *Magamba Coal Mine* iliyoko Rukwa; *Kabulo Ridge* iliyoko Kiwiri na *Katewaka Coal Ltd* iliyoko Maganga Matitu, Njombe. Machimbo hayo yanakadiriwa kuwa na uwezo wa kutoa makaa ya mawe tani 2,254,080 kwa mwaka. Uzalishaji wa makaa ya mawe unategemea kwa kiasi kikubwa mahitaji yaliyo tayari kwa matumizi ya viwanda ili kuepusha ukusanyaji mkubwa unaoweza kuleta athari za mlipuko wa moto kutokana na makaa yenyewe. Kutokana na bei ndogo na ubora wa makaa ya mawe yanayozalishwa nchini, zaidi ya viwanda 15 vimeanza kutumia makaa ya mawe kama chanzo cha nishati na hivyo kuachana na matumizi ya mafuta mazito pamoja na kuni katika kuendesha mitambo yao ya uzalishaji. Matumizi hayo ya kuni yamekuwa kwa kiasi kikubwa yakichangia katika uharibifu wa mazingira nchini. Matumizi ya makaa ya mawe kwa viwanda hivyo yanakadiriwa kuwa tani 1,048,056 kwa mwaka sawa na tani 75,338 kwa mwezi. Aidha, makaa hayo yanauzwa nje ya nchi katika nchi za Kenya, Uganda na Rwanda (*Jedwali Na 10b* na *10c*).

**j) KAIZEN**

**82.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) imekuwa ikitekeleza Mradi wa *Strengthening Manufacturing Enterprises through Quality and Productivity Improvement (KAIZEN)*. Mradi huo unalenga kuongeza ubora wa bidhaa, tija na kupunguza

gharama za uzalishaji bila gharama kubwa kwa kiwanda. Awamu ya Kwanza ya Mradi ilijielekeza katika kutoa mafunzo ya uelewa wa dhana ya KAIZEN kwa Watanzania na mafunzo ya kutekeleza dhana ya KAIZEN kwa viwanda katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro. Katika awamu hiyo ambayo ilimaliza muda wake mwezi Juni 2016, Watanzania 2,100 walihamasishwa na kupata uelewa wa dhana ya KAIZEN, viwanda 52 vya mfano vilifundishwa na kuanza kutekeleza dhana ya KAIZEN, wakufunzi wa wakufunzi (Master Trainers) 13 walipata mafunzo ya kina ya KAIZEN hapa nchini na Japan ili kuwawezesha kutoa mafunzo kwa wakufunzi (Trainers) na viwandani na *Trainers* wanane walipatia mafunzo ya KAIZEN nchini. Ili kuhamasisha viwanda vingine kujiunga na dhana ya KAZIEN, mwezi Oktoba, 2016 viwanda vilivyoshinda katika kutekeleza dhana ya KAIZEN vilipewa zawadi pamoja na wakufunzi wa wakufunzi bora. Mkakati wa kutekeleza dhana KAIZEN, 2016-2020 uliandaliwa na kupitishwa. Aidha, maandalizi yanafanyika ya kuanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa KAIZEN mwezi Julai, 2017. Awamu hiyo itaongeza mikoa mitano zaidi ya kufundisha dhana ya KAIZEN viwandani na hivyo kuwa mikoa minane inayotekeleza dhana hiyo. Mikoa mipya ni Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza na Singida.

#### 4.2.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

##### a) Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

**83.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilipanga kuifanyia mapitio Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003 ambapo Wizara imekamilisha hatua ya kutathmini utekelezaji wa sera ambao ni msingi muhimu katika kufanya mapitio ya sera hiyo. Lengo la tathmini hiyo ilikuwa ni kutambua mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sera hiyo ili ziwe msingi wa mapitio. Jukumu hilo muhimu limefanikiwa kutokana na ushirikiano mzuri na Shirika la Kazi Duniani (ILO), *International Fund for Agriculture Development* (IFAD) na *Financial Sector Deepening Trust* (FSDT).

## **b) Kuhamasisha Halmashauri Kutenga Maeneo**

**84.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuhamasisha utengaji wa maeneo katika Halmashauri zote nchini. Wizara imefuatilia utekelezaji wa utengaji wa maeneo katika mikoa ya Lindi, Morogoro, Singida na Tanga. Katika mkoa wa Lindi Halmashauri zilizotenga maeneo ni za Manispaa ya Lindi, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Kilwa, Ruangwa, Liwale na Nachingwea. Mkoa wa Tanga umetenga maeneo katika Manispaa ya Tanga, Halmashauri za Wilaya za Handeni, Korogwe, Mkinga, Muheza na Kilindi. Katika Mkoa wa Singida, Halmashauri zilizotenga maeneo ni Manispaa ya Singida, Halmashauri za Wilaya za Iramba, Ikungi na Manyoni. Halmashauri zilizotenga maeneo katika Mkoa wa Morogoro ni Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Wilaya ya Ifakara. Mikoa mingine ambayo imetenga maeneo ni pamoja na Arusha, Dodoma, Geita, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Njombe na Shinyanga. Pamoja na maeneo tuliyotembelea na kufanya tathmini, mwikio wa zoezi hilo nchini ni mzuri.

**85.** *Mheshimiwa Spika*, kwa kutambua mahitaji ya wadau wetu (Serikali ngazi ya Mkoa na Wilaya) tumeandaa Mwongozo juu ya Ujenzi wa Viwanda. Kitabu hicho kinaeleza jinsi ya kuandaa taswira ya Mkoa, Wilaya, Kata mpaka Kijiji kwa kuonesha bayana fursa za kujenga viwanda. Pia, ufafanuzi umetolewa jinsi ya kutenga maeneo ya kujenga viwanda kwa kulenga viwanda vidogo sana, viwanda vidogo na vya kati. Kitabu hicho kinabainisha umuhimu na majukumu ya taasisi mbalimbali katika kutoa ushauri juu ya ujenzi wa viwanda ikiwemo na ujenzi wa miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi. Ni matumaini yetu kuwa kwa kutumia mwongozo huo mikoa na wilaya zote nchini zitakuwa na uelewa na mwamko sawa katika kujenga uchumi wa viwanda.

## **c) Utekelezaji wa Mradi wa MUVI**

**86.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kufuatilia

utekelezaji wa Mradi wa Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) kwa kila robo mwaka kwa kutembelea mikoa yote ambako mradi unatekelezwa. Mradi huo umetekelezwa kwa miaka tisa kuanzia mwezi Julai, 2007 hadi mwezi Machi, 2017. Lengo la mradi lilikuwa ni kusaidia katika jitihada za kupunguza umasikini kwa kuendeleza wajasiriamali vijijini kupitia minyororo ya thamani ya mazao yaliyochaguliwa. Mradi huo ulianzishwa na Wizara na kutekelezwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kupitia kwa wataalam waelekezi. MUVI ilitekelezwa katika Wilaya 19 za Mikoa 7 ya Iringa, Manyara, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma na Tanga.

**87. Mheshimiwa Spika**, tangu kuanzishwa mradi huo, huduma zimetolewa kwa familia 105,449 ambazo ni asilimia 92 ya lengo na umeweza kuzalisha ajira za moja kwa moja 13,757. Mradi umewezesha uanzishaji wa huduma mpya ambazo zimesaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji na zinaweza kuigwa na kuendelezwa hata baada ya mradi kukamilika. Huduma zilizoanzishwa ni pamoja na uendeshaji wa mashamba darasa ya mbegu; miradi ya uongezaji thamani mazao; miundombinu 23 ya masoko; huduma ya uuzaji kwa pamoja vikundi 618; uanzishaji wa vikundi 30 vya kuweka na kukopa (SACCOS); utaratibu wa upatikanaji wa taarifa za masoko; na mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima 53,503 na kilimo biashara kwa wakulima 48,203.

**88. Mheshimiwa Spika**, huduma zote hizo zimerahisisha shughuli za uzalishaji na kuongeza tija. Kwa mfano uanzishaji wa mashamba ya mbegu bora kwa mazao ya alizeti, maharage na ufuta vimesaidia kuongeza uhakika wa upatikanaji wa mbegu kwa asilimia 68. Mafunzo ya mbinu bora za kilimo pamoja na kilimo biashara vimehamasisha wakulima kuzingatia mambo ya msingi yanayofanya uzalishaji wao kuwa na tija. Asilimia 89 ya wazalishaji washiriki walikiri kuwa uzalishaji na tija vimeongezeka na asilimia 93, kuwa mbinu za kisasa za uzalishaji walizowezeshwa kupata zimewasaidia kuongeza ufanisi na tija.

**d) Mfuko wa NEDF**

**89.** *Mheshimiwa Spika*, Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF) ulianzishwa mwaka 1994 kwa Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Madhumuni ya Mfuko huo ni kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo Tanzania Bara kwa lengo la kuondoa umaskini kwa kuanzisha na kuendeleza miradi yao. Tathmini ya utekelezaji wa Mfuko iliyofanywa inaonesha kuwa bado mahitaji ya huduma kutoka kwenye mfuko ni makubwa kuliko uwezo uliopo. Mfuko tangu ulipoanzishwa mwaka 1994 hadi Machi 2017 umepokea jumla ya maombi 211,977 yenye kuhitaji mikopo ya thamani ya Shilingi 161,589,513,000, lakini umeweza kutoa mikopo kwa maombi 85,130 tu yenye thamani ya Shilingi 61,368,432,000 ambayo ni sawa na asilimia 40 tu ya mahitaji. Kwa kipindi cha miaka 23 ya uhai wake, Mfuko umewezesha kupatikana ajira mpya 172,083 nchini kote. Mikopo hiyo ilitokana na mtaji wa Shilingi 5,051,000,000 uliotolewa na Serikali.

**90.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017 jumla ya wajasiriamali 2,593 walipewa mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 3.92 na mikopo hiyo iliwezesha kupata ajira 9,424. Katika mikopo iliyotolewa, asilimia 48 ilitolewa kwa wanawake, asilimia 51 ni wanaume na asilimia moja kwa ubia. Aidha, asilimia 33 ya mikopo ilitolewa chini ya NEDF ilitolewa katika miradi iliyo vijijini. Serikali inaendeleza juhudi za kuukuza mfuko huo ili uwe kitovu cha kukuza viwanda vidogo. Fedha walizokopeshwa wajasiriamali kwa mwaka huu ni kutokana na marejesho ya wakopaji wa awali bila kuhusisha Shilingi bilioni 2.4 zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017.

**4.2.3 Sekta ya Biashara**

**a) Biashara kati ya Nchi na Nchi**

**91.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/



2017, Wizara imeendelea na juhudi ya kutafuta fursa za masoko na uwekezaji baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa. Kwa upande wa nchi na nchi, Wizara imeratibu na kufanya majadiliano mbalimbali ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi nyingine. Wizara iliratibu ziara ya kibiashara na ujumbe wa kiserikali kutoka Poland mwezi Julai 2016. Ziara hiyo ilikuwa ni muendelezo wa majadiliano ya kuhimiza wawekezaji kutoka Poland kuwekeza nchini. Moja ya masuala muhimu yaliyojadiliwa katika ziara hiyo ni kuharakisha uanzishwaji wa Kiwanda cha Uunganishaji wa Matrekta nchini (URSUS) na matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kuhifadhi mazao ya kilimo.

**92. Mheshimiwa Spika,** Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China zimekubaliana kushirikiana kutekeleza Mpango wa *FOCAC Johannesburg Action Plan 2016-2018* ambao unalenga kukuza uhusiano wa Afrika na China katika eneo la biashara, uwekezaji na uchumi. Katika kutekeleza makubaliano hayo, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Ubalozi wa China nchini imeandaa Mpango Kazi wa Kutekeleza Maazimio ya FOCAC ambayo yamewasilishwa Serikali ya China kwa ajili ya kupata ufadhili. Mpango Kazi huo umejumuisha miradi ya viwanda, nishati, miundombinu, fedha, kilimo, elimu na TEHAMA.

**93. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu ziara ya ujumbe wa kiserikali kutoka Ukraine. Hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza kwa viongozi wa nchi hiyo kufanya ziara ya kibiashara nchini. Ujumbe huo ulifanya mazungumzo na Wizara na kupata fursa ya kutembelea Maonesho ya Viwanda kwenye viwanja vya SabaSaba, Dar es Salaam na kukutana na wazalishaji hususan wajasiriamali wadogo na kujionea bidhaa za viwandani. Wizara iliwaomba wawekezaji kutoka Ukraine kuhamasisha wawekezaji nchini kwao ili Maonesho ya SabaSaba yanayofuata waje kuonesha viwanda au mashine za kuzalisha bidhaa kama walizoziona kwenye maonesho hayo.

**94. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliandaa ziara ya kibiashara kati ya Tanzania na Ujerumani nchini. Katika ziara hiyo, Wizara iliweza kutangaza fursa za biashara na uwekezaji

zilizopo nchini na kuvutia wawekezaji kutoka Ujerumani kuja kuwekeza Tanzania. Maeneo ambayo Ujerumani wameonesha nia ya uwekezaji ni katika uongezaji thamani wa bidhaa za kilimo na biashara ya bidhaa za kilimo (agro-processing and agri-business). Wizara pia iliandaa na kuratibu ziara ya ujumbe wa kibiashara kutoka Austria. Ziara hiyo ilisaidia wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Austria kuona fursa za uwekezaji nchini na kukutana na wafanyabiashara wa Kitanzania kupitia Maonesho ya SabaSaba ambapo walipata fursa ya kubadilishana uzoefu, kuona bidhaa za Tanzania na kuahidi kuzichangamkia. Baadhi ya fursa zilizovutia ugeni huo ni sekta za gesi na mafuta, kilimo na ujenzi wa viwanda. Wizara inafuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa ziara hizo zinazaa matunda. Vilevile, Wizara imefanya majadiliano na mabalozi wa nchi mbalimbali nchini zikiwemo Morocco, India, Sweden, Italy, Uingereza, Denmark, Ubelgiji, Sweden, Belarus, Czech, Cuba na Japan.

**95. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki katika mikutano ya Tume ya Pamoja (Joint Permanent Commission) kati ya Tanzania na Kenya, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia. Lengo la mikutano hiyo ya pamoja ni kujadili na kukubaliana namna ya kurahisisha biashara, kukuza uwekezaji na kuimarisha diplomasia ya uchumi kati ya Tanzania na nchi hizo. Katika kurahisisha biashara mipakani hususan kwa wafanyabiashara wadogo, Tanzania na Malawi zimekubaliana kuanzisha Kituo cha Pamoja cha Mpakani (OSBP) na kuingia makubaliano ya kuanzisha Mkataba wa Mfumo wa Kurahisisha Biashara (*Simplified Trade Regime -STR*). Makubaliano ya kuanzisha huduma kama hiyo kati ya Tanzania na Zambia yalisainiwa tarehe 27 Januari, 2017. Aidha, katika kuimarisha ushirikiano baina ya Tanzania na Uturuki, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Biashara na Uchumi uliofanyika mjini Ankara, Uturuki mwezi Januari 2017. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa makubaliano yaliyofanyika Dar es Salaam, Tanzania mwezi Novemba, 2012. Katika mkutano huo, nchi hizo mbili zilikubalina kushirikiana zaidi katika masuala yanayohusu biashara na uwekezaji.

**96. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki katika makongamano mbalimbali kama sehemu ya kuendeleza mahusiano ya kibiashara na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi nyingine,. Kupitia Kongamano la Biashara na Uwekezaji la China na Afrika (*Chinese Business and Investment Forum*) lililofanyika mwezi Septemba 2016, nchini China, mamlaka za uwekezaji ziliingia makubaliano ya ushirikiano kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji na mauzo ya bidhaa zao. Katika makongamano hayo, Wizara iliweza kutumia fursa hiyo kuhimiza upande wa China kuharakisha kukamilisha utaji saine wa mkataba wa biashara baina ya Tanzania na China. Vilevile, Wizara iliratibu Kongamano la Biashara na Mkutano wa Pamoja kati ya Tanzania na Rwanda iliyofanyika mwezi Desemba 2016 mjini Dar es Salaam. Suala la msingi lililoadiliwa ni kuhamasisha biashara baina ya nchi hizo hususan kuondoa vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru ambapo Rwanda iliridhia kuondoa vikwazo hivyo kwenye mchele kutoka Tanzania. Hivi sasa wafanyabiashara wa mchele kutoka Tanzania wanauza mchele nchini Rwanda bila kutozwa kodi ya ushuru wa forodha. Aidha, Wizara iliratibu Kongamano la Kibiashara kati ya Tanzania na Ubelgiji lililofanyika mwezi Novemba, 2016. Kongamano hilo lilisaidia kupanua fursa zaidi za biashara na uwekezaji kwa wafanyabiashara wa nchi hizo mbili. Maeneo yaliyowavutia wawekezaji kutoka Ubelgiji ni masuala ya uzalishaji viwandani, miundombinu, dawa za binadamu, usafirishaji na ujenzi.

**97. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) iliratibu kongamano la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Morocco lililofanyika tarehe 22 Oktoba, 2016. Katika Kongamano hilo jumla ya mikataba 21 ya ushirikiano ilisainiwa. Mikataba iliyosainiwa ilihusisha masuala yafuatayo; kuanzisha ushirikiano baina ya Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) na kile cha Morocco (The Moroccan Center for Export Promotion - Maroc Export), sekta za nishati na madini, gesi, kilimo, anga, fedha, utalii na uvuvi ambapo Morocco imeonesha nia ya kujenga kiwanda kikubwa cha usindikaji samaki hapa nchini. Aidha, kupitia kongamano hilo, Serikali

ya Morocco imeonesha nia ya kuanzisha safari za ndege za moja kwa moja kati ya Rabat na Dar es Salaam. Wizara pia ilishiriki katika Kongamano la Biashara kati ya Tanzania na Comoro lililofanyika Zanzibar mwezi Novemba 2016. Kongamano hilo lilikutanisha takriban wafanyabiashara 50 kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Comoro. Kupitia kongamano hilo, nchi zote mbili zilikubaliana kuruhusu Meli ya M/V Mapinduzi, inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inayobeba tani 600 za mzigo kuanza safari za kwenda Comoro.

**98. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki katika Kongamano la Biashara na Uchumi kati ya Uturuki na Afrika lililofanyika mjini Istanbul nchini Uturuki mwezi Novemba, 2016 na ilinadi fursa za biashara na uwekezaji na kuhamasisha washiriki kuja kuwekeza nchini. Vilevile katika kuhakikisha mihadi iliyowekwa wakati wa kongamano hilo inatekelezwa, Wizara imeweza kuratibu ziara ya Kampuni ya *Agir Haddecilik* ya nchini Uturuki kuja nchini kuangalia fursa za uwekezaji. Kampuni hiyo ni moja ya kampuni kubwa nchini humo inayojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa za chuma. Aidha, kupitia ziara yao nchini, kampuni hiyo imeonesha nia ya kuwekeza katika Sekta ya Chuma.

**99. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Kibiashara (2<sup>nd</sup> Joint Commercial Committee-JCC) kati ya Tanzania na Uturuki uliofanyika mwezi Januari, 2017 nchini Uturuki. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kufuatilia utekelezaji wa makubaliano ya mkutano wa kwanza wa JCC uliofanyika Dar es Salaam mwezi Novemba 2012 pamoja na kuibua maeneo mapya ya ushirikiano ili kukuza na kuendeleza biashara na uwekezaji. Mkutano huo pia ulijadili na kukubaliana kuhusu ziara ya kiserikali ya Mheshimiwa Rais wa Uturuki nchini Tanzania. Aidha, ziara ya Mheshimiwa Rais wa Uturuki ilifanyika mwezi Januari 2017 ambapo mikataba 9 ilisainiwa. Mikataba hiyo ilihusisha sekta za viwanda, afya, elimu, ulinzi na ujenzi. Ziara hiyo pia ilihusisha kongamano la biashara ambapo pande zote mbili ziliendelea kunadi fursa za biashara na uwekezaji.

**100. Mheshimiwa Spika**, ili kufaidika na fursa ya AGOA, Wizara kwa kushirikiana *East African Trade and Investment Hub* (EATIH) na wadau wengine nchini imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa AGOA. Mkakati huo unalenga kuhamasisha wadau nchini kuchangamkia fursa hiyo kutokana na nyongeza ya miaka 10 ya fursa ya AGOA ambayo sasa itafikia ukomo mwaka 2025. Mkakati huo umejikita kwenye sekta nne za kipaumbele ambazo ni nguo na mavazi, bidhaa za kazi za mikono, ngozi na bidhaa zake na usindikaji wa bidhaa za kilimo. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na EATIH kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati huo wa AGOA.

## **b) Biashara ya Kikanda**

**101. Mheshimiwa Spika**, katika majadiliano ya biashara ya kikanda, Wizara imetetea msimamo wa Tanzania wa kutosaini Mkataba wa EPA na kuendelea kushawishi nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuunga mkono msimamo huo wa Tanzania. Wizara ilifanikiwa kutekeleza suala hilo kupitia Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji (SCTIFI) uliofanyika mwezi Januari hadi Februari, 2017 jijini Arusha. Kutokana na msimamo huo, licha ya Kenya na Rwanda kutia saini, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeshindwa kusaini Mkataba huo hali inayotoa fursa kwa Tanzania na Jumuiya hiyo kutafakari kwa mapana zaidi kuhusu Mkataba wa EPA.

**102. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeshiriki katika zoezi linaloendelea la kufanya mapitio ya Ushuru wa Pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Common External Tariff-CET). Zoezi hilo ni sehemu ya utekelezaji wa Itifaki ya Ushuru wa Forodha wa Pamoja wa EAC na limezingatia pia maelekezo ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kutaka kufanya mapitio ya CET kila baada ya miaka mitano. Lengo la mapitio hayo ni kushughulikia changamoto za utekelezaji wa CET kuweza kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na biashara na pia yana akisi maendeleo yanayojitokeza katika utekelezaji wa Mkakati wa Viwanda wa Jumuiya. Aidha, Wizara, kwa kushirikiana na

wadau, tayari imeunda kikosi kazi cha kitaifa kitakachoshiriki katika zoezi hilo kitaifa na kikanda ambacho kitazingatia mapendekezo yenye maslahi mapana ya Taifa.

**103. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki katika kupitisha Mkakati wa Viwanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mkakati huo (2015-2063). Wizara ilifanikiwa kutekeleza jukumu hilo kwa kushiriki kikamilifu kupitia Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika mwezi Machi, 2017 mjini Lozitha, Swaziland. Mkakati huo unaendana na dhima ya Serikali ya Awamu ya Tano ya ujenzi wa uchumi wa viwanda hasa ikizingatiwa kuwa Mkakati huo umejikita katika maeneo makuu matatu ambayo ni: uendelezaji viwanda; kukuza ushindani; na kuhimiza mtangamano wa kikanda.

**104. Mheshimiwa Spika,** kupitia mkutano huo, Tanzania imefanikiwa kupata upendeleo maalum (dispensation) wa kutoza ushuru sukari inayotumika kwa matumizi ya nyumbani kutoka nchi za SADC. Katika upendeleo huo, Tanzania itaendelea kutoza ushuru wa asilimia 25 kwa sukari ya aina hiyo kutoka nchi za SADC kwa kipindi cha mwaka mmoja. Wizara pia imewasilisha ombi la kupatiwa upendeleo kama huo kwa kipindi cha miaka mitatu kwa karatasi za vifungashio. Upendeleo huo unalenga kutoa fursa kwa wazalishaji wa bidhaa hizo nchini kujenga uwezo zaidi ili kukabiliana na ushindani wa bidhaa kama hizo kutoka SADC.

**105. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilishiriki katika kuandaa na kuwasilisha Waraka Serikalini kuhusu kuomba Serikali iridhie utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Huduma kwa nchi za SADC. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliratibu maandalizi na mawasilisho ya Waraka husika. Ni matarajio yetu kuwa utekelezaji wa Itifaki hiyo utafungua fursa zaidi kwa watoa huduma katika sekta mbalimbali nchini kuweza kutoa huduma zao bila vikwazo vya kibiashara katika nchi wanachama wa SADC. Aidha, Itifaki hiyo pia inatoa fursa kwa kila nchi mwanachama

kuruhusu huduma na watoa huduma kutoka nchi nyingine wanachama kutoa huduma kwenye maeneo watakayopendekeza. Hali hiyo itaongeza ushindani katika sekta za huduma zitakazofunguliwa na hivyo kuongeza tija na urahisi kwa watumiaji wa huduma hizo.

**106. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Utatu-*Tripartite Free Trade Area-TFTA* kwa jumuiya za *COMESA-EAC-SADC*. Majadiliano hayo yalikamilika mwezi Aprili, 2015 na hatimaye wakuu wa nchi na serikali wa nchi zinazounda Jumuiya hizo walihitimisha majadiliano ya awamu ya kwanza na kusaini Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Utatu mwezi Juni 2015. Majadiliano katika baadhi ya maeneo ambayo hayakuwa yamekamili wakati wa utiwaji saini, yamekamili mwezi Novemba, 2016. Faida kubwa inayotarajiwa kupatikana katika utekelezaji wa Mkataba huo ni pamoja na kuongezeka kwa fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania kwenye Soko la *TFTA* kutokana na kupunguzwa kwa vikwazo vya kufanya biashara pamoja na kuwa na vigezo vya uasilia wa bidhaa vilivyo rahisishwa vinavyoweza bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya hizo kufikia vigezo hivyo na kutambulika katika Soko la *TFTA*. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau tayari inaendelea na zoezi la kukusanya maoni ya wadau kwa lengo la kuandaa Waraka kuomba Serikali kuridhia Mkataba wa uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Utatu- *TFTA*.

**107. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki na kuweza kutetea kikamilifu misimamo ya Taifa katika majadiliano yanayoendelea yanayohusu uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (Continental Free Trade Area-CFTA). Katika mkutano uliofanyika mjini Addis Ababa, Ethiopia mwezi Machi, 2017, Wizara ilichangia katika majadala na kupitisha rasimu ya Taratibu za Majadiliano ya CFTA (Draft Modalities for CFTA) kwenye maeneo ya Biashara ya Bidhaa na Huduma. Maeneo mahsusni yanayojadiliwa na ambayo Wizara inayasimamia ni kuhusu masuala ya Usalama wa Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea (SPS); Vikwazo Visivyo vya Kiushuru vya Kibiashara (NTBs) na Vikwazo vya Kiufundi vya

Kibiashara (TBT); Uasili wa Bidhaa (RoO); Biashara ya Huduma; masuala ya Sheria; *Trade Remedies*; na Taratibu za Forodha na Uwezeshaji wa Biashara. Wizara imejizatiti katika kuhakikisha kuwa maslahi ya Tanzania yanazingatiwa katika majadiliano hayo.

### c) Biashara ya Kimataifa

**108. Mheshimiwa Spika**, katika kupanua fursa za masoko na biashara kupitia majadiliano ya biashara ya kimataifa, Wizara imeshiriki katika kuandaa mwongozo wa miaka minne ijayo wa Shirika la UNCTAD. Mpango huo ulipitishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Mawaziri wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD XIV) uliofanyika mjini Nairobi, Kenya mwezi Julai, 2016. Kwa kuzingatia mpango huo, UNCTAD itajikita katika kutafiti, kuchangia pamoja na kutatua changamoto za kibiashara na maendeleo hususan kwa nchi maskini na zinazoendelea. Hiyo ni pamoja na kukuza uchumi shirikishi na endelevu kupitia biashara na kuchangia utekelezaji na ufuatiliaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs, 2030). Wizara ilitumiafursaya mkutano huokufanya majidiliano ya kuhamasisha biashara na uwekezaji nchini ambapo ujumbe wa Tanzania uliweza kukutana na kufanya mazungumzo na ujumbe kutoka Austria, Cuba, Hungary, Jamaica, Kenya, Poland, Sudani ya Kusini, Uganda, Venezuela, Umoja wa Ulaya; na mashirika ya UNCTAD, WTO, TRAPCA na Sekretariati ya nchi za ACP.

**109. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanzisha Kituo cha Taarifa za Biashara za Kimataifa (*WTO Reference Center*) ambacho kipo Wizarani. Kituo hicho kitawezesha taasisi za Serikali na binafsi kupata nyaraka na taarifa mbalimbali za biashara ambazo zitasaidia kukuza Sekta ya Biashara nchini. Wizara pia imewasilisha taarifa za viwango vipya 44 vya ubora (*notifications of technical Standards*) kwenye Shirika la Biashara la Dunia kwa bidhaa za mbolea, matunda, vyakula vya wanyama na vileo. Tayari Wizara imetoa ufafanuzi na kutetea *notifications* kwa viwango vilivyowasilishwa kupitia Mkutano wa Kamati ya Vikwazo vya Kiufundi vya Shirika la



Biashara Duniani (*WTO TBT Committee*) uliofanyika Uswisi, Geneva mwezi Machi, 2017.

**110. Mheshimiwa Spika**, Wizara imewajengea uwezo maafisa watano kupitia mafunzo ya mfumo wa kieletroniki (*ePing notification alert system*) yaliyofanyika Desemba, 2016 Kampala – Uganda, ili waweze kushiriki kikamilifu katika kutekeleza mikataba ya WTO hususan kwenye eneo la utoaji na upokeaji wa taarifa za kibiashara katika masuala ya Vikwazo vya Kiufundi na Kibiashara (TBT); na Usalama wa Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea (SPS).

**111. Mheshimiwa Spika**, ili kusogeza karibu huduma ya kuwajengea uwezo wadau kwenye masuala ya kibiashara, Wizara imeratibu zoezi la upatikanaji wa kozi maalum ya majadiliano ya biashara katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Chini ya ufadhili wa WTO, wanafunzi kutoka nchi zote wanachama wanaoongea kiingereza watapata mafunzo katika chuo hicho. Hiyo ni fursa muhimu ya kuwapatia mafunzo wataalamu wetu, lakini pia kutokana na wingi wa washiriki kutoka sehemu mbalimbali duniani, chuo chetu kikongwe kitapata fursa ya kutangazwa zaidi kote duniani. Mafunzo hayo yanayotegemewa kuanza mwaka ujao wa fedha yataendelea kwa miaka mitatu mfululizo.

**112. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) wa Uwezeshaji Biashara (WTO Trade Facilitation Agreement). Mkataba huo, unalenga kupunguza gharama za ufanyaji biashara kwa kuhakikisha kuwa miundombinu muhimu inakuwepo na inaratibiwa kwa pamoja ili kupunguza muingiliano wa majukumu. Katika maandalizi hayo, Wizara imeunda Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (National Trade Facilitation Committee) mwezi Agosti, 2016 kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba huo ili kusimamia utekelezaji wa Mkataba huo. Aidha, Wizara imewasilisha maombi ya kupata ridhaa ya Tanzania kuridhia Mkataba wa Urahisishaji Biashara.

**113. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha Kamati za Kitaifa

ya Kuondoa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Ushuru (Non Tariff Barriers-NTBs), Vigezo vya Biashara vya Afya ya Mimea na Wanyama (Sanitary and Phytosanitary Measures-SPS), Vigezo vya Biashara vya Kiufundi (Technical Barriers to Trade-TBT) na Uwezeshaji Biashara (Trade Facilitation-TF), Wizara imeendelea kuratibu mikutano ya kamati hizo nchini na kushiriki mikutano ya kamati za kikanda kwa lengo la kujadili na kutatua changamoto katika maeneo hayo kwa lengo la kurahisisha biashara.

**114. Mheshimiwa Spika**, baadhi ya mafanikio ya juhudi hizo ni kuondolewa kwa NTBs nane (8) ambazo ni tozo ya Dola za Kimarekani 300 kwa malori ya Rwanda yanayobeba chumvi kupitia njia ya Mbuga ya Saadani, tozo ya asilimia 1.5 ya maendeleo ya reli, ucheleweshaji wa kutoa mizigo bandarini kwa kutumia siku 10, idadi ya mizani kutoka 17 hadi kufikia mizani 3 kwa ushoroba wa kati (central corridor), tofauti ya masaa ya kazi katika mipaka ya Rusumo na Kabanga kwa kuanzisha mfumo wa OSBP; tozo kwa bidhaa za dawa kutoka Kenya, tozo ya asilimia 35 kwenye mafuta ya kula kutoka Kenya na maafisa wa TRA wanaofanya kazi Kenya chini ya mfumo wa himaya moja wa forodha (single customs territory), na kumalizamudawakazimapema (kufunga ofisisaa 9 alasiri). Uondoaji wa NTBs hizo umechangia kwa kiasi kikubwa katika kurahisisha biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kupitia Kamati ya Kitaifa ya NTBs, Wizara imeshirikiana na *Tanzania Gender Networking Programme (TGNP)* na TMEA kuendesha mafunzo kwa wafanyabiashara wanawake 34 wanachama wa Chama cha Wanawake wa Tanzania Wafanyabiashara Mipakani (WATABAM) wanaofanya biashara katika mipaka ya Holili, Mutukula na Namanga. Mafunzo hayo yalihusu masuala ya vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru na fursa za masoko zilizopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla.

**115. Mheshimiwa Spika**, katika kupambana na bidhaa zinazotoka nje ya nchi na kuuzwa nchini chini ya bei halisi ya sokoni duniani, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeratibu

zoezi la kuandika upya Sheria ya *Anti-dumping and Countervailing Measures*. Aidha, Wizara imekwishaandaa rasimu ya Sheria na Waraka wa kupata maamuzi ya Serikali ili iridhie kuandika upya sheria hiyo. Sheria hiyo inalenga kuzuia uingizwaji wa bidhaa nchini zinazouzwa chini ya bei halisi ya bidhaa hizo sokoni (Dumping price) ili kuhakikisha kunakuwepo na ushindani wa haki kwenye soko. Vilevile, sheria hiyo itasaidia kulinda viwanda na wafanyabiashara nchini kwa kuweka utaratibu wa kisheria wa kujilinda na bidhaa zinaouzwa nchini chini ya bei halali ya soko kwa kipindi husika. Kutokana na umuhimu wake, tunatarajia sheria hiyo ianze kutumika rasmi katika mwaka 2017/2018.

#### **4.2.4 Sekta ya Masoko**

**116. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Masoko ina jukumu la kuvipatia viwanda malighafi, kuvilinda, kuuza bidhaa za viwanda, kumlinda mlaji na kuhakikisha ubora na ushindani ulio haki. Katika kujenga uchumi wa viwanda, Wizara imesimamia majukumu chini ya sekta hiyo kwa lengo la kuongeza tija katika sekta zote husika.

##### **a) Udhhibiti wa Ubora na Viwango vya Bidhaa**

**117. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia mashirika yake ya TBS, WMA na FCC ina jukumu la kuhakikisha kuwa bidhaa na huduma zinazozalishwa na kutolewa kwa mlaji zinakidhi viwango. Kwa mwaka 2016/2017, taasisi ya TBS na FCC kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali hususan TRA, Jeshi la Polisi na TFDA imeendelea kudhibiti ubora wa bidhaa ili kulinda afya za watumiaji, mazingira pamoja na kuleta ushindani wa haki katika biashara. Pamoja na kusimamia ubora wa bidhaa za viwanda vyetu, kipaumbele kimewekwa katika kuzuia bidhaa zisizo na ubora na bidhaa bandia kuingia katika soko. Umuhimu wa kuzuia bidhaa unatokana na ukweli kuwa bidhaa hizo huuzwa kwa bei ya chini na hivyo kuleta ushindani usio wa haki kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda kwa kuzingatia viwango. Hivyo, udhibiti wa bidhaa bandia na zisizo na ubora ni hatua muhimu katika kulinda viwanda vya ndani.

**118. Mheshimiwa Spika**, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea na ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi kabla ya kuletwa nchini, kukagua bidhaa bandarini na mipakani na bidhaa zilizopo sokoni. Ili kuimarisha mifumo ya udhibiti ubora wa bidhaa nchini, Wizara inaandaa Sera ya Taifa ya Viwango (National Quality Policy) pamoja na Mkakati wake ambapo andiko la kitaalamu (Concept Note) limeandaliwa na Taasisi ya *Trade Mark East Africa* (TMEA) imeridhia kugharamia maandalizi yake. Pamoja na maandalizi ya Sera, Wizara imeanza kufanya mapitio ya Sheria ya Viwango Na. 2 ya Mwaka 2009 ili kuongeza kasi ya maendeleo ya viwanda nchini. Maoni ya wadau yamekusanywa na uchambuzi unaendelea ili kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo katika ngazi inayofuata. Vilevile, Wizara imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ushindani na kuyawasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa hatua zaidi.

**119. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imeendelea kufanikisha juhudi za kulinda haki za wabunifu na rasimu ya Sera ya Miliki Bunifu pamoja na mkakati wake imeandaliwa na kujadiliwa ngazi ya awali ya maamuzi Serikalini. Wizara inaboresha rasimu hiyo ili iwasilishwe kwa maamuzi ya mwisho. Aidha, Wizara imeandaa marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya mwaka 1999 ili kuimarisha ulinzi wa haki miliki za wadau mbalimbali.

## **b) Bei ya Bidhaa, Mazao Makuu ya Chakula na Mifugo**

### **(i) Bei za Mazao Makuu ya Chakula**

**120. Mheshimiwa Spika**, jukumu la Wizara yetu ni pamoja na kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kutoa taarifa ya bei za mazao makuu ya chakula, mifugo na baadhi ya bidhaa muhimu nchini kwa wadau. Katika msimu wa 2016/2017, bei ya mazao makuu ya chakula kama vile mahindi, maharage, mchele, ngano, uwele, ulezi na mtama zimeongezeka kwa viwango tofauti ikilinganishwa na msimu wa 2015/2016. Kwa mfano, wastani wa bei ya mahindi kwa gunia la kilo 100 iliongezeka kutoka Shilingi 59,873 msimu wa 2015/2016 hadi kufikia Shilingi 99,527 msimu wa 2016/2017, sawa na ongezeko

la asilimia 66.23. Bei ya mchele kwa gunia la kilo 100 iliongezeka kutoka wastani Shilingi 177,340 msimu wa 2015/16 hadi Shilingi 191,289 msimu wa 2016/17. Bei ya gunia la maharage la kilo 100 iliongezeka kutoka Shilingi 162,383 mwaka 2015/2016 hadi kufikia Shilingi 178,101 mwaka 2016/2017, sawa na ongezeko la asilimia 9.68. Kupanda huko kwa bei ya mazao makuu ya chakula kumechangiwa na kushuka kwa ugavi kutokana na uhaba wa mvua katika msimu wa kilimo wa 2016/2017. Bei ya mazao mengine ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.11**.

**(ii) Bei za Mifugo**

**121. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, wastani wa bei ya jumla ya ng'ombe wa daraja la pili ilishuka kutoka wastani wa Shilingi 1,110,227 mwaka 2016 hadi Shilingi 1,105,321 mwezi Machi, 2017, sawa na upungufu wa asilimia 8.9. Bei ya ng'ombe wa daraja la tatu ilishuka kutoka Shilingi 830,888 mwaka 2016 hadi shilingi 731,300 mwezi Machi, 2017, sawa na upungufu wa asilimia 11.9. Kushuka kwa bei hizo kumechangiwa na kushuka kwa ubora wa mifugo kutokana na uhaba wa malisho. Aidha, uhaba wa malisho uliwafanya wafugaji kuuza mifugo kwa wingi na hivyo bei kushuka. Wastani wa bei ya mifugo ni kama ilivyoonekana katika **Jedwali Na.12a**.

**(ii) Bei ya Mbogamboga na Matunda**

**122. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na TAHA kupitia ufadhili wa Serikali ya Uswisi, imeanzisha Mfumo wa Taarifa za Masoko ya Matunda na Mbogamboga ambapo programu maalum inayotumia simu za kiganjani huwafikishia wakulima taarifa za bei na masoko kwa wakati. Wakusanya taarifa za masoko 20 wa TAHA wamepatiwa mafunzo na simu za kiganjani zinazotumika katika kukusanya na kusambaza taarifa hizo.

**123. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusambaza taarifa za mazao na mifugo kwa wadau kwa njia ya radio, luninga, ujumbe wa simu za kiganjani, mitandao ya kompyuta

na magazeti. Taarifa za bei za mazao makuu ya chakula zilikusanywa kutoka katika masoko 26 ya miji ya mikoa na bei za rejareja kutoka masoko 114. Aidha, Wizara imeboresha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa hizo kwa kuwapatia wakusanyaji taarifa wote 140 simu za kiganjani za kisasa (smart phones) zinazotumika kukusanya na kutuma taarifa hizo kwa wakati.

**(iii) Bei ya Baadhi ya Bidhaa za Viwandani (Sukari na saruji)**

**124. Mheshimiwa Spika**, bei ya sukari imeongezeka kutoka wastani wa Shilingi 2,256 kwa kilo mwezi Aprili, 2016 hadi kufikia wastani wa Shilingi 2,628 mwezi Aprili, 2017 sawa na ongezeko la asilimia 17. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji ambazo zimesabisha sukari kuuzwa kwa bei ya jumla ya wastani ya Shilingi 2,000 kwa kilo. Bei ya saruji imeshuka kutoka wastani wa Shilingi 12,000 kwa mfuko wa kilo 50 jijini Dar es Salaam mwezi Aprili, 2016 hadi kufikia wastani wa Shilingi 9,500 mwezi Aprili, 2017 sawa na punguzo la asilimia 20.83. Bei ya saruji jijini Mwanza imepungua kutoka Shilingi 16,800 hadi Shilingi 16,500 na Arusha kutoka Shilingi 14,000 hadi Shilingi 12,500. Kushuka kwa bei ya saruji nchini ni matokeo ya ongezeko ya uzalishaji wa bidhaa hiyo kutoka katika viwanda vya ndani (**Jedwali Na. 12b**).

**c) Kutangaza Bidhaa za Tanzania**

**125. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) iliwezesha Maonesho ya 40 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF). Katika maonesho hayo, mataifa 30 yalishiriki ikilinganishwa na mataifa 25 yaliyoshiriki katika Maonesho ya 39 mwaka 2015. Makampuni 2,500 yalishiriki katika maonesho ya mwaka 2016 ikilinganishwa na makampuni 2,305 yaliyoshiriki katika mwaka 2015, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.6. Kati ya makampuni hayo, 501 yalikuwa ya kutoka nje ya nchi na 1,999 yalikuwa ni makampuni ya ndani ya nchi. Aidha, Wizara sita (6) na taasisi 37 za Serikali zilishiriki.

**126. Mheshimiwa Spika**, katika maonesho hayo, maulizo ya bidhaa kwa soko la nje (export enquiries) yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 119.91 yakilinganishwa na maulizo ya thamani ya Dola za Kimarekani milioni 108.6 katika Maonesho ya 39 ya mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 10.41. Bidhaa zilizopata maulizo kwa wingi ni kahawa, korosho, chai, bidhaa za vyakula, asali, viungo (iliki na tangawizi) na bidhaa za sanaa za mikono. Maulizo ya bidhaa kutoka nje (import enquiries) yamepungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 90.5 katika maonesho ya mwaka 2015 hadi Dola za Kimarekani milioni 89.77 katika maonesho ya mwaka 2016.

**127. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara pamoja na Taasisi 11 zilizo chini yake zilishiriki Maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Ngongo Mkoani Lindi. Katika maonesho hayo, jumla ya wajasiriamali 28 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mbeya, Mtwara, Pwani na Zanzibar waliwezesha kushiriki na kuonesha bidhaa zao kupitia banda la Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

#### **d) Kuimarisha Biashara za Mipakani**

**128. Mheshimiwa Spika**, jitihada za kuimarisha biashara za mipakani zimewezesha kuanzishwa kwa vituo nane (8) vya Ukaguzi wa Pamoja Mipakani (One Stop Border Posts – OSBP) baina ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC. Vituo hivyo ni:- Holili/Taveta (Tanzania na Kenya); Sirari/ Isebania (Tanzania na Kenya); Namanga/Namanga (Tanzania na Kenya); Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi); Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda); Mtukula/Mtukula (Tanzania na Uganda); Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya) na Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia). Pamoja na ukaguzi wa pamoja katika mipaka hiyo, utaratibu wa biashara kwa wafanyabiashara wadogo katika mipaka hiyo (Simplified Trade Regime – STR) unatumika katika mipaka yote yenye vituo hivyo.

**129. Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha ujenzi wa Kituo cha

Ukaguzi wa Pamoja cha Mpaka wa Tunduma/Nakonde upande wa Tanzania, mkandarasi wa ujenzi wa Kituo hicho Kampuni ya *Nadhra Engineering Construction Company Limited* ameanza ujenzi mwezi Novemba, 2016. Ujenzi huo unagharamiwa na Shirika la *Trade Mark East Africa* (TMEA). Ujenzi unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18. Aidha, Serikali inatarajia kujenga Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Mpakani katika mpaka wa Kasumulu/ Songwe (Tanzania/Malawi) ili kuendeleza biashara na nchi jirani ya Malawi.

#### 4.2.5 Sekta ya Uwekezaji

##### a) Kuhamasisha Uwekezaji wa Ndani

**130. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara iliendelea na jukumu lake la kuratibu na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi nchini kwa kushirikiana na taasisi nyingine za sekta ya umma na sekta binafsi kupitia njia mbalimbali. Mnamo mwezi Septemba, 2016, Wizara ilishiriki katika Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Morogoro lililolenga kuhamasisha uwekezaji katika mkoa huo na mikoa ya jirani. Vile vile, Wizara ilishiriki katika uzinduzi wa Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja ya Mkoa wa Simiyu ambayo inalenga kuhamasisha uwekezaji utakaotumia fursa na rasilimali zinazopatikana katika wilaya za mkoa huo.

##### b) Kuhamasisha Uwekezaji Kutoka Nje ya Nchi

**131. Mheshimiwa Spika**, katika kuvutia wawekezaji wa nje na kuwaunganisha wafanyabishara wa Tanzania na wale wa nje, Wizara iliandaa makongamano mahsusi yaliyofanyika nchini kati ya Tanzania na nchi za nje. Nchi ambazo zilileta ujumbe wa wafanyabiashara nchini ni pamoja na Austria, Belgium, China, Finland, India, Morocco, Rwanda na Uturuki. Vilevile, Wizara kupitia Kituo cha Uwekezaji kiliandaa mikutano ya uwekezaji katika nchi rafiki kwa uratibu wa ofisi za ubalozi na sekta binafsi katika nchi za China, India, Israel, Italia, Kenya, Misri na Rwanda. Wizara imeanzisha utaratibu wa kuwasiliana na wawekezaji wa nje kupitia balozi zetu za nje. Chini ya utaratibu huo, mabalozi wetu wanapewa taarifa



maalum zinazowasaidia kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko ya bidhaa zetu nje.

**132. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeendelea kupokea wageni binafsi na taasisi za umma kutoka nchi za nje kuja kuangalia fursa za uwekezaji nchini. Wageni hao walitoka nchi za Afrika ya Kusini, China, India, Italia, Lebanoni, Marekani, Misri, Ufaransa, Uganda, Uingereza na Umoja wa Falme za Kiarabu. Baadhi ya sekta zilizoonesha kuvutiwa kwa uwekezaji ni pamoja na uzalishaji wa betri za kuhifadhi nishati ya jua, uzalishaji wa magadi soda, dawa za binadamu na vifaa tiba, ufugaji wa ng'ombe wa kisasa na usindikaji wa maziwa, kilimo cha miwa na uzalishaji sukari, nguo na mavazi, mbolea, saruji, juisi za matunda, bidhaa za kemikali za petroli, sigara, usindikaji wa kahawa, mita za maji, uzalishaji wa umeme, ujenzi wa miundombinu, kuunganisha magari na ujenzi wa nyumba za makazi. Ili kufanikisha wageni hao kuwekeza, Wizara iliratibu mikutano na Wizara na taasisi mbalimbali kwa lengo la kupata taarifa mbalimbali za uwekezaji kutoka kwenye sekta husika ili kuwawezesha wawekezaji kufanya uamuzi sahihi wa uwekezaji.

### c) Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji

**133. Mheshimiwa Spika**, ili kuharakisha ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini, ni jukumu la Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kuhakikisha sheria, kanuni na utendaji wa sekta ya umma unakuwa rafiki. Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani imeonesha nia ya dhati ya kuendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji kama inavyojidhihirisha katika juhudi za kupiga vita rushwa, kuongeza uwajibikaji na utendaji kwenye sekta ya umma na kudhibiti ukwepaji wa kodi.

**134. Mheshimiwa Spika**, kutokana na jitihada zinazoendelea, Tanzania imepanda nafasi katika ripoti za dunia za urahisi wa kufanyaji biashara. Kwa mfano, katika Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu Urahisi wa Kufanya Biashara (*Ease of Doing Business*) ya mwaka 2017 inaonesha Tanzania imepanda

nafasi 12 kutoka nafasi ya 144 mwaka 2016 mpaka nafasi ya 132 mwaka 2017 kati ya nchi 190 duniani. Katika ripoti hiyo, Tanzania pia imepanda kwa kigezo cha kasi ya maboresho kutoka wastani wa 50.59 mwaka 2016 mpaka 54.48 mwaka 2017 ambao ni juu ya wastani wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara wa 49.51. Baadhi ya vigezo ambavyo Tanzania imefanya vizuri ni upatikanaji wa mikopo na usimamizi wa mikataba ambapo kati ya nchi 190 Tanzania imekuwa ya 44 na 59 mtawalia. Vigezo ambavyo hatujafanya vyema na nafasi zake kwenye mabano vinajumuisha taratibu za kuanzisha biashara (135), kupata vibali vya ujenzi (136), urahisi wa kulipa kodi (154) na urahisi wa taratibu za forodha (180). Aidha, katika ripoti ya mwaka 2016 ya Taasisi ya *Heritage Foundation* ya Marekani inayopima uhuru wa kiuchumi, imeonesha kuwa katika Afrika Mashariki, Tanzania ni ya pili kwa kuwa nafasi ya 105 baada ya Rwanda iliyoshika nafasi ya 51 kati ya nchi 180 duniani.

**135. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa na unafuu kwa baadhi ya vigezo, Serikali inatambua mapungufu ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi. Utafiti uliofanywa wa Timu ya Serikali uliofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya uratibu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji umeainisha mambo yanayopaswa kufanyiwa kazi ili kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

**136. Mheshimiwa Spika**, shughuli za uwekezaji zinahitaji uratibu na ushirikiano mzuri wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha, Serikali inatambua pia changamoto wanazozipata katika kuanzisha au kupanua shughuli zao za uzalishaji na uwekezaji. Katika kuimarisha mahusiano na ushirikiano huo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango iliitisha mkutano wa mashauriano (Dialogue Meeting) pamoja na sekta binafsi tarehe 11 Aprili, 2017 uliohudhuriwa na viongozi wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge na wafanyabiashara zaidi ya 200. Majadiliano ya mkutano huo yalienda vizuri na yalisaidia sana kuongeza ari na utashi wa sekta binafsi kushirikiana na Serikali katika jitihada za maboresho ya sekta ya umma na usimamizi ili kurahisisha mazingira ya biashara na kukuza uchumi. Aidha, sekta binafsi

Ilielezea pia changamoto ambazo kama zitafanyiwa kazi zitasaidia kuimarisha ubia na upendo kwa sekta ya umma na sekta binafsi.

#### **d) Uboreshaji wa Mazingira ya Kufanya Shughuli**

**137.** Mheshimiwa Spika, ili nchi ivutie na kukuza uwekezaji wa ndani na kuvutia wawekezaji kutoka nje, yapo mambo manne muhimu ya kufanya. Kwanza, ni lazima nchi iwe na amani na utulivu. Katika hilo tunamshukuru Mungu nchi yetu inafanya vizuri. Pili, ni lazima mwenendo wa uchumi wa nchi uwe na utulivu, uimara na uendelevu, yaani kuwe na macroeconomic stability and sustainability. Vigezo mbali mbali vya kiuchumi vinaonesha kuwa nchi yetu inaendelea kufanya vizuri kwenye mwenendo wa uchumi. Tatu, ni lazima nchi iwe na miundombinu na huduma nzuri za kuwezesha ufanyaji wa shughuli za uchumi. Hii ni pamoja na kuwa na barabara nzuri, reli inayofanya kazi kwa ufanisi, bandari zinazofanya kazi kwa ufanisi, usafiri mzuri wa barabara, anga na kwenye maji na kadhalika. Kadhalika ili kufanikisha uwekezaji ni muhimu kuwa na nishati ya uhakika na ya bei nafuu, na ni lazima upatikanaji wa maji uwe na uhakika. Jambo la nne la muhimu katika kuvutia na kukuza uwekezaji ndani ya nchi ni kuweka mazingira ya kiseria, kisheria, kikanuni na kiutendaji ambayo ni wezeshi kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiuchumi. Tunapozungumzia mazingira mazuri ya kufanya shughuli za kiuchumi tunazungumzia hayo mambo manne, yaani; amani na utulivu, mwenendo mzuri wa uchumi wa nchi, miundombinu bora na huduma nzuri wezeshi na mwisho ni kuwa na sera, sheria, kanuni na utendaji ambao unalenga kuwezesha shughuli za kiuchumi za wananchi na wawekezaji kwa ujumla.

#### **e) Uratibu wa Urahisi wa Kufanya Shughuli**

**138.** *Mheshimiwa Spika*, uendelezaji na uimarishaji wa uwekezaji pamoja na mambo mengine unahitaji kuwepo kwa mfumo thabiti wa uratibu wa urahisi wa kufanya shughuli. Chini ya mfumo huo, taarifa mbalimbali toka kwa wadau hupokelewa, huchambuliwa na kufanya majadiliano

na Serikali au sekta binafsi kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara. Kwa kutambua umuhimu wa kurahisisha ufanyaji wa shughuli, mwezi Oktoba, 2016, Wizara ilianzisha rasmi Dawati la Kuratibu Wepesi wa kufanya Shughuli (*Ease of Doing Business* - EODB) ili kushughulikia changamoto zinazojitokeza katika kufanya shughuli za kiuchumi kwa ufanisi.

**139. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Dawati la Kuratibu Wepesi wa kufanya Shughuli limepokea na kushughulikia masuala yanayohusu kodi kwenye sukari na marejesho ya kodi; Ushuru wa Forodha kwenye uagizaji wa mafuta na sabuni; na malighafi yanayotumika kuzalisha *Automotive Leaf Spring*; *Gypsum Board* na bidhaa zake. Dawati limeshughulikia kwa kina vigezo vinavyopelekea bidhaa zinazozalishwa nchini kuwa aghali katika soko la ndani ikilinganishwa na bidhaa zinazotoka nje. Kwa kutaja baadhi, lipo tatizo linalohitaji ufumbuzi kwani, kwa mfano, wakati vyandarua vinavyotoka nje ya nchi havitozwi baadhi ya ushuru na kodi, malighafi za kuzalisha bidhaa hizo nchini hutozwa ushuru. Katika Sekta ya Ngozi ambayo tunaitegemea kuzalisha ajira nyingi, ngozi zinazozalishwa nchini moja ya vigezo vinavyoinyima faida ya ushindani ni kemikali zinazotumika kuongeza thamani ya ngozi hizo kutozwa kodi wakati ngozi zinazotoka nje hazitotwi kodi huko zinakozalishwa.

**140. Mheshimiwa Spika**, uratibu chini ya Dawati hilo ni endelevu na unahusisha uratibu wa masuala yanayopokelewa, kuyachambua, kuyaelekeza katika sekta husika, kuwa na vikao vya kisekta na wadau wake kwa lengo la kuchambua hoja na hatimaye kuwasilisha mapendekezo katika *Tax Task Force* wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Serikali ya kila mwaka. Hivyo, nitoe rai kwa wadau wote kuwasilisha masuala yanayokwamisha utekelezaji wa ujenzi wa uchumi wa viwanda na masuala yote ya kisekta kwa wakati. Wizara itashukuru kupata ushirikiano wa uhakika pale tutakapohitaji maelezo au taarifa zaidi za kuwezesha kuyafahamu kwa undani masuala husika, kufanya tathmini na hivyo kushauri na kutoa maamuzi sahihi.

### 4.3 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA WIZARA

#### 4.3.1 Shirika la Maendeleo la Taifa

##### **(i) Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga – Njombe**

**141. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara kupitia NDC iliendelea na majadiliano juu ya mauziano ya umeme kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Ubia ya TCIMRL. Mfumo uliokubalika na pande zote mbili ni mwekezaji kujenga mtambo wa kufua umeme, kumiliki na kuendesha (Build Own and Operate - BOO). Mauzo ya umeme kwa TANESCO hayajumuishi gharama za uwekezaji. Kuhusu ujenzi wa mradi, Kamati ya Taifa ya Uwekezaji imepitia kwa mara nyingine vivutio vilivyooombwa na mwekezaji kwa lengo la kutafuta manufaa zaidi kwa Taifa katika mradi huo. Suala la umeme na vivutio litawasilishwa kwa mamlaka za maamuzi wakati wowote ili mradi uanze. Aidha, mwekezaji amekwisha wasilisha nchini fedha za fidia na amehakikishia Wizara kuwa yupo tayari kulipa fidia kwa watu watakaopisha mradi pindi apatapo Tangazo la Serikali (Government Notice - GN) kuhusu vivutio.

##### **(ii) Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO, Kibaha**

**142. Mheshimiwa Spika**, mradi unaojengwa katika Eneo la Viwanda la TAMCO, Kibaha lenye ukubwa wa ekari 232 utahusisha sekta za uunganishaji magari, viwanda vya nguo na mavazi na viwanda vya dawa za binadamu. Hadi Aprili, 2017, mgawanyo wa Eneo la Viwanda la TAMCO, Kibaha ulikuwa umekamilika. Katika mgawanyo huo, viwanda vya nguo na mavazi vimetengewa ekari 95, viwanda vya magari ekari 64 na eneo la ekari 73 limetengwa kwa ajili ya Sekta ya Viwanda vya Dawa za Binadamu na Vifaa Tiba. Wawekezaji waliokwisha jitokeza mpaka sasa ni pamoja na Kampuni ya *Global Packaging* walioanzisha kiwanda cha vifungashio na Kampuni ya Kuunganisha Matrika ya *URSUS*. Aidha, wawekezaji walio katika majadiliano ili kuwekeza katika eneo

hilo ni pamoja na Kampuni ya Magari ya TATA na Kampuni ya URSUS inayopanga kuunganisha mabasi hapa nchini.

**143. Mheshimiwa Spika**, katika eneo la ekari 95 lililotengwa kwa ajili ya viwanda vya nguo na mavazi katika eneo la Viwanda TAMCO, Wizara kupitia NDC inajadiliana na *Gatsby Africa* kupitia Kitengo cha Nguo na Mavazi (Textile Development Unit-TDU) kwa ajili ya kusaidia kuendeleza eneo kwa kuandaa Mpango Kabambe (*detailed Master Plan*) na kuvutia uwekezaji. Andiko la Makubaliano (MoU) tayari limetiwa saini kati ya Wizara na *Gatsby Africa*.

**144. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia NDC imekamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (Biolarvicides), *Tanzania Biotech Ltd* na uzalishaji umeanza. Ili kukamilisha mradi huo, Serikali kupitia Wizara ilitoa Shilingi bilioni 2.1 kulipia gharama za ukandarasi na madeni ya wafanyakazi. Aidha, NDC ilipata mkopo wa Shilingi bilioni 4.553 kutoka NSSF kama mtaji wa kuanza uzalishaji wa kibiashara. Uzalishaji ulianza mwezi Januari, 2017 na kufikia Aprili, 2017 lita 101,080 za Viuadudu zilikuwa zimeuzwa. Kati ya hizo, lita 100,000 ziliuzwa nchini Niger kwa Dola za Kimarekani 460,000 sawa na Shilingi bilioni 1.012; lita 440 zenye thamani ya Shilingi milioni 17.424 ziliuzwa kwa Taasisi ya Madaktari Wasio na Mipaka (Doctors Without Borders); lita 200 zenye thamani ya Shilingi milioni 2.64 ziliuzwa kwa Kampuni ya *Mabao Investment and General Pest Control*, na lita 440 zenye thamani ya Shilingi milioni 5.808 ziliuzwa kwa Halmashauri ya Mji wa Geita.

**145. Mheshimiwa Spika**, wakati uzalishaji wa Viuadudu ukiendelea, mazungumzo yanakamilishwa na Wilaya ya Mbogwe kununua lita 800 zenye thamani ya Shilingi 10,560,000 na Madaktari Wasio na Mipaka kununua lita 500 zenye thamani ya Shilingi 19,000,000. Aidha, juhudi zakutafuta soko la ndani na nje zinaendelea kwa kuhusisha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ikiwa ni utekelezaji wa Mkataba wa Manunuzi (Offtake Agreement) kati yake na NDC. Kampuni ya *LABIOFAM* imeonesha utayari wa kuuza Viuadudu vinavyozalishwa katika kiwanda hicho kwenye masoko yake katika nchi mbalimbali. Aidha, Kampuni

ya *Tanzania Biotech Ltd* inayozalisha Viuadudu husika imeelekezwa kuimarisha Kitengo cha Masoko ili kuweza kutangaza na kuuza bidhaa hiyo muhimu katika kupambana na ugonjwa wa malaria.

**(iii) Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka, Arusha**

**146. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Uchimbaji Magadi Soda unatekelezwa na Wizara kupitia NDC katika Bonde la Engaruka, Wilaya ya Monduli. Mradi unahusu ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha magadi soda tani milioni moja kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya viwanda hususan vya dawa, vioo na sabuni. Aidha, katika mwaka 2016/2017, utafiti wa kina wa maji safi (detailed hydrological study) kwa ajili ya matumizi ya kiwanda, usanifu wa miundombinu ya maji na utayarishaji wa *Bill of Quantities* (BoQ) vimefanyika. Taarifa ya *BoQ* inategemewa kuwasilishwa mwezi Juni, 2017.

**147. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia NDC imekutana na kampuni mbili kutoka China ambazo zimeonesha nia ya awali ya kuwekeza katika Mradi wa Magadi Soda wa Engaruka. Kampuni hizo ni *Inner Mongolia Berun Holding Company Ltd* ambayo ilitembelea mradi huo mwezi Julai, 2016 na *China National Complete Plants Import and Export Cooperation Ltd* iliyotembelea mradi husika mwezi Agosti, 2016. Katika ziara hizo, Kampuni hizo zilichukua sampuli za magadi soda kwa ajili ya utafiti wa kimaabara. Pia, makampuni hayo yalifanya ukaguzi wa reli na barabara kutoka Arusha hadi Tanga na Bandari ya Tanga ili kuwa na uhakika wa usafirishaji. Taarifa kuhusu nia ya kuwekeza katika mradi huo itapatikana pindi makampuni husika yatakapowasilisha mapendekezo yao. Aidha, upekuzi wa makampuni hayo unafanyika kupitia balozi zetu.

**(iv) Kiwanda cha Kutengeneza Matairi Arusha**

**148. Mheshimiwa Spika**, kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imefanya utafiti uliolenga kuangalia namna bora ya kufufua Kiwanda cha Matairi Arusha. Taarifa ya awali imebaini kuwa ili kiwanda hicho kiweze kuendelea mambo makuu manne

yanatakiwa kuzingatiwa. Kwanza, mitambo iliyopo ambayo ilifungwa kwenye miaka ya 60 ikiwa imetumika haifai kwa uzalishaji wa kiushindani. Pili, inatakiwa kufungwa mitambo inayotumia teknolojia ya kisasa itakayoweza kiwanda kufanya kazi kwa ufanisi na kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Tatu, kiwanda kipanuliwe ili kiweze kuzalisha matairi ya aina mbalimbali na kwa wingi ili kupata faida ya uzalishaji kwa wingi (economies of scale). Nne, kiwanda hicho kiendeshwe na Sekta Binafsi, Serikali ikiwa mbia kwa hisa zinazolingana na rasilimali za kiwanda zilizopo.

#### **4.3.2 Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa Ajili ya Mauzo Nje**

##### **(i) Bagamoyo SEZ**

**149. Mheshimiwa Spika**, mradi wa Bagamoyo SEZ unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya Kwanza itaendelezwa kwa ubia kati ya Kampuni ya *Merchants Port Holdings Company Limited* (CMPort) ya China na Mfuko wa Hifadhi ya Hazina wa Serikali ya Oman (State General Reserve Fund-SGRF). Awamu hiyo itahusisha eneo la hekta 3,000 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari (Sea Port) kwenye eneo la hekta 800 na uendelezaji wa Eneo Maalum la Viwanda (Portside Industrial City) kwenye eneo la hekta 2,200. Awamu hiyo inahusisha pia ujenzi wa miundombinu wezeshi (barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano) ili kuunganisha eneo la mradi na maeneo mengine ya nchi. Eneo linalobakia la hekta 6,800 litaendelezwa katika Awamu ya Pili itakayokwenda sambamba na awamu ya kwanza kwa kuzingatia Mpango Kabambe wa mradi.

**150. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza kasi ya ulipaji wa fidia kwa watu ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kupisha mradi wa Bagamoyo SEZ, tarehe 7 Desemba, 2016 Serikali iliamua sekta binafsi ipewe nafasi kubwa ya kutekeleza mradi huo ikiwepo kulipa fidia. Kufuatia maamuzi hayo, tarehe 30 Machi, 2017, wawekezaji waliwasilisha andiko la kuendeleza hekta 3,000. Eneo litakaloendelezwa na wawekezaji hao linajumuisha eneo ambalo halijalipiwa fidia.



Andiko hilo linapitiwa na wataalam wa Serikali kabla ya kuendelea na majadiliano kati ya Serikali na wabia hao.

**151. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa huduma muhimu zinafika katika eneo la mradi, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa miundombinu wezeshi ikiwemo barabara kutoka Tegeta hadi Bagamoyo na kutoka Bagamoyo hadi Mlandizi; mradi wa maji kutoka Bwawa la Kidunda hadi Bagamoyo; na Bomba la Gesi kutoka Tegeta hadi Bagamoyo. Aidha, maandiko ya miradi ya miundombinu wezeshi (barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano) kwa ajili ya kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo Jukwaa la Ushirikiano baina ya China na Afrika (FOCAC) yamekamilika.

#### **(ii) Kuendeleza Mradi wa Kurasini Logistic Centre**

**152. Mheshimiwa Spika**, eneo la Kurasini lina ukubwa wa ekari 62, ambapo kiasi cha fidia kilicholipwa ni Shilingi bilioni 101 kwa kaya 1,019. Eneo hilo limetangazwa kwa wawekezaji tarehe 20 Desemba, 2016 kupitia Gazeti la *Daily News*. Jumla ya makampuni matatu yameonesha nia ya kuendeleza eneo hilo. Taratibu za kumpata mwekezaji atakayeliendeleza kwa kujenga miundombinu pamoja na kuleta waendeshaji wa viwanda mbalimbali zinaendelea chini ya Mamlaka ya EPZ. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ inakamilisha mapendekezo mahsusi kuhusu utaratibu wa ubia utakaotumika kwa ajili ya maamuzi ya Serikali.

#### **(iii) Star City SEZ**

**153. Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya *Star City* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya Watanzania na Wasingapore inayojishughulisha na ujenzi wa maeneo ya uwekezaji wa viwanda (industrial parks) nchini, inaendeleza eneo la ekari 10,661 lililoko eneo la Kingolwira, Mkoa wa Morogoro. Kati ya eneo hilo, ekari 500 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu, ekari 100 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya rufaa na ekari 1,000 kwa ajili ya makazi ya wananchi wa Morogoro wanaopisha mradi huo. Eneo litakalobakia la ekari

9,061 ni mahsusi kwa utekelezaji wa mradi wenyewe. Kwa kuanzia Kampuni ya ubia itaweka miundombinu kwa ajili ya viwanda. Jiwe la msingi la kiwanda cha kwanza katika eneo hilo cha mavazi ya michezo cha *Mazava Fabrics Ltd* kitakachotumia eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 25,000 liliwekwa tarehe 19 Desemba, 2016. Kiwanda hicho kinategemewa kutoa ajira 7,000. Hata hivyo, mradi huo haukuanza kwa kasi ya kuridhisha kutokana na madai ya Manispaa ya Morogoro kutaka mradi utekelezwe baada ya Mpango Kabambe wa Mji wa Morogoro kukamilika, kutokuwepo kwa kituo kikubwa cha kupoozea umeme (Power Station) na uvamizi wa sehemu ya eneo la mradi.

#### **(iv) SEZ Zilizotangazwa**

**154. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Maeneo Maalum ya Uwekezaji (Special Economic Zone - SEZ) manane (8) yalikitidhi vigezo vya kuanzisha SEZ na kutangazwa. Maeneo hayo ni: *Manyara Special Economic Zone, Magnis Technologies (Tanzania) Ltd, Eliyafood Overseas Ltd, Texland Africa Ltd, Spincast Engineering Ltd, Mara Special Economic Zone, Kigamboni SEZ Co. Ltd* na *Nuts Depots and Plus Co. Ltd*. Uanzishaji wa maeneo hayo maalum ya uwekezaji utaongeza kasi ya ujenzi wa viwanda kutokana na faida za vivutio vinavyoendana na maeneo hayo.

#### **(v) Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**155. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za Serikali kuongeza ajira nchini, Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ kwa kushirikiana na wawekezaji na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi na Ajira) kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi ilibuni na kuanzisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa vijana juu ya stadi za uzalishaji viwandani. Mafunzo hayo yanahusu usanifu, ukataji na ushonaji wa mavazi yanayosafirishwa nje ya nchi na kuuzwa katika masoko ya kimataifa kama vile AGOA. Mpango wa mafunzo hayo umeanza kutekelezwa kwa Kiwanda cha *TOOKU Garments Ltd* kilichoko katika Eneo Maalum la Viwanda la Benjamin William Mkapa (BWM SEZ) lililopo Mabibo, Dar es Salaam na Kiwanda cha *Mazava*

*Fabrics* kilichopo Morogoro. Lengo ni kukuza na kuimarisha mfumo huo ambao unaunganisha fursa za mafunzo na ajira viwandani. Kwa sasa uwezo wa Kituo cha Mafunzo cha Mabibo ni kudahili vijana kati ya 300 hadi 400 kila baada ya miezi mitatu na Kituo cha Morogoro ni kudahili vijana wasiopungua 200. Mpaka sasa jumla ya vijana 2,000 wamepata mafunzo hayo ambapo Kiwanda cha *TOOKU Ltd* kimefundisha vijana 1,600 na *Mazava* vijana 400.

**156. Mheshimiwa Spika**, lengo la mafunzo hayo ni kukidhi mahitaji na kwenda sambamba na kasi ya uwekezaji wa viwanda vya Tanzania hususan Kiwanda cha *TOOKU Garments Ltd* kilichopo Mabibo na *Mazava Fabrics* kilichopo Morogoro. Viwanda hivyo viwili vitaongeza idadi ya wafanyakazi kufikia 7,000 kila kimoja ambapo kwa sasa idadi ya wafanyakazi walioajiriwa ni 2,000 kwa kila kiwanda. Aidha, uwepo wa wafanyakazi wengi wenye ujuzi na weledi katika Sekta ya Mavazi utavutia viwanda vya aina hiyo kuwekeza nchini. Mamlaka ya EPZ itaendelea kuanzisha na kuendeleza mfumo na utaratibu huo katika maeneo mengine yatakayoanzishwa kama *Special Economic Zone (SEZ)*.

#### **4.3.3 Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania**

**157. Mheshimiwa Spika**, maendeleo endelevu ya viwanda yanahitaji pia masuala ya utafiti na hususan katika kubuni teknolojia mpya na rahisi zinazotumika katika uzalishaji ubora unaokidhi masharti ya soko la ndani na nje. Katika mwaka 2016/2017, TIRDO imeendelea na taratibu za kukamilisha usimikaji wa mtambo wa kurejeleza taka za ngozi. Baada ya kukamilika usimikaji, TIRDO imeanza kutoa mafunzo kwa Sekta ya Ngozi kuhusu uhifadhi na urejelezaji (recycling) wa taka za ngozi kwa kuziongezea thamani na kuhifadhi mazingira. Mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalam yamefanyika kwa Afisa Mtafiti mmoja na mafundi mchundo wawili kwa lengo kujiandaa kuendesha mafunzo mara baada ya kusimika mtambo.

**158. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuhakikisha malighafi za hapa nchini zinatumika katika uzalishaji viwandani, TIRDO

kupitia maabara yake ya makaa ya mawe iliweza kupima na kutoa takwimu za ubora wa makaa ya mawe yanayopatikana nchini. Kupitia takwimu hizo, Serikali iliweza kumaliza mgogoro uliokuwepo baina ya wawekezaji wa viwanda vya saruji kikiwemo Kiwanda cha DANGOTE kuhusu ubora wa makaa ya mawe yanayopatikana nchini. Maabara hiyo ya makaa ya mawe ya TIRDO inatambulika kitaifa na imerasimishwa kuwa ndio maabara mahsusi katika kuainisha ubora wa makaa ya mawe nchini. Hivi sasa maabara hiyo imepewa jukumu la kubuni na kuboresha teknolojia ya briketi ya makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Tayari Wizara imeunda kamati inayowahusisha TIRDO, NDC na Nyumbu (TATC) kuanzisha kiwanda kikubwa cha briketi ya makaa ya mawe. Mara kiwanda hicho kitakapofanya kazi kitasaidia kupunguza athari ya utumiaji wa kuni na mkaa. Katika kutekeleza jukumu hilo, TIRDO inashirikisha Washirika wa kimataifa, miongoni mwao ni Ubalizi wa India kupitia taasisi ya CSIR – India, na Serikali ya Uturuki kupitia taasisi yake ya Utafiti ya Tubitak. TIRDO tayari imeshapata mwekezaji kutoka Uturuki kupitia taasisi ya Tubitak ambaye atawekeza kwenye teknolojia ya kuzalisha briketi.

**159. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuhaulisha teknolojia zitakazowezesha uanzishwaji wa viwanda, TIRDO kwa kushirikiana na wilaya ya Maswa inafanya tathmini juu ya teknolojia ya uzalishaji chaki iliyobuniwa na TIRDO na kuhaulishwa SIDO ili iweze kuboresha chaki zinazozalishwa ziweze kuwa katika ubora zaidi. Wilaya ya Maswa kupitia kiwanda chake cha uzalishaji chaki tayari imekwishaanza uzalishaji na kusambaza maeneo mbalimbali nchini. TIRDO pia inaongoza timu ya wataalamu kutoka Taasisi za Serikali zinazounda kamati ya kuanzisha viwanda vya pamba za mahospitali pamoja na maji ya dripu katika Mkoa wa Simiyu.

**160. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuimarisha ushiriki wa taasisi na wataalamu wa ndani katika Sekta ya Mafuta na Gesi (Wahandisi na Mafundi), TIRDO kwa kushirikiana na sekta binafsi imeanzisha program ya kutoa mafunzo maalum ya kuhakiki na kuwapatia vyeti tambuzi vya kimataifa (international certification) wanaofanya kazi za ufundi kama

vile kuchomelea, kuhakiki ubora wa maungio na kuimarisha usalama kazini. Mafunzo hayo yanalenga kuhakikisha kuwa ushiriki wa Watanzania (local content) katika sekta hiyo muhimu ikizingatiwa kuwa Taifa linatarajia kuendesha miradi mikubwa kama vile ya Bomba la Mafuta Ghafi toka Uganda mpaka Tanga. Sekta hiyo inahitaji wataalam walio hakikiwa (certified) na wenye umakini na weledi katika kufanya kazi. Mafunzo hayo yakitolewa hapa nchini yatasaidia kupunguza gharama za kupeleka wataalam nje ya nchi kupata mafunzo hayo.

#### **4.3.4 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo**

**161. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) limebuni na kuendeleza teknolojia zitakazowezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati. Teknolojia zilizobuniwa na kuendelezwa katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na mashine ya kutengeneza tofali zinazohifadhi joto (refractory bricks); jokofu litakalotumika kuhifadhi maiti au bidhaa mbalimbali; kiteketezi kidogo kinachobebeka (portable incinerator) kwa ajili ya zahanati na maabara za afya. TEMDO wamebuni mtambo wa kusindika na kusafisha mafuta ya kula na mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji. Vilevile, chini ya ufadhili wa REA imekamilisha usimikaji wa mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya upepo na jua katika Kituo cha Olduvai Gorge, Ngorongoro inayozalisha KW 20 (*Jedwali Na. 13*).

#### **4.3.5 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini**

**162. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia CAMARTEC kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeweza kutatua changamoto iliyopo kwenye upatikanaji wa mashine au vifaa vya kupandia, kupalilia, kuvunia na kuchakata mazao kabla ya kwenda sokoni au viwandani. Katika juhudi za kuondokana na changamoto hizo, CAMARTEC imeshirikiana na Kampuni ya *ELMI* kuboresha vipandio vya kutumia trekta (tractor-drawn planters) ambavyo sasa vinafanya kazi kwa ufanisi zaidi kwenye mikoa ya Arusha na Manyara. Pia

taasisi imeshirikiana na shirika lisilo la kiserikali la *BIORE* kutengeneza vipandio vya pamba vinavyokokotwa na ng'ombe kwa wakulima wa mkoa wa Simiyu. CAMARTEC kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Selian (SARI) imefanya majaribio ya mashine inayoendeshwa na trekta za matairi mawili (power tiller) za kupandia mazao.

**163. Mheshimiwa Spika,** CAMARTEC kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya *biogas* wa kujenga mitambo mikubwa katika Shule ya Sekondari Visitation Sanya Juu Mkoa wa Kilimanjaro, Sekondari ya Emboret na Mswakini Mkoa wa Manyara, Shule ya Msingi Mmasani iliyopo Dar es Salaam, na Gereza la Karanga Mkoani Kilimanjaro. Teknolojia hiyo pia imetumika kwenye ujenzi wa mtambo wa maji taka katika hospitali ya CCBRT na nyumba za kuishi za TBA Bunju B kupitia mafundi waliopata mafunzo CAMARTEC.

#### 4.3.6 Kampuni ya Mbolea Tanzania

**164. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Mbolea Tanzania (Tanzania Fertilizer Co. Ltd -TFC) iliendelea na jukumu lake la kusambaza mbolea nchini. Katika mwaka 2016/2017 Kampuni ilipewa jukumu la kusambaza mbolea yote iliyokuwa na ruzuku ya tani 32,394. Hadi tarehe 30 Aprili, 2017, jumla ya tani 27,500 sawa na asilimia 85 ya mbolea imesambazwa katika Halmashauri za mikoa 20 ya Iringa, Ruvuma, Njombe, Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Songwe, Mbeya, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Morogoro, Dodoma, Pwani, Mtwara, Kagera, Mara, Arusha, Singida. Usambazaji unaendelea katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro na Tanga. Kampuni hiyo pia imesambaza mbolea tani 1,753 ambayo haina ruzuku katika baadhi ya Mikoa hiyo. Hatua hiyo inafanya jumla ya mbolea iliyosambazwa na Kampuni ya TFC kuwa tani 29,253 hadi tarehe 30 Aprili, 2017.

**165. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya TFC imekuwa ikifanya majadiliano na Kampuni *Sirius Metals* ya Uingereza inayomiliki mashapo ya *Polyhalyde* ya Yorkshire, Uingereza. Nia ya majadiliano hayo ni kuanzisha kampuni ya ubia ya

kutengeneza mbolea za aina ya NPKs kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini na *Potash* kutoka Uingereza mbolea ambayo itakuwa na ubora wa hali ya juu. Kampuni ya TFC pia ilisaini Makubaliano ya Awali na Kampuni ya OCP ya Morocco tarehe 24 Oktoba, 2016 kwa ajili ya kununua mbolea za aina mbalimbali kabla ya uzalishaji haujaanza nchini.

#### **4.3.7 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo**

**166. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) ndio Taasisi ya Serikali yenye dhamana ya kuendeleza viwanda vidogo nchini. Chini ya dhamana hiyo, Shirika la SIDO linajikita zaidi katika kuwezesha Watanzania wenye nia ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo popote pale walipo. Aidha, katika mwaka 2016/2017 SIDO imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:-

##### **a) Uendelezaji na Uenezaji wa Teknolojia**

**167. Mheshimiwa Spika**, SIDO inamiliki vituo vya maendeleo ya teknolojia saba katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Lindi na Shinyanga. Vituo hivyo vinajihusisha na uendelezaji wa teknolojia na utengenezaji wa mashine na vipuli na kutoa huduma za kiufundi kwa wajasiriamali wadogo mijini na vijijini. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya teknolojia mpya 30 zimetengenezwa na kuboreshwa kupitia vituo vya SIDO vya uendelezaji teknolojia (Technology Development Centre-TDCs). Huduma za ushauri wa kiufundi zilitolewa kwa wajasiriamali 3,433. Juhudi za kutafuta teknolojia kwa ajili ya mahitaji ya wajasiriamali wadogo ziliendelea, jumla ya teknolojia 73 zilipatikana kwa ajili ya matumizi ya wajasiriamali wadogo. Teknolojia zilizosambazwa zililenga uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo, upunguzaji wa matumizi ya miti na mazao yake kama nishati, zana za kilimo, vifaa vya ujenzi, usindikaji wa ngozi na utengenezaji wa bidhaa zake, uchujaji wa asali na utengenezaji wa mishumaa, sabuni na useketaji. Teknolojia hizo zimesaidia kuongeza tija na kuimarisha ubora wa bidhaa za wajasiriamali.

## **b) Uanzishaji wa Miradi ya Viwanda Vidogo Vijijini**

**168. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kutoa huduma vijijini ili kuwawezesha wananchi walio wengi waweze kutumia fursa zilizopo. Mwelekeo wa utekelezaji ulilenga zaidi kuhakikisha kuwa kila wilaya inakuwa na bidhaa ya kuitambulisha kutokana na rasilimali zilizopo wilayani humo. Chini ya Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja (One District One Product – ODOP) viwanda vidogo vipya 161 ambavyo vilitengeneza ajira 1,098 katika wilaya mbalimbali vimeanzishwa mwaka 2016/2017. Pia, mkakati huo unatekeleza Sera ya Maendeleo ya Viwanda ambayo inalenga kusambaza viwanda hadi ngazi za vijiji.

## **c) Mafunzo**

**169. Mheshimiwa Spika**, SIDO imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali ikiwa ni moja ya chachu ya kuimarisha na kuendeleza shughuli za biashara na miradi ya uzalishaji. Mafunzo yaliyotolewa ni ya ujasiriamali; ujuzi maalum wa kiufundi katika uzalishaji mali na kuimarisha mbinu za kibiashara na uendeshaji wa miradi ya kiuchumi kwa walengwa hasa menejimenti, masoko, ubora wa bidhaa, mbinu za uzalishaji mali, na uongozi wa vikundi/vyama. Jumla ya wajasiriamali 5,750 kupitia kozi 230 wamepata mafunzo yaliyowawezesha kupata maarifa na stadi za kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali. Mafunzo hayo yalifanyika mikoa yote nchini.

## **d) Ushauri**

**170. Mheshimiwa Spika**, jumla ya wajasiriamali wahitaji 8,911 walipatiwa huduma za ushauri katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na uendelezaji wa biashara na shughuli za uzalishaji. Aidha, katika kukuza na kuchochea viwanda vidogo jumla ya wajasiriamali 3,433 waliweza kupatiwa ushauri wa ki-ufundi na maendeleo ya teknolojia. Ushauri ulilenga zaidi kupunguza ama kumaliza matatizo ya biashara ya wajasiriamali, kuwawezesha kuweka mipango yao ya biashara vizuri na kuitekeleza, kudhibiti ubora wa bidhaa, utengenezaji na utunzaji wa mitambo.



**e) Huduma za Masoko**

**171. Mheshimiwa Spika,** SIDO huwaelimisha wajasiriamali mbinu za kukabiliana na changamoto za masoko. Wajasiriamali husaidiwa kutambua hali na mahitaji ya soko kutokana na tafiti zilizofanyika na pia hushirikishwa katika maonesho mbalimbali ya bidhaa na huduma zinazoandaliwa na SIDO au Taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi. Jumla ya maonesho matatu (3) ya kanda yaliyowashirikisha wajasiriamali 603 yaliandaliwa na SIDO na kuwawezesha washiriki kufanya mauzo taslimu na oda ya shilingi milioni 237.7. Aidha, vituo vya habari vya SIDO vimeweza kutoa habari za fursa mbalimbali kwa wajasiriamali 2,732. Huduma hiyo imewawezesha wajasiriamali licha ya kupata taarifa mbali mbali za biashara kutangaza bidhaa zao kupitia 'website' ya SIDO. Pia Shirika liliendelea kujenga uwezo wa wajasiriamali kupata na kutumia taarifa za masoko kupitia TEHAMA, ambapo jumla ya wajasiriamali wadogo 3,535 walinufaika na huduma hiyo.

**f) Huduma za Fedha**

**172. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutoa mikopo kutoka Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara na Wananchi (NEDF), na Mfuko wa Dhamana kwa Wajasiriamali Wadogo (*Credit Guarantee Scheme*.) Jumla ya wajasiriamali 2,593 walipewa mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 3.92 na mikopo hiyo iliwezesha kupata ajira za watu 9,424. Katika mikopo iliyotolewa asilimia 48.4 ilitolewa kwa wanawake na asilimia 33 ya mikopo ilitolewa kwa miradi iliyo vijijini kupitia NEDF. Aidha, Mfuko wa Dhamana kwa Wajasiriamali Wadogo uliwezesha wajasiriamali tisa kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 215 katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro na Singida.

**g) Viatamizi**

**173. Mheshimiwa Spika,** mpango wa viatamizi hutumika kuwalea wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia,

mawazo na bidhaa mpya kwa kuwajengea miundo mbinu ya kisasa na kuwapatia ushauri ili waweze kukuza ubunifu wao na hatimaye kunufaisha jamii. Katika mwaka 2016/2017, Mkakati wa kuendeleza ubunifu wa teknolojia, mawazo na bidhaa mpya kwa wananchi umeendelezwa kupitia viatamizi. Wajasiriamali wenye ubunifu wamejengewa uwezo kwa kuwezesha kupata mahali pa kufanyia kazi, kupewa miundombinu ya kisasa na kuwapatia ushauri ili waweze kukuza ubunifu wao na hatimaye kuzalisha bidhaa. Jumla ya bidhaa 35 zilibuniwa na kutengenezwa zikihusisha usindikaji wa vyakula, nishati jadidifu, bidhaa za ngozi, na mashine za aina mbalimbali. Aidha, SIDO imeendelea kufanya kazi na Washirika wa Maendeleo ili iweze kupeleka huduma zake kwa wananchi wengi zaidi. Kwa ufadhili wa UNIDO, SIDO imeweza kukamilisha kongano ya ubanguaji wa korosho iliyopo katika Mtaa wa Viwanda wa SIDO Mkoani Mtwara.

#### **h) Kuboresha Huduma Zitolewazo na SIDO**

**174. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha 2016/2017, SIDO imetengeneza mifumo mbalimbali ili kuimarisha usimamizi wa kazi za shirika ambayo ni:

- (i) Mfumo wa TEHAMA wa kusimamia taarifa za shirika (Management Information System) ;
- (ii) Kuimaimarisha Mfumo wa kusimamia mfuko wa kuendeleza wajasiriamali na mahesabu ya shirika (Loan Performer ) katika shughuli za uhasibu na mikopo;
- (iii) Kutengeneza Mfumo wa kuratibu utendaji wa vituo vya kuendeleza teknolojia (Manufacturing); na
- (iv) Kuanza utengenezaji wa Tovuti ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO *Web Portal*).

#### **4.3.8 Shirika la Viwango Tanzania**

**175. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Viwango limeendelea na

udhibiti wa ubora wa bidhaa kutoka nje ya nchi kwa kufanya ukaguzi wa bidhaa hizo katika nchi zinakotoka. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, jumla ya vyeti vya ubora (*Certificate of Conformity- CoCs*) 23,606 vimetolewa sawa na asilimia 73 ya malengo ya kutoa jumla ya vyeti 32,000 vya ubora wa bidhaa zitokazo nje ya nchi ikilinganishwa na vyeti 29,872 vilivyotolewa mwaka 2015/2016. Aidha, Shirika la Viwango limeendelea kushirikiana na mashirika mengine ya Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake na limesaini hati ya makubaliano (MoU) na Tume ya Ushindani (FCC) Februari, 2017, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) mwezi Novemba, 2016 na liko katika hatua za kufikia makubaliano ya kusaini hati ya makubaliano na SIDO.

**176. Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kutekeleza majukumu yake, TBS inashirikiana na taasisi mbalimbali za serikali kama vile NIT, TPA, PBPA, TIRDO na BRELA. Katika kuimarisha udhibiti ubora, Shirika la Viwango Tanzania kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na taasisi zingine za serikali kama TRA, GCLA, EWURA, TanTrade, SUMATRA na NEMC limefanya ukaguzi wa kushtukiza sokoni ili kuhakikisha kuwa bidhaa hafifu, zilizo chini ya kiwango na ambazo si salama kwa mazingira pamoja na afya ya mlaji zinaondolewa sokoni.

**177. Mheshimiwa Spika**, TBS kwa kushirikiana na Taasisi nyingine waliteketeza tani 6.9 ya nguo za ndani zilizotumika, tani 1.2 za nyama na soseji, lita 106,909 za vilainishi vya injini (lubricants), betri 244 za magari, betri 1430 za sola. Vilevile, Shirika lilifanya ukaguzi wa mabati kanda ya ziwa na pwani kwa waagizaji na watengenezaji (viwanda 24), zoezi ambalo lilifanikisha kuteketeza mabati 84,000 ambayo hayakukidhi viwango. Takribani lita 94,869 za vilainishi vya injini na Bendera za Taifa kтони 200 zilirudishwa katika nchi zilikutoka pamoja na aina 11 za pombe kali kтони 123,942 zilizofungashwa kwenye vifungashio vya plastiki vilizuliwa kuingia sokoni.

**178. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2017, leseni 179 za nembo ya ubora ya TBS zimetolewa, sawa na 81.4% ya lengo la kutoa leseni 220 kwa mwaka 2016/2017. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 42 zilitolewa kwa wajasiriamali

wadogo kwa bidhaa za korosho, maji ya kunywa, mafuta ya alizeti, mvinyo, mikate, rosella, siagi ya karanga, jemu, hiliki, pilipili manga, unga wa soya, unga wa mahindi, kahawa, mafuta ya kujipaka, chaki, sabuni ya maji, sabuni ya kuogea, mabati, vigae, simenti na grisi. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo nchini kwa kutumia fedha za ndani na msaada wa Mfuko wa Maendeleo wa Ulaya (EDF). Hadi kufikia Machi, 2017, mafunzo yalitolewa kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wadau mbalimbali wapatao 1,523 wa sekta ndogo za viungo, mbogamboga na matunda, asali, alizeti pamoja na waagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi na mawakala wa forodha. Wajasiriamali hao walitoka katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Singida na Tabora. Aidha, mafunzo hayo ambayo yaliwalenga zaidi wajasiriamali wadogo na wadau mbalimbali yalijikita zaidi katika dhana nzima za kuzingatia mifumo bora ya kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kupata masoko pamoja na kusimamia ubora wa bidhaa hizo.

**179. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili 2017, jumla ya mitambo 4,283 ilifanyiwa ugezi ikiwa ni sawa na asilimia 57.1 ya lengo la mwaka la kufanyia ugezi wa mitambo 7,500. Katika kipindi hicho, Shirika limeandaa viwango 173 katika kilimo, chakula, uhandisi na vifungashio, sawa na asilimia 57.7 ya lengo la kutayarisha viwango 300 kwa mwaka. Shirika pia liliendelea kusimamia viwango vya kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora.

**180. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya sampuli 11,832 zilipimwa katika maabara mbalimbali za Shirika kwa lengo la kuhakiki ubora wake, hii ni sawa na 157.8% ya lengo la kupima sampuli 7,500 kwa mwaka. Ongezeko hili limesababishwa na Shirika kuimarisha usimamizi na udhibiti wa ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa nchini hususan Bandari ya Dar es Salaam. Pia, kufuatia makubaliano na TRA kutumia mfumo wa TANCIS kubaini mizigo inayopitia bandarini hali ya udanganyifu uliokuwa ukifanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu wakati wa kutoa mizigo imepungua. Juhudi hizi ziliongeza idadi ya sampuli za kupima na hivyo kuongeza mapato ya

Shirika ambapo kufikia mwezi Machi 2017, Shirika lilivuka lengo kwa kukusanya asilimia 126 ya lengo la makusanyo ya mwaka mzima.

**181. Mheshimiwa Spika**, Shirika liliendelea kudumisha umahiri katika maabara zake nne ambazo zilishapata vyeti vya umahiri kwa kukaguliwa na *Southern African Development Community Accreditation* (SADCAS) tarehe 2 hadi 4 Novemba, 2016. Maabara hizo ni maabara ya ugezi, kemia, chakula na nguo. Aidha, mipango ya kupanua wigo wa umahiri ili kuongeza kiwango cha upimaji (*tests and matrices*) ulifanyika. Halikadhalika, miongozo ya ubora (Quality manuals) kwa kila maabara iliandikwa na kuiasili katika maabara zote za Shirika. Maabara ya uhandisi Ujenzi (Building and Construction) iko tayari kutuma maombi ya kupata umahiri. Vilevile, maabara ya uhandisi umeme na maabara ya uhandisi mitambo zipo katika hatua za kuhakikiwa uwezo wao zikilinganishwa na maabara nyingine katika upimaji (proficiency testing) kabla ya kutuma maombi ya kupatiwa cheti cha umahiri. Shirika la Viwango Tanzania linafanya juhudi za kuhakikisha maabara za uhandisi umeme, uhandisi mitambo, uhandisi ujenzi na vifungashio zinapata umahiri.

**182. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya vyeti vya ukaguzi wa magari 24,634 vimekwishatolewa, sawa na asilimia 61.6 ya malengo ya vyeti 40,000. Aidha, kati ya magari hayo yaliyokaguliwa, magari 1,381 yalikaguliwa upya baada ya matengenezo (failed and re-tested after repair) na magari 29 yalikataliwa baada ya kushindwa kukidhi matakwa ya viwango vya ubora.

**183. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi, 2017, Shirika lilifungua ofisi katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Mbeya. Shirika pia limefungua ofisi mbili katika mipaka ya Tunduma na Kasumulo. Shirika limeimarisha vituo vilivyopo kwa kuongeza watumishi kutoka mmoja hadi wawili kwa kila kituo. Aidha, Shirika liko katika mpango ya kufungua ofisi katika mikoa ya Mtwara na Dodoma kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2016/2017.

**184. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi, 2017, Shirika lilifanikiwa kufungua ofisi mbili katika mipaka ya Tunduma na Kasumulo. Shirika halikufungua ofisi ya Mtambaswala kutokana na uhaba wa watumishi katika Shirika. Aidha, shirika liliimarisha vituo vilivyokuwepo kwa kuongeza watumishi kutoka mmoja hadi wawili kwa kila kituo. Katika kipindi hicho, Shirika lilifanikiwa kufungua ofisi katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Mbeya. Aidha, Shiriki liko katika mpango wa kufungua ofisi katika mikoa ya Mtwara na Dodoma kabla ya mwisho wa mwaka 2016/2017.

#### **4.3.9 Chama cha Hakimiliki Tanzania**

**185. Mheshimiwa Spika**, hadikufikia Machi 2017, COSOTA imesajili wanachama (Kampuni, Vikundi na watu binafsi) wapatao 376 ikilinganishwa na wanachama 283 mwaka 2015/2016. Pia, imesajili kazi 2,074 ikilinganishwa na kazi 1,586 mwaka 2015/2016. Aidha, jumla ya Hati ya Uthibitisho wa Kazi (clearance certificate) 716 zilitolewa ikilinganishwa na hati 356 mwaka 2015/2016. Ongezeko la usajili kwa mwaka 2016/2017 ukilinganishwa na mwaka 2015/2016 limetokana na elimu iliyotolewa sambamba na uhamasishaji uliofanyika. Vilevile, katika kipindi hicho, COSOTA imekusanya mirabaha ya Shilingi 130,646,678.30 na kutoa leseni 482 kwa matumizi ya maonesho kwa umma na utangazaji. Makusanyo ya mwaka 2016/2017 yameongezeka ukilinganisha na mwaka 2015/2016 kutokana na kuweza kufika kwenye maeneo ambayo awali hayakuwa yamefikwa hususan katika Mkoa wa Dar es Salaam. Katika makusanyo hayo, asilimia 70 hugawanywa kwa wasanii, asilimia 30 hutumika kwa uendeshaji wa shughuli za COSOTA. Makusanyo ya Julai hadi Disemba 2016 ambayo yalikuwa Shilingi. 86,979,997 yaligawiwa mwezi Februari 2017 na makusanyo ya Januari hadi Juni 2017 yatagawiwa mwishoni mwa mwezi Juni au Julai 2017.

**186. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia COSOTA imeendelea kusuluhisha migogoro ya hakimiliki na hakishiriki ambapo migogoro 9 kati ya migogoro 26 imeshughulikiwa. Kesi nyingine za hakimiliki na hakishiriki za jinai na za madai zilizofunguliwa na Jamhuri au wadau wenyewe zinaendelea

katika mahakama mbalimbali ndani na nje ya Dar es Salaam. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara kupitia COSOTA imefanya ukaguzi wa kazi za sanaa zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Manyara na Mwanza.

**187. Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa urasimishaji wa kazi za filamu na muziki unasimamiwa kwa ushirikiano wa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Habari Utamaduni, Michezo na Wasanii. Kwa kupitia taasisi zake (Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Chama cha Hakimiliki na Hakishiriki Tanzania (COSOTA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Bodi ya Filamu imeandaa utaratibu wa pamoja wa kurasimisha kazi za filamu kwa wamiliki wa kazi za filamu na muziki au waliopewa mamlaka ya kuzalisha na kusambaza kazi za filamu na muziki zenye stempu za TRA baada ya kupata uthibitisho toka taasisi zilizotajwa hapo juu. Matumizi ya Stempu yanarasimisha uuzwaji wa CD, DVD na kanda ili kukusanya kodi, kuzuia na kupunguza uharamia wa kazi za sanaa. Matumizi ya stempu pia husaidia katika kutofautisha kazi zilizo halali na zile zisizo halali. Aidha, kutokana na ushirikiano huo, takwimu za mwaka 2016/2017 kwa operesheni moja ya mwaka 2017 zimekamatwa kazi zaidi ya 1,964,605. Ongezeko hilo limetokana na ushirikiano wa Kamati ya Urasimishaji kwa Usimamizi iliyoongozwa na kuratibiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa.

#### **4.3.10 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania**

**188. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ina jukumu la kuendeleza biashara ya ndani na ya nje kwa kuendeleza bidhaa (product development), masoko, kuwezesha biashara, kutoa taarifa za biashara na ushauri kuhusu masuala ya sera za biashara. Katika jitihada za kuendeleza bidhaa za ngozi, TanTrade kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) Kampasi ya Mwanza iliratibu mafunzo ya uboreshaji wa ngozi katika hatua mbalimbali za mnyororo wa thamani kuanzia uchinjaji, uchunaji, usindikaji na utengenezaji wa

bidhaa za ndani. Mafunzo hayo yalifanyika Mkoani Kilimanjaro ambapo washiriki 51 wakiwemo wafanyabiashara, maafisa ugani wa Manispaa na Kata, wasimamizi wa machinjio, wasindikaji na watengenezaji wa bidhaa za ngozi walishiriki mafunzo hayo.

**189. Mheshimiwa Spika**, kulingana na takwimu za Shirika la Chakula Duniani (FAO), Tanzania huzalisha tani 34,000 za asali kwa mwaka ikiwa ni ya pili barani Afrika baada ya nchi ya Ethiopia. Uzalishaji wote ni asilimia 24.6 ya uwezo wake wa uzalishaji. Changamoto za sekta ya asali ni pamoja na uzalishaji wa asali yenye ubora, vifungashio na masoko ya uhakika. Ili kutatua changamoto hizo, TanTrade kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Chuo cha Nyuki Tabora, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) na Taasisi ya *Singida Youth Entrepreneurs Consultancy and Cooperative Society* (SYECCOS) imeratibu mafunzo ya uzalishaji, usindikaji, ufungashaji na biashara ya asali kwa kuzingatia mahitaji ya soko ndani na nje ya nchi. Jumla ya wadau 197 kutoka mikoa ya Katavi, Singida na Tabora wamepeva mafunzo kwa vitendo kwa kutembelea na kutumia mitambo iliyopo SIDO-Singida, Chuo cha Nyuki Tabora na Shamba la Nyuki la Iyungi (Iyungi Bee Farm).

**190. Mheshimiwa Spika**, TanTrade iliandaa mafunzo ya ujasiriamali kuhusu ubora na ufungashaji wa bidhaa za viungo. Mafunzo yalitolewa kwa wazalishaji 202 waliowakilisha vikundi 45 vya wakulima na wafanyabiashara wa viungo kutoka Halmashauri za Wilaya za Morogoro Vijijini (Matombo), Mvomero (Nyandira) na Kilosa (Malolo). Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wazalishaji na wafanyabiashara wa viungo na malimbichi nchini kuongeza ubora wa bidhaa, kujua mbinu za namna ya kuongeza thamani na kutumia vifungashio sahihi ili kukidhi ushindani katika soko. Mathalani, mahitaji ya viungo katika soko la Ulaya ni wastani wa tani 750,000 kwa mwaka. TanTrade inahamasisha na kuunganisha wazalishaji wa viungo ili



kuwezesha Tanzania kuuza wastani wa tani 100,000 kwa mazao ya pilipili manga, tangawizi kavu na mdalasini.

**191. Mheshimiwa Spika**, TanTrade iliandaa mafunzo ya mbinu za uzalishaji, ubora, ufungashaji na masoko kwa wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti, Ufuta, Nazi na Mbogamboga Wilayani Ruangwa na Masasi. Mafunzo yalitolewa kwa watu 89 ambao ni wawakilishi wa vikundi mbalimbali vya wasindikaji, wakulima na wafanyabiashara katika sekta hiyo ndogo. Mikoa ya Lindi na Mtwara huzalisha wastani wa tani 50,000 za ufuta na alizeti kwa mwaka. Hivyo mafunzo hayo yalilenga kuhamasisha uongezaji thamani mazao hayo ili kuongeza uzalishaji. Mahitaji ya ufuta na alizeti kwa soko la ndani ni mara mbili ya uwezo wa kuzalisha mazao hayo.

**192. Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza soko la ndani na nje, TanTrade imefanya utafiti wa mazao ya ufuta na mbaazi ili kuweza kubaini hali halisi ya uzalishaji, ubora, vifungashio na matumizi ya vipimo sahihi. Utafiti ulisaidia kubaini bidhaa ambazo zinahitajika katika soko na kuendeleza masoko hayo kupitia mnyororo mzima wa thamani ili kuhamasisha uongezaji wa thamani katika mazao hayo. Kutokana na utafiti huo TanTrade imepanga kutoa mafunzo kwa wakulima katika mikoa ya Lindi na Mtwara, kuratibu upatikanaji wa mbegu kwa vikundi vya wakulima ili kukidhi mahitaji ya masoko na kutathmini mifumo ya masoko ya ufuta ikiwa ni pamoja na kuondoa madalali ambao ni kikwazo kikubwa kwa mkulima mdogo.

**193. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2016 TanTrade iliratibu Maonesho ya 40 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) 2016 yaliyofanyika katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. Julius K. Nyerere, Barabara ya Kilwa kuanzia tarehe 28 Juni hadi tarehe 8 Julai, 2016. Jumla ya makampuni 2,500 yalishiriki katika Maonesho hayo, ukilinganisha na makampuni 2,302 yaliyoshiriki katika Maonesho ya 39 mwaka 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.6. Kati ya makampuni yaliyoshiriki, 501 ni washiriki kutoka nje ya nchi na 1,999 ni washiriki kutoka ndani zikiwemo Wizara sita (6) na Taasisi za Serikali thelathini na saba (37).

**194. Mheshimiwa Spika**, maonesho hayo yalishirikisha jumla ya nchi 30 za kigeni ambazo ni Afrika Kusini, Australia, Bulgaria, Brazil, China, Ghana, Ufaransa, India, Indonesia, Italia, Iran, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Malawi, Mauritius, Misri, Msumbiji, Pakistani, Singapore, Syria, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Bulgaria, Rwanda, Sudani ya Kusini, Urusi na Vietnam. Ushiriki huu ni sawa na ongezeko la nchi tano ikilinganishwa na mwaka 2015 ambapo jumla ya nchi 25 zilishiriki. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za uhamasishaji Maonesho kupitia Balozi za Tanzania nje ya nchi na Balozi zinazowakilisha Nchi zao hapa Nchini.

**195. Mheshimiwa Spika**, TanTrade pia iliandaa mikutano baina ya wafanyabiashara "B2B" kuanzia tarehe 02 – 06 Julai, 2016 ambapo jumla ya wafanyabiashara wa ndani 200 na 15 kutoka nje ya nchi walikutana. Lengo kuu lilikuwa kuwaunganisha wazalishaji na wanunuzi mbalimbali katika sekta za ufugaji wa kuku, biashara ya maziwa, ufuta na asali; mbogamboga, matunda, alizeti na korosho. Katika mkutano huo, mikataba ya mauzo isiyofungani yenye thamani ya Shilingi. 320,000,000 ilisainiwa.

**196. Mheshimiwa Spika**, TanTrade iliandaa Maonesho ya Kwanza ya Viwanda vya Tanzania yaliyofanyika katika Uwanja wa Maonesho wa Mwalimu J. K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam kuanzia tarehe 7 – 11 Desemba, 2016. Maonesho hayo yalishirikisha jumla ya Taasisi 16 za Serikali zikiwemo Wizara na Mashirika ya Umma; viwanda vikubwa na vya kati 80 na Taasisi 3 za Fedha. Katika Maonesho hayo, viwanda vidogo vipatavyo 340 vilishiriki chini ya uratibu wa Taasisi zinazoweza Wajasiriamali. Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) SIDO - Taasisi ya SIDO iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali 80 katika Banda lililotengwa kwa ajili ya Viwanda vidogo vilivyopo chini ya SIDO;

(ii) TALEPA - Taasisi ya TALEPA iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali 23 wenye viwanda vya ngozi;

(iii) TAFOPA - Taasisi ya TAFOPA iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali 30 wenye viwanda vya usindikaji wa vyakula; na

(iv) Kijani Kibichi - Taasisi ya Kijani Kibichi iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali 200 wenye viwanda vidogo kwenye sekta za kilimo, maliasili, uvuvi, ufugaji na sanaa za mikono.

**197. Mheshimiwa Spika**, TanTrade ilishiriki katika Maonesho ya SIDO yaliyofanyika Mkoani Tabora kuanzia tarehe 7 hadi 12 Septemba, 2016, Maonesho ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika Mbeya kuanzia tarehe 27 Septemba hadi 3 Oktoba, 2016 pamoja na Maonesho ya Kanda ya Pwani yaliyofanyika Wilayani Bagamoyo kuanzia tarehe 26 Oktoba hadi 30 Oktoba 2016. Lengo kuu la ushiriki wa Mamlaka katika Maonesho hayo ni kutangaza huduma mbalimbali za TanTrade kwa wananchi. Aidha, TanTrade kupitia maonesho hayo ilifanya tathmini ya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wenye viwanda vidogo ili kubaini hatua za kuchukua kwa ajili ya kuendeleza bidhaa zao.

**198. Mheshimiwa Spika**, TanTrade ilisimamia Maonesho na semina ya ufugaji kuku na ndege "Tanzania Poultry Show" yaliyofanyika katika Hoteli ya *Blue Pearl* kuanzia tarehe 7 hadi 8 Oktoba, 2016. Maonesho hayo yaliandaliwa na Umoja wa Watotoleshaji wa Vifaranga vya Kuku na Ndege Wanaofugwa (TPBA) Tanzania "Poultry Breeders Association" ambayo yalitoa fursa na kuwakutanisha wadau mbalimbali katika kujenga na kutengeneza mtandao wa biashara.

#### **4.3.11 Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala**

**199. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, makampuni 22 yalisajiliwa kutumia stakabadhi za ghala na ghala 28 zilitumika katika kuhifadhi mazao ya korosho, kahawa, mpunga na mahindi. Bodi ya Kusimamia Stakabadhi za Ghala kwa kushirikiana na wadau ilirejesha matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa zao la korosho katika Wilaya ya Tunduru ambapo kilo 15,301,004 za korosho zimekusanywa

na kuuzwa kupitia Mfumo katika msimu huu wa 2016/2017 ukilinganisha na kilo 7,394,705 zilizokusanywa na kuuzwa katika msimu wa 2011/2012 ambao ndio ulikuwa msimu wa mwisho kuuza kupitia Mfumo wa Stakabadhi. . Aidha, mafunzo kwa wadau wakuu wa mfumo yalitolewa kwa njia ya semina kwa kushirikiana na Taasisi za fedha za NMB PLC Ltd, CRDB PLC Ltd, Baraza la Nafaka la Afrika Mashariki (EAGC), Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi za Mazao.

**200. Mheshimiwa Spika**, kuundwa kwa Kamati za Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuatia marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi za Ghala Na. 10 ya mwaka 2005 yaliyofanyika mwaka 2015 kumeongeza ufanisi katika kusimamia mfumo wa stakabadhi za ghala msimu wa 2016/2017. Bei ya zao la korosho kwa wakulima imeongezeka hadi wastani wa Shilingi 3,400.00 kwa kilo ikilinganisha na Shilingi 2,350.00 kwa kilo msimu wa 2015/2016 ikiwa ni ongezeko la asilima 44.6. Usimamizi huo pia umeongeza kiwango cha korosho kilichokusanywa na kuuzwa kupitia mfumo wa stakabadhi kufikia tani 249,912.00 ukilinganisha na tani 155,244 zilizokusanywa msimu wa 2015/16. Aidha, ufanisi wa utendaji wa Waendesha Ghala umezidi kuimarika kwa kupungua kwa wastani wa upotevu kutoka 0.072% kwa msimu 2015/2016 hadi kufikia 0.0024% kwa msimu wa 2016/17.

**201. Mheshimiwa Spika**, katika kuhamasisha uanzishwaji wa soko la bidhaa, Bodi ya Kusimamia Stakabadhi za Ghala kwa kushirikiana na Mamlaka ya Masoko na Mitaji (CMSA), imetoa mafunzo kwa wadau wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Singida na Dodoma. Mafunzo hayo pia yalitolewa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kanda ya Kusini ambao walipatiwa mafunzo ya uanzishwaji wa soko la bidhaa. Aidha, Bodi kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia imeanzisha mfumo wa kieletroniki wa utoaji wa taarifa kati ya wadau ili kufanikisha uanzishwaji wa minada ya kieletroniki ya soko la bidhaa. Aidha, Kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Greenwich na ufadhili wa Umoja wa Ulaya pamoja na *African Rural & Agricultural Credit Association (AFRACA)* Bodi iliandaa mafunzo ya Mfumo wa

Stakabadhi kwa washiriki 25 kutoka nchi za Nigeria, Ghana, Zambia, Msumbiji na Kenya yalifanyika Mkoani Arusha.

#### 4.3.12 Tume ya Ushindani

**202. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Ushindani ina jukumu muhimu la kulinda ustawi wa viwanda vya ndani kwa kuzuia bidhaa bandia kuingia katika soko la ndani. Wawekezaji katika viwanda wa ndani na wanaotoka nje ya nchi hufanya uwekezaji baada ya kujiridhisha kuwa bidhaa watakazozalisha zitalindwa na sera za ushindani wa haki. Hivyo, Tume ya Ushindani ni Taasisi muhimu katika maendeleo ya viwanda nchini. katika mwaka 2016/2017, Tume ya Ushindani imeendelea kulinda na kuendeleza ushindani katika soko. Jumla ya mashauri 25 ya mikataba ya miungano ya makampuni yamefanyiwa mapitio ili kubaini kama miungano hiyo inaweza kufifisha ushindani katika soko na uchumi kwa ujumla. Jumla ya malalamiko 22 yamefanyiwa uchunguzi, kati ya hayo malalamiko 20 yameamuliwa na uchunguzi unaendelea kwa malalamiko mawili. Aidha, katika kumlinda na kumtetea mlaji, malalamiko 15 ya walaji yamepokelewa, malalamiko 13 yametatuliwa kwa mlaji kurudishiwa fedha, kupatiwa bidhaa nyingine au kutengenezewa bidhaa. Malalamiko mawili yako kwenye majadiliano.

**203. Mheshimiwa Spika,** katika kushughulikia uondoaji wa mikataba inayomkandamiza mlaji anaponunua bidhaa au huduma (standard form consumer contracts); kanuni zimeandaliwa na kuwekwa kwenye tovuti ya Tume. Notisi imeshatolewa kuwa, uwasilishaji wa mikataba hiyo kwa uhakiki umeanza tangu Januari, 2017. Uchunguzi wa awali pamoja na uandaaji wa notisi ya kesi moja inayohusu kuondolewa/ kutengenezwa kwa magari yaliyookuwa na hitilafu vimekamilika. Aidha, uchunguzi katika makampuni mawili ya magari kuhusu ubovu uliokwishagundulika kimataifa unaoweza kuhatarisha maisha ya mtumiaji unaendelea.

**204. Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti bidhaa bandia, ukaguzi bandarini na bandari kavu (ICDs) Dar es Salaam

uliwezesha kukamatwa kwa makontena 46 yaliyokuwa na bidhaa bandia. Wahusika waliadhibiwa kulingana na Sheria ya Alama za Bidhaa (merchandise Mark Act, 1963) kama ilivyorekebisha na zoezi hilo ni endelevu. Vilevile, Tume ilifanya kaguzi 12 za kushtukiza katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Shinyanga na Dar es Salaam ambapo watuhumiwa 29 walikamatwa wakiuza bidhaa bandia kinyume na Sheria. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na nyembe, viatu, pombe kali, dawa za kung'arisha viatu, dawa za kuuwa waduu na simu za viganjani.

**205. Mheshimiwa Spika**, Tume inashirikiana na Wizara kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji. Andiko la kitaalamu (Concept Note) pamoja na Hadiduzu Rejeazimeandaliwailikumtafuta Mshauri Mwelekezi kufanya utafiti na kuandaa Rasimu ya Sera hiyo. Aidha, marekebicho ya sheria ya ushindani ambayo yalisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 2015 na kurejeshwa kwa mapitio zaidi yameandaliwa na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

#### **4.3.13 Baraza la Ushindani**

**206. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2016/2017, Baraza limeendelea kusikiliza mashauri yatokanayo na mchakato wa ushindani wa biashara na udhibiti katika sekta za nishati na maji, usafirishaji na mawasiliano. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Baraza lilikua na jumla ya kesi za rufaa 12 na maombi 26 na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa 38. Katika kipindi hicho, Baraza liliweza kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri 14 na mashauri 24 yanaendelea na yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Baraza linaendelea kupokea mashauri mapya na kusikiliza mashauri yaliyobaki. Aidha, Baraza limeendelea kuwapatia mafunzo watumishi wake katika jitihada za kuboresha utendaji wao na kuwaongezea weledi wa kushugulikia mashauri yanayowasilishwa katika Baraza. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya watendaji 8 waliwezesha kupata mafunzo hayo ndani ya nchi.

**207. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kutangaza shughuli

za Baraza kwa wadau wake, Baraza limeweza kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kupitia Maonesho ya Kimataifa ya Kibiashara ya Saba Saba pamoja na Maonesho ya Wakulima ya NaneNane yaliyofanyika Mkoani Lindi. Pia, Baraza limeweza kuendesha semina kwa Madiwani, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na viongozi mbalimbali wa asasi za kiraia katika Mkoa wa Dodoma kwa nia ya kulitangaza Baraza kwa wadau wake. Aidha, Baraza limeweza kuendesha vipindi kwa njia ya redio, kufanya machapisho na semina mbalimbali kwenye mkoa kwa nia ya kujitangaza.

#### **4.3.14 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni**

**208. Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeendelea na kuboresha utoaji wa huduma kwa wadau, chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212; Sheria ya Kusajili Majina ya Biashara Sura ya 213; Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura ya 326; Sheria ya Hataza Sura ya 217 na Sheria ya Leseni za Viwanda Sura 46..

##### **a) Usajili wa Majina ya Biashara**

**209. Mheshimiwa Spika**, Wakala imejiandaa kutoa huduma kwa wananchi na wawekezaji wa ndani na wa nje kwa njia ya kielektroniki na tayari huduma zifuatazo zinatolewa kwa njia ya mtandao: usajili wa Majina ya Biashara (Online Business Names Registration), mabadiliko ya baada ya usajili wa majina ya biashara (post registration activities for Business Names), upekuzi wa majina (Online Company Name clearance), kuomba taarifa mbali mbali za makampuni, majina ya biashara yaliyosajiliwa (official search for Companies and Business Names), na taarifa za alama za biashara. Hivi sasa wateja hawalazimiki kuandika barua na kufuata majibu katika ofisi za BRELA Dar es Salaam kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Aidha, malipo ya ada yanafanyika kwa njia ya mtandao Mobile NMB bank na CRDB Simbanking, Mpesa na Tigopesa au kupitia matawi ya Benki za CRDB na NMB popote Tanzania Bara.

##### **b) Kupeleka huduma karibu na wananchi**

**210. Mheshimiwa Spika**, sambamba na kutoa huduma kwa

njia ya mtandao kwa baadhi ya huduma zilizotajwa hapo juu, Wakala imefungua Ofisi Mtwara ambayo inahudumia mikoa ya Ruvuma na Lindi; Mjini Mbeya kwa ajili ya kuhudumia mikoa ya Iringa, Njombe, Katavi na Songwe; Mjini Mwanza kuhudumia mikoa ya Kagera, Mara, Geita, Simiyu na Shinyanga. Wakala inaendelea na taratibu za kufungua ofisi nyingine Dodoma na Mjini Arusha. Kufanikiwa kwa ufunguzi wa ofisi za kanda umechangiwa pia na juhudi kubwa za Wakuu wa Mikoa husika.

### **c) Kupunguza muda wa kuhudumia wateja**

**211. Mheshimiwa Spika**, Wakala imeendelea kutekeleza mipango ya kupunguza muda wa kuwahudumia wananchi na hivi sasa cheti cha usajili wa majina ya biashara kinapatikana kwa saa 1-2, Usajili wa Kampuni unafanyika ndani ya siku 1-3 ikiwa mwombaji amewasilisha nyaraka zote zilizotimiza masharti ya kisheria. Aidha, Wakala imeweka bayana muda wa kuhudumia mteja kwenye tovuti pamoja na namba za simu na majina ya wakuu wa Idara na vitengo wanaohusika ikiwepo namba ya simu ya kiganjani ya Afisa Mtendaji Mkuu. Utaratibu huu umesaidia kupunguza malalamiko na kuondoa kero mbali mbali kwa kusaidia wananchi wengi wanaotaka maelezo

### **d) Kutoa huduma za BRELA kwa njia ya mtandao**

**212. Mheshimiwa Spika**, BRELA iliingia mkataba na Kampuni ya Norway Registers Development AS (NRD) ya Norway tarehe 28 Agosti, 2016 kwa ajili ya kujenga mfumo mpana wa kutoa huduma zote za Wakala kwa njia ya Mtandao. Mfumo huu, utaunganishwa na taasisi nyingine kama vile Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, OR-TAMISEMI (leseni za Biashara) Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, TRA, NIDA, RITA, TIC, TCRA, Uhamiaji, PPRA, SSRA na Taasisi nyingine za udhibiti zitakazokuwa tayari kuunganishwa na mfumo huu. Hivyo, mfumo huo unategemewa kutoa huduma kwa kielektroniki kwa pamoja (Electronic One Stop Shop) ili kupunguza na kuondoa urasimu katika kuanzisha biashara. Aidha, mkakati huu utaboresha nafasi ya nchi yetu kwenye



viwango vya ufanyaji biashara duniani (Doing Business Ranking) na hususan uanzishwaji wa Biashara (starting business ranking) na hivyo kuvutia wawekezaji wa nje.

#### **e) Uhamasishaji wa usajili na urasimishaji wa Biashara**

**213. Mheshimiwa Spika**, Wakala imetoa elimu ya usajili na kuhamasisha umuhimu wa kurasimisha biashara kwa njia mbali mbali ikiwemo vipindi/onyesho fupi kwenye runinga kwa kupitia TBC, ITV na Clouds TV, sambamba na vipindi vya radio na TV. Pia, Wakala imeshiriki maonesho ya Nanenane na Sabasaba na kutoa vipeperushi na majarida mbali mbali yanayoonyesha taratibu za usajili na gharama zake. Vilevile, Wakala imeanzisha utaratibu mpya wa kuelimisha umma juu ya umuhimu wa usajili na urasimishaji wa biashara katika ngazi za Wilaya na Tarafa kwa kutumia vyombo vya habari na kutoa huduma za usajili papo kwa hapo. Elimu na uhamasishaji huo umefanyika katika Mikoa ya Mbeya, Songea, Njombe, Arusha, Tanga, Mwanza, Mara, Geita, Simiyu, Shinyanga, Songwe na Rukwa.

#### **f) Shughuli za Usajili**

**214. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa shughuli za usajili tangu kuanzishwa rasmi kwa Wakala hadi Marchi 2017 jumla ya Makampuni 134,187 yalikuwa yamesajiliwa; Majina ya Biashara 428,576 yamekwisha sajiliwa, alama za biashara na huduma 55,418 na hataza 624 zimekwisha tolewa na leseni 6,606 za viwanda zimetolewa. Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 wakala ilisajili Makampuni 6,014, Majina ya Biashara 14,066, Usajili alama za Biashara na Huduma 2,544, Usajili Leseni za Biashara 105 na Hataza 15. Kutokana na jitihada za uhamasishaji katika kipindi cha 2016/2017 idadi ya usajili imeongezeka ukilinganisha na mwaka 2015/2016.

#### **4.3.15 Wakala wa Vipimo**

**215. Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Vipimo imeendelea kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa matumizi ya vipimo vilivyo sahihi nchini ambapo hadi kipindi cha robo

ya tatu ya mwaka 2016/2017, vipimo 453,524 vilihakikiwa na vipimo 12,459 vilirekebishwa. Wakala pia imeimarisha ukaguzi wa bidhaa zote zilizofungashwa katika mipaka ya Nchi, Mikoa na Wilaya. Wakala imendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia Maonesho ya Sabasaba na Maonesho ya NaneNane yaliyofanyika kitaifa mkoani Lindi. Aidha, Wakala kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile luninga, redio na mitandao ya kijamii imeendelea kutoa elimu kuhusu ufungashaji na matumizi ya vipimo sahihi.

**216. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo imeendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi sahihi ya vipimo katika maeneo yaliyohusu ufungashaji batili maarufu kama ‘lumbesa”. Pamoja na matakwa ya kisheria, Wakala imetekeleza jukumu hili kwa mafanikio kwa kuzingatia ushauri wa waheshimiwa wabunge na maagizo ya Mhe. Waziri Mkuu. Kutokana na ukaguzi kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017, kaguzi 6,249 zilifanywa na kukuta wakosaji 4,620 (74%) ambao wote walitozwa faini ya jumla ya Shilingi 639,144,000. Jitihada za ukaguzi wa mizani ikiwemo uelimishaji wa wadau ulichangia kwa kiasi kikubwa wakulima kupata malipo stahiki kwa mazao ya pamba na korosho kwa msimu huu.

**217. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa udhibiti wa udanganyifu na wizi kupitia mizani wakati wa ununuzi wa zao la pamba; Wizara kupitia Wakala wa Vipimo ilifanya ukaguzi wa mizani ya kununulia pamba kabla na wakati wa msimu wa ununuzi ili kubaini udanganyifu unaofanywa na wanunuzi. Ukaguzi huo ulifanyika katika mikoa ya Tabora, Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Simiyu na Geita. Timu ya wakaguzi ilizifikia wilaya 21 za mikoa hiyo, kufanya uhakiki wa mizani pamoja na kutoa Elimu kwa wadau katika maeneo hayo hususani wakulima wa zao la Pamba. Katika ukaguzi huo mizani 668 ilikaguliwa, kati ya hiyo mizani 640 ilikuwa ikipima kwa usahihi ambayo ni sawa na asilimia 96.8 ya mizani yote iliyokaguliwa, mizani 28 ilichezewa kwa makusudi ambayo ni asilimia 4.2. Jumla ya kesi 29 zilifunguliwa mahakamani, kati ya hizo watuhumiwa 19 walitozwa faini na mahakama kwa makosa waliyofanya. Watuhumiwa 3 walihukumiwa vifungo na mizani 8 ilitaifishwa mahakamani.

Kesi ambazo zinaendelea mahakamani zipo 7. Aidha, elimu iliyotolewa kwa wakulima imewafanya wao wenyewe kuwa walenzi na kuzuia mizani kuchezeza na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya kudhibiti udanganyifu kwa wakulima wanapouza pamba.

**218. Mheshimiwa Spika**, pamoja na elimu kabla na baada ya msimu wa ununuzi kuanza, wakosaji wote kufikishwa mahakamani na sio kutumia utaratibu wa kuwafilisha (compounding) na kutozwa faini na mkaguzi wa vipimo kwa mujibu wa sheria ya Vipimo sura na. 340 iliyofanyiwa mapitio 2002 uliokuwa ukitumika miaka ya nyuma angeweza kufifilishwa Uamuzi wa kuwapeleka mahamani ilikuwa ni mbinu za kiutendaji kukabiliana na adhabu ndogo/faini zilizokuwa zikitozwa na hivyo kutoshawishi kuacha kufanya makosa kwa makusudi. Ukaguzi huo umeonekana kurudisha ari ya wakulima kulima pamba kwa wingi msimu ujao. Aidha, wakulima wengi waliuza pamba safi isiyochanganywa na mchanga au maji kutokana na wakulima kulipwa kulingana na uzito halisi wa pamba yao.

**219. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo ilifanya ukaguzi maalum wa mizani itumikayo katika ununuzi wake ni zao la korosho kwa mikoa ya Mtwara na Ruvuma, ambapo wilaya za Tandahimba, Mtwara vijijini, Newala na Tunduru zilifikiwa. Uhakiki huo ulikwenda sambamba na utoaji wa elimu kwa wakulima na wanaushirika wa Vyama vya Msingi. Ukaguzi huo ulifanyika kwa Vyama vya Msingi 271 na kuhakiki mizani 900 ambapo mizani 575 (64%) ilikuwa sahihi na mizani 325 (36%) zilikatazwa kutumika. Elimu iliyotolewa na wakulima kuweza kushuhudia uhakiki wa mizani ya kununulia korosho umesaidia wakulima wengi kuacha kuuza korosho kwa kutumia vipimo batili maarufu "kangomba". Hali hii imepunguza kwa kiasi kikubwa wanunuzi "vishoka" kwenda kuwarubuni wakulima. Hivyo wakulima wengi walihamasika kuuza korosho katika Vyama vya Msingi na kunufaika na bei nzuri iliyopangwa na Serikali, kwani mazao yao yalipimwa na kulipwa kwa haki sawa na jasho lao. Hali hiyo imewatia moyo wakulima na kuhamasika kuongeza uzalishaji zaidi wa zao hilo.

**220. Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Vipimo pia iliendelea kufanya uhakiki wa mizani inayotumika kununulia ufuta wakati wa msimu. Uhakiki ulifanyika katika mkoa wa Lindi katika Wilaya za Lindi Vijini, Kilwa na Ruangwa ambapo ilifanikiwa kuvifikia vijiji 24 na vyama vya msingi nane. Mizani 72 zilihakikiwa na mizani 8 (11%) zilipitishwa wakati mizani 64 (89%) zilikataliwa. Wakosaji wote walitozwa faini, Mizani zote zisizoruhusiwa kwa matumizi ya biashara zilizuiliwa na Wanunuzi walipewa ushauri kuhusu mizani inayotakiwa kutumika katika biashara. Wakati ukaguzi wa mizani ukiendelea elimu ilitolewa kwa wakulima na wanunuzi wa ufuta kuhusu matumizi sahihi ya vipimo.

**221. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imeendelea kuongeza juhudi katika ukaguzi wa vituo vya kuuzia gesi ya majumbani (LPG). Ukaguzi umefanyika katika *Gas plant* zinazopokea na kufungasha gesi, vituo vya kuuzia gesi vya jumla na rejareja ili kuwalinda walaji na udanganyifu katika uzito wa mitungi ya gesi. Aidha, katika kudhibiti udanganyifu huo, Wizara imechukua hatua zifuatazo;

(i) Kuitisha mikutano na wadau katika sekta ya gesi hususan wafungashaji ili kuwakumbusha kuzingatia uzito sahihi wakati wa ufungashaji, kusisitiza matumizi ya *sea/zinazoweza* kuzuia refilling inayofanywa na baadhi ya wauzaji wa jumla wasio waaminifu;

(ii) Ukaguzi katika Makampuni yanayofungasha gas ili kuhakiki mifumo ya ujazaji gesi na mizani inayotumika. (Gas plant) Oryx, Mihan, Cam Gas, Lake Gas, Alpha Gas, Manji's O Gas), na

(iii) Ukaguzi wa kushitukiza kwa wauzaji wa jumla na rejareja lengo kuu lilikuwa kwanza ni kuhakikisha kila kituo kinachouza gesi kinakuwa na mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2016 mpaka Februari, 2017.

**222. Mheshimiwa Spika**, Wakala imefanya ukaguzi kwa wauzaji wa jumla na rejareja kwa vituo 1,038 ambapo vituo

715 (69%) vilikuwa na mizani na vituo 323 (31%) havikuwa na mizani. Kutokana na mapungufu yaliyobainika, wahusika walipewa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo na kwa wasio na mizani walipewa muda wa kuhakikisha wananunua mizani na ukaguzi na ufuatiliaji unaendelea. Aidha, Wakala iliendelea kutoa elimu kwa wadau ili kuhakikisha mlaji anapata uzito stahiki wa gesi.

**223. Mheshimiwa Spika,** Wakala imeendelea kufanya ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa katika viwanda vya ndani ya nchi, mipakani na bandarini na kutoa elimu ya ufungashaji kwa wadau. Ukaguzi umeimarishwa kwa bidhaa zote zilizofungashwa kutoka nje ya nchi kupitia katika mipaka ya Namanga mkoani Arusha, Horohoro - Tanga, Holili - Kilimanjaro, Sitali -Mara, Mtukura- Kagera, Kasumuru Mbeya na Bandari ya Dar es salaam. Ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kupitia Bandarini na Mipakani, umefanikishwa kiasi kikubwa kwa kutumia Mfumo wa TANCIS wa Mamlaka ya Mapato (TRA). Mfumo huu umewezesha kupokea taarifa za bidhaa zote zinazolingia nchini kupitia mipakani na bandari ya Dar es Salaam.

#### **4.3.16 Kituo cha Uwekezaji Tanzania**

##### **a) Usajili, Umiliki na Mgawanyo wa Miradi ya Uwekezaji**

**224. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Kituo kilifanikiwa kusajili jumla ya miradi 242 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,079 inayotarajiwa kutoa ajira mpya zipatazo 17,385. Sekta iliyoongoza kwa idadi ya usajili wa miradi ni uzalishaji/usindikaji viwandani, ikifuatiwa na sekta ya majengo ya biashara, utalii, na usafirishaji. Sekta zinazotarajiwa kutoa ajira kwa wingi zaidi ni sekta ya uzalishaji viwandani, ikifuatiwa na sekta ya majengo ya biashara, usafirishaji na sekta ya utalii. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa katika kipindi hicho, wawekezaji wageni waliongoza kwa kusajili miradi 105, sawa na asilimia 43 ya miradi yote; wakati miradi ya ubia kati ya Watanzania na wageni ni 76 sawa na asilimia 32, miradi 61 iliyobaki sawa na asilimia 25 inamilikiwa na watanzania.

Aidha, katika kipindi hicho, Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kusajili miradi 119, sawa na asilimia 49 ya miradi yote iliyoandikishwa. Mkoa wa Arusha ulifuatia kwa kusajili miradi 30 (sawa na asilimia 12), na kufuatiwa na Mkoa wa Pwani ukiwa na miradi 26 (sawa na asilimia 11). Mkoa wa Mwanza ulikuwa na miradi 19 (sawa na asilimia 8), na mikoa iliyobaki kila mmoja ilisajili chini ya miradi 10. Nchi kumi zinazoongoza kwa uwekezaji nchini katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ni China, ikifuatiwa na India, Kenya, Uingereza, Mauritius, Oman, Falme za Kiarabu (U.A.E), Canada na Marekani.

#### **b) Huduma kwa Wawekezaji**

**225. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Kituo kimeimarisha mfumo wake wa utoaji wa Huduma za Mahala Pamoja za Kuhudumia Wawekezaji (One Stop Centre), na pia kufanya maboresho ya mfumo huo. Katika kuendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia duniani, Kituo kipo katika hatua za mwisho za kukamilisha utaratibu wa utoaji huduma zake kupitia njia ya mtandao ili kuwawezesha wawekezaji popote pale walipo duniani waweze kuwasilisha maombi yao ya vibali na leseni mbalimbali. Huduma hiyo ya utoaji leseni na vibali inatekelezwa kupitia mradi wa *Tanzania Investment Window* (TIW) ambao unalenga kuweka mtandao wa ushirikiano wa mifumo ya usajili, leseni na vibali mbalimbali kupitia wadau hususan usajili wa ardhi (Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi), usajili wa makampuni (BRELA), utoaji vivutio na ulipaji kodi (TRA), utoaji vibali vya kazi (Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Walemavu) na utoaji vibali vya ukaazi (Uhamiaji). Baada ya kukamilika kwa mradi huo, huduma zote zikiwepo za utoaji Cheti cha Uwekezaji, Uhamiaji, Vibali vya Kazi, Upatikanaji wa Ardhi na Kufungua Kampuni zitazotolewa kwa mfumo wa mtandao (online registration).

#### **c) Huduma Zilizotolewa kwa Wawekezaji**

**226. Mheshimiwa Spika**, katika kuitikia ushauri uliotolewa na

Waheshimiwa Wabunge wa kupanua Huduma za Mahala Pamoja (One Stop Centre), Kituo cha Uwekezaji kimefanya ukarabati wa jengo linalotumika hivi sasa ili kuongeza ufanisi ikiwa ni pamoja na kuongeza Idara nyingine za Serikali ambazo zinahusika katika kutoa vibali na leseni. Taasisi zilizoongezwa ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Baraza la Mazingira (NEMC) na Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Ujenzi (AQRB). Kitengo hicho kilifunguliwa rasmi mwezi Oktoba, 2016.

**227. Mheshimiwa Spika**, kitengo cha Leseni za Biashara kilifanikiwa kushughulikia masuala 244 yanayohusu leseni ambapo leseni za biashara 71 zilitolewa. Kitengo cha Kazi kilifanikiwa kutoa jumla ya vibali 3,117 vya daraja A kwa ajili ya wamiliki wa makampuni (wenye hisa) na daraja B kwa ajili ya wafanyakazi. Idara ya Uhamiaji ilitoa Hati za Ukaazi daraja A zipatazo 283 na daraja B zipatazo 2,295. Kitengo cha TRA kilifanikiwa kuhudumia jumla ya wateja 1,311 kwa kuwapatia huduma za ushauri wa masuala yanayohusu kodi kama vile usajili wa Namba ya Mlipa Kodi, aina za kodi zinazotakiwa kulipwa na wawekezaji.

**228. Mheshimiwa Spika**, kitengo cha Ardhi kiliendelea kutoa hudumaza ushauri kwa wawekezaji katika masuala mbalimbali ya ardhi pamoja na kuainisha maeneo yenye ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Kitengo kilifanikiwa kutoa Hati Zisizo Asili (Derivative title) 28 kwa wawekezaji. Pia Ofisi za Kanda zimeshirikiana na viongozi wa mikoa husika katika kutafuta na kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji kwenye mikoa yao. Tayari Kituo kimeanza kuandaa taarifa mahususi kuhusu miundombinu ya maji, umeme, barabara na reli kwenye maeneo husika kwa ajili ya kilimo cha miwa na uanzishwaji wa viwanda vya sukari.

#### **d) Miradi ya Uwekezaji**

**229. Mheshimiwa Spika**, kituo kimeendelea kuvutia wawekezaji kuwekeza nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya maombi sita mapya ya miradi ya uwekezaji mahiri yalisajiliwa na kufanyiwa kazi ili kuwasilishwa katika Kamati

ya Taifa ya Uwekezaji Rasilimali (NISC) kwa maamuzi. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Kusindika Matunda wa *Sayona Fruits*, Mradi wa Kuzalisha Vigae (ceramic tiles) wa *Goodwill Ceramics*, Mradi wa Hospitali wa *Pan African Multispeciality Health Centre*, Mradi wa Kusindika Gesi ya LPG wa *Mihan Gas*, Mradi wa Kuzalisha Vigae wa *Twyford* na Mradi wa Kiwanda cha Saruji wa *Hengya Cement*. Utekelezaji wa miradi hiyo kwa pamoja itagharimu Dola la Kimarekani bilioni 2.68 na itazalisha jumla ya ajira za moja kwa moja 13,885 na zaidi ya ajira 38,520 zisizo za moja kwa moja. Miradi mitano kati ya sita tayari iko katika hatua za ujenzi.

#### e) Elimu kuhusu Uwekezaji

**230. Mheshimiwa Spika**, kituo kimeendelea kutekeleza Mkakati wa Mahusiano na Elimu kwa Umma kwa kutoa elimu kupitia radio, televisheni, mtandao na makala mbalimbali kwenye magazeti yetu ya ndani ili kuelimisha jamii kuhusu faida za uwekezaji na kuhakikisha kuwa idadi kubwa ya Watanzania inafikiwa. Mkakati huo umelenga kuongeza ushirikiano kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii ili kuondoa dhana hasi kuhusu uwekezaji zinazotokana na uelewa duni juu ya manufaa ya uwekezaji. Pia, Kituo kililenga katika kuelimisha wawekezaji wa ndani kujisajili na Kituo ili kupatiwa huduma mbalimbali zinazotolewa kituoni. Katika utoaji wa elimu, Kituo kimejikita katika kuwaelimisha wawekezaji wa ndani na wa nje kufuata Sheria na taratibu zilizopo ikiwa ni pamoja na kulipa kodi kwa wakati.

#### f) Uhamasishaji Uwekezaji

**231. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Kituo cha Uwekezaji kiliratibu ushiriki katika makongamano ya uwekezaji katika nchi za China, Israeli, Kenya, Mauritius na Misri. Makongamano hayo yalihudhuriwa na zaidi ya wafanyabiashara 420 kutoka nchi mbalimbali. Ushiriki katika makongamano hayo ulitupatia fursa ya kutoa taarifa mbalimbali zenye lengo la kuhamasisha uwekezaji nchini ikiwemo mada juu ya hali ya uchumi, fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini, mazingira ya uwekezaji na vivutio



vinavyotolewa kwa wawekezaji. Makongamano hayo yalitoa nafasi ya kufanyika kwa mikutano baina ya wafanyabiashara na kati ya wafanyabiashara na Serikali. Pia Kituo kiliweza kushiriki katika Maonesho ya Uwekezaji Afrika (Africa Investment Forum) yaliyofanyika nchini Rwanda.

**232. Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Uwekezaji kilishiriki katika maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika makongamano na mikutano ya uwekezaji na kupokea ujumbe wa wafanyabiashara kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Afrika ya Kusini, China, Ethiopia, Finland, India, Japan, Korea ya Kusini, Mauritius, Marekani, Misri, Morocco, Oman, Singapore, Ubelgiji, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Urusi, Uturuki na Zimbabwe. Aidha, kituo kilihamasisha uwekezaji wa ndani ya nchi uliohusisha zaidi ya washiriki 700 wengi wao wakiwa ni wafanyabiashara. Makongamano hayo yalikusha washiriki kutoka taasisi za umma na binafsi na yalilinga kukutana na wafanyabiashara na kuwapatia taarifa muhimu kuhusu masuala ya uwekezaji na pia kuwawezesha kuzitambua na kuchangamkia fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali hapa nchini. Vilevile kituo kwa kushirikiana na Ofisi za Mikoa na Wilaya, Kituo kilihamasisha uwekezaji kwa kuandaa na kuibua fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo hayo na kuzitangaza kwa wawekezaji wa ndani na wa nje.

**233. Mheshimiwa Spika**, kituo kimekuwa kikishiriki kila mwaka katika maonesho mbalimbali ya kitaifa kama vile Sabasaba, na Nanenane ikiwa na lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zitolewazo na Kituo, faida za kituo kwa wawekezaji hasa wananchi, kutoa elimu ya uwekezaji, fursa za uwekezaji zilizopo katika maeneo husika na vivutio vitolewavyo kupitia Kituo kwa wawekezaji. Aidha, Kituo kiliweza kushiriki katika Maonesho ya Nanenane katika Kanda za Kusini (Lindi), Kaskazini (Arusha) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) pamoja na Maonesho ya Sabasaba, SIDO na Maonesho ya Viwanda ya Tanzania ambapo wananchi wengi waliweza kutembelea banda la Kituo na kupata elimu hiyo.

#### 4.3.17 Chuo cha Elimu ya Biashara

**234. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) ilipanga kujenga na kuboresha miundombinu ya Chuo katika Kampasi za Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya; kuongeza uwezo wa wahadhiri katika mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya shahada za uzamili na uzamivu; na kupitia upya mitaala yote ili kuendana na uhitaji wa soko la ajira. Katika kukabiliana na uhaba wa miundombinu, Chuo cha Elimu ya Biashara tunatekeleza mradi wa kuongeza ghorofa tatu (Vertical Extension) katika jengo la sasa la "Cafeteria" kwa ajili ya maktaba mpya, madarasa, ofisi pamoja na kumbi za mihadhara kwa Kampasi ya Dar es Salaam.

**235. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi hizo Chuo kilinunua eneo lote lenye ekari 10.9 la shule ya sekondari iliyokuwa inaitwa *Hill Crest* kule Nyasaka, Mwanza. Ukarabati wa majengo na kuongeza miundo mbimu umeenza ili kuendeleza kampasi ya Mwanza. Chuo pia kimekamilisha kazi ya kuandaa Mpango Kabambe wa eneo lenye ukubwa wa ekari 54.9 lililopo lganzo jijini Mbeya kwa ajili ya ujenzi wa kampasi ya Mbeya. Juhudi hizo zinatoa nafasi kubwa ya kusogeza huduma ya elimu ya biashara kwa wananchi walio wengi. Kwa ujumla wake, kumekuwa na mabadiliko chanya katika kuboresha miundo mbinu kwa mwaka 2016/2017. Mabadiliko hayo yamejikita katika kuboresha miundo mbinu ya madarasa, kumbi za mihadhara, hosteli, na ofisi za waalimu katika kampasi za Dar es Salaam na Dodoma. Kuboreshwa kwa miundo mbinu pamoja na ujenzi wa Kampasi za Mwanza, Mbeya na Zanzibar kutakiwezesha Chuo kukidhi mahitaji yake ikiwa ni pamoja na kuwa na mazingira wezeshi katika kutoa huduma zake za kufundisha, utafiti pamoja na ushauri elekezi.

**236. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Elimu ya Biashara imeendelea kuimarisha uwezo wa wahadhiri wake ambapo katika kipindi cha mwaka 2016/2017, jumla ya watumishi saba, (6 mafunzo ya Shahada ya Uzamili na 1 mafunzo ya Shahada ya Uzamivu) wamehitimu mafunzo yao na sasa

wanalitumikia Taifa kwa kutumia elimu na ujuzi wao katika kufundisha. Aidha, watumishi 52 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi kwa ufadhili wa Serikali na Wahisani.

*Watumishi wa CBE waliopo katika mafunzo ya muda mrefu*

Na.	Ngazi ya Elimu ya Mafunzo	Idadi	Me	Ke	Ndani ya Nchi	Nje ya Nchi
1	Shahada ya Uzamivu (Ph.D)	27	21	6	14	13
2	Shahada ya Uzamili	21	19	2	16	5
3	Shahada ya Awali	2	0	2	2	0
4	Stashahada (Diploma)	2	0	2	2	0
	<b>Jumla</b>	<b>52</b>	<b>40</b>	<b>12</b>	<b>34</b>	<b>18</b>

**Ufunguo:** Me - Wanaume  
Ke - Wanawake

**Chanzo:** CBE, 2017

**237. Mheshimiwa Spika,** Chuo kupitia watumishi wake kimefanya tafiti na kutoa machapisho ya jumla ya tafiti 36, kati ya hizo 34 zimechapishwa ndani na mbili nje ya chuo. Machapisho hayo yanayolenga kuisaidia jamii na Taifa kwa ujumla kujikwamua kutoka kwenye changamoto mbalimbali zinazotukabili. Baadhi ya chapisho hizo ni:

*i) Adoption of Bus Rapid Transit(BRT) as a Solution in Combating Traffic Congestion and Fostering Economic Development in Africa;*

- ii) *Enhancing Access and Usage of Agricultural Information Towards Poverty Eradication and Environmental Degradation in Muleba and Misenyi in Kagera, Tanzania;*
- iii) *Stigmatization Among Female Students in Science Related Courses in TVETS in Tanzania;*
- iv) *Role of the College of Business Education (CBE) In The Fast Growing Business in The Energy and Mineral Sector in Tanzania; na*
- v) *Improving Public Service Delivery in Tanzania through Kaizen: A Review of Empirical Evidence.*

**238. Mheshimiwa Spika**, katika kutimiza azma ya Serikali na kufuata Diraya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo 2016/17 – 2020/2021 unaolenga kuifanya Tanzania kuwa na Uchumi wa kati kupitia ukuaji wa viwanda, Chuo kimepitia upya na kuifanyia marekebisho mitaala yake yote ili kuendana na uhitaji wa soko. Sambamba na hilo Chuo kimekamilisha uanzishwaji wa shahada mbili ya Uzamili kwa mwaka 2016/2017 ambazo ni “Master in International Business Management” na “Masters in International Supply Chain Management” ambazo zinatarajiwa kuanza rasmi mwaka wa masomo 2017/2018 mara idhini itakapopatikana kutoka NACTE. Aidha, Chuo kimeanzisha shahada za uzamili kwenye TEHAMA na Maendeleo (ICT for Development) na TEHAMA katika Usimamizi Miradi (IT- Project Mangement) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Stockholm cha nchini Sweden. Kozi zimeanza rasmi mwaka 2016/2017.

**239. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Elimu ya Biashara kimeendelea kuleta chachu ya maendeleo nchini kwa kutoa idadi kubwa ya wataalamu katika nyanja mbalimbali za biashara na viwanda kwa ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya wanafunzi 3,118 walihitimu katika fani mbalimbali.

*Idadi ya Wanafunzi waliohitimu Mwaka 2016 katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)*

Na.	Ngazi ya Elimu	Me	Ke	Jumla
1	Astashahada	474	489	963
2	Stashahada	607	599	1206
3	Shahada	445	491	936
4	Stashahada za Uzamili	11	2	13
	<b>Jumla Kuu</b>	<b>1,537</b>	<b>1,581</b>	<b>3,118</b>

**240. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia ubora wa Chuo cha Elimu ya Biashara kwa kuhakikisha kuwa kinazingatia viwango na vigezo vilivyowekwa na mamlaka za kusimamia elimu nchini ikiwemo NACTE na TCU. Kutokana na usimamizi huo na kwa ushirikiano mkubwa na uongozi wa Chuo, CBE imefanikiwa kushinda tuzo ya ubora ya Mwaka (College of the Year) ya mwaka 2016 katika mashindano yanayoandaliwa na "Tanzania Leadership Award."

**241. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara katika mwaka 2016/2017 imeendelea na mikakati ya kukiwezesha Chuo kuwa kituo cha Ubona (Centre for Excellence) katika kutoa wataalamu wa fani ya Sayansi ya Vipimo katika Viwanda (Legal and Industrial Metrology) katika Ukanda wa Nchi za Kusini mwa Afrika – SADC. Katika kutekeleza hilo, Chuo kimeendelea kuboresha maabara zake kwa kuongeza vifaa mbalimbali na kuboresha miundombinu na vitendea kazi katika majengo yanayotumika kutolea elimu hiyo. Vilevile, Serikali imeendelea kusomesha wahadhiri katika ngazi ya shahada ya uzamivu (PhD) katika nchi ya Urusi na ndani ya nchi. Hadi sasa jumla ya wahadhiri watano wako masomoni, kati yao wahadhiri wanne (akiwemo mwanamke 1) wako nchini Urusi na Mhadhiri mmoja yupo nchini katika mafunzo hayo.

**242. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara iliweza kufanya tafiti kubwa za kibiashara, kiuchumi na kijamii kufuatia hatua ya Serikali ya awamu ya tano kuhamia Dodoma. Kufuatia tafiti hizo, Chuo cha Elimu ya Biashara kiliandaa kongamano kubwa la kitaaluma lililoshirikisha wadau mbalimbali kwa lengo la kuibua na kujadili zaidi juu ya fursa zinazopatikana katika mkoa wa Dodoma.

#### **4.4 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU NA UTOAJI WA HUDUMA**

##### **a) Ajira za Watumishi**

**243. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ikama ya mwaka 2016/2017 iliyoidhinishwa, Wizara ilikuwa na jumla ya watumishi 256 ambapo wanawake walikuwa 102 sawa na asilimia 40 na wanaume 154 sawa na asilimia 60. Kwa taarifa ya hadi mwezi Machi, 2017, Wizara ina jumla ya Watumishi 249, kati ya hao Viongozi ni 4, Wachumi ni 50, Watakwimu 14, Wahandisi 5, Maafisa Tawala 7, Maafisa Utumishi 5, Maafisa Sheria 4, Maafisa TEHAMA 5, Maafisa Ugavi 6, Maafisa Biashara 68, Maafisa Habari 2, Wakaguzi wa Ndani 6, Wahasibu 18, Wasaidizi wa Maktaba 2, Wasaidizi wa Kumbukumbu 12, Wapokezi 3, Fundi Sanifu 2, Makatibu Mahsus 17, Wasaidizi wa Ofisi 6 pamoja na Madereva 13. Hata hivyo, Wizara haikuweza kuajiri wala kupandisha vyeo watumishi kwa mwaka 2016/2017 kwa kuwa, Serikali iliahirisha utekelezaji wa utoaji ajira mpya, ajira mbadala pamoja na masuala yote yanayohusisha marekebisho ya mishahara yanayotokana na upandishwaji vyeo kwa watumishi hadi maelekezo yatakapotolewa.

##### **b) Mafunzo**

**244. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara iliandaa Mpango wa Mafunzo wa muda wa mwaka mmoja ili kujenga uwezo kwa rasilimali watu na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Wizara ilipanga kuwapeleka watumishi kumi na sita (16) katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi kumi na nane (18) katika mafunzo

ya muda mfupi. Hadi kufikia Aprili, 2017, Wizara imekwisha peleka watumishi nane (8) katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi (28) katika mafunzo ya muda mfupi, ndani na nje ya nchi.

#### **c) Upimaji wa Utendaji Kazi wa Watumishi**

**245. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imehakikisha kuwa watumishi wote wanasaini mikataba yao ya kazi kwa wakati ili kutekeleza programu ya kuboresha utumishi wa umma na kuimarisha utendaji unaojali matokeo na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Kwa kuzingatia hayo, jumla ya watumishi 248 kati ya 256 wamesaini mikataba ya kazi kwa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKA) na kufanya mapitio ya nusu mwaka mwezi Desemba, 2016 na wasimamizi wao. Watumishi nane (8) hawakuweza kusaini mikataba yao kwa kuwa wapo mafunzoni. Aidha, inatarajiwa kufikia mwisho wa mwezi Juni, 2017 kila mtumishi atafanyiwa tathmini ya utendaji wake wa kazi kwa kipindi cha mwaka mzima kwa kutumia utaratibu huo wa MWAMTUKA.

#### **d) Michezo na Afya za Watumishi**

**246. Mheshimiwa Spika**, katika dhana ya michezo kwa afya, furaha na ufanisi kazini, kwa mwaka 2016/2017, Wizara imeshiriki katika mabonanza mawili (2) yaliyohusisha washiriki kutoka taasisi mbalimbali za umma. Lengo la kushiriki michezo hiyo ilikuwa ni kujenga afya za watumishi kupitia mazoezi na michezo. Aidha, kufuatia agizo la Serikali kwa watumishi kufanya mazoezi jumamosi ya pili kila mwezi, Wizara imewahimiza watumishi kujenga tabia ya kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao na kujikinga na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) yanayoweza kuepukika kama vile, uzito uliopitiliza, shinikizo la damu na kisukari.

#### **e) Baraza la Wafanyakazi**

**247. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuwashirikisha watumishi katika vikao vya

maamuzi kupitia Baraza la Wafanyakazi ili waweze kutetea maslahi yao. Kwa mwaka 2016/2017, Wizara imefanya kikao kimoja tarehe 24 Machi, 2017 ambapo Baraza la Wafanyakazi lilipitia, kushauri na kuridhia mapendekezo ya Wizara kuhusu Mipango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2017/2018.

#### **f) Kuhamia Makao Makuu Dodoma**

**248. Mheshimiwa Spika**, kufuatia Agizo la Serikali la kuhamishia shughuli zake Makao Makuu ya Nchi Dodoma, Wizara imepanga kuhamisha watumishi wake katika awamu nne: Awamu ya kwanza Watumishi 43, awamu ya pili Watumishi 58, awamu ya tatu watumishi 81 na Awamu ya nne watumishi 67. Aidha, kila awamu inahusisha kuhamisha vifaa na mifumo ya utendaji ikiwemo Mifumo ya Mitandao ya Kompyuta. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Wizara imekwishahamisha watumishi 43 wakiwemo viongozi wake wakuu (Waziri, Katibu Wakuu wawili (2) na Naibu Katibu Mkuu). Awamu ya pili inategemewa kukamilika ifikapo Agosti, 2017, Awamu ya Tatu itakamilika ifikapo mwezi Februari, 2018 na awamu ya nne ifikapo mwezi Januari, 2019 kama ilivyoelekezwa.

#### **g) Usimamizi wa Mapato na Matumizi**

**249. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakikisha kwamba, kila anayefanya biashara hapa nchini anakuwa na leseni halali inayolingana na biashara anayoifanya. Aidha, Maafisa Biashara wa Wizara na Sehemu ya Ufuatiliaji na Uperembaji (M & E Section) wakishirikiana na Maafisa Biashara walio katika Halmashauri na Manispaa zote nchini wamefanya ukaguzi na kuchukua hatua za kisheria kwa mfanyabiashara yeyote aliyepatikana akifanya biashara bila leseni au leseni stahili.

**250. Mheshimiwa Spika**, kuhusu usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia leseni za biashara, Wizara imehakikisha kuwa kila anayefanya biashara anakuwa na leseni halali kulingana na biashara anayofanya. Aidha, Wizara imeweka mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato



ambapo mtandao huo utaunganishwa na BRELA na hivyo kurahisisha leseni zote za biashara kupatikana katika kituo kimoja kadhalika, hali hii itarahisisha ufuatiliaji na uperembaji kupitia ofisi za kanda na BRELA.

**251. Mheshimiwa Spika**, kuhusu matumizi, Wizara imehakikisha kuwa matumizi ya fedha yanafanywa kulingana na Sheria, kanuni, taratibu za fedha na Ununuzi Serikalini. Ili kufanikisha lengo hili, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo na kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Kitengo cha Uhasibu na Kitengo cha Ununuzi na Ugavi.

#### **h) Usimamizi wa Ununuzi**

**252. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia shughuli mbalimbali za Ununuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016) na Kanuni zake za mwaka 2013, GN 446. Katika kutekeleza majukumu yanayohusu usimamizi wa ununuzi, Wizara kupitia Kitengo chake cha Ununuzi kimetekeleza majukumu yafuatayo;

(i) Mpango wa Ununuzi umeandaliwa ambao utekelezwaji wake ulikuwa ni wa kiwango cha wastani kutokana na kukosekana kwa fedha za kutosha kwenye Idara na Vitengo kwa mwaka 2016/2017;

(ii) Vikao vya Bodi ya Zabuni vitatu viliratibiwa, vikiwemo viwili vya dharura na kimoja cha kawaida na kufanikisha upatikanaji wa ridhaa ya Bodi katika mambo mbalimbali yanayohusu ununuzi Wizarani;

(iii) Ununuzi na kugawa bidhaa na huduma mbalimbali kwa mujibu wa Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2016/2017 umefanyika ambapo taarifa za Ununuzi za kila mwezi na kila robo ya mwaka ziliandaliwa na kuwasilishwa kwenye Taasisi ya kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA);

(iv) Mali za Wizara (Physical Verification and stock taking) kwa mwaka 2016/2017 zimehakikiwa na kufanikisha uhuishaji

wa Daftari la Mali za Wizara (Updating Asset Register) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004; na

(v) Ushirikiano na Idara ya Utawala na Rasilimali Watu katika kufanikisha zoezi la kuhamisha vifaa vya Wizara kuhamia Dodoma awamu ya kwanza umefanyika kwa ufanisi.

## **i) Masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

**253. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia matumizi bora na sahihi ya vifaa na mifumo ya TEHAMA kwa watumishi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji huduma kwa wadau wa ndani na wa nje. Katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Wakala wa Serikali Mtandao imekamilisha kazi ya utengenezaji wa Mfumo na Mtandao wa Tovuti ya Biashara ya Kitaifa (National Business Portal). Mafunzo juu ya matumizi ya mfumo huo yamefanyika kwa ngazi mbali mbali, na sasa Wizara imeanza maandalizi ya kuuzindua rasmi mfumo huo ili uanze kutumika. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha tovuti yake kwa kuhisha taarifa zake na kuuhabarisha umma juu ya kazi mbalimbali zinazotekelezwa kwa kupitia tovuti yake ([www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz)). Wizara itaendelea kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa miaka inayofuatia ili kuboresha utoaji huduma na taarifa kwa umma ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

## **j) Huduma za Sheria**

**254. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yanayohusu usimamizi wa sheria, Wizara kupitia Kitengo cha Sheria imetekeleza majukumu yafuatayo;

i) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Vipimo (Sura 340)"The Weight and Measures Act (Cap 340) kupitia marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 3/ 2016 ili kudhibiti

vipimo visivyo sawa na kuhakikisha kuwa sheria hii inaendana na muda uliopo sasa;

*ii)* Imefanyia marekebisha Kanuni za Vipimo (The Weight and Measures (General) Regulations 2016. Pia, imeandaa Kanuni za Vipimo vya Umeme na Gesi asilia "The Weight and Measures (Metrological Control of Electricity and Natural gas Meters) Regulations 2017 ili kuendelea kumlinda mtumiaji;

*iii)* Imeandaa alama za Viwango 21(Prescribed Standards Marks) kwa bidhaa mbalimbali ili kuendelea kumlind

a mtumiaji wa bidhaa kupitia GN No. 290 ya 2016; na

*iv)* Imeandaa Mikataba ya watoa huduma wote kwa Wizara.

#### **4.5 MASUALA MTAMBUKA**

##### **a) Kushughulikia Malalamiko**

**255. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016/2017, Wizara imeweza kutoa huduma kwa wadau wa ndani na nje kupitia Dawati la Kutoa Msaada kwa kushughulikia malalamiko na kero mbalimbali hususan katika Sekta za viwanda, biashara, masoko na uwekezaji. Wadau wamenufaika kupitia huduma hiyo kwa malalamiko na kero zao kupatiwa ufumbuzi. Katika kushughulikia malalamiko ya wateja, Wizara imebaini kuwepo kwa muingiliano wa sekta zetu na sekta nyingine kama vile sekta za kilimo, uvuvi, nishati na mawasiliano. Malalamiko ya sekta nyingine hupelekwa katika wizara na taasisi husika kwa hatua stahiki.

##### **b) Kupambana na Rushwa**

**256. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa kutoa elimu na maelekezo kwa watumishi wake juu ya kufuata sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma kwa lengo la kuboresha utendaji kazini na utoaji wa

huduma bora bila kupokea au kutoa rushwa. Hadi kufikia Mei, 2017 hakuna mtumishi yeyote wa Wizara aliyeshitakiwa kwa kupokea au kutoa rushwa.

#### **c) Usimamizi wa Mazingira**

**257. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imefanya tathmini ya athari ya mazingira kwa kushirikiana na NEMC kabla viwanda kuanzishwa, imekagua hali ya mazingira viwandani katika viwanda vilivyoanza uzalishaji, na imeshiriki kutoa maoni kuhusu utekelezaji wa usitishaji wa vifungashio vya plastiki vya ujazo mdogo vinavyofungashiwa pombe kali (maarufu kwa jina la VIROBA) linalotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira. Aidha, Wizara kupitia, CAMARTEC imekuwa ikihamasisha matumizi ya biogas badala ya mkaa na kuni ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti.

#### **d) Mapambano ya UKIMWI**

**258. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe, usafiri na virutubisho kwa Watumishi watatu (3) wenye maambukizi ya VVU na waliojitambulisha ili kuwaweka katika hali ya afya bora na kudumu zaidi kwenye utumishi wa umma. Aidha, Kamati ya UKIMWI ya Wizara ilifanya kikao mwezi Desemba, 2016 kwa ajili ya kufanya maandalizi ya semina elekezi kabla ya mwezi Juni, 2017 itakayotoa elimu kwa watumishi wote kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza.

#### **e) Jinsia**

**259. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Tanzania Gender Networking Programme (TGNP) mwezi Julai, 2016 ilifanya mafunzo kwa wanawake wafanyabiashara 34 wa mipakani;- Namanga, Holili na Mutukula ambao ni wanachama wa chama cha Wanawake wa Tanzania Wafanyabiashara Mipakani (WATABAM). Mafunzo hayo yalihusu masuala ya vikwazo vya biashara visivyokuwa vya

kiushuru na kuelimishwa juu ya fursa za masoko zilizopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla; kushiriki mafunzo ya kuwawezesha wafanyabiashara wanawake katika kukuza uchumi kupitia biashara mwezi Novemba, 2016; na kushiriki warsha kuhusiana na taarifa ya wafanyabiashara wanawake ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Novemba, 2016. Lengo la warsha hiyo lilikuwa ni kuelezea changamoto zinazowakabili mipakani na kuzitafutia ufumbuzi ili waweze kukuza biashara zao.

**260. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na *UN Women* ilifanya tafiti mbalimbali za kuangalia fursa na changamoto zinazowakabili wanawake walioajiriwa viwandani, wanaofanya biashara au wenye viwanda ambazo ni:-

*i)* Utafiti kwenye maeneo maalum ya uwekezaji ya viwanda (EPZ/SEZ) katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga na Shinyanga. Utafiti ulibaini kuwa kuna pengo kubwa la ajira *Gender Gap* kati ya wanawake na wanaume kwenye maeneo hayoyauwekezaji pamoja na changamoto nyingizina zowakabili wanawake wanao fanya kazi katika maeneo hayo;

*ii)* Utafiti katika Maonesho ya Kimataifa ya 40 ya Sabasaba kuanzia tarehe 28 hadi 8 Julai, 2016 utafiti huo ulibaini changamoto iliyokuwa ikiwakabili wajasiriamali wadogo ambayo ni pamoja na kiingilio kikubwa katika maonesho hayo kilichopelekea watu kushindwa kuingia kwa wingi kujionea bidhaa walizokuwa wakizionesha na uhaba wa vifungashio bora;

*iii)* Utafiti juu ya utekelezaji wa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (2008) katika mikoa ya, Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro na Morogoro. Utafiti huo ulilenga kujua fursa zilizopo, changamoto na pengo lililopo katika masuala ya kijinsia katika utekelezaji wa sera hiyo. Utafiti huo ulionesha kuwa watendaji wengi na wajasiriamali hawaifahamu sera na kupelekea utekelezaji wake kuwa mgumu. Aidha, katika utafiti huo wajasiriamali walishauriwa kuongeza juhudi katika kuongeza thamani mazao ya kilimo na kuepuka kuuza

bidhaa ghafi hasa kwa wale wanaosafirisha nje ya mipaka ya Tanzania ili kujiongezea kipato zaidi.

**261. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia ilishiriki kwenye kikao cha 61 cha Hali ya Wanawake Duniani (CSW 5961) kilichofanyika New York, Marekani mwezi Marchi, 2017. Kikao hicho pamoja na mambo mengine kilifanikiwa kupima utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia - MDG pamoja na kuangalia changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa juhudi za kuleta usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi, kijamii na kisiasa (Women Economic Empowerment in the Changing World of Work.)

**262. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nitoe Malengo ya Mwaka 2017/2018 ya Wizara (Idara za Kisekta) na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

## **5.1 MALENGO YA MWAKA 2017/2018**

### **5.2 IDARA ZA KISEKTA**

#### **5.1.1 Sekta ya Viwanda**

**263. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ina malengo yafuatayo:-

*(a) Kuendeleza jitihada za kuhamasisha sekta binafsi kuendeleza viwanda vilivyopo na kuanzisha viwanda vipya*

*i) Kuwekeza nguvu kwenye viwanda vinavyotoa ajira nyingi (nguo na mavazi na ngozi);*

*ii) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya vioo baada ya kupata mafanikio ya ujenzi wa viwanda vya saruji na vigae;*

*iii) Kuendeleza Sekta ya Mafuta ya Kula;*

*iv) Kuhamasisha uongezaji wa uzalishaji wa sukari kwa kuhimiza viwanda vinavyozalisha chini ya uwezo wa uzalishaji kuongeza uzalishaji;*

v) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya madawa ya binadamu; na

vi) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuunganisha magari na matreka.

*(b) Kuendeleza viwanda mama na miradi ya kimkakati*

i) Kukamilisha mapitio ya vivutio vya uwekezaji na kuanza utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga;

ii) Kutafuta mwekezaji atakeyeingia ubia na Serikali kwa ajili ya kuendesha Kiwanda cha Matairi Arusha kwa misingi ya kibiashara; na

iii) Kukamilisha utafiti wa faida za kiuchumi za Mradi wa Magadi wa Engaruka na kuanza utekelezaji.

*(c) Kuendeleza jitihada za kubainisha na kutenga maeneo ya ujenzi wa viwanda*

i) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa kuzingatia msambao wa viwanda nchi nzima;

ii) Kuhamasisha sekta binafsi kuendeleza maeneo ya uwekezaji yaliyokwishatengwa; na

iii) Kuendeleza makongano ya viwanda kwa sekta za nguo, ngozi na mafuta ya alizeti.

*(d) Kujenga mfumo wa taarifa za sekta mbalimbali za viwanda nchini*

i) Kuanzisha utambulisho maalum wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa;

ii) Kukusanya taarifa za viwanda kissekta na kuzichambua kwa lengo la kufuatilia mwenendo wa viwanda wakati wote; na

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

*iii)* Kutafuta rasilimali za kujenga mfumo wa kielektroniki wa kuendesha taarifa za viwanda.

*(e) Kufanya tathmini ya mahitaji ya ujuzi maalum wa viwanda na kuuendeleza*

*i)* Kubainisha wataalam wenye ujuzi maalum katika Sekta ya Nguo na Mavazi;

*ii)* Kubainisha wataalam wenye ujuzi maalum katika Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi;

*iii)* Kubainisha wataalam wenye ujuzi maalum katika Sekta ya Samani; na

*iv)* Kubainisha wataalam wenye ujuzi maalum katika Sekta ya Vito na Madini.

*(f) Kujenga uwezo wa taasisi za utafiti zilizochini ya Wizara*

*i)* Kuongeza uwezo wa mifumo ya uvumbuzi;

*ii)* Kuimarisha uwezo wa maabara za utafiti;

*iii)* Kuhamasisha usambazaji wa teknolojia zinazobuniwa na taasisi hizo; na

*iv)* Kuhamasisha sekta binafsi kutumia teknolojia husika.

*(g) Kushirikiana na Msajili wa Hazina na wizara za kisekta kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa visivyofanya kazi vinafanya kazi*

*i)* Kukamilisha tathmini ya viwanda vyote vilivyobinafsishwa;

*ii)* Kupitia mikataba ya ubinafsishaji yaviwanda visivyofanya kazi; na

*iii)* Kuhamasisha uwekezaji mpya katika viwanda hivyo.



### 5.1.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

**264. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

*(a) Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo na biashara ndogo*

*i) Kutoa mwongozo kwa Serikali ngazi ya Mkoa na Wilaya namna ya kujenga viwanda vidogo ;*

*ii) Kuhamasisha Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa kutenga maeneo ya ujenzi wa viwanda na biashara kwa kulenga mahitaji ya sasa na baadae;*

*iii) Kubaini tabaka la kati na kulihamasisha kujenga viwanda vidogo; na*

*iv) Kukamilisha mwongozo wa taarifa muhimu kwa wajasiriamali wadogo wanapoanzisha biashara.*

*(b) Kuwezesha uanzishwaji wa kongano za samani*

*i) Kwa kushirikiana na wadau kuainisha na kutenga maeneo ya kujenga kongano la samani;*

*ii) Kuhamasisha wajasiriamali katika fani ya samani kufanya kazi sehemu moja na kwa pamoja; na*

*iii) Kutafuta rasilimali za kuendeleza kongano la samani.*

*(c) Kuendelea na kazi ya kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003*

*i) Kuendelea na tathmini ya utekelezaji wa sera ya sasa; na*

*ii) Kushirikisha wadau mbalimbali katika kufanya mapitio ya tathmini na kutoa mtazamo wa sera inayoandaliwa.*

*(d) Kuendelea kusimamia Mfuko wa Kuwaendeleza Wajasiriamali Wadogo (NEDF)*

*i) Kuongeza mtaji wa Mfuko;*

*ii) Kuratibu kwa karibu wajasiriamali wote wanaofaidika na mfuko huo; na*

*iii) Kuhakikisha kwa kutumia mfuko huo, mtandao wa viwanda unaenea nchi nzima.*

*(e) Kutumia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kama nyezo ya kujenga viwanda*

*i) Kulifanyia mageuzi Shirika la SIDO ili lishiriki kikamilifu katika ujenzi wa viwanda;*

*ii) Kuhamasisha wananchi kupitia maonesho juu ya ushiriki katika ujenzi wa viwanda;*

*iii) Kupitia maonesho kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutumia bidhaa za ndani; na*

*iv) Kuhamasisha ubunifu na matumizi ya teknolojia kupitia viatamizi.*

### **5.1.3 Sekta ya Biashara**

**265. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

*(a) Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji;*

#### **• Biashara baina ya Nchi na Nchi**

*i) Kuratibu na kushiriki majadiliano ya kibiashara baina ya nchi na nchi kupitia Tume za Pamoja za Biashara (Joint Trade*

Commissions); na kushiriki katika majadiliano ya kibiashara na diplomasia baina ya nchi na nchi kupitia Tume za Pamoja za Kudumu (Joint Permanent Commissions). Lengo la majadiliano hayo ni kuimarisha mahusiano ya kibiashara na diplomasia ya kiuchumi, kuibua maeneo mapya ya ushirikiano na kutatua changamoto za kibiashara baina ya Tanzania na nchi hizo;

*ii)* Kukamilisha mpango kazi wa utekelezaji kwa ajili ya kuongeza mauzo kwenye Soko la Marekani kupitia Mpango wa AGOA. Hiyo ikiwa ni pamoja na kubuni miradi ya uongezaji thamani katika maeneo ya bidhaa zilizoainishwa kwenye mkakati wa kitaifa wa AGOA;

*iii)* Kuratibu na kushiriki katika jumbe/ziara za biashara nchi rafiki, ndani na nje ya nchi, zikiwemo China, India, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mauritius, Misri, Sudani ya Kusini, Urusi, Uturuki na Vietnam kwa lengo la kuimarisha biashara kati Tanzania na nchi hizo. Ziara hizo zinalenga kushirikisha sekta binafsi na kuunganisha sekta hiyo na wenzao kutoka nje katika kubaini fursa nafuu za biashara; na

*iv)* Kuratibu na kushiriki katika makongamano ya biashara ndani na nje ya nchi.

• ***Biashara za Kikanda***

*i)* Kuendelea na utekelezaji wa Itifaki za Soko la Pamoja na Ushuru wa Pamoja za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Common Market and Customs Union Protocols) kwa lengo la kurahisisha na kuimarisha biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya hiyo. Maeneo yatakayowekewa mkazo ni pamoja na Uimarishaji wa Biashara ya Huduma, na Ushuru wa Forodha wa Pamoja (Common External Tariff-CET); na Uondoaji wa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru (Non-Tariff Barriers-NTBs);

*ii)* Kuendelea na utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Hiyo ikiwa ni pamoja kushiriki majadiliano ya biashara ya huduma; kusimamia ustawi wa uzalishaji na biashara ya sukari na

karatasi za vifungashio kutoka Tanzania; na kushiriki katika utekelezaji wa Mkakati wa Viwanda wa SADC uliozinduliwa hivi karibuni kwa lengo la kuongeza uzalishaji na biashara ya bidhaa za viwandani ndani na nje ya SADC. Tunatarajia kuwa juhudi hizo zitasaidia kuongeza biashara ya Tanzania katika SADC;

*iii)* Kuratibu na kushiriki katika majadiliano yanayoendelea ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu (Tripartite Free Trade Area-TFTA) linalojumuisha Kanda za COMESA,EAC na SADC; na

*iv)* Kuratibu na kushiriki katika majadiliano yanayoendelea ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (*Continental Free Trade Area-CFTA*). Majadiliano hayo yatakapokamilika yatapanua zaidi soko na wigo wa wafanyabiashara nchini kufanya biashara katika Bara la Afrika. Aidha, tutatumia fursa hiyo kuvutia uwekezaji zaidi nchini na kuuzwa kwa unafuu katika masoko mapana ya kikanda na Afrika kwa ujumla.

• ***Biashara za Kimataifa***

*i)* Kushiriki katika majadiliano ya kutunga sheria za kibiashara kimataifa kupitia Mkutano wa 11 wa WTO wa Majadiliano Ngazi ya Mawaziri (WTO Ministerial Conference) unaotarajiwa kufanyika nchini Argentina mwaka 2017;

*ii)* Kushiriki katika majadiliano katika Kamati za Biashara za Kudumu za WTO (TBT, SPS na Trade Facilitation);

*iii)* Kuimarisha kamati za kitaifa za kusimamia urahisishaji wa biashara nchini ambazo ni;

• Kamati ya Kusimamia Uondoaji wa Vikwazo vya Kibiashara Visivyokuwa vya Kiushuru (NTBs);

• Kamati ya Urahisishaji Biashara (National Trade Facilitation Committee);

- Kamati ya Usimamizi wa Masuala ya Afya za Binadamu, Wanyama na Mimea (National SPS Committee); na
- Kamati ya Vikwazo vya Biashara vya Kiufundi (National TBT Committee).

*(b) Kukamilisha mapendekezo ya uandikaji upya wa Sheria ya Anti-Dumping and Countervailing Measures. Sheria hiyo ikikamilika, itasaidia kuvilinda viwanda na wafanyabiashara nchini dhidi ya athari ya bidhaa shindani zinazouzwa nchini kwa bei ya chini kwa udanganyifu, tofauti na bei halisi ya soko;*

*(c) Kuratibu zoezi la kuridhiwa kwa Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) wa Urahisishaji wa Biashara (Trade Facilitation Agreement-TF). Wizara itawasilisha rasimu ya pili ya Waraka wa kuridhiwa Mkataba huo ambao utaongeza chachu ya maboresho yanayoendelea nchini ya kurahisisha ufanyaji biashara. Kupitia Mkataba huo, Tanzania itapata fursa za ziada za kifedha na kiufundi kuzidisha kasi ya maboresho ya ufanyaji biashara nchini;*

*(d) Kuendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kitaifa ya Urahisishaji Biashara (National Committee for Trade Facilitation), na*

*(e) Kuratibu na kushiriki kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa katika mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa na mengineyo ikiwemo UNCTAD, CFC na ITC.*

#### **5.1.4 Sekta ya Masoko**

**266. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018; Wizara itatekeleza yafuatayo:-

*(a) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji*

*i) Kuondoa tozo, kero, ada zinazojirudia na kurazinisha majukumu ya taasisi za udhibiti;*

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

*ii)* Kuondoa mwingiliano wa majukumu ya taasisi za umma ili kupunguza gharama za uanzishaji na uendeshaji wa biashara;

*iii)* Kuhakikisha huduma za usajili wa biashara unafanyika kupitia mitandao ya kompyuta (online registration) na usajili wa makampuni ufanyike kwa muda mfupi kadiri iwezekanavyo; na

*iv)* Kuhamisha jukumu la utoaji wa leseni za biashara toka Wizarani (Daraja A) kwenda BRELA na kutolewa katika kanda za Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Mbeya, Mtwara na Mwanza.

*(b) Kuwaunganisha wazalishaji na masoko*

*i)* Kuwahamasisha wakulima kuzalisha na kuwaunganisha na viwanda vya usindikaji;

*ii)* Kushirikiana na viwanda kutafuta masoko ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini;

*(c) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala*

*i)* Kuhamasisha sekta binafsi kujenga maghala;

*ii)* Kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa maeneo yote yanayozalisha zao la korosho;

*iii)* Kuanzisha matumizi ya Mfumo kwa mazao ya ufuta, mbaazi, mahindi na nafaka; na

*iv)* Kuunganisha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Mazao na Bidhaa (commodity exchange)

*(d) Kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vituo maalum vya kuuzia mazao*

*i)* Kusimamia matumizi ya vituo hivyo ili vitumike kwa uuzaji na ununuzi wa mazao;

ii) Kuhamasisha ushindani wakati wa kununua na kuuza ili mkulima apate bei nzuri; na

iii) Kusimamia na kuhimiza matumizi ya vipimo rasmi kwa nia ya kumlinda mlaji.

*(e) Kuimarisha biashara na masoko ya mipakani*

i) Kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kujenga Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi Mipakani;

ii) Kutoa elimu kwa jamii ya wafanyabiashara kuhusu fursa na taratibu za kufanya biashara ya mipakani (cross border trade); na

iii) Kubainisha vikwazo vya kufanya biashara mipakani na kushirikiana na mamlaka nyingine katika kuviondoa.

*(f) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania*

i) Kuwapatia mabanda wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo na makundi maalum kutangaza bidhaa kupitia maonesho;

ii) Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali na wafanyabiashara wa Tanzania katika maonesho ya ndani na nje ya nchi; na

iii) Kuratibu ushiriki wa sekta binafsi na wataalam wa Serikali katika safari maalum za kutafuta fursa za masoko nje ya nchi.

*(g) Kuimarisha na kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Masoko*

i) Kupanua wigo wa vyanzo na aina ya taarifa za masoko; na

ii) Kutoa vitendea kazi vya kisasa kwa vyanzo vya taarifa na kukuza matumizi ya TEHAMA kukusanya na kusambaza taarifa muhimu za masoko.

*(h) Kuandaa na kupitia Sera, Sheria na Kanuni za mbalimbali*

*i) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji (National Consumer Protection Policy);*

*ii) Kuandaa Sera ya Taifa ya Viwango (National Quality Policy);*

*iii) Kukamilisha Sera na Mkakati wa Miliki Bunifu;*

*iv) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 na Kanuni zake;*

*v) Kukamilisha Marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya Mwaka 1999;*

*vi) Kuandaa Kanuni za utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Vipimo ya 2016;*

*vii) Kushirikiana na OR-TAMISEMI kuandaa sheria ndogo ya kusimamia matumizi ya vipimo rasmi katika biashara ngazi ya vitongoji, vijiji na wilaya ; na*

*viii) Kuandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje.*

### **5.1.5 Sekta ya Uwekezaji**

**267. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

*(a) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996;*

*i) Kuratibu uwepo wa mazingira bora ya uwekezaji;*

*ii) Kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini; na*

*iii) Kuhamasisha wawekezaji wa ndani kuchangamkia fursa za uwekezaji za kikanda na kimataifa.*



*(b) Kukamilisha mapitio ya Sera, Mkakati na Sheria ya Uwekezaji*

- i) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996;*
- ii) Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Uwekezaji ya 1997; na*
- iii) Kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji.*

*(c) Kufuatilia miradi ya uwekezaji nchini*

- i) Kuratibu uanzishwaji wa kamati ya kitaifa ya kufuatilia uwekezaji nchini; na*
- ii) Kufanya tathmini ya miradi yote iliyowekezwa nchini.*

*(d) Kuratibu kwa karibu uwekezaji katika sekta maalum*

- i) Kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya sukari;*
- ii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu (deep sea) na viwanda vya samaki; na*
- iii) Kuanzisha na kuboresha vivutio vya uwekezaji katika viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi "Light Manufacturing".*

## **5.2 TAASISI CHINI YA WIZARA**

### **5.2.1 Shirika la Maendeleo la Taifa**

**268. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018; Wizara kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) itatekeleza malengo yafuatayo:

*(a) Kukamilisha mapitio ya vivutio na Mkataba wa Utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma na kuanza utekelezaji;*

*(b) Kuendelea kutafuta mwekezaji wa kutekeleza Mradi wa Kuzalisha Magadi wa Engaruka;*

(c) Kuendelea kutafuta mwekezaji atakayeingia ubia na Serikali kwa ajili ya kufufua Kiwanda cha Matairi cha Arusha;

(d) Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa Kufufua Kiwanda cha KMTC;

(e) Kuhamasisha utekelezaji wa Mradi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta katika eneo la TAMCO;

(f) Kuendeleza utekelezaji wa mradi wa viwanda vya kusindika nyama Dodoma, Kibaha na Pwani;

(g) Kuendelea kutafuta mwekezaji kwa ajili ya kuendeleza mradi wa kuzalisha mafuta kutokana na michikichi;

(h) Kuendelea kutafuta mwekezaji kwa ajili ya wa Mradi wa Kilimo cha Ufuta katika Kijiji cha Mandawa;

(i) Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Miundombinu katika Eneo la Viwanda la TAMCO Kibaha;

(j) Kuanzisha upembuzi yakinifu wa kuanza ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Asili (biofertilizer) katika eneo la Kiwanda cha Biolarvicides (viuadudu);

(k) Kugawa eneo la viwanda (*Cadastral survey*) eneo la KMTC; na

(l) Kwa kushirikiana na RAHCO kutafuta mwekezaji kwa ajili ya kuanzisha mgodi wa mawe wa kuzalisha kokoto za zege, reli, ujenzi na kiwanda cha kutengeneza nguzo za umeme, taa za barabarani na simu (*concrete electric poles*), Muheza Tanga.

### 5.2.2 Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania

**269. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuendelea kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;

(b) Kuanzisha na kuhakiki maabara ya makaa ya mawe, mafuta na gesi itakayokuwa na viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

(c) Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ngozi jinsi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama 'Leather boards';

(d) Kuendelea na kukamilisha mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya mazingira, kemia na ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

(e) Kuanzisha na kuhakiki (Accreditation) maabara ya vipimo vya chuma kigumu (Iron and Steel metallurgy laboratory);

(f) Kufanya matengenezo ya vifaa vya maabara ya mazingira, chakula na kemia;

(g) Kutafiti vigezo vya uzalishaji wa chuma cha pua (steel bar production parameter) katika viwanda/mashine za kawaida za chuma (conventional rolling mill); na

(h) Kuendelea kukamilisha mapitio ya Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO kwa kuwasilisha ripoti ya mapitio ya sheria kwa Wizara mama (Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji) na hatimaye kupelekwa Bungeni.

### **5.2.3 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo**

**270. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kujenga uwezo wa taasisi katika kubuni, kuendeleza na kusambaza teknolojia kwa kuboresha (upgrade) na kukarabati vitendea kazi (maschine na vifaa mbalimbali) vya karakana ya kuunda na kuendeleza chasili, kuboresha vitendea kazi katika ofisi za usanifu zikiwemo programu zitumikazo katika shughuli za ubunifu na usanifu na kuongeza ujuzi wa wafanyakazi wa taasisi katika teknolojia ya utengenezaji wa hali ya juu;

(b) Kuboresha, kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji na utumiaji kibiashara wa mitambo ya kusindika mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za mafuta. Mitambo hiyo inahusisha mashine za kusafisha mbegu, kukamua, kuchuja na kusafisha mafuta (refining);

(c) Kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji kibiashara wa teknolojia za kuzalisha bidhaa za marumaru kama vile vigae vya marumaru (ceramic tiles) kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini;

(d) Kuboresha teknolojia za kuteketeza taka ngumu na hatarishi zitokanazo na utoaji wa huduma za afya na huduma za udhibiti kwa lengo la kulinda afya na mazingira;

(e) Kubuni na kuendeleza teknolojia jadidifu hususan mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji na nishati ya upepo na mtambo wa kutengeneza kuni na mkaa utokanao na mabaki ya mimea au vumbi la makaa ya mawe, na

(f) Kufanya utafiti kuhusu aina ya vifaa vya pikipiki na vifaa vya pikipiki za miguu mitatu vinavyoweza kutengenezwa nchini na kufanya majaribio na kutengeneza utaratibu wa kuunda (manufacturing process) vipuri vya pikipiki hapa nchini kwa kuwezesha wajasiriamali watengenezaji.

#### **5.2.4 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini**

**271. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kujenga uelewa na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kununua zana za kilimo zilizofanyiwa majaribio nchini;

(b) Kujenga maabara kwa ajili ya majaribio ya zana za kilimo;

(c) Kutafiti mahitaji, kuendeleza na kutengeneza teknolojia mbalimbali za kilimo na ufundi vijijini hasa kwenye uendelezaji wa teknolojia ya trekta la CAMARTEC (CFT), teknolojia za vipandio za kukokotwa na ng'ombe na kuvutwa na trekta (planters), na mashine za kuvuna na kuchakata mazao ya mifugo, alizeti, mbaazi, mahindi na mpunga (agro-processing) kwa kushirikiana na wadau wetu wa ndani (wabunifu, wajisiliamali, vyo vikiu na mashirika ya sio ya kiserikali); na

(d) Kutafiti na kuendeleza usambazaji wa teknolojia za matumizi bora ya nishati ya kuni, mkaa na biogesi kwa kushirikiana na wajasiriamali, makampuni binafsi, mafundi, Wizara ya Nishati na Madini, Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) na wadau wetu wa maendeleo ambao ni *Africa Biogas Partnership Programme (ABPP)*.

### 5.2.5 Kampuni ya Mbolea Tanzania

**272. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kukamilisha majadiliano ya kuanzisha mtambo wa kutengeneza mbolea aina ya NPKs nchini;

(b) Kuanza utekelezaji wa Makubaliano ya Awali (MoU) na Kampuni ya OCP ya Morocco wa kununua mbolea kutoka Kampuni hiyo na kuisambaza nchini; na

(c) Kuendelea kununua na kusambaza mbolea za aina mbalimbali nchini.

## 5.2.6 Mamlaka ya Kuendeleza Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje

**273. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Mamlaka ya Kuendeleza Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo Nje (EPZA) itatekeleza yafuatayo:

### **a) Bagamoyo SEZ**

*i)* Kuratibu usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu ya ndani ya mradi kwa awamu ya kwanza;

*ii)* Kuratibu uboreshaji wa makazi holela (*Regularization and upgrading*) ya maeneo ya makazi ya Kiromo, Mlingotini na Zinga; na

*iii)* Kuratibu ujenzi na usambazaji wa miundombinu ya nje, umeme na maji kufikia eneo la mradi, (*offsite infrastructure*).

### **b) Kurasini Trade and Logistic Centre**

*i)* Kuhakikisha upatikanaji wa hati miliki ya eneo lote la mradi; na

*ii)* Kuingia ubia na sekta binafsi katika kuendeleza na kuendesha mradi.

### **c) SEZ za Bunda, Kigoma, Manyoni, Mtwara, Ruvuma na Tanga**

*i)* Kumalizia malipo ya fidia katika maeneo ya mradi yaliyofanyiwa uthamini ya Kigoma, Manyoni, Ruvuma na Tanga SEZ;

*ii)* Kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu ya ndani katika maeneo ya mradi wa Kigoma;

*iii)* Kupima viwanja (survey) na gharama za usajili wa hati miliki katika maeneo ya miradi ya Bunda, Kigoma, Manyoni na Tanga; na

iv) Kuendelea kutangaza miradi kitaifa na kimataifa na kuendeleza shughuli zote za maaendeleo ya miradi ya Ruvuma na Tanga.

### **5.2.7 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo**

**274. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) itatekeleza malengo yafuatayo:

**a) Kujenga maeneo ya viwanda katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, na Simiyu;**

i) Kujenga miundombinu ya viwanda (barabara, mifumo ya maji, Umeme na mitaro ya maji machafu) katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, na Simiyu;.

ii) Kujenga mabanda ya viwanda kumi na moja katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, na Simiyu;

iii) Kujenga ofisi za SIDO za kutolea huduma katika mikoa mipya ya Geita na Simiyu ; na

iv) Kusajili viwanda vyote vidogo nchini.

**b) Kuimarisha uwezo wa uhawilishaji wa teknolojia;**

i) Kuimarisha Kituo cha Maendeleo ya Teknolojia cha Shinyanga; na

ii) Kuwezesha utengenezaji na usambazaji wa teknolojia rahisi za vijijini.

**c) Kutekeleza Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja (ODOP);**

i) Kupitia upya maelezo na takwimu za kila Wilaya na kutengeneza maandiko yatayotumiwa na watu kuanzishia miradi ; na

ii) Kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo.

**d)** *Kuhakikisha upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali* - Kwa kuuongezea mtaji Mfuko wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wananchi (NEDF).

### 5.2.8 Chama cha Hakimiliki Tanzania

**275. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza makusanyo ya mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za sanaa / muziki na kugawa kwa wasanii;

(b) Kuendeleza mazungumzo na mashirika ya utangazaji ili waanze kulipia mirabaha;

(c) Kutoa elimu kwa wananchi na wadau wa sanaa kuhusiana na mambo ya Hakimiliki na Hakishiriki;

(d) Kufanya ukaguzi wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki (anti piracy raids);

(e) Kushughulikia migogoro na kesi za Hakimiliki na Hakishiriki;

(f) Kushughulikia marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na.7/1999 na Kanuni za Leseni na kanuni zingine zinazohusiana na Hakimiliki; na

(g) Kuendelea kusajili wanachama wasanii na kazi zao.

### 5.2.9 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala

**276. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuandaa Sera ya Uwekezaji, uendeshaji wa Akaunti ya Kinga ya utendaji kwa waendeshaji wa ghala na Sera ya Mafunzo ili kuongeza ufanisi;



(b) Kufuatilia vibali vya ajira kujaza nafasi zilizo wazi katika ikama ya Bodi;

(c) Kuandaa mkutano wa wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

(d) Kuainisha na kufanya ukaguzi wa ghala zilizosajiliwa chini ya mfumo na zinazotarajiwa kusajiliwa;

(e) Kutafuta na kuboresha vyanzo vya ndani vya mapato kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Bodi;

(f) Kuandaa warsha za kisekta kwa wadau kama chombo cha kupata mrejesho wa uendeshaji wa Mfumo kutoka kwa wadau wa zao husika;

(g) Kupata mtaalamu/mshauri mwelekezi kwa ajili ya kuandaa, Sera ya Uwekezaji, Sera ya kuendesha Akaunti ya Kinga ya Utendaji pamoja na taratibu za ndani juu ya utoaji wa leseni za kuendesha ghala;

(h) Kupitia upya Mpango Mkakati wa Bodi ili kuainisha na kuyaondoa majukumu yaliyokwisha kutekelezwa na kuongeza majukumu mengine ya kipaumbele katika taasisi;

(i) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo husika;

(j) Kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi kwa wadau wote ili waelewe na kutekeleza kwa ufanisi;

(k) Kushiriki katika Maonesho ya Sabasaba na Nanenane ili kutoa elimu ya mfumo kwa wadau hususan wadau wa kilimo; na

(l) Kufanya maandalizi ya kuhamia Dodoma.

#### **5.2.10 Baraza la Ushindani**

**277. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa udhibiti na ushindani wa kibiashara nchini;

(b) Kuongeza uwezo wa Baraza katika kushughulikia kesi zinazohusu masuala ya ushindani wa kibiashara kwa kuwaongezea ujuzi Wajumbe wa Baraza, Watumishi wa Baraza sambamba na maboresho katika mifumo ya utendaji kazi wa Baraza;

(c) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza, umuhimu katika uchumi pamoja na namna ya kuwasilisha rufaa katika Baraza; na

(d) Kuendelea kushughulikia masuala mtambuka ikiwa ni pamoja na utawala bora na mapambano dhidi ya UKIMWI na Virusi vya UKIMWI.

#### **5.2.11 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni**

**278. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018; Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuendelea kuboresha mifumo na taratibu za utoaji huduma kwa kutumia njia za kiteknolojia ili kutoa huduma bora na kwa wakati;

(b) Kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua vituo vya kutoa huduma mikoani na wilayani;

(c) Kuboresha mifumo ya uwajibikaji, weledi na uadilifu kwa watumishi wa BRELA;

(d) Kujenga mifumo thabiti ya mawasiliano ndani na nje ya ofisi;

(e) Kupitia upya muundo wa wakala ili uweze kwenda na wakati;

(f) Kupitia sheria zote zinazosimamiwa na Wakala ili ziweze kwenda na wakati;

(g) Kuendelea kutoa Elimu na Uhamasishaji wa Usajili na Urasimishaji wa Biashara kwa wananchi katika ngazi za mikoa na wilaya; na

(h) Kuanzisha utoaji wa leseni za biashara daraja la kwanza kwa ngazi za kanda.

### 5.2.12 Wakala wa Vipimo

**279. Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukagua na kusimamia matumizi sahihi ya vipimo 745,702;

(b) Kutoa elimu kwa umma kupitia maonesho saba (Sabasaba, Nanenane, MOWE), kuandaa na kufanya vipindi kumi vya televisheni na radio na matangazo matano kuhusu matumizi sahihi ya vipimo;

(c) Kuiboresha kanzidata ya vipimo itakayotumiwa wakati wa kupanga mipango ya Wakala;

(d) Kununua vitendea kazi yakiwemo magari kumi na vihakiki mita za maji, umeme na gesi;

(e) Kuanzisha na kutekeleza Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) ili kuimarisha utunzaji wa takwimu mbalimbali;

(f) Kuongeza idadi ya watumishi 96 na kuwaongezea uwezo wa kitaalam waliopo ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia;

(g) Kufanya maboresho ya ofisi nne za Wakala wa Vipimo katika mikoa Tanzania Bara na kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Upimaji Matenki ya Mafuta Misugusugu Kibaha;

(h) Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika kutekeleza majukumu ya Wakala; na

(i) Kuongeza juhudi katika ukaguzi wa bidhaa

zilizofungashwa kwenye maeneo mbalimbali ya mipakani, bandarini na viwandani kwa lengo la kuhakiki uzito, ujazo, vipimo vya urefu au namba kwa lengo la kumlinda mlaji.

### **5.2.13 Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji**

**280. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (NCAC) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuifanyia marekebisho Sheria ya Tume ya Ushindani ili iweze kuruhusu ajira ya Afisa Mtekelezaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Mtetezi wa Mlaji;

(b) Kuanda hadidu za rejea za Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji; na

(c) Kumwandaa Mtaalamu Mwelekezi kuandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji.

### **5.2.14 Shirika la Viwango la Taifa**

**281. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Shirika la Viwango la Taifa (TBS) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia kwa nguvu zote ubora wa bidhaa hasa zinazotoka nje ili kulinda viwanda vya ndani;

(b) Kutayarishawiwango 350 vyakitaifakatikasektandogondogo, ambavyo kati ya hivyo 120 ni vya uhandisi (Engineering) na 230 ni vya usindikaji (Process Technology);

(c) Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 240 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo (SMEs);

(d) Kukagua ubora wa bidhaa 34,000 zitokazo nchi za nje kabla ya kuingia nchini (Pre-shipment Verification of Conformity to Standards- PVoC (CoCs));

*(e)* Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 42,000 za magari yaliyotumika (used motor vehicles) yanayoingizwa nchini;

*(f)* Kutoa hati 45 chini ya Mpango wa Msaada wa Kiufundi kwa Wauzaji wa Bidhaa za Nje (Technical Assistance to Expoters - TAE);

*(g)* Kutoa mafunzo na semina 30 kuhusu viwango na udhibiti wa ubora (Quality Assurance Training) kwa wadau mbalimbali;

*(h)* Kupima sampuli 10,000 za bidhaa mbalimbali;

*(i)* Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 8,000;

*(j)* Kufungua ofisi mpya tano za mipakani;

*(k)* Kujenga maabara mpya ya kisasa (New TBS Test House);

*(l)* Kuanzisha na kufungua ofisi mpya tano za kanda, (Kanda ya Kaskazini-Arusha, Kanda ya Nyanda za Juu-Mbeya, Kanda ya Ziwa- Mwanza, Kanda ya Kati-Dodoma na Kanda ya Kusini- Mtwara); na

*(m)* Kuajiri wafanyakazi 136 kwa kibali cha mwaka 2015/2016 na wafanyakazi 114 kwa mwaka 2017/2018.

### **5.2.15 Tume ya Ushindani**

**282. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza yafuatayo:

*(a)* Kudhibiti na Kupambana na Uingizaji na Uzalishaji wa Bidhaa Bandia;

*i)* Tume ya Ushindani itafanya kaguzi za kushtukiza katika mikoa mbalimbali. Kaguzi hizo zitahusisha bidhaa mbalimbali kama vile zitakavyowekwa kwenye mpango kazi wa mwaka

husika na zile zitakazoripotiwa na Wamiliki wa Hataza (brand owners);

*ii)* Tume ya Ushindani itaendelea na ukaguzi bandarini na katika bandari kavu (ICDs) kama itakavyotakiwa katika mpango kazi wa mwaka 2017/18;

*iii)* Tume ya Ushindani inaendelea kujipanga katika mpango kazi wake wa mwaka 2017/18 ili kuweza kuwa na ofisi katika mikoa mbalimbali kama ambavyo imekuwa ikiombwa/ ikishauriwa kwa nyakati tofauti tofauti, na kuanzia mikoa inayotarajiwa ni Tanga, Arusha na Mwanza; na

*iv)* Kuendelea na juhudi za kupambana na kuthibiti bidhaa bandia ambazo zinachangia katika kudidimiza soko la Tanzania.

*(b) Uchunguzi na Usikilizaji wa Kesi za Ushindani;*

*i)* Kuendelea kuchunguza na kuchukua hatua za kisheria juu ya mashauri mbalimbali yahasuyo makubaliano yanayofifisha ushindani "Anti- competitive agreement";

*ii)* Kuchunguza mashauri yahasuyo miungano ya makampuni ambayo haikutolewa taarifa kwenye Tume "Un-notified mergers"; na

*iii)* Kuchunguza na kuchukua hatua za utekelezaji wa sheria juu ya mashauri yahasuyo matumizi mabaya ya nguvu katika soko "Abuse of market power".

*(c) Utafiti wa Masoko ili Kubaini Matatizo ya Ushindani Usio wa Haki na Masoko husika na Hatua za Kurekebisha;*

*i)* Kufanya utafiti katika Sekta ya Afya zitakazohusisha upitiaji wa maandiko, uandaaji wa andiko dhana na ukusanyaji wa takwimu na taarifa muhimu kutoka maeneo mbalimbali; na

*ii)* Kufanya utafiti katika sekta nyingine kama itakavyoagizwa.

*(d) Kumlinda na Kumuelimisha Mlaji;*

*i) Kuendelea kushughulikia malalamiko ya walaji wa bidhaa na huduma;*

*ii) Kufanya mapitio na usajili wa mikataba ya walaji;*

*iii) Kushiriki katika kutengeneza Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji;*

*iv) Kuendelea kusikiliza na kushughulikia malalamiko kuhusu bidhaa zisizo salama; na*

*v) Kuandaa miongozo kuhusu sheria ya kumlinda mlaji na mikataba inayomkandamiza mlaji.*

#### **5.2.16 Kituo cha Uwekezaji Tanzania**

**283. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) itatekeleza yafuatayo:

*(a) Kufanya uhamasishaji kwa kuwalenga wawekezaji wa nje (Targeted Investment Promotion) na pia kufanya uhamasishaji wa wawekezaji wa ndani ili kuvutia wawekezaji kwenye sekta muhimu zitakazokuza uchumi wa nchi kwa haraka hususan Sekta ya Viwanda;*

*(b) Kuimarisha Kitengo cha Kuperemba Miradi ya Uwekezaji (Monitoring and Evaluation) kwa lengo la kuhakiki miradi iliyoandikishwa TIC;*

*(c) Kutembelea miradi iliyosajiliwa na TIC kwa lengo la kutatua matatizo yanayowakabili wakati wa kutekeleza miradi yao;*

*(d) Kuwasaidia wawekezaji kupata vibali na hati mbalimbali za kisheria ili waweze kuwekeza hapa nchini;*

*(e) Kufanya tafiti mbalimbali zitakazotumika kuishauri Serikali kuhusu Sera ya Uwekezaji;*

(f) Kuhudumia wawekezaji kwa kuboresha huduma mahali pamoja (One Stop Shop) na kuwezesha usajili kwa njia ya mtandao;

(g) Kuchapisha na kusambaza taarifa sahihi kwa wawekezaji kuhusu fursa za uwekezaji pamoja na upatikanaji wa mitaji ya wabia;

(h) Kushirikiana na Serikali kutafuta maeneo yenye ardhi inayofaa kuwekeza kwa ajili ya wawekezaji;

(i) Kuwasaidia wajasiliamali wadogo na wa kati kuibua fursa za uwekezaji na pia kuwaunganisha na wafanyabiashara wakubwa (Business Linkages) kwa lengo la kukuza biashara zao na kuongeza kipato;

(j) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; na

(k) Kutekeleza mkakati wa kukitangaza kituo na kazi zake kwa wawekezaji na wanaotaka kuwekeza (Information and Communication Campaign) ili wafahamu vivutio vya uwekezaji vilivyopo nchini.

## 5.2.17 Chuo cha Elimu ya Biashara

**284. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kukamilisha ujenzi wa ghorofa tatu katika Jengo la 'Cafeteria' (Vertical Extension of Cafeteria Building) Kampasi ya Dar es Salaam kwa ajili ya maktaba mpya, madarasa pamoja na kumbi za mihadhara;

(b) Kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa ghorofa tisa katika Kampasi ya Dar es Salaam;

(c) Ujenzi na ukarabati wa majengo katika Kampasi ya Mwanza;



(d) Awamu ya pili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya katika eneo la Iganzo;

(e) Ujenzi wa Kampasi ya Zanzibar;

(f) Kuboresha mifumo ya TEHAMA; na,

(g) Kuimarisha uwezo wa watumishi (Capacity building) katika mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya shahada za uzamili na uzamivu.

## 5.2.18 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania

**285. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) itatekeleza yafuatayo:-

(a) *Kuboresha Upatikanaji wa Soko la Bidhaa na Huduma zinazozalishwa Nchini;*

Katika kutimiza jukumu hilo, TanTrade kwa kushirikiana na Mamlaka zingine za Serikali na sekta binafsi, imedhamiria kuboresha uratibu wa maonesho ya biashara yanayofanyika hapa nchini yakiwemo Maonesho ya 41 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Maonesho ya Nanenane na Maonesho ya SIDO. Pia itaratibu na kuongoza misafara na mikutano ya kibiashara, kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Maonesho ya Kibiashara ya Kigali-Rwanda, Nairobi-Kenya, Maputo-Msumbiji na Bujumbula – Burundi. Vilevile, itaratibu Tamasha la Biashara Mjini Zanzibar na pia kukusanya na kusambaza kwa wadau mbalimbali hususan wazalishaji na wafanyabiashara wa Tanzania taarifa za biashara na masoko ya bidhaa mbalimbali zinazozalishwa hapa nchini.

(b) *Kuratibu na Kudhibiti Uendeshaji wa Maonesho ya Kimataifa Nchini kwa Mujibu wa Sheria;*

Mamlaka itaendelea kutoa vibali kwa waandaji wote wa maonesho ya kimataifa yatakayoandaliwa nchini na nje ya nchi na kuhakikisha kuwa waandaaji hao wanafuata

taratibu za uandaaji wa maonesho kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya ubora kiwemo usalama wa watembeleaji, usafi, upatikanaji wa huduma muhimu zikiwemo choo na matibabu ya dharula, mpangilio wa majengo na usafiri wa uhakika.

*(c) Kuimarisha na Kujengea Uwezo Sekta Ndogo na ya Kati ya Biashara (SMEs) ili iweze Kujindesha Kiushindani;*

TanTrade itaendelea na jukumu lake la msingi la kuwajengea wazalishaji na wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs) uwezo kwa njia ya mafunzo, kuwapa taarifa za biashara na masoko, kutatua changamoto na vikwazo vya kiutendaji na kuweka mazingira rafiki ya kibiashara ili waweze kufikia vigezo vya ushindani na kuongeza tija na ufanisi kimataifa katika uzalishaji na biashara zao.

*(d) Kuongeza Ushindani katika Sekta ya Biashara;*

TanTrade kwa kushirikiana na sekta binafsi, taasisi na wizara za serikali itahimiza uchakataji wa bidhaa asili za Tanzania ikiwemo mazao ya kilimo, misitu, uvuvi na madini kabla hazijauzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Hatua hiyo imelenga kuongeza thamani ya bidhaa husika, ajira kwa rasilimali za Tanzania ikiwemo rasilimali watu (wafanyakazi), ardhi na madini. TanTrade kwa kushirikiana na vituo vya uwekezaji TIC, ZIPA na EPZA itahimiza utengenezaji wa bidhaa za mwisho (Final Consumer Goods) kwa maliasili zinazozalishwa hapa nchini zikiwemo nguo, bidhaa za ngozi, unga wa kakao, mafuta ya kupikia, kwa kutaja machache.

### **5.3 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU NA UTOAJI WA HUDUMA**

#### **5.3.1 Maendeleo ya Rasilimali Watu**

**286. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza yafuatayo:

*(a)* Kuhamishia watumishi 81 Makao Makuu ya Nchi Dodoma katika Awamu ya Tatu;

(b) Kuajiri watumishi wapya 23 wa kada mbalimbali ili kuziwezesha Idara na Vitengo kupata rasilimali watu ya kutosha ili kutoa huduma bora inayotarajiwa;

(c) Kupandisha vyeo watumishi 143 wa kada mbalimbali;

(d) Kujenga uwezo kwa rasilimali watu kwa kuwapeleka watumishi kumi na tano katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi hamsini katika mafunzo ya muda mfupi katika vyo mbalimbali ambayo yatawasaidia kuboresha utendaji wao wa kazi na kukidhi mahitaji ya kimuundo katika kada mbalimbali;

(e) Katika Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKA au OPRAS), Wizara itatekeleza yafuatayo;

i) Kutoa mafunzo kwa watumishi wapya watakaoajiriwa kuhusu namna ya ujazaji wa fomu za OPRAS;

ii) Kuhakikisha kuwa watumishi wote wanasaini mikataba yao ya kazi kwa wakati;

iii) Kufanya mapitio ya nusu mwaka; na

iv) Kufanya tathmini ya utendaji kazi wa watumishi wa mwaka mzima kwa wakati.

(f) Kuwa na program mbalimbali za michezo kwa lengo la kujenga afya za watumishi, kushirikiana na kufahamiana;

(g) Kuendelea na uratibu wa masuala ya uendeshaji wa shughuli za Wizara;

(h) Kuratibu shughuli za utoaji huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Taratibu, Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma; na

(i) Kuhakikisha watumishi watakaohitimisha ajira zao wanalipwa mafao kwa wakati.

### 5.3.2 Usimamizi wa Ununuzi

**287. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuandaa Mpango wa Ununuzi wa Wizara kwa mwaka 2017/2018;

(b) Kuratibu vikao vya Bodi ya Zabuni;

(c) Kufanya ununuzi na kugawa bidhaa na huduma mbali mbali kwa mujibu wa Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2017/2018 ambapo taarifa za ununuzi za kila mwezi na kila robo ya mwaka zitaandaliwa na kuwasilishwa kwenye Taasisi ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA); na

(d) Kuhakiki mali za Wizara (Physical Verification and stock taking) kwa mwaka 2017/2018 na kufanikisha uhuishaji wa Daftari la Mali za Wizara (Updating Asset Register) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka 2001 na Kanuni zake, na GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

### 5.3.3 Masuala Mtambuka

#### (a) Kudhibiti Rushwa

**288. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi wake kwa kuweka mikakati mbalimbali na kutoa mafunzo ya sheria mbalimbali za kazi, kanuni na taratibu zinazotoa miongozo ya utoaji wa huduma bora na uwajibikaji katika utumishi wa umma na kuhakikisha kuwa zinafuatwa. Aidha, Wizara itahakikisha kuwa inawachukulia hatua za kinidhamu watumishi ambao watabainika kujihusisha na vitendo vya rushwa. Pia, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya elimu ya Huduma kwa Mteja kwa watumishi ili kuwapatia mbinu za utoaji huduma bora kwa wateja wake wa ndani na nje ya Wizara.

#### (b) Mazingira

**289. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara itahakikisha inaongeza uelewa kwa wenye viwanda

juu ya matumizi ya mitambo ya kisasa katika uzalishaji ili kupunguza utiririshaji wa majitaka hususan yale yaliyo na kemikali ambayo huchafua vyanzo vya maji na pia kwa viwanda kupunguza uzalishaji wa taka ngumu.

**(c) Kupambana na UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza**

**290. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) mahala pa kazi kwa kutoa huduma bora kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI waliojiweka wazi kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhamasisha watumishi juu ya masuala ya UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza pamoja na upimaji wa afya zao kwa hiari mara kwa mara.

**(d) Masuala ya Jinsia**

**291. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Dawati la Jinsia itatekeleza yafuatayo:

*i)* Kuhuisha masuala ya jinsia katika mipango ya uzalishaji wa mazao na mnyororo wa thamani katika bidhaa zinazozalishwa;

*ii)* Kushiriki katika mikutano ya kitaifa na kimataifa katika masuala ya kijinsia; na

*iii)* Kuandaa semina ya kuwajengea uwezo waratibu wa masuala ya jinsia Wizarani na katika Taasisi zilizo chini ya Wizara juu ya uratibu wa masuala ya jinsia, ufuatiliaji na tathmini.

**5.3.4 Usimamizi wa Mapato na Matumizi**

**292. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuhakikisha kwamba, kila anayefanya biashara hapa nchini anakuwa na leseni halali inayolingana na biashara anayoifanya. Aidha,

Maafisa Biashara wa Wizara na Kitengo cha Ufuatiliaji na Uperembaji (M & E Section) wakishirikiana na Maafisa Biashara walio katika Halmashauri na Manispaa zote nchini watafanya ukaguzi na kuchukua hatua za kisheria kwa mfanyabiashara yeyote atakayepatikana akifanya biashara bila leseni au leseni stahiki.

**293. Mheshimiwa Spika,** Wizara itahakikisha inafanya matumizi kulingana na kanuni, taratibu na sheria za fedha za Serikali. Matumizi yote yatafanyika kulingana na mpangilio wa Bajeti ya Wizara (objective, targets and activities). Wizara katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, itaendelea kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kiweze kuhakikisha taratibu zote za fedha zinafuatwa na malipo yanafanyika kulingana na vipaumbele vilivyowekwa kwenye Bajeti ya Wizara. Aidha, Wahasibu wataendelea kupewa mafunzo ili kupanua taaluma zao na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Pia yatafanyika mafunzo ya muda mfupi kazini juu ya sheria, taratibu na kanuni za fedha na manunuzi ya umma kwa Wahasibu, Maafisa Ugavi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakurugenzi na Wahasibu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Lengo ni kuwapa mwangaza wa kuzijua sheria, taratibu na kanuni za msingi juu ya usimamizi wa fedha za Serikali. Mtumishi atakayefanya kinyume, sheria itachukua mkondo wake.

**294. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa niwasilishe maombi ya fedha kwa mwaka 2017/2018.

## **6.1 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018**

### **6.2 MAPATO YA SERIKALI**

**295. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi **20,000,000,000** kutokana na ada za leseni, uuzaji wa nyaraka za zabuni na faini kwa kukiuka sheria ya leseni za biashara.

### **6.3 MAOMBI YA JUMLA YA FEDHA**

**296. Mheshimiwa Spika,** maombi ya fedha kwa ajili ya

Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2017/2018 yapo katika Mafungu Mawili ambayo ni Fungu 44 (Viwanda) na Fungu 60 (Biashara na Uwekezaji). Kwa mwaka 2017/2018, Wizara imetengewa kwa Fungu 44 na Fungu 60 jumla ya Shilingi **122,215,109,750** kwa Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha, hizo Matumizi ya Kawaida ni Shilingi **42,024,732,750** na Matumizi ya Maendeleo ni Shilingi **80,190,377,000**.

#### 6.4 MAOMBI YA FEDHA FUNGU 44

**297. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu 44 (Viwanda) imetengewa jumla ya Shilingi **98,012,870,000** kwa ajili yakutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi **24,172,493,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **73,840,377,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa zinajumuisha Shilingi **4,569,373,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **19,603,120,000** kwa ajili ya Mishahara (PE). Kati ya fedha za Mishahara zilizotengwa, zinajumuisha **Shilingi 3,289,552,000** za Mishahara ya Wizara na Mishahara ya Mashirika chini ya Wizara (**Fungu 44**) **Shilingi 16,313,568,000**. Aidha, fedha za Matumizi Mengineyo yaani **Shilingi 4,569,373,000** ni kwa ajili ya Wizara (**Fungu 44**). Mashirika chini ya Wizara (**Fungu 44**) kwa mwaka huu wa fedha hayakutengewa Matumizi Mengineyo (OC).

**298. Mheshimiwa Spika**, fedha za Matumizi ya Maendeleo **Shilingi 73,840,377,000** zilizotengwa, zinajumuisha **Shilingi 73,575,068,000** fedha za ndani na Shilingi **265,309,000** fedha za nje. Aidha, katika fedha za ndani, **Shilingi 10,960,000,000** sawa na **asilimia 15** ya fedha za Matumizi ya Maendeleo ni kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 62,615,068,000** sawa na **asilimia 85** ya fedha za Matumizi ya Maendeleo ni kwa ajili ya Mashirika chini ya Wizara. Fedha za nje zote ni kwa ajili ya taasisi chini ya Wizara hususan katika kuboresha viwango katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

## 6.5 MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO ZA NDANI

**299. Mheshimiwa Spika**, fedha za ndani za Maendeleo, zimeelekezwa katika miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Miradi Mikubwa ya Kielelezo; Miradi ya Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi; Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO Kibaha; Kuendeleza Kongano za Viwanda; Kuendeleza Tafiti za Maendeleo ya Viwanda; Kuendeleza Viwanda Vidogo, Biashara Ndogo, Ujasiriamali na Kuongeza mtaji kwenye Mfuko wa NEDF.

**300. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 200,000,000** sawa na **asilimia 0.3** ya Bajeti ya Maendeleo (**Fungu 44**), zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza Miradi Mikubwa ya Kielelezo katika kuratibu na ufuatiliaji wa kazi za miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga katika Mkoa wa Njombe. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,070,000,000** sawa na **asilimia 2.8** ya Bajeti ya Maendeleo (**Fungu 44**) zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda ambayo ni pamoja na Mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka na Mradi wa Kufufua Kiwanda cha Matairi (General Tyre) Arusha.

**301. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 26,559,200,000** sawa na **asilimia 36.2** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44), zimetengwa kwa ajili ya Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Kanda hizo ni:- Kanda ya Bagamoyo (Technological Park), Tanga, Kigoma, Ruvuma na Manyoni ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Kituo cha Biashara cha Kurasini; hususan katika kukamilisha malipo ya fidia kwa wakazi watatu ambao nyumba zao hazikuthaminiwa hapo awali baada na Mthamini Mkuu wa Serikali wakati wa zoezi la uthamini.

**302. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 12,939,068,000**. sawa na **asilimia 17.6** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44), zimetengwa kwa ajili ya uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO, Kibaha ikiwa ni pamoja na kuendeleza viwanda vya nguo na Kiwanda cha Matrekta cha (URSUS). Vilevile, jumla



ya **Shilingi 10,500,000,000** sawa na **asilimia 14.3** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44), zimetengwa kwa ajili ya Kuendeleza Kongano za Viwanda hususan Kongano la Ngozi na Bidhaa za Ngozi Dodoma. Kimsingi, Kongano husaidia kuondoa changamoto za miundombinu duni, ukosefu wa mitaji, masoko na teknolojia duni na kuleta ufanisi kwenye viwanda vidogo, vya kati na vikubwa.

**303. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 6,500,000,000** sawa na **asilimia 8.9** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44), zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza tafiti za maendeleo ya viwanda katika taasisi za TIRDO, TEMDO na CAMARTEC.

**304. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 14,146,800,000** sawa na **asilimia 19.3** ya Bajeti ya Maendeleo, zimetengwa kwa ajili ya Kuendeleza Viwanda Vidogo, Biashara Ndogo na Ujasiriamali ikiwa ni pamoja na kujenga maeneo ya viwanda katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, Njombe, na Simiyu; Kutekeleza Mkakati wa Wilaya Moja Biadhaa (ODOP), na kuuongezea mtaji Mfuko wa NEDF. Vilevile, jumla ya **Shilingi 460,000,000** sawa na **asilimia 0.6** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44) , zimetengwa kwa ajili ya **Counter part funds** katika miradi ya *Gender, Trade Mainstreaming, KAIZEN Program, na UNIDO Programme*. Mchanganuo wa matumizi ya fedha za maendeleo unapatikana katika Kitabu cha nne cha Makadirio ya Fedha za Serikali kwa mwaka 2017/2018 katika Fungu 44.

## 6.6 MAOMBI YA FEDHA FUNGU 60

**305. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu la 60:Biashara na Uwekezaji imetengewa jumla ya Shilingi **24,202,239,750** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi **15,964,331,000** ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **6,350,000,000** ni ya Bajeti Matumizi ya Maendeleo.

**306. Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 1,887,908,750** za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 14,076,422,250** kwa ajili

ya Mishahara. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo zinajumuisha **Shilingi 1,805,185,000** za Matumizi Mengineyo ya Wizara na **Shilingi 82,723,750** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo kwa taasisi chini ya Wizara. Aidha, kati ya fedha ilizotengwa kwa ajili ya Mishahara zinajumuisha **Shilingi 1,116,186,000** Mishahara ya Wizara na **Shilingi 14,848,145,000** Mishahara ya taasisi chini ya Wizara (Fungu 60).

## 6.7 MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO

**307. Mheshimiwa Spika**, kati ya **Shilingi 6,350,000,000** Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo zilizotengwa kwa mwaka 2017/2018 (Fungu 60), **Shilingi 2,000,000,000** ambazo ni **asilimia 308**.

**31.5** ya fedha za Fungu 60 zimetengwa kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 4,350,000,000** ambazo ni **asilimia 65.5** zimetengwa kwa ajili ya taasisi chini ya Wizara. Fedha hizo zimeelekezwa katika Mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) na Mradi wa Kuimarisha taasisi chini ya Wizara (*Institution Support*) mtawalia. **Mheshimiwa Spika**, katika fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya kuimarisha taasisi chini ya Wizara zinajumuisha **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) hususan kuchangia katika kujenga jengo la maabara ya kisasa litakalokuwa na ghorofa sita; **Shilingi 1,650,000,000** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uhakiki na upimaji (*Secondary and working standards*) kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa Wakala wa Vipimo; **Shilingi 500,000,000** kwa ajili ya kuendeleza biashara hususan kuandaa Mpango Kabambe wa Kuboresha Miundombinu ya Uwanja wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa wa Mwalimu Julius K. Nyerere Barabara ya Kilwa Dar- es Salaam, na **Shilingi 200,000,000** kwa ajili ya kuboresha Mfumo wa Usajili wa Kazi za Wanachama wa COSOTA wanaojishughulisha na kazi za ubunifu kwa njia ya mtandao.

**309. Mheshimiwa Spika**, katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP), **Shilingi 2,000,000,000** zimetegwa kwa ajili ya kukuza masoko ya mazao ya kilimo; kuimarisha mnyororo wa thamani na kuwezesha wakulima kuunganishwa na masoko; Kufanya tafiti za mwenendo wa masoko ya mazao makuu ya chakula

na mifugo; kufuatilia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa Zao la Korosho katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani; na Kupanua wigo wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa mazao ya alizeti, mahindi, mchele, na ufuta.

**310. Mheshimiwa Spika** mchanganuo wa fedha za Matumizi ya Maendeleo unapatikana katika Kitabu cha Nne cha Makadirio ya Fedha za Serikali kwa mwaka 2017/2018 katika Fungu: 60.

## 7.0 HITIMISHO

**311. Mheshimiwa Spika**, wajenzi wa nchi ni wananchi. Hivyo, napenda kuwashukuru kwa dhati Watanzania wote kwa uzalendo wenu wa kuitendea haki na kuipigania kwa kauli na vitendo ajenda ya kitaifa ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Ndiyo, tumepiga hatua kwenda mbele, lakini inatubidi kuongeza nguvu, mbinu na maarifa zaidi ili vita hiyo iwe na medani zinazokidhi aina na namna ya mapambano ya kiushindani yaliyopo na yajayo. Siri ya wazi ya ushindi ni uwajibikaji wa kila mmoja wetu na kuwepo ushirikiano usio na shaka na endelevu wa wadau wetu. Serikali kwa upande wake itaendeleza na kuboresha ulinzi kwa sekta, kuweka mazingira ya uwekezaji, uendelezaji, ujenzi na uboreshaji wa viwanda, biashara na masoko ili wadau wote waweze kutumia ipasavyo fursa zilizopo na zijazo. Naomba Watanzania wote na wote wenye mapenzi mema kwa nchi yetu muendeleee kutuamini na kutupa ushirikiano unaohitajika. Tunaamini tuko katika njia na mwelekeo sahihi. Sasa tusonge mbele kwa pamoja kwa nia na ari moja

**312. Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz).

**313. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - KAIMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu 44 kwa mwaka 2016/2017 na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi Fungu 44 na Fungu 60 ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji na majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu 44 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara Fungu 44 - Viwanda na Fungu 60 - Biashara na Uwekezaji, kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya viwanda inawezekana, Kamati inaipongeza Serikali kwa nia yake njema ya kutaka kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025 kwa kupitia viwanda, Kamati inaamini kuwa katika kutekeleza nia hii njema Serikali ihamasishe zaidi kuanzisha viwanda ambavyo vinatumia zaidi malighafi zinazopatikana hapa nchini hususani malighafi zinazotokana na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwanufaisha Watanzania wengi kwa wakati mmoja. Uwepo wa viwanda vya namna hiyo vitahamasisha kilimo na ufugaji kwa vile soko litakuwepo, hivyo ajira itapatikana kwenye kilimo, ufugaji na viwandani pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika kutekeleza majukumu yake, ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya

98(1), Kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi ya maendeleo iliyotekelezwa chini ya Wizara kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati ilitembelea shughuli nyingine zinazohusiana na sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji wakiwa wadau wa Wizara na hatimaye Wajumbe kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) Kamati ilikutana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kuchambua na kujadili mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha maombi ya fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge lako Tukufu kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango; Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli; Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 20 kutokana na ada za leseni, nyaraka za zabuni na faini ya kukiuka sheria ya leseni. Uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo:-

(a) Katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia robo ya tatu ni shilingi bilioni 10.7 tu sawa na asilimia 53.9 ndizo zilikuwa zimekusanywa. Kwa matokeo haya ni vigumu kufikiwa lengo la makusanyo ya shilingi bilioni 20 ifikapo tarehe 30 Juni, 2017.

(b) Kamati iligundua lengo lilikuwa ni kukusanya

asilimia 24.4 ya bajeti iliyopitishwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 tofauti na mwaka uliotangulia ambapo lengo lilikuwa ni kukusanya asilimia 14.2 ya bajeti iliyoidhinishwa.

(c) Katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi kufikia mwezi Machi, 2016 lengo lilifikiwa kwa asilimia 74 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2016/2017 katika kipindi cha robo ya tatu lengo lililofikiwa ilikuwa ni asilimia 53 tu. Ni maoni ya Kamati kuwa lengo lililowekwa halikuzingatia uwezo

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 81.8 Katika fedha hizo shilingi bilioni 41.8 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 40 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Februari, 2017 (robo ya tatu ya mwaka wa fedha) Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 34.6 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zilizopo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 44.4 tu ya fedha zote zilizotengwa katika bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kati ya fedha hizi shilingi bilioni 27.1 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 64.8, shilingi bilioni 41.8 fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, kati ya shilingi bilioni 27.1 fedha zilizopelekwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida shilingi bilioni 24.5 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 3.5 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kati ya shilingi bilioni 40 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 7.5 tu ndizo zilikuwa zimepokelewa na Wizara, kiasi hiki ni sawa na asilimia 18.9 ya fedha zote za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka fedha 2016/17 Kamati ilibaini kwamba:-

(i) Haikuridhishwa na mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina jambo linalopelekea kukwama kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

(ii) Fedha kutoka hazina zimekuwa zikipelekwa kwa kuchelewa sana. Mfano hadi kufikia Machi, 2017 kati ya shilingi bilioni 40 fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 7.5 tu, ndizo zilizokuwa zimepelekwa na Wizara jambo hili linapelekea kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kwamba ni wakati muafaka sasa Serikali kubadilika na kutoa fedha kwa wakati ili kutimiza malengo ya Watanzania ya kuwa na Tanzania ya viwanda ifikapo 2025. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha na Serikali ya mwaka 2015/2016; kwa mujibu wa kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na inayotekelezwa na Wizara hii. Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo kwa lengo la kujionea hali halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake. Aidha, Kamati ilitembelea shughuli za viwanda kwa lengo la kujionea mafanikio na changamoto katika uendeshaji wa sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu 44 iliidhinishiwa shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kutekeleza mradi Namba 6260 unaojulikana kama *NDC-Industrial Park (TAMCO - Kibaha)*; mradi huu ni kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya viwanda. Mradi huu unatekelezwa chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*). Jukumu la Shirika la maendeleo la Taifa katika kuanzisha miradi ya aina hii ni kutafuta ardhi ya mradi, kujenga miundombinu inayohitajika na kuvutia wawekezaji kwa ajili ya kujenga viwanda katika maeneo hayo. Lengo la Shirika ni kuendeleza eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipya.

Mheshimiwa Naibu Spika Kamati ilielezwa faida zitakazopatikana iwapo mradi huu utatekelezwa. Ni kivutio kwa wawekezaji wengi, mradi huu ukikamilika unatarajiwa kuwa na miundombinu yote wezeshi kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, eneo hili la viwanda lipo katika barabara kuu ya Dar es Salaam - Morogoro hivyo kurahisisha usafirishaji wa malighafi na bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea maelezo kuhusu changamoto za utekelezaji wa mradi huu kuwa ni ukosefu wa fedha jambo linalokwamisha utekelezaji wake. Mahali eneo la *TAMCO* lilipo tayari ni kivutio muhimu kwa wawekezaji wetu. Hili linajidhihirisha kwa sababu ya kuwa na wawekezaji walionyesha nia ya kuwekeza pamoja na kuwa bado miundombinu yake haijakamilika. Kamati inaishauri Serikali ipeleke fedha zilizosalia kwa ajili utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Pia miradi ya aina hii itekelezwe katika maeneo mengine ya uwekezaji yaliyotengwa katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitembelea katika Kiwanda cha Saruji yaani *Tanga Cement* na kueleza baadhi ya changamoto zinazowakabili kama ifuatavyo:-

(i) Changamoto kubwa ya kwanza ni kutokuwepo kwa nishati ya umeme ya uhakika. Kukatika mara kwa mara kwa nishati hii muhimu kunawapunguzia uwezo wa kuzalisha lakini pia kunasababisha uharibifu wa malighafi na mitambo;

(ii) Serikali kutoa motisha kwa wazalishaji wa saruji, uamuzi wa Serikali kutoa motisha kwa baadhi ya wazalishaji wa saruji huku wengine wakiachwa wakilalamikiwa na wadau wa sekta hiyo, hatua hii itasababisha baadhi ya wazalishaji wa saruji kuzalisha kwa gharama kubwa na hivyo kupunguza ushindani katika soko;

(iii) Kuzuia uingizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi. Serikali imezuia kuagiza makaa ya mawe kutoka nje ya nchi wakati yaliyopo hayatoshelezi mahitaji. Hatua hii



imeongeza bei ya makaa ya mawe yanayozalishwa hapa nchini pamoja na ukweli kuwa makaa ya mawe yanayoyazalishwa hayatoshelezi mahitaji lakini pia uzalishaji wake kutoka Mkoani Ruvuma unakabiliwa na changamoto ya ubovu wa miundombinu. Miundombinu ya reli iliyopo haina uwezo wa kuhimili mizigo mizito, barabara inayokwenda mahali machimbo yalipo hupitika kwa shida sana wakati wa masika. Makaa ya mawe yanachangia asilimia 70 ya gharama zote za kuzalishaji wa saruji hivyo kuongeza sana gharama za uzalishaji; na

(iv) Serikali iliingia mkataba na Kampuni ya *Tanga Cement* kwa kupitia *TIC*; katika mkataba huo Serikali iliahidi kutoa msamaha wa kodi ya zui baada ya kampuni kukidhi vigezo vilivyowekwa kisheria na *Tanzania Investment Centre*. Hadi kufikia Machi, 2017 hakuna tangazo lililotolewa kwenye Gazeti la Serikali (*Government Notice*) ili kutoa msamaha ulioahidiwa pamoja na ukweli kwamba mkataba huo ulisainiwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017; wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo Serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii.

Kwanza, Serikali iweke kipaumbele katika kuweka mazingira wezeshi kwa viwanda vinavyoajiri watu wengi kwa mfano viwanda vya nguo vinavyotumia pamba, viwanda vya korosho, kahawa na mbegu za mafuta.

Pili, Serikali ihakikishe viwanda vya ndani vinapatiwa mazingira safi ya ushindani.

Tatu, Serikali iongeze hisa kwa viwanda ambavyo ina hisa chache. Hatua hii itasaidia kulinda maslahi ya Serikali

na wafanyakazi kama ilivyofanyika kwa kiwanda cha *General Tyre*. Viwanda hivi ni *TANELEC* na Urafiki na vinginevyo.

Nne, Serikali itekeleze miradi ya Liganga na Mchuchuma ambayo ni miradi ya kipaumbele kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano 2020/2021 ili kuchochea kukua kwa viwanda nchini. Kamati haijaridhishwa tunaomba Serikali iyafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2017/2018; Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imepanga kukusanya shilingi bilioni 20 kutokana na ada ya leseni, nyaraka za zabuni na faini kwa kukiuka sheria ya leseni. Uchambuzi wa Kamati ulibainisha mambo yafuatayo:-

Moja, lengo lililowekwa ni kukusanya asilimia 16 ya fedha zinazoombwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia nane ya lengo la makusanyo ya asilimia 24 ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Pili, makadirio ya makusanyo ya mwaka wa fedha 2017/2018 ni sawa na makadirio ya mwaka wa fedha unaoishia ambayo hayakufikiwa aidha kwa sababu hayakuwa halisi au juhudi za ukusanyaji hazikuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona ni vema Wizara ikajiwekea lengo la makusanyo kwa kuzingatia uwezo wao wa kukusanya. Aidha, Serikali iangalie upya changamoto zilizopelekea kutofikia malengo hayo na ifanye jitihada za kukabiliana na changamoto hizo ili kuhakikisha wanafikia malengo wanayojiwekea hususani katika kipengele cha uuzaji wa nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 122.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa Fungu 44 na Fungu 60; kati ya fedha hizo shilingi bilioni

80.1 sawa na asilimia 65.6 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na shilingi bilioni 42.0 sawa na asilimia 34.4 ya fedha zote zinazooombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo huu ni kwa mafungu yote mawili, Fungu 44 na Fungu 60 ambalo linahusiana na mambo ya Biashara na Uwekezaji. Bajeti inayopendekezwa ya shilingi bilioni 122 ni zaidi kwa asilimia 49.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 81.8 zilizo dhinishwa katika mwaka wa fedha ullopita yaani 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu 44 - Viwanda limetengewa jumla ya shilingi bilioni 98.1 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 80 ya shilingi bilioni 122 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 24.17 sawa na asilimia 24.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 73.8 sawa na asilimia 75.3 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya shilingi bilioni 24.2 fedha zilizoombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 19.6 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 4.56 ni bajeti ya matumizi mengineyo (OC).

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 60 linalohusiana na masuala ya Biashara na Uwekezaji; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu Namba 60 imetengewa jumla ya shilingi bilioni 24.2 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 20 ya bajeti yote ya Wizara na shilingi bilioni 122, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 17.8 sawa na asilimia 73.8 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 6.3 sawa na asilimia 26 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja sehemu ya tano ya hotuba yangu ambayo inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na mwenendo usioridhisha katika kutoa fedha hasa zile za miradi ya maendeleo hivyo kuchelewesha utekelezaji wake. Aidha,

kiasi kinachopelekwa ni kidogo hivyo kushindwa kuanza mchakato wa utekelezaji. Kwa mara nyingine tena Kamati inaishauri Serikali itoe fedha za maendeleo kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya viwanda; nishati ya umeme ni muhimu sana katika uchumi unaotegemea viwanda kama ambavyo Serikali yetu inakusudia. Kamati ilipata fursa ya kuvitembelea baadhi ya viwanda, miongoni mwa changamoto kubwa zilizotajwa ni pamoja na kukosekana mara kwa mara kwa nishati hii muhimu, wakati mwingine hata pale inapopatikana kuwa katika kiwango kidogo kushindwa kuendesha mitambo. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya usambazaji wa nishati ya umeme wa kutosha na wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua uwepo wa mipango mizuri ya Serikali katika kukabiliana na upungufu wa nishati ya umeme nchini, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Kamati inaishauri Serikali ikamilishe mapema mipango yake ya kuongeza nishati hii kwa ajili ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesitisha uingizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi, lakini makaa yanayozalishwa yatoshelezi mahitaji ya sasa ya soko. Kamati inaishauri Serikali kwamba wakati inahasisha uwekezaji katika uchimbaji wa makaa ya mawe yaliyopo hapa nchini, iruhusu uingizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi ili uzalishaji katika viwanda vinavyotumia nishati hii visikwame katika kipindi hiki cha mpito.

Kamati inashauri Serikali iangalie namna bora ya kuwezesha benki ya rasilimali Tanzania (*Tanzania Investment Bank*) ili ifungue matawi mikoani pia kuiongezea mtaji hatua ambayo itasaidia mikopo kuwafikia Watanzania walio wengi. Pia Kamati inashauri Serikali itumie benki hii katika kutafuta fedha za miradi mikubwa ya maendeleo kutoka nje ya nchi ili kujenga miradi muhimu ya miundombinu na barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ushindani usio wa haki kati ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Sababu kubwa inayotajwa ni baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu kuingiza bidhaa hizo kwa njia za panya na kukwepa kulipa kodi. Malalamiko pia yapo kuhusu viwango vidogo vya kodi vinavyotowza kwa baadhi ya bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi. Hali hii inapelekea bidhaa hizo kuuzwa kwa bei rahisi kuliko zile zinazozalishwa hapa nchini. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha udhibiti katika mipaka yake ili bidhaa zote zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zilipiwe kodi stahiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto ya kukosekana kwa soko kwa baadhi ya bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini, kwa sababu ya kukosa ubora au gharama za uzalishaji kuwa juu. Mfano ni Kiwanda cha Viuadudu - Kibaha ambacho kinakabiliwa na ukosefu wa soko kwa bidhaa zake na hivyo kusitisha uzalishaji. Kamati inaishauri Serikali kwamba ili kuepuka kuwa na viwanda vingi ambavyo havizalishi kila anayekusudia kuanzisha kiwanda kipya kufanya utafiti wa kutosha kuhusu soko la bidhaa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabishara wamelalamikia wingi wa mamlaka za udhibiti ambazo zinafanya kazi zinazofanana na hivyo kuonesha kama kero kwa wafanyabiashara kwa mfano, *TBS, TFDA, OSHA, Fire* na kadhalika. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali izipitie upya sheria za uanzishaji wa mamlaka hizi na kuona uwezekano wa kaguzi hizo kufanywa na mamlaka moja ila kuwe na uwezekano wa ku-*share* majibu kwa mamlaka nyingine. Aidha, gharama za kaguzi zipitiwe upya na kupunguzwa kwa kuwa zimelalamikiwa na wafanyabiashara wengi kuwa ni kikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya uwekezaji; kukinzana kwa Sheria za Uwekezaji na Sheria ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) hususan kwa uwekezaji wa kimkakati kama wawekezaji wa viwanda vya madawa ya kilimo, mifugo na vyandarua kwa kupambana na ugonjwa wa malaria,

kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) uwekezaji wa namna hii unapunguza ushindani na bidhaa shindani zinazolingia kutoka nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kwamba uwekezaji wa kimkakati upate fursa ya kuwa *zero rated*, hatua hii itaongeza ushindani na bidhaa zinazolingia kutoka nje pia kulinda viwanda vyetu vya ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna malalamiko mengi kutoka kwa wawekezaji kuhusu urasimu usio na tija wakati wa kupata taarifa na vibali mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya mazingira ya kufanya biashara hapa nchini ili kuwavutia wawekezaji wengi zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uwekezaji wa kimkakati kama miradi ya Liganga na Mchuchuma, mradi wa Magadi Soda wa Ziwa Natron na Magadi Soda wa Engaruka Serikali iharakishe kutangaza katika Gazeti la Serikali ili misamaha ya kodi iliyoombwa ipatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *General Tyre* Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuamua kuutekeleza kwa kutafuta mwekezaji. Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya utekelezaji, kwa vile kukamilika kwake kutaongeza mchango katika pato la Taifa, pia kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wamelalamikia suala la utoaji wa vivutio vya uwekezaji kuwa hauko sawa miongoni mwa wawekezaji. Wawekezaji kutoka nje ya nchi wamekuwa wakipatiwa vivutio vingi zaidi, hivyo kuwakatisha tamaa wawekezaji wa ndani wanapotaka kuwekeza. Mfano muwekezaji Dangote amepewa gesi na makaa ya mawe kwa bei nafuu zaidi wakati wawekezaji wa aina yake hawajapata. Kamati inaishauri Serikali kuwa motisha ambazo zinaweza kutolewa kwa wawekezaji wote wa ndani na nje ni vizuri wote wakapatiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya uwekaji wa miundombinu wezeshi katika mradi wa *NDC Industrial Park (TAMCO Kibaha)*, Kamati

inaamini kwamba mradi huu ukikamilika utakuwa kivutio kwa wawekezaji wengi pia iangaliwe namna ya kuanzisha miradi mingine ya aina hii katika maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wengi wa uwekezaji wakiwemo wafanyabiashara na wenye viwanda wameendelea kulalamikia uwepo wa utitiri wa kodi na kuongezeka kiholela kwa kodi mbalimbali katika viwanda na biashara mbalimbali, kwa mfano, kuwekwa kwa VAT kwenye huduma ya mizigo inayopita bandarini (*VAT on auxiliary service on transit goods*), imepunguza sana biashara katika Bandari ya Dar es Salaam. Kamati inaendelea kuishauri Serikali ipitie upya kodi na tozo hizi kwa lengo la kuzipunguza ili kuhamasisha uwekezaji nchini na kuharakisha ujenzi wa viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kusema, Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza katika kujenga mazingira bora ya uwekezaji nchini ili kujenga nchi ya viwanda. Kamati inaunga mkono na kupongeza hatua zote zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji. Kamati inaiomba Serikali iongeze juhudi za kuweka mazingira ya uwekezaji nchini kuwa ya kuvutia. Kufanya hivyo kutaharakisha kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mheshimiwa Charles Mwijage, Makatibu Wakuu, Dkt. Adelhelm Meru na Profesa Adolph Mkenda, pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa

maoni na michango mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Orodha hiyo mtaiona kwenye ripoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana wewe kwa uongozi wako thabit pamoja na Spika wa Bunge la Bunge la Kumi la Moja, ninawashukuru pia Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge. Aidha, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kashilillah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndugu Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Ndugu Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Ndugu Wilfred Magova na Ndugu Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 44 na Fungu 60, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kiasi cha shilingi 122,215,109,201 ambapo shilingi bilioni 42.1 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 80.2 ni kwa ajili Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti.

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA  
NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA  
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI, FUNGU 44  
KWA MWAKA 2016/2017 NA MAONI YA KAMATI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI FUNGU 44 NA FUNGU  
60 YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni



za Bunge , Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, **Fungu 44-Viwanda** na kwa Mwaka wa fedha **2016/2017** na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara **Fungu 44-Viwanda** na **Fungu 60-Biashara na Uwekezaji** kwa Mwaka wa Fedha **2017/2018**.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ya Viwanda inawezekana, Kamati inaipongeza Serikali kwa nia yake njema ya kutaka kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025 kwa kupitia viwanda. Kamati inaamini kuwa katika kutekeleza nia hii njema Serikali ihamasishe zaidi kuanzisha Viwanda ambavyo vinatumia zaidi malighafi zinazopatikana hapa nchini hususani malighafi zinazotokana na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwanufaisha Watanzania wengi kwa wakati mmoja. Uwepo wa viwanda vya namna hiyo vitahamasisha kilimo na ufugaji kwa vile soko litakuwepo, hivyo ajira itapatikana kwenye kilimo, ufugaji na viwandani pia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika kutekeleza majukumu yake, ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1), Kamati ilipata fursa ya kutembelea Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati ilitembelea shughuli nyingine zinazohusiana na sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji wakiwa wadau wa Wizara na hatimaye Wajumbe kuishauri Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2), Kamati ilikutana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ili kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017, kuchambua na kujadili mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inalenga kuliomba Bunge lako tukufu kuidhinisha maombi ya Fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, lakini pia kutoa mapendekezo kwa Bunge lako tukufu kuhusu masuala kadhaa ambayo Kamati inaamini ni muhimu yakafanyiwa kazi.

## **2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.**

### **2.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2016/2017.

#### **2.1.1 Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **20,000,000,000** kutokana na ada za leseni, nyaraka za zabuni na faini ya kukiuka sheria ya leseni. Uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo:-

i) Katika mwaka wa fedha 2016/2017, hadi kufikia robo ya tatu ni Shilingi **10,781,488,987.18** tu sawa na asilimia **53.9** ndizo zilikuwa zimekusanywa. Kwa matokeo haya ni vigumu kufikiwa lengo la makusanyo ya shilingi **20,000,000,000** ifikapo tarehe 30 Juni, 2017.

ii) Lengo lilikuwa ni kukusanya asilimia **24.4** ya bajeti iliyopitishwa katika Mwaka wa Fedha **2016/2017** tofauti na mwaka uliotangulia ambapo lengo lilikuwa ni kukusanya asilimia **14.2** ya Bajeti iliyoidhinishwa.

iii) Katika Mwaka wa fedha 205/16 hadi kufikia mwezi

Machi, 2016 lengo lilifikiwa kwa asilimia **74**. Ukilinganisha na mwaka wa fedha 2016/17 katika kipindi cha robo ya tatu lengo lilofikiwa ni asilimia **53** tu. Ni maoni ya kamati kuwa lengo lililowekwa halikuzingatia uwezo.

### **2.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa jumla ya shilingi **81,871,992,000**. Katika fedha hizo shilingi **41,871,992,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **40,000,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Februari, 2017, robo ya tatu ya mwaka wa fedha Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi **34,694,182,650** kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **42.4** tu ya fedha zote zilizotengwa katika Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kati ya fedha hizi Shilingi **27,118,672,025** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia **64.8** ya Shilingi **41,871,992,000** fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, kati ya Shilingi **27,118,672,025**, fedha zilizopelekwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida Shilingi **23,536,396,450** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **3,582,275,575** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2017, kati ya Shilingi **40,000,000,000** zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi **7,566,620,625** tu ndizo zilikuwa zimepokelewa na Wizara, kiasi hiki ni sawa na asilimia **18.92** ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka fedha **2016/2017**, Kamati ilibaini kwamba:-

i) Haikuridhishwa na mwenendo nzuri wa wa

upatikanaji wa fedha kutoka Hazina jambo linalopelekea kukwama kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

ii) Fedha kutoka hazina zimekuwa zikipelekwa kwa kuchelewa sana. Mfano hadi kufikia Machi, 2017 kati ya shilingi **40,000,000,000** fedha za miradi ya Maendeleo ni shilingi **7,566,620,625** tu ndizo zilikuwa zimepelekwa na Wizara jambo hili linapelekea kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kwamba ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kubadilika na kutoa fedha kwa wakati ili kutimiza matarajio ya watanzania ya kuwa na Tanzania ya Viwanda ifikiapo 2025.

## **2.2 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2016, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na inatekelezwa na Wizara hii.

Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo kwa lengo kujionea hali halisi na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake. Aidha, Kamati ilitembelea shughuli za Viwanda kwa lengo la kujionea mafanikio na changamoto katika uendeshaji wa Sekta ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu **44** iliidhinishwa shilingi **9,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza mradi namba **6260** unaojulikana kama *NDC-Industrial Park (TAMCO-Kibaha)* .Mradi huu ni kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). Jukumu la Shirika la Maendeleo la Taifa katika kuanzisha miradi ya aina hii ni kutafuta ardhi ya Mradi, kujenga miundombinu inayohitajika na kuvutia

wawekezaji kwa ajili ya kujenga Viwanda katika maeneo hayo. Lengo la Shirika ni kuendeleza eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipya.

Mpango wa matumuzi ya ardhi katika eneo la TAMCO lenye ukubwa wa ekari **230** ni kama ifuatavyo:-

Na	Matumizi ya Ardhi	Ukubwa (Ekari)
1	Viwanda vya nguo na mavazi (Textile and Garments)	95
2	Viwanda vya kuunganisha magari na mitambo mbalimbali	64
3	Viwanda vya Kibaidjia na Vfaa-tiba	43
4	Huduma mbalimbali za uzalishaji	5
5	Mabwawa ya kutibu maji taka (oxidation ponds)	5
6	Barabara na maegesho ya magari	18

**Mheshimiwa Spika**, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi ni kukamilika kwa mpango wa matumizi ya ardhi (Land Use Plan) na upimaji wa viwanja kulingana na Mpango ulioidhinishwa na Mamlaka husika (Cadastral Survey). Pia usanifu (*Engineering design*) wa matangi ya maji safi, mabwawa ya maji taka na mfumo (network) wa kusambaza maji safi na kukusanya taka umekamilika. Kwa upande wa barabara, usanifu umefanyika kwa kipande cha urefu wa Km 1 ambapo sehemu yanye urefu wa meta 400 tayari imejengwa kwa kiwango cha lami mpaka kilipo kiwanda cha Viuadudu (Biolarvicides).

**Mheshimiwa Spika**, miundombinu inayohitajika katika Eneo la mradi ni barabara, kituo cha kupoozea umeme, mtandao wa nyaya za kusambaza umeme, matanki ya kuhifadhi maji safi, mabwawa ya kutibu maji yaliyotumika na mitandao ya mabomba kwa ajili ya kusambaza maji safi na kukusanya maji taka. Makadirio ya gharama za kujenga miundobinu hiyo ni Shilingi **Bilioni 16.4**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa faida zitakazopatikana iwapo mradi huu utatekelezwa kuwa, ni kivutio kwa wawekezaji wengi. Mradi huu ukikamilika unatarajiwa kuwa na miundombinu yote wezeshi kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, eneo hili la Viwanda lipo katika barabara kuu ya Dar es salaam Morogoro hivyo kurahisisha usafirishaji wa malighafi na bidhaa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea maelezo kuhusu Changamoto za utekelezaji wa mradi huu kuwa ni ukosefu wa fedha jambo linalokwamisha utekelezaji wake. Mahali eneo la TAMCO lilipo tayari ni kivutio muhimu kwa wawekezaji wetu. Hili linajidhihirisha kwasababu ya kuwa na wawekezaji walionyesha nia ya kuwekeza pamoja na kuwa bado miundombinu yake haijakamilika. Kamati inaishauri Serikali ipeleke fedha zilizosalia kwa ajili utekelezaji wa mradi huu ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Pia miradi ya aina hii itekelezwe katika maeneo mengine ya uwekezaji yaliyotengwa katika sehemu mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilitembelea katika kiwanda cha Saruji Tanga (Tanga Cement PLC) na kuelezwa baadhi ya changamoto zinazowakabili kama ifuatavyo:-

i) **Kutokuwepo kwa nishati ya Umeme ya uhakika.**  
**Mheshimiwa Spika**, kukatika mara kwa mara kwa nishati hii muhimu kunawapunguzia uwezo wa kuzalisha lakini pia kunasababisha uharibifu wa malighafi na mitambo;

ii) **Serikali kutoa motisha kwa baadhi ya wazalishaji wa Saruji**

**Mheshimiwa Spika**, Uamuzi wa Serikali kutoa motisha kwa baadhi ya wazalishaji wa Saruji huku wengine wakiachwa unalalamikiwa na wadau wa sekta hiyo. Hatua hii itasababisha baadhi ya wazalishaji wa Saruji kuzalisha kwa gharama kubwa hivyo kuwapunguzia ushindani katika Soko;

iii) **Kuzuia uingizaji wa Makaa ya Mawe kutoka nje ya nchi**  
**Mheshimiwa Spika**, Serikali imezuia kuagiza makaa ya mawe

kutoka nje ya nchi wakati yaliyopo hayatoshelezi mahitaji. Hatua hii imeongeza bei ya Makaa ya mawe ya yanayozalishwa hapa nchini. Pamoja na ukweli kuwa makaa ya mawe yanayoyazalishwa hayatoshelezi mahitaji lakini pia usafirishaji wake kutoka Mkoani Ruvuma unakabiliwa na changamoto ya ubovu wa miundombinu. Miundombinu ya Reli iliyopo haina uwezo wa kuhimili mizigo mizito. Barabara inayokwenda mahali machimbo yalipo hupitika kwa shida sana wakati wa masika. Makaa ya mawe yanachangia asilimia 70 ya gharama zote za kuzalishaji wa Saruji hivyo kuongeza sana gharama za uzalishaji; na

iv) **Serikali iliingia Mkataba na Kampuni ya Tanga Cement kwa kupitia TIC**

**Meshimiwa Spika**, katika Mkataba huo Serikali iliahidi kutoa msamaha wa Kodi ya Zuio baada ya kampuni kukidhi vigezo vilivyowekwa kisheria na *Tanzania Investment Centre* (TIC). Hadi kufikia Machi, 2017 hakuna Tangazo lililotolewa kwenye Gazeti la Serikali, ili kutoa msamaha uliokuwa ulioahidiwa pamoja na ukweli kwamba Mkataba huo ulisainiwa mwaka 2009.

**3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo serikali haikuyatekeleza ipasavyo kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii.

i) ***Serikali iweke kipaumbele katika kuweka mazingira wezeshi kwa viwanda vinavyoajiri watu wengi, mfano viwanda vya nguo vinavyotumia pamba, viwanda vya korosho, kahawa na mbegu za mafuta.*** Maelezo yaliyotolewa na Wizara ni kuwa imetekeleza agizo hili kwa kuwahimiza Tawala za Mikoa kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa

viwanda. Kamati haijaridhishwa na utekelezaji huu kwani utengaji wa maeneo tu hatuoshi. Hivyo basi Kamati inashauri kuwa maeneo yanayotengwa yapimwe na kuwekewa miundombinu ili kuyafanya kuwa tayari ili muwekezaji akija akute eneo lipo tayari kwa yeye kuanza uwekezaji wake.

ii) ***Serikali ihakikishe viwanda vya ndani vinapatiwa mazingira safi ya ushindani*** Maelezo ya Serikali ni kuwa wameandaa waraka maalumu na kuwakilisha kwenye Baraza la Mawaziri ikipendekeza mbinu na mikakati ya kupambana na matatizo ya ushinda katika sekta ya ushindani. Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa agizo hili, na inashauri Serikali ichukue hatua za makusudi tena za haraka katika kuhakikisha mazingira ya ushindani yanakuwa safi kwa manufaa ya mlaji, kwani pia yatakutia wawekezaji kuja kuwekeza au kupanua uwekezaji wao kwa wale waliopo sokoni.

iii) ***Serikali iongeze hisa kwa viwanda ambavyo ina hisa chache. Hatua hii itasaid-ia kulinda maslahi ya Serikali na wafanyakazi kama ilivyofanyika kwa kiwanda cha General tyre. Viwanda hivyo ni TANELEC na URAFIKI na vinginevyo.*** Maelezo ya serikali kuhusu kiwanda cha TANELEC, ni kwamba Wizara inajadiliana na Msajili wa Hazina juu ya njia bora ya kuongeza hisa za Serikali. Kuhusu Kiwanda cha URAFIKI Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alipewa jukumu la kukagua Hesabu za Kiwanda hicho na Taarifa siyo nzuri. Kamati inaendelea kusesitiza utekelezaji wa agizo hili, kwani hatua zilizochukuliwa mpaka sasa si za kuridhisha.

iv) ***Serikali itekeleze miradi ya Liganga na Mchuchuma ambayo ni miradi ya kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2020/2021 ili kuchochea kukua kwa viwanda hivi.*** Maelezo ya Serikali ni kuwa yalitolewa maelekezo na Baraza la Mawaziri kuwa mkataba wa Miradi hii upitiwe upya. Kamati ya Makatibu Wakuu iliundwa nakupitia mkataba huo na kutoa mapendekezo ya vivutio kwa kuzingatia maslahi ya Taifa. Mapendekezo hayo yanasubiri kujadiliwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji kabla ya kujadiliwa na muwekezaji. Kamati inaendelea kuishauri



Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hii kwani utekelezaji wake utachochea sekta ya Viwanda nchini.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

##### **4.1 Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

###### **Makisio ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imepanga kukusanya shilingi bilioni **20** kutokana na ada za leseni, nyaraka za zabuni na faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni. Uchambuzi wa Kamati uulibainisha mambo yafuatayo:-

i) Lengo lililowekwa ni kukusanya asilimia **16** ya fedha zinazoombwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **8** ya lengo la makusanyo ya asilimia **24** mwaka wa fedha 2016/2017.

ii) Makadirio ya makusanyo ya mwaka wa fedha **2017/2018** ni sawa na makadirio ya mwaka wa fedha unaoishia ambayo hayakufikiwa aidha kwa sababu hayakuwa halisi au juhudi za ukusanyaji hazikuwa nzuri.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona ni vyema Wizara ikajiwekea lengo la makusanyo kwa kuzingatia uwezo wao wa kukusanya. Aidha, Serikali iangalia upya changamoto zilizopelekea kutofikia malengo hayo na ifanye jitihada za kukabiliana na changamoto hizo ili kuhakikisha wanafikia malengo wanayojiwekea hususani katika kipengele cha uuzaji wa nyaraka za zabuni.

###### **Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi **122,215,109,201** kwa ajili

ya matumizi ya Kawaida na miradi ya Maendeleo kwa mafungu 44 na 60. Kati ya fedha hizo Shilingi **80,190,377,451** sawa na asilimia **65.6** ni kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo na Shilingi **42,024,731,750** sawa na asilimia **34.4** ya fedha zote zinazoombwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo huu ni kwa mafungu yote mawili (2) Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara na Uwekezaji. Bajeti inayopendekezwa ya Shilingi **122,215,109,201** ni zaidi kwa asilimia **49.2** ikilinganishwa na Shilingi **81,871,992,000** zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha **2016/2017**.

**i) FUNGU 44 -VIWANDA**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu **44-Viwanda** imetengewa jumla ya shilingi **98,012,869,451** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **80** ya shilingi **122,215,109,201** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi **24,172,492,000** sawa na asilimia **24.7** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **73,840,377,451** sawa na asilimia **75.3** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya shilingi **24,172,492,000** fedha zilizoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Shilingi **19,603,120,000** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Shilingi **4,569,372,000** ni Bajeti ya Matumizi Mengineyo(OC).

**ii) FUNGU 60- BIASHARA NA UWEKEZAJI**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha **2017/2018**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu **60-Biashara na Uwekezaji**, imetengewa jumla ya Shilingi **24,202,239,750** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **20** ya bajeti yote ya Wizara, shilingi **122,215,109,201**. Kati ya fedha hizo shilingi **17,852,239,750** sawa na asilimia **73.8** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **6,350,000,000** sawa na asilimia **26** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya shilingi **17,852,239,750** fedha zilizoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida Shilingi **15,964,331,000** sawa na asilimia **66** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi. Kiasi kinachosalia Shilingi **1,887,908,750** sawa na asilimia **8** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa na mwenendo usioridhisha katika kutoa fedha hasa zile za miradi ya mendeleo hivyo kuchelewesha utekelezaji wake. Aidha kiasi kinachopelekwa ni kidogo hivyo kushindwa kuanza mchakato wa utekelezaji. Kwa mara nyingine tena, Kamati inaishauri Serikali itoe fedha za maendeleo kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

### 5.1 Sekta ya Viwanda

**Mheshiwa Spika**, nishati ya Umeme ni muhimu sana kwa Uchumi unaotegemea viwanda kama ambavyo Serkali yetu inakusudia. Kamati ilipata fursa ya kuvitembelea baadhi ya viwanda, miongoni mwa changamoto kubwa zilizotajwa ni pamoja na kukosekana mara kwa mara kwa nishati hii muhimu. Wakati mwingine hata pale inapopatikana kuwa katika kiwango kidogo hivyo kushindwa kuendesha Mitambo. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya usambazaji wa nishati ya umeme wa kutosha na wa uhakika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua uwepo wa mipango mizuri ya Serikali katika kukabiliana upungufu wa Nishati ya Umeme nchini lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Kamati inaishauri Serikali ikamilishe mapema mipango yake ya kuongeza nishati hii kwa ajili ya ujenzi wa Uchumi wa viwanda nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imesitisha uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi lakini makaa yanayozalishwa hayatoshelezi mahitaji ya sasa ya soko. Kamati inaishauri Serikali kwamba wakati inahamasisha uwekezaji katika uchimbaji wa makaa ya mawe yaliyopo hapa nchini, iruhusu uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi ili uzalishaji katika viwanda vinavyotumia nishati hii usikwame katika kipindi hiki cha mpito.

**Mheshimiwa Spika**, kamati inaishauri serikali iangalie namna bora ya kuiwezesha Benki ya Rasilimali Tanzania (Tanzania

Investment Bank) ili ifungue matawi Mikoani lakini pia kuiongezea Mtaji, hatua ambayo itasaidia Mikopo kuwafikia watazania walio wengi. Pia Kamati inaishauri Serikali iitumie Benki hii katika kutafuta fedha za miradi mikubwa ya maendeleo kutoka nje ya nchi ili kujenga miradi muhimu ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na Viwanja vya ndenge.

## 5.2 Sekta ya Biashara

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na ushindani usio wa haki kati ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Sababu kubwa inayotajwa ni baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu kuingiza bidhaa hizo kwa njia za panya na kukwepa kulipa Kodi. Malalamiko pia yapo kuhusu Viwango vidogo vya kodi vinavyotozwa kwa baadhi ya bidhaa zinazolingia kutoka nje ya nchi. Hali hii inapelekea bidhaa hizo kuuzwa kwa bei rahisi kuliko zile zinazozalishwa hapa nchini. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha udhibiti katika mipaka yake ili bidhaa zote zinazolingizwa kutoka nje ya nchi zilipiwe Kodi stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto ya kukosekana kwa Soko kwa baadhi ya bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini, kwa sababu ya kukosa ubora au gharama za uzalishaji kuwa juu. Mfano ni Kiwanda cha Viadudu Kibaha ambacho kinakabiliwa na ukosefu wa Soko kwa bidhaa zake na hivyo kusitisha uzalishaji. Kamati inaishauri Serikali kwamba ilikuepuka kuwa na viwanda vingi ambavyo havizalishi kila anayekusudia kuanzisha Kiwanda kipya kufanya utafiti wa kutosha kuhusu soko la bidhaa husika.

**Mheshimiwa Spika**, wafanyabishara wamelalamikia wingi wa mamlaka za udhibiti ambazo zinafanya kazi zinazofanana na hivyo kuonekana kama kero kwa wafanyabiashara. Mfano TBS, TFDA, OSHA, FIRE, n.k. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali izipitie upya sheria za uanzishaji wa mamlaka hizi na kuona uwezekano wa kaguzi hizo kufanywa na mamlaka moja ila kuwe na uwezekano wa kushea majibu kwa mamlaka nyingine. Aidha, gharama za

kaguzi zipitiwe upya na kupunguzwa kwa kuwa zimelalamikiwa na wafanyabiashara wengi kuwa ni kikwazo.

### 5.3 Sekta ya Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, kukinzana kwa sheria za uwekezaji na sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) hususani kwa uwekezaji wa kimkakati kama wawekezaji wa viwanda vya madawa ya kilimo, mifugo, na vyandarua vya kupambana na ugonjwa wa Malaria. Kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika uwekezaji wa namna hii kunapunguza ushindani na bidhaa shindani zinazolingia kutoka nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali, kwamba uwekezaji wa kimkakati upate fursa ya kuwa *zero rated*, hatua hii itaongeza ushindani na bidhaa zinazolingia kutoka nje lakini pia kulinda viwanda vya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, Bado kuna malalamiko mengi kutoka kwa wawekezaji kuhusu urasimu usio na tija wakati wa kupata taarifa na vibali mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya mazingira ya kufanya biashara hapa nchini ili kuwavutiwa wawekezaji wengi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uwekezaji wa kimkakati kama Miradi ya Liganga na Mchuchuma; Mradi wa Magadi Soda wa Ziwa Natron na Magadi Soda wa Engaruka Serikali iharakishe kutangaza katika Gazeti la Serikali ili misamaha ya kodi iliyoombwa ipatikane kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa General Tyre kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuamua kuutekeleza kwa kutafuta mwekezaji. Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya utekelezaji, kwa vile kukamilika kwake kutaongeza mchango katika pato la Taifa lakini pia kuongeza ajira.

**Mheshimiwa Spika**, wawekezaji wamelalamikia suala la utoaji wa vivutio vya uwekezaji kuwa hauko sawa miongoni mwa wawekezaji. Wawekezaji kutoka nje ya nchi wamekuwa wakipatiwa vivutio vingi zaidi hivyo kuwakatisha tamaa wawekezaji wa ndani wanapotaka kuwekeza. Mfano

muwekezaji Dangote amepewa gesi na makaa yamawe kwa bei nafuu zaidi wakati wawekezaji wa aina yake hawajapata. Kamati inaishauri Serikali kuwa motisha ambazo zinaweza kutolewa kwa wawekezaji wote wa ndani na nje ni vizuri wote wakapatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuongeze kasi ya uwekaji wa miundombinu wezeshi katika Mradi wa NDC-*Industrial Park (TAMCO-Kibaha)*, Kamati inaamini kwamba mradi huu ukikamilika utakuwa kivutio kwa wawekezaji wengi lakini pia iangaliwe namna ya kuanzisha miradi mingine ya aina hii katika maeneo mengine nchini.

**Mheshimiwa Spika**, wadau wengi wa uwekezaji wakiwemo wafanyabiashara na wenyeviwanda wameendelea kulalamikia uwepo wa utitiri wa kodi na kuongezeka kiholela kwa kodi mbalimbali katika viwanda na biashara mbalimbali. Kwa mfano kuwekwa kwa VAT kwenye huduma ya mizigo inayopita bandarini (*VAT on auxiliary service on transit goods*) imepunguza sana biashara katika Bandari ya Dar es Salaam. Kamati inaendelea kuishauri Serikali izipitie upya kodi na tozo hizi kwa lengo la kuzipunguza ili kuhamasisha uwekezaji nchini na kuharakisha ujenzi wa Viwanda katika nchi yetu.

## 6.0 HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza katika kujenga mazingira bora ya uwekezaji nchini ili kujenga nchi ya Viwanda. Kamati inaunga mkono na kupongeza hatua zote zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji. Kamati inaiomba Serikali iongeze juhudi za kuweka mazingira ya uwekezaji nchini kuwa ya kuvutia. Kufanya hivyo kutaharakisha kuifanya Tanzania kuwa nchi ya Viwanda nay a kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Charles Mwijage (Mb), Makatibu Wakuu, Dr. Adelhelm Meru na Prof. Adolph Mkenda, pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Viwanda,

Biashara na Uwekezaji kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika kipindi cha mwaka ujao wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni na michango mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini.

(i)	Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo Mb	Mwenyekiti
(ii)	Mhe. Vicky Pascal Kamata, Mb	Mjumbe
(iii)	Mhe. Salim Hassan Turkey, Mb	Mjumbe
(iv)	Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe
(v)	Mhe Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb	Mjumbe
(vi)	Mhe. Khatib Said Haji, Mb	Mjumbe
(vii)	Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb	Mjumbe
(viii)	Mhe. Munira Mustafa Khaibu, Mb	Mjumbe
(ix)	Mhe. Anthony Calist Komu, Mb	Mjumbe
(x)	Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
(xi)	Mhe. Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Mb	Mjumbe
(xii)	Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb	Mjumbe
(xiii)	Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
(xiv)	Mhe. Balozi Dkt Diodorus Kamala, Mb	Mjumbe
(xv)	Mhe. Jesca David Kishoa, Mb	Mjumbe
(xvi)	Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb	Mjumbe
(xvii)	Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb	Mjumbe
(xviii)	Mhe. Anatropia Theonest, Mb	Mjumbe
(xix)	Mhe. Faida Mohammed Bakar, Mb	Mjumbe
(xx)	Mhe. Suleiman Ahmed Sadick, Mb	Mjumbe
(xxi)	Mhe Ibrahim Hassanali Raza, Mb	Mjumbe
(xxii)	Mhe. Abdulaziz M. Abood, Mb	Mjumbe
(xxiii)	Mhe. Dkt. Raphael M. Chegeni, Mb	Mjumbe
(xxiv)	Mhe. Sylvestry Francis koka, Mb	Mjumbe
(xxv)	Mhe. Gimbi Dotto Massaba, Mb	Mjumbe
(xxvi)	Mhe. Martha Mosses Mlata, Mb	Mjumbe
(xxvii)	Mhe. Joyce John Mukya, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe kwa uongozi wako thabit kwa Bunge la 11; niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge. Aidha, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashillah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bw. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu **44** na **60**, kwa mwaka wa fedha **2017/2018** kiasi cha shilingi **122,215,109,201** ambapo shilingi **42,024,731,750** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **80,190,377,451** ni kwa ajili matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Stanslaus Haroon Nyongo, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA  
MAZINGIRA**

17 Mei, 2017

**NAIBU SPIKA:** Kabla sijamwita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa watu wa Taarifa Rasmi za Bunge. Kamati inasema haikuiridhishwa na mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha, nadhani hiyo sentensi ikae vizuri ili Kiswahili kiwe kinasomeka sawa sawa kwa ajili ya hao watakaokuja kujisomea hapo baadae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Antony Calist Komu.



**MHE. ANTONY C. KOMU - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZANI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa mwenye afya njema. Ninamshukuru Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Jimbo la Hai na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa imani yake kubwa kwangu, naomba pia nimshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda na pia naomba niishukuru familia yangu kwa usaidizi na uvumilivu wao ambao wameuonesha wakati nikitekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini kwa imani yao kwangu na ushirikiano wanaonipa katika kusukuma maendeleo ya Jimbo letu, ninaahidi kwamba nitaendelea kuwawakilisha vizuri kwa uadilifu na umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda Tanzania; ukisoma kitabu cha Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 5.7 kwa ajili ya uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimkati kwenye sekta ya uzalishaji (*manufacturing*), lakini katika hali halisi Serikali imeahidi au imefanya *commitment* ya shilingi bilioni 659 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukisoma makadirio yaliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu ili kupitishwa kama bajeti ya maendeleo kwenye eneo la viwanda ni shilingi bilioni 2.38 sawa na asilimia 0.36 ya fedha zote za maendeleo zilizotakiwa kutolewa na Serikali katika sekta ya maendeleo kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulielezea Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla inapojigamba kuwa inajenga Tanzania ya viwanda. Tanzania ya viwanda itajengwa kwa

bajeti ipi? Kwa sababu hakuna *commitment* ya kibajeti katika sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 96.5 ya viwanda vyote ambayo ni 50,656 ni viwanda vidogo vinavyoajiri wafanyakazi mmoja mpaka tisa. Asilimia 3.5 vinatoa ajira kuanzia watu kumi na kuendelea. Takwimu hizi hazitoi matumaini makubwa ya kuingia katika uchumi wa viwanda. Hivi viwanda vya mtu mmoja mpaka kumi ni kujidanganya. Miongoni mwa viwanda hivi, viwanda 119 ni mashirika au viwanda ambavyo vilibinafsishwa na kati yake viwanda 74 vikiwa vinafanya kazi au vizima, 44 vinaendelea vizuri, 13 vinalegalega na 17 vimefungwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nayo imekuwa ni hadithi ya muda mrefu na ukizingatia kwamba viwanda hivi ambavyo vimefungwa ndivyo viwanda vikubwa, maana yake ni viwanda kama vile vya Urafiki, *Mwatex*, viwanda vya ngozi na kadhalika. Bila aibu taarifa ya Wizara ya Viwanda inasema kuwa baadhi ya viwanda vilivyo binafsishwa vilitumika kama dhamana kukopa benki na fedha hizo zilitumika kwa shughuli nyingine badala ya kuviendeleza, huu ni udhaifu kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iache kuwa na ndimi mbili katika utendaji wake, iweje tu Polisi wa Usalama Barabarani waweze kuadhibu mtu anayebadili matumizi ya gari lake, labda gari la mizigo akasafirishia abiria anaadhibiwa hapo kwa hapo, inashindikana kwa waliogeuza viwanda kuwa maghala ya bidhaa toka nje au malisho ya mbuzi kuadhibiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbo wa Wizara pamoja na Msajili wa Hazina kwamba inafanya upembuzi wa utendaji wa mikataba ya viwanda au mashirika ili kufikia uamuzi wa kunyang'anya viwanda au mashirika yanayolegalega na kuwapa wawekezaji wenye uwezo umekuwa ukijirudia kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema ikaeleweka

maeneo haya yanayohodhiwa kwa majina ya viwanda lakini hakuna viwanda ni maeneo yaliyokwisha endelezwa kimkakati kwa uwekezaji wa viwanda, hivyo ni uwendawazimu kuhubiri kila siku kuwa Serikali inahamasisha kutenga maeneo kwa ajili ya viwanda bila kujiuliza yaliyokwishatengwa na kuendelezwa yanafanyiwa kazi gani, kwani kila Mji ulikuwa na maeneo ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa inayovikabili viwanda nchini ni pamoja na ukosefu wa mitaji, teknolojia ya uzalishaji kupitwa na wakati hasa vile vilivyobinafsishwa, malighafi isiyokuwa ya uhakika, umeme, maji, urasimu katika kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali, mlolongo wa kodi na kutoshirikishwa katika kufikia maamuzi yenye athari kwa viwanda. Changamoto hizi bado zipo na zitaendelea kuwepo kwa kuwa Serikali haina mkakati wowote maalumu wa kibajeti wa kuondoa changamoto hizi ila ni nyimbo zile zile yaani *business as usual*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti usioridhisha katika miradi ya kimkakati. Fidia ya maeneo ya EPZ na SEZ, hili ni jambo la kiseru na kisheria ambalo limekuwepo kwa muda mrefu na kila mwaka limekuwa likipewa fedha chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji japo hazilingani kabisa na mahitaji.

Aidha, ni wajibu wa Serikali kisheria kujenga miundombinu ili kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wawekezaji katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya *Special Economic Zones*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 jambo hili limetoweka kabisa katika bajeti, halitajwi popote pamoja na ukweli kwamba wananchi katika maeneo kadhaa nchini walishapisha maeneo yao na wamenyimwa kabisa kufanya maendelezo yoyote wakisubiri fidia za maeneo yao, mfano ni Bagamoyo mchakato wa kutwaa maeneo ya wananchi ulianza toka mwaka 2007 na kukamilika mwaka 2010 kwa uthamini wa hekta 5,742.5

ambapo kilihitajika kiasi cha shilingi bilioni 50.2 kama fidia, mpaka leo ni hekta 2,560.8 tu sawa na shilingi bilioni 28.36 tu ndizo zilizokwisha tolewa kama fidia mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo ya randama ya Wizara yenyewe kiasi kinachohitajika kufanya fidia katika eneo hili kwa sasa ni shilingi bilioni 51.3 zikijumuisha na riba ya ucheleweshaji. Ninajua kuwa Mheshimiwa Waziri amekuwa akisema fidia ya eneo hili itafanywa na mwekezaji binafsi, Kambi Rasmi Bungeni inataka kujua ni lini mwekezaji huyo atalipa fidia na ni kiasi gani na kwa masharti yapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hili kwa maamuzi ya Baraza la Mawaziri la Serikali ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli limepelekwa kwa sekta binafsi, jambo ambalo linakosa uhakika wa kufanyika na halina tena ukomo wa muda wa kutekelezwa. Aidha, hatua hii ni ushahidi dhahiri wa Serikali ya Awamu ya Tano kukwepa jukumu lake la kisera na kisheria na kuendeleza tabia yake ya kutojali athari mbaya zinazoweza kusababishwa na maamuzi yake kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya maeneo maalum ya uwekezaji *SEZ Act No. 2 of 2006* na 2011 kama ilivyofanyiwa marekebisho 2012, uendelezaji wa miundombinu katika maeneo hayo kwa mujibu wa sheria hii ni jukumu la Serikali, lakini maeneo hayo kwa asilimia kubwa yameishia kuambulia visingizio kama ufinyu wa bajeti, hivyo maeneo karibu yote yaliyokwisha fidia hayajafanyiwa maendeleo yoyote mfano *Bagamoyo Special Economic Zone* hekta 2,399.6; Kigoma, Tanga ekari 1,363; Bunda ekari 3,255; Mererani hekta 530 na Ruvuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupata mwekezaji atakayejenga miundombinu ni ndoto ya mchana, ukizingatia gharama zinazohitajika katika eneo hilo.

Eneo lingine ni mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga. Huu ni mradi wa muda mrefu wa kimkakati na una faida nyingi. Utahusisha ujenzi wa kinu cha umeme, utatoa umeme wa makaa ya mawe ambapo

umeme wa makaa ya mawe utakuwa msaada mkubwa kwa nchi kwani hautegemei tabia nchi kama ilivyo vyanzo vingine vya umeme. Utatoa ajira na utatoa mapato mengi makubwa yatokanayo na makaa yenyewe na chuma chenyeuwe.

Mhesheshimiwa Naibu Spia pamoja na faida zote hizo bado mradi huu haujapewa uzito unaostahili kila siku kuna hadithi mpya katika utekelezaji wa mradi huu licha ya maagizo mengi ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya mwisho ya Serikali yalikuwa kila hatua imeshachukuliwa na mradi huu utanza robo ya kwanza ya mwaka huu wa 2017. Maelezo ya leo ya Serikali yaliyopo katika randama yanasema Baraza la Mawaziri lililokaa tarehe 7 Disemba, 2016, lilielekeza mkataba wa mradi wa mchuchuma na liganga upitiwe upya. Kufuatia maelekezo hayo Kamati ya Makatibu Wakuu iliundwa na kupitia mkataba huo na kutoa mapendekezo ya vivutio vitakavyozingatia maslahi ya Taifa. Kulinda maslahi ya Taifa ni muhimu sana kwani maelezo yote ya awali hayajawahi kueleza mapungufu hayo na hivi kweli hii ndiyo sababu ya mradi huo kutokuanza muda wote?

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ni kana kwamba huu mradi ndiyo unabuniwa kwa mara ya kwanza na sasa ni vigumu kuamini kama kweli yule mbia aliyekwishatambuliwa ataendelea au laa. Maelezo ya Serikali yamekuwa yakibadilika kila siku kutegemea ni nani anapewa taarifa hiyo kama ilivyojidhihirisha hapo juu. Mwenendo wa aina hii, hauwezi kufikisha nchi yetu kwenye uchumi wa viwanda kama inavyohubiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufufuaji wa Kiwanda cha *General Tyre*: katika mwaka wa fedha 2016/2017, mradi wa kufufua Kiwanda cha *General Tyre* ulitengewa shilingi 150,000,000 kwa ajili ya kuandaa andiko la mradi, kuendeleza mashamba ya mpira na kutafuta mbia mpya. Mwaka huu wa fedha 2017/2018 Wizara inaomba jumla ya shilingi 70,000,000 kutafuta mbia, lakini utafiti uliofanywa na

wataalam wa ndani inaonesha kuwa mitambo iliyopo katika kiwanda hicho haifai kabisa kulingana na teknolojia ya sasa. Kiwanda hicho kinahitaji kupanuliwa ili kiweze kuzalisha kwa wingi kuweza kushindana na soko la Kimataifa na imeshauri kiendeshwe na sekta binafsi na Serikali iwe mbia kulingana na thamani ambazo zipo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo mengine yaliyo katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018 katika ukurasa wa 20, yanasema baada ya taarifa ya awali ya wataalam, Serikali inatafakari nini yatakuwa matumizi sahihi zaidi ya eneo la kiwanda hicho, mwekezaji aliyekuwa ameomba kuwa mbia katika kufufua kiwanda ameomba kupatiwa eneo la kuweka kiwanda kipya cha matairi eneo la *TAMCO* Kibaha. Kwa sasa kiwanda hicho kinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo hakuna kitu kinachoitwa Kiwanda cha Matairi cha *General Tyre* kwa maana ya mitambo ila kuna eneo ambalo palikuwepo na Kiwanda cha Matairi cha *General Tyre* na mabaki ya kiwanda hicho ambayo kwa lugha fasaha na ya uwazi zinapaswa kuondolewa kupisha uwekezaji sahihi. Bila kuweka jambo hili wazi mbele ya Bunge lako Tukufu na maamuzi yakafanyika hicho kinachoitwa kiwanda cha matairi cha *General Tyre* Arusha kitaendelea kuwa kama mfereji wa kutumia fedha za umma kama zilivyokwisha tumika huko nyuma bila matokeo. Ni vema tukajiuliza katika kutenga fedha hizi shilingi 70,000,000 zinazoombwa sasa hivi, taarifa ya wataalam imezingatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe maelezo kuwa ni kwa nini katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*National Five Year Development Plan*) ya 2016/2017 mpaka 2021. Kiwanda cha *General Trye* kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kilipaswa kutengewa jumla ya shilingi 22,000,000,000 na sio 70,000,000. Kiasi hicho kilichotengwa ni kidogo mno kuweza kufanya kazi zilizokusudiwa na kuwezesha kiwanda hicho kuanzishwa tena upya kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha Viuadudu Kibaha na Kiwanda cha *TANELEC* Arusha; hiki ni kiwanda kilichotajwa na Serikali kama ni cha kimkakati. Kimekabidhiwa shirika la *NDC* baada ya ujenzi wake kukamilika kwa mkopo wenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 22.307 na wenye riba ya asilimia 12 utakaorejeshwa kwa miaka kumi ni mali ya Serikali hiki kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kiwanda hicho kianze kuzalisha kimepewa na Serikali jumla ya shilingi bilioni 2.1 na pia kimekopa jumla ya shilingi bilioni 4.5 na kimeanza kuzalisha hadi Februari, 2017 kimezalisha dawa kiasi cha lita 100,000 ambazo zimeuzwa nchini Niger kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.012. Nchi yetu ambayo inatumia fedha nyingi sana kupambana na malaria na ndiyo ugonjwa unaoongoza kuuu haijanunua hata lita moja. Wizara ya Afya imeshapitishiwa bajeti yake ya mwaka 2017/2018 na hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya dawa kutoka Kiwanda cha Viuadudu Kibaha. Kiwanda hiki hakiwezi kuwa endelevu kama Serikali yetu haitaweza kupanga na kuwa na soko la uhakika la ndani ambalo ni dhahiri lipo lakini hakuna uratibu ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kiwanda hicho ambacho kina uwezo wa kuzalisha lita 6,000,000 kwa mwaka na kujiendesha hakizalishi kwa kuwa hakina soko la bidhaa zake na kinaendelea kulipa gharama mbalimbali za uendeshaji kama wafanyakazi, umeme na kadhalika. Kwa maneno mengine kiwanda hicho kwa sasa kinaendeshwa kwa hasara ukiachilia mbali uwekezaji uliokwishafanywa katika kiwanda hicho.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo ya kina juu ya jambo hili ambalo kwa mtazamo wake linafanana na hujuma kwa azma ya Taifa letu kuelekea uchumi wa viwanda. Aidha, Kambi Rasmi Bungeni inataka pia kujua ni jitihada gani zimefanywa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ndani ya Serikali katika kupata soko la bidhaa za viuadudu Kibaha kwa kuwa ni jukumu la kisera na ni nini kikwazo hasa katika kupata soko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kiwanda cha dawa ya viuadudu linafanana kwa kiasi kikubwa na lililopo katika kiwanda cha *TANELEC* Arusha, ambacho mtumiaji mkubwa wa bidhaa zake ni ingepaswa kuwa *TANESCO*, kwa visingizio mbalimbali vilivyopo ndani ya uwezo wa Serikali kama ikiamua kujiratibu, *TANESCO* imekuwa ikinunua bidhaa zinazopatikana *TANELEC* toka nje ya nchi na kukiacha kiwanda hicho taabani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati *TANESCO* wameshindwa kununua transfoma zinazotengenezwa na *TANELEC* kwa sababu ya taratibu za manunuzi, wateja wakubwa wa *TANELEC* ni majirani zetu wa Kenya, Uganda, Zambia na Msumbiji ambao mazingira yao yanafanana sana hata taratibu zao za manunuzi. Hii ni changamoto kwetu kama Taifa lazima Serikali ikubali kutatua changamoto hizi na kuwezesha viwanda vyetu kwenda mbele. Masuala haya ya urasimu, muingiliano wa vyombo vyetu vya udhibiti, mlolongo wa kodi na taratibu mbaya za manunuzi zinazopewa nguvu na sheria zetu wenyewe zimekuwa kama nyimbo tu au misahafu isiyoweza kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, haingii akilini ni kwa nini Serikali haioni ukweli huu na kuchukua hatua au ndiyo maana kuna msemo unaosema sikio la kufa halisikii dawa? Mataifa yaliyoendelea kiviwanda hayakuendelea na kufikia yalipo kwa bahati mbaya, yalifikia hatua hiyo kwa kujenga uwezo wake wa ndani, kwa kujenga mazingira ya kutumia bidhaa zake na kuwapa wataalam wake wa ndani fursa ya kujenga uzoefu na uwezo hata kwa kutoa ruzuku inapobidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Mary Nagu akiwa Waziri kwa Wizara hii alianzisha kampeni ya *buy Tanzania use Tanzania*, hii ni kauli mbiu yenye maana kubwa sana kiviwanda, hiyo kauli mbiu imeishia wapi? Leo viwanda vingi havina soko la bidhaa zake kutokana na uholela wa kununua bidhaa kutoka nje. Kila siku nchi inaanza upya akiondoka Waziri Mwijage akija Waziri mwingine, Mwijage atakuwa ameondoka na mafaili yake kama ilivyotokea kwa Mheshimiwa Mary Nagu.



Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupoteza dira katika sera za biashara nchini; mkanganyiko wa mwelekeo wa sera Kitaifa, katika miaka ya 1990 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianza kutekeleza mageuzi makubwa ya kiuchumi (*economic reforms*) kwa kubinafsisha mashirika na viwanda vyote vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali na vilivyokuwa havifanyi vizuri. Lengo kuu la kufanya hivyo ni kuiondoa Serikali katika uendeshaji wa moja kwa moja wa shughuli za uzalishaji wa biashara na kuipa nafasi zaidi ya kutoa huduma za jamii, kujenga miundombinu, kutunga sera na kujenga mazingira wezeshi na rafiki kwa sekta binafsi na kuwekeza katika mashirika na viwanda vya kimkakati vinavyoweza kuchochea mageuzi ya kiviwanda katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya takribani miaka 27 toka sera hii ianze kutekelezwa, Serikali ya Awamu ya Tano ya CCM imeamua kurudi nyuma na kuanza tena kushiriki moja kwa moja katika shughuli za uzalishaji au kiuchumi na biashara. Mfano mzuri ni tangazo la Serikali kuwa nyumba zote za Serikali zitajengwa na *Tanzania Bulding Authority Agency (TBA)* na inasemekana pia ipo nia ya kutaka *SUMA JKT* ipewe kandarasi zote za ujenzi wa barabara za Serikali jambo ambalo limeleta hofu kubwa katika sekta hii ya ujenzi ambayo ina mchango mkubwa katika mafanikio tunavyojivunia leo.

Mheshimiwa Waziri Makame Mbarawa (Mbunge) alipokuwa anawasilisha hotuba yake alilieleza Bunge lako Tukufu kuwa Wakandarasi waliosajiliwa ni 8,475 na alieleza mipango mbalimbali ya kuwaendeleza makandarasi hao. Swali la msingi hapa hivi hawa wakandarasi anaowazungumzia Mheshimiwa Mbarawa watafanya nini na wapi ikiwa kandarasi zote zinafanywa sasa na *agency* za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni uamuzi wa Serikali kuamua kuingia katika biashara ya ndege kwa yenyewe kununua ndege mbili na tayari imeshaagiza nyingine nne kwa gharama ya zaidi ya dola 231.2 tena kwa fedha

taslimu kinyume kabisa na utamaduni uliozoeleka duniani kote kibiashara. Maamuzi yote haya siyo sahihi kiuchumi kwa kuwa sekta binafsi ni mdau mkubwa na muhimu kwa uchumi wa Taifa lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahali pengine duniani Serikali zimeacha kufanya biashara zenyewe na kuchukua mkondo wa kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya kuwezesha sekta binafsi kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na viongozi wa kitaifa ambao hutoa matamko holela yasiyoendana na sera zilizopo, matamshi ambayo kimsingi yanayumbisha utulivu wa mazingira ya biashara nchini na kuathiri pato la Taifa kwa ujumla kwani yameonesha mtazamo hasi kwa sekta binafsi. Kwa mfano, agizo la Mheshimiwa Rais ya kufuta leseni ya mtafiti wa madini katika eneo la Geita kwa sababu tu alilalamikiwa na wananchi hapo kwa papo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni Serikali kuzuia kusafirisha mchanga ghafla tena tayari makontena yakiwa yameshafika bandarini kana kwamba yalikuwa yanatoroshwa. Marufuku ya Serikali juu ya matumizi ya pombe ya konyagi inayopatikana katika vifungashio vinavyojulikana kama viroba kuanzia tarehe Mosi Machi, 2017 jambo ambalo limewagharimu watu wengi uchumi wao hadi kujiua. Nimkumbuke mwanachi wa Jimbo langu Ndugu Peter John Mselia aliyepoteza maisha katika sekeseke hili. Mungu aiweke mahali roho yake pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke wazi kwamba hatuungi mkono matumizi ya pombe ile ya viroba, lakini ingewezekana marufuku hii ikafanyika kwa utaratibu ambao ni mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu mbovu wa sekta ya viwanda na biashara; Serikali imeshindwa kwa kiwango kikubwa kuratibu vyombo vyake vinavyotoa huduma mbalimbali katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji hususan vile vya udhibiti na uratibu. Yapo malalamiko mengi

yanayo onesha kuwa vyombo, Wakala wa Serikali wamekuwa wakiongeza urasimu na gharama zisizo na tija na hata kusababisha kufa kwa miradi kadhaa au kushindikana kwa miradi kadhaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni mgogoro unaokinyemelea kiwanda cha *Tanga Cement*. Baada ya kiwanda cha *Tanga Cement* kukidhi vigezo vyote vya kisheria kama ilivyoainishwa na *TIC* kiwanda hiki kilitambuliwa kama mradi wa kimkakati na hivyo Serikali kupitia *TIC* ikatoa vivutio kadhaa vikiwemo msamaha wa kodi kwa wataalam washauri toka nje ya nchi, kodi ya zuio *withhold tax* kwa manunuzi ya mitambo na vipuri vyake, mwaka 2009 mkataba ukaingwiwa kati ya Serikali na mwekezaji wa kiwanda hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilipata mkopo wa kujenga mradi huu toka taasisi ya fedha za Afrika Kusini na mikataba yao iliingiwa kwa kuzingatia unafuu uliotolewa na Serikali kupitia *TIC*, lakini taasisi nyingine ya Serikali ilikuja kufanya ukaguzi na kutaka kodi zote zilipwe ikiwa ni jumla ya shilingi bilioni 17. Madai ya *TRA* ni kwamba makubaliano ya *Tanga Cement* na *TIC* hayakuwa kwenye Gazeti la Serikali, hivyo kisheria hayakubaliki jukumu ambalo lilipaswa kufanywa chini ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hicho kwa sasa kipo kwenye mkanganyiko mkubwa kutokana na msimamo huo wa *TRA* kwani fedha hizo zinazodaiwa hazipo, wataalam washauri walishalipwa na wanaoendelea kushauri sasa hivi wanafanya kulingana na nafuu ambayo imetolewa. Huu ni mfano mmoja tu ipo mingi. Mfano *A to Z*, Mgodini wa Almasi Mwadui, *Tanga Fresh*, viwanda vya nguo na mavazi vyote vina matatizo kama hayo ambayo yanatokana na Serikali kushindwa kufanya uratibu miongoni mwa vyombo vyake. Hii mifano ni michache ambayo nilipata fursa ya kutembelea wakati nikiwa kwenye safari au ziara za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yote iingie kwenye *Hansard* na naomba kuhitimisha kwa kukushukuru

sana kwa kunipa nafasi na niombe sana Serikali iache kufunga masikio kwenye mambo ambayo ni ya msingi ili tuweze kujenga nchi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI MHESHIMIWA ANTHONY CALIST KOMU (MB)  
WIZARA YA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI KUHUSU  
MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA  
2016/2017 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 –  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo  
la mwaka 2016)*

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu nikiwa mwenye afya njema kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa heshima kubwa naomba nimshukuru Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb) wa Hai na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KRUB) kwa imani yake kubwa kwangu na Waziri kivuli mwenzangu wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara, Mhe. Cecil David Mwambe (Mb).

**Mheshimiwa Spika**, Niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Moshi vijijini kwa imani yao kwangu, na ushirikiano wanaonipa katika kusukuma maendeleo ya jimbo letu ninaahidi kwamba nitaendelea kuwawakilisha vizuri kwa uadilifu na umakini mkubwa. Aidha, niwashukuru na

kuwapongeza waheshimiwa wabunge hasa wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano mzuri katika kuhakikisha Bunge linatimiza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Mwisho lakini si kwa umuhimu ni kwa familia yangu ambayo imekuwa msaada mkubwa sana katika kutekeleza majukumu yangu.

## 2.0 SEKTA YA VIWANDA TANZANIA

### 2.1 Bajeti isiyoakisi Maendeleo ya Viwanda (Hewa):

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa Serikali ya awamu ya tano na zile zote zilizotangulia zinashindwa kuongoza mageuzi ya viwanda nchini kutokana na kuendesha masuala nyeti ya Kitaifa bila kuzingatia nyakati husika na kukubali kujifunza kutoka wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Dira ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kiviwanda ifikapo mwaka 2025 haina uhalisia, sio kwa sababu ilichelewa kupangwa bali ni kwa sababu Serikali ya CCM haiwezi kuongoza kadiri ya dira inazojiwekea yenyewe. Ili Tanzania ifanikiwe kuwa ya uchumi wa kati kiviwanda ifikapo mwaka 2025 basi sharti sekta ya uzalishaji (manufacturing) ichangie wastani wa chini wa asilimia 40 katika pato la Taifa ifikapo 2025.

**Mheshimiwa Spika**, leo hii takaribani miaka 8 kabla ya mwaka 2025, sekta ya viwanda vya uzalishaji (manufacturing) inachangia asilimia 5.2 tu ya pato la Taifa kwa mujibu wa kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (National Five Year Development Plan, 2016/17 – 2020/21).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali ya CCM imechoka kiuwezo, kiakili, kiutashi na kidhamira, hata kama Rais Magufuli akifanikiwa kukaa madarakani kwa miaka 8 ijayo mpaka kufikia mwaka 2025, yeye na Serikali yake yote hataweza kabisa kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kiviwanda kwa sababu ili afanye hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inampa changamoto kuwa kila mwaka wa fedha

ikiwamo mwaka huu wa 2017/2018, sekta ya uzalishaji (manufacturing) inapaswa kukua kwa asilimia 4.35 kila mwaka wa fedha mpaka ifikapo mwaka 2025 ili kufikia lengo la kuifanya 'manufacturing' ichangie asilimia 40 ya pato la Taifa na hatimaye Tanzania kuwa ya uchumi wa kati kiviwanda!

**Mheshimiwa Spika**, Ukisoma kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (National Five Year Development Plan, 2016/17 – 2020/21 Serikali ilijipangia kutumia jumla ya Shilingi Trilioni 5.78 kwa ajili ya uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimkakati kwenye sekta ya uzalishaji (manufacturing), wakati ahadi (commitment) ya Serikali pekee ikiwa ni bilioni 659 – angalia **Jedwali la 1 hapo chini**.

**Mheshimiwa Spika**, Lakini pia ukisoma makadirio yaliyowasilishwa ndani ya Bunge lako tukufu ili kupitishwa kama bajeti ya Maendeleo kwenye eneo la viwanda ni Shilingi Bilioni 2.38 sawa na asilimia 0.36 (0.36%) ya fedha zote za Maendeleo zilizotakiwa kutolewa na Serikali hii ya CCM kama sehemu ya ahadi (commitment yake). – angalia **Jedwali la 2 hapo chini**.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaposema hoja ya Tanzania ya viwanda ni hoja hewa, inamaanisha inachokisema. Kwa 'facts' ambazo tayari tumezianisha katika jedwali la 1 na 2, ni wazi kuwa hakuna Tanzania ya viwanda inayoimbwa kila kukicha na Serikali ya CCM.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulielezea Bunge lako tukufu na Watanzania kwa ujumla inapojigamba kuwa inajenga Tanzania ya viwanda, je Tanzania ya Viwanda itajengwa kwa bajeti ipi? Wakati bajeti yake ni asilimia 0.36 ya fedha zote walizotakiwa kupunga kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Asilimia 96.5 ya viwanda vyote ambayo ni viwanda 50,656 ni viwanda vidogo vinavyoajiri wafanyakazi 1 hadi 9. Asilimia 3.5 vinatoa ajira kuanzia watu 10 na kuendelea. Takwimu hizi hazitoi matumaini makubwa ya kuingia katika uchumi wa viwanda Hivi viwanda vya mtu mmoja mpaka kumi ni kujidanganya, ndio maana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hujigamba kuwa navyo kwa ajili ya kuvigawa.

**Jedwali 1:**

Uwekezaji katika Sekta ya Uzalishaji (Manufacturing Sub Sector)		
Jina la Mradi	Mpango wa Bajeti 2017/2018 TZS Bilioni	Government Commitment for 2017/2018 Under Five Yrs Development Plan of 2016/17-2020/21 TZS Bilioni
Bagamoyo SEZ	3,412	402.1
Kurasini Logistics Center	220	
Mtwara SEZ (Freeport Zone)	12	0.9
Kigoma SEZ	10	5
Tanga SEZ	5	2.7
Ruvuma SEZ	3	2.6
Bunda SEZ	3	2.8
Morogoro - Star City SEZ	337	13
Industrial Park Interventions	23	20.6
MSMEs Parks Strategic Choices	29	13.3
Automotive industry Strategic Choices	160	70.7
Petro and Chemical Industries Strategic Choices	1,144	30.5
Development of Pharmaceutical Industries Strategic Choices	27	5
Textile and Clothing Industries	10	9.5
Building and Construction Industries Strategic Choices	76	5
Leather Industry Strategic Choices	8	3
Agro processing strategic Choices	129	47.2
Iron and Coal Strategic Choices	179	25.01
<b>JUMLA</b>	<b>5,787</b>	<b>659</b>

Chanzo: URT (2016) National Five Year Development Plan 2016/17 - 2020/21, Page 230 - 241

Jedwali 2:

Miradi ya Uwekezaji wa Viwanda Kimkakati iliyotengewa fedha 2017/2018 Fungu 44	
Jina la Mradi	Kiasi cha Fedha za Maendeleo kilichotengwa kwenye Bajeti, 2017/2018 TZS
Lake Natron	2,000,000,000
Revival of General Tyre and Rubber Plant	70,000,000
Integrated Industrial Development	10,000,000
Mchuchuma Coal to Electricity Project	100,000,000
Liganga Vanadium Titanium	100,000,000
KAIZEN	100,000,000
<b>JUMLA</b>	<b>2,380,000,000</b>

Chanzo: Volume IV - Public Expenditure Estimates Development Vote  
(PART A), Page 70 & 71

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013, inaonyesha kuwa Tanzania ina jumla ya viwanda 50,656 ambavyo vipo katika mikoa mbalimbali hapa nchini, lakini miongoni mwake ni viwanda/mashirika 119 ambayo yalibinafsishwa na kati yake 74 vikiwa vinafanya kazi (vizima), 44 vinaendelea vizuri, 13 vinalegalega na 17 vimefungwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, Hii nayo ni hadithi ya siku nyingi na bahati mbaya hivi ndivyo viwanda vikubwa vyenye kuajiri watu wengi na vinavyotumia mali ghafi za ndani zinazotokana



na mifugo na kilimo mfano vile vya nguo kama Urafiki, mwater, kilitex na mutex, na vya ngozi nk. Hatua za Serikali haziridhishi kwa kiwango kikubwa kwani maelezo yao mbele ya kamati ya viwanda, Biashara na Mazingira kuhusiana na vile ambavyo vinalegalega/vimefungwa au wawekezaji wamebadili matumizi/makubaliano Serikali iliambia kamati wahusika wamewanyima ushirikiano hata mahali pengine wamefungiwa nje ya magate.

**Mheshimiwa Spika**, bila alibu taarifa ya wizara inasema kuwa baadhi ya viwanda vilivyo binafishwa vilitumika kama dhamana kukopa benki na fedha hizo zilitumika kwa shughuli nyingine badala ya kuviendeleza, huu ni udhaifu kwa upande wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iache kuwa na ndimimbili katika utendaji wake, iweje tu polisi wa barabarani waweze kuadhibu mtu anayebadili matumizi ya gari lake labda gari la mizigo akasafirishia abiria hapo kwa hapo ishindikane kwa waliogeza viwanda kuwa maghala ya bidhaa toka nje au malisho ya mbuzi?

**Mheshimiwa Spika**, wimbo wa Wizara pamoja na msajili wa Hazina kwamba inafanya upembuzi wa utendaji na mikataba ya viwanda/mashirika ili kufikia uamuzi wa kunyang'anya viwanda/mashirika yanayolegalega nakuwapa wawekezaji wenye uwezo umekuwa ukijirudia kila mara.

**Mheshimiwa Spika**, hoja hapa ni lini kazi hii itakamilika? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kurejea upya mpango wake wa Maendeleo ya Taifa wa miaka 5 na mpango wa mwaka wa fedha 2017/2018 na kueleza ni kwa namna gani Serikali itashiriki zoezi la kufufua viwanda vilivyofia mikononi mwa wawekezaji waliomilikishwa viwanda hivyo kutokana na sera mbovu ya ubinafsishaji ambayo ilikosa umakini kwa kiwango kikubwa sana hivyo kutoa mwanya mkubwa wa kuua sekta ya viwanda badala ya kuiendeleza.

**Mheshimiwa Spika**, Ni vema ikaeleweka maeneo haya yanayohodhiwa kwa majina ya viwanda lakini hakuna viwanda ni maeneo yaliyokwisha endelezwa kimkakati kwa uwekezaji wa viwanda hivyo ni uendawazimu kuhubiri kila siku kuwa Serikali inahamasisha kutenga maeneo kwa ajili ya viwanda bila kujiuliza yaliyokwisha tengwa na kuendelezwa yanafanyiwa kazi gani, kwani kila mji ulikuwa na maeneo ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, sio busara kupigana kugundua tairi ambalo wenzetu walishagundua. Aidha, Kambi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kufanya mapitio upya ya uwekezaji uliofanyika katika msingi wa ujenzi wa viwanda hapa nchini ili kuja na hatua za makusudi katika Maendeleo ya sekta ya viwanda hapa nchini. Msukumo uwekwe zaidi kwenye mazao ya chakula, misitu, mifugo na biashara kama Kahawa, Korosho, Mpira, Pamba, Mchikichi, Katani, Mawese, alizeti n.k Mageuzi ya viwanda duniani hutegemea Maendeleo ya watu, hasa wakulima wa mazao ya chakula na biashara, wafugaji na wavuvi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muda mrefu wananchi wa Tanzania wanaolima mazao wameshindwa kuinua hali zao za maisha kutokana na sera ya uwezesaji wa kimitaji na mazingira magumu ya biashara kuwabana katika uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo kuweza kuyaongezea mazao yao thamani kama vile vya kukamua mafuta ya alizeti nk.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa inayovikabili viwanda nchini ni pamoja na ukosefu wa mitaji, teknolojia ya uzalishaji kupitwa na wakati (vilivyobinafsishwa), malighafi isiyokuwa na uhakika, umeme, maji, urasimu katika kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali, mlolongo wa kodi na kutoshirikishwa katika kufikia maamuzi yenye athari kwa viwanda.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni**, inaona kwamba changamoto hizi bado zipo na zitaendelea kuwepo kwa kuwa Serikali haina mkakati wowote maalumu wa kibajeti wa kuondoa changamoto hizi ila ni nyimbo zile zile (Business as usual).

## 2.2 Utekelezaji wa Bajeti Usioridhisha katika miradi ya kimkakati

**Mheshimiwa Spika**, si rahisi kuamini lakini ni ukweli kuwa maelezo ya Serikali katika utekelezaji wa bajeti na miradi mbalimbali yamejengwa katika misingi ya ujanja ujanja unaolenga kufunika ukweli halisi ili mambo yapite tu.

**Mheshimiwa Spika**, nitarejea mifano michache inayoweza kuthibitisha ninachoeleza. **Fidia ya maeneo ya EPZ na SEZ:** Hili ni jambo la kisera na kisheria ambalo limekuwepo kwa muda mrefu na kila mwaka limekuwa likipewa fedha chini ya wizara ya viwanda, biashara na uwekezaji japo hazilingani kabisa na mahitaji. Aidha ni wajibu wa Serikali kisheria kujenga miundombinu ili kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wawekezaji katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya SEZ.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka huu wa fedha 2017/2018 jambo hili limetoweka kabisa katika bajeti halitajwi popote pamoja na ukweli kwamba Wananchi katika maeneo kadhaa nchini walishapisha maeneo yao na wamenyimwa kabisa kufanya maendeleo yoyote wakisubiri fidia za maeneo yao. Maeneo yaliyotengwa yana jumla ya hekta **31,000** lakini ambayo yamefidiwa ni takriban hekta **10,000** tu.

**Mheshimiwa Spika**, nitarejea mifano michache ili kuonyesha hali ilivyo kama Bagamoyo SEZ mchakato wa kutwaa maeneo ya Wananchi ulianza toka 2007 na kukamilika mwaka 2010 kwa uthamini wa hekta 5,742.5 ambapo kilihitajika kiasi cha shilingi bilioni 50.2 kama fidia lakini mpaka leo ni hekta 2,560.8 tu sawa na shilingi bilioni 28.36 tu ndizo zilizokwisha tolewa kama fidia mpaka sasa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo ya randama ya Wizara yenyewe kiasi kinachohitajika kufanya fidia katika eneo hili kwa sasa ni shilingi bilioni 51.3 zikijumisha na riba ya ucheleweshaji. Ninajua kuwa Mhe. Waziri amekuwa akisema fidia ya eneo hili itafanywa na mwekezaji binafsi. Kambi Rasmi Bungeni itataka kujua ni lini mwekezaji huyo atalipa fidia na ni kiasi gani na kwa masharti yapi.

**Mheshimiwa Spika**, jukumu hili kwa maamuzi ya Baraza la Mawaziri la Serikali ya Mh Rais John Pombe Magufuli limepelekwa kwa sekta binafsi jambo ambalo linakosa uhakika wa kufanyika na halina tena ukomo wa muda wa kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, hatua hii ni ushahidi dhahiri wa Serikali ya awamu ya tano kukwepa jukumu lake la kisera na kisheria na kuendeleza tabia yake ya kutojali athari mbaya zinazoweza kusababishwa na maamuzi yake kwa Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa sheria ya maeneo maalumu ya uwekezaji (SEZ Act Nos 2 of 2006 & 2011) uendelezaji wa miundombinu katika maeneo hayo kwa mujibu wa sheria hii ni jukumu la Serikali lakini maeneo hayo kwa asilimia kubwa yameishia kuambulia visingizio kama ufinyu wa bajeti hivyo maeneo karibu yote yaliyokwisha fidiwa hayajafanyiwa maendeleo yoyote mfano Bagamoyo special economic zone hekta 2,399.6, Kigoma, Tanga ekari 1,363, Bunda ekari 3,255, Mererani hekta 530.87, na Ruvuma.

### **2.3. Kupata Mwekezaji atakayejenga Miundombinu ni ndoto ya mchana**

**Mheshimiwa Spika**, eneo jingine ni mradi wa makaa ya mawe ya mchuchuma na chuma cha liganga. Huu ni mradi wa muda mrefu ambao umetajwa na Serikali kuwa ni mradi wa kimkakati kwa kuwa utachochea maendeleo ya viwanda. Mradi huu una faida zifuatazo:-

a. Mradi wa Mchuchuma na Liganga utahusisha ujenzi wa Kinu cha Umeme chenye uwezo wa Megawati 600 ambapo 250 zitatumika katika Kiwanda cha Chuma na nyingine 350 zitapelekwa kwenye Gridi ya Taifa kwa ajili ya kuongeza nguvu katika nishati ya umeme.

b. Tanzania kwa sasa itakuwa na umeme wa gesi, maji na umeme wa makaa ya mawe ambapo umeme wa makaa ya mawe utakuwa msaada mkubwa kwa nchi kwani hautegemei tabianchi kama ilivyo vyanzo vingine vya umeme.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na faida zote hizo bado mradi huu haujapewa uzito unaostahili kila siku kuna hadithi mpya katika utekeleza ji wa mradi huu. Licha ya maagizo mengi ya Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, moja ya maagizo ya kamati ya Viwanda, Blashara na Mazingira ya Bunge la kumi ni kuharakisha utekelezaji wa mradi huu muhimu na wa lazima kwa maendeleo endelevu ya Viwanda. Mwaka jana Bunge lilirudia tena agizo hilo na maelezo ya Serikali yalikuwa kila hatua imeshachukuliwa na mradi huo utanza robo ya kwanza ya mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya leo ya Serikali yaliyopo katika randama yanasema Baraza la Mawaziri lililokaa tarehe 7 Desemba 2016 na kuelekeza mkataba wa mradi wa mchuchuma na liganga upitiwe upya. Kufuatia maelekezo hayo kamati ya makatibu wakuu iliundwa na kupitia mkataba huo na kutoa mapendekezo ya vivutio vitavyozingatia maslahi ya Taifa. Kulinda maslahi ya Taifa ni muhimu sana lakini kwanini maelezo yote ya awali hayajawahi kueleza mapungufu hayo na hivi kweli hii ndiyo sababu ya mradi huo kutokuanza muda wote? Hatua hii ni kana kwamba huu mradi ndio unabuniwa kwa mara ya kwanza na sasa ni vigumu kuamini kama mbia aliyekwisha ambuliwa ataendelea au la.

**Mheshimiwa Spika**, majibu mengi ya Serikali katika wizara hii ni ya kupigishana "sound" au blaa blaa!! tu, huo ni ushahidi tosha kuwa Serikali ya CCM ikiwa ni pamoja na hii ya awamu ya tano ni kusema ili mradi muda upite kwa kuwa haingii akilini kuwa mradi huu maelezo yake ndiyo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya Serikali yamekuwa yakibadilika kila siku kutegemea ni nani anapewa taarifa hiyo kama ilivyojidhihirisha hapo juu. Mh Spika mwenendo wa aina hii hauwezi kuifikisha nchi kwenye uchumi wa viwanda kama inavyohubiriwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi Bungeni inaitaka Serikali

kusema ukweli katika mizania hii ambayo inahusu uchumi sekta ambayo inahitaji kuaminiwa na wadau wengine.

#### 2.4. Ufufuaji wa kiwanda cha General tyre Arusha

**Mheshimiwa Spika**, Mh Spika, katika mwaka wa fedha 2016/17 utaona kuwa mradi wa kufufua kiwanda cha General tyre kasma (1210) zilitengwa **shilingi milioni 150** kwa ajili ya mradi huo kuandaa andiko la mradi, kuendeleza mashamba ya mpira na kutafuta mbia mpya.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka huu wa fedha 2017/2018 wizara inaomba jumla ya sh 70,000,000 kutafuta mbia lakini utafiti uliofanywa na wataalamu wa ndani inaonyesha kuwa mitambo iliyopo katika kiwanda hicho haifai kabisa kulingana na teknolojia ya sasa, kiwanda hicho kinahitaji kupanuliwe ili kiweze kuzalisha kwa wingi kuweza kushindana na soko la kimataifa na imeshauri kiendeshwe na sekta binafsi na Serikali iwe mbia kwa thamani ambazo zipo hapo.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo mengine yaliyo katika kitabu cha mpango wa maendeleo wa Taifa 2017/2018 uk. 20 yanasema baada ya taarifa ya awali ya wataalam hao Serikali inatafakari nini yatakuwa matumizi sahihi zaidi ya eneo la kiwanda hicho, mwekezaji aliyekuwa ameomba kuwa mbia katika kufufua kiwanda ameomba kupatiwa eneo la kuweka kiwanda kipyaa cha matairi eneo la TAMCO Kibaha, kwa sasa kiwanda hicho kinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo hakuna kitu kinachoitwa kiwanda cha matairi cha General tyre kwa maana ya mitambo ila kuna eneo ambalo palikuwepo na kiwanda cha matairi cha General tyre na mabaki ya kiwanda hicho ambayo kwa lugha fasaha na ya uwazi zinapaswa kuondolewa kupisha uwekezaji sahihi.

**Mheshimiwa Spika**, bila kuweka jambo hili wazi mbele ya Bunge lako tukufu na maamuzi yakafanyika hicho kinachoitwa kiwanda cha matairi cha General tyre Arusha

kitaendelea kuwa kama mfereji wa kutumia fedha za umma kama zilivyokwishatumika huko nyuma bila matokeo. Mh Spika, ni vema tukajiuliza katika kutenga fedha hizi sh. 70,000,000 zinazoombwa, taarifa ya wataalamu imezingatiwa?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe maelezo kuwa ni kwanini katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (National Five Year Development Plan, 2016/17 – 2020/21, kiwanda cha General Trye kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kilipaswa kutengewa jumla ya Shilingi bilioni 22 na sio milioni 70. Kiasi hicho kilichotengwa ni kidogo mno kuweza kufanya kazi zilizokusudiwa na kuwezesha kiwanda hicho kuanzishwa tena upya kwa tija.

## **2.5. Kiwanda cha Viuadudu kibaha na kiwanda cha TANALEC Arusha**

**Mheshimiwa Spika**, Hiki ni kiwanda kilichotajwa na Serikali kama ni cha kimkakati kimekabidhiwa shirika la maendeleo la Taifa (NDC) baada ya ujenzi wake kukamilika kwa mkopo wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 22.307 na wenye riba ya aslimia 11 utakaorejeshwa kwa miaka 10.

**Mheshimiwa Spika**, ili kiwanda hicho kianze kuzalisha kimepewa na Serikali jumla ya sh 2,100,000,000 na pia kimekopa jumla ya sh. 4,553,010,000 na kimeanza kuzalisha na hadi February 2017 kimezalisha dawa kiasi cha lita 100,000 ambazo zimeuzwa nchini Niger kwa kiasi cha sh 1,012,000,000 tu. Nchi yetu ambayo inatumia fedha nyingi sana kupambana na malaria na ndio ugonjwa unaoongoza kwa kuua haijanunua hata lita moja. Wizara ya afya imeshapitishiwa bajeti yake ya 2017/2018 na hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya dawa toka Viaududu Kibaha. Kiwanda hiki hakiwezi kuwa endelevu kama Serikali yetu haitaweza kujipanga na kuwa na soko la uhakika la ndani ambalo ni dhahiri lipo lakini hakuna uratibu ndani ya Serikali (coordination).

**Mheshimiwa Spika**, Leo kiwanda hicho ambacho kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 6 kwa mwaka na kujiendesha hakizalishi kwa kuwa hakina soko la bidhaa zake na kinaendelea kulipa gharama mbalimbali za uendeshaji kama wafanyakazi, umeme nk. Kwa maneno mengine kiwanda hicho kwa sasa kina endeshwa kwa hasara ukiachilia mbali uwekezaji uliokwishafanywa katika kiwanda hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi Bungeni inataka maelezo ya kina juu ya jambo hili ambalo kwa mtazamo wake linafanana na hujuma kwa azma ya Taifa letu kuelekea uchumi wa Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kambi Rasmi Bungeni inataka pia kujua ni jitihada gani zimefanywa na wizara ya Viwanda, Biashara na uwekezaji ndani ya Serikali katika kupata Soko la Bidhaa za Viuadudu Kibaha kwa kuwa ni jukumu lake kiseru na ni nini kikwazo hasa inapozingatiwa katika andiko la mradi huu la mwaka 2010 linaonyesha umuhimu wa kiwanda hiki ni haja kubwa ya kukabiliana na tatizo la ugonjwa wa malaria nchini

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la Viuadudu linafanana kwa kiasi kikubwa na lililopo katika kiwanda cha TANALEC Arusha ambacho mtumiaji mkubwa wa bidhaa zake ingepaswa kuwa TANESCO lakini kwa visingizio mbalimbali vilivyopo ndani ya uwezo wa Serikali kama ikiamua kujiratibu. TANESCO imekuwa ikinunua bidhaa zinazopatikana TANALEC toka nje ya Nchi na kukiacha kiwanda hicho taabani.

**Mheshimiwa Spika**, wakati TANESCO wameshindwa kununua Transformer zinazotengenezwa na TANALEC kwa sababu ya taratibu za manunuzi, wateja wakubwa wa TANALEC ni majirani zetu wa Kenya, Uganda, Zambia na Msumbiji ambao mazingira yao yanafanana sana hata taratibu zao za manunuzi. Hii ni changamoto kwetu kama Taifa lazima Serikali ikubali kutatua changamoto hizi na kuwezesha viwanda vyetu kwenda mbele.

**Mheshimiwa Spika** ni wakati mwafaka sasa Serikali kuacha



visingizio na kuchukua hatua za maksudi kuona kuwa viwanda vya ndani vinapata fursa katika soko la ndani kwani faida zake ni nyingi kwa uchumi wetu ukilinganisha na visingizio vinavyotolewa eti bei ni kubwa na taratibu za manunuzi haziruhusu lakini moja ya sababu ya bei kuwa juu ni kodi zinazotowwa na Serikali yenyewe na kwa kiasi fulani urasimu unaozalishwa na vyombo vyetu wenyewe vya udhibiti kwa kuongeza gharama za uendeshaji, nyingi ya taasisi hizi hukinzana katika utendaji wake na hufanya jambo ambalo linaweza kufanywa na taasisi moja na kupata matokeo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, masuala haya ya urasimu, mwingiliano wa vyombo vyetu vya udhibiti, mlolongo wa kodi na taratibu mbaya za manunuzi zinazopewa nguvu na sheria zetu wenyewe zimekuwa kama nyimbo tu au misahafu isiyoweza kurekebishwa.

**Mheshimiwa Spika**, haingii akilini ni kwanini Serikali haioni ukweli huu na kuchukua hatua au ndio maana kuna msemu unaosema sikio la kufa halisikii dawa?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema sasa ni muda mwafaka masuala yote haya ya bei na taratibu zetu za manunuzi kuangaliwa upya na kuweka utaratibu unaokubalika kisheria unaohami viwanda vyetu vya ndani kwani utakuwa na tija kubwa zaidi kuanzia kwenye ajira ambazo nazo huzalisha kodi nyingine nyingi kama mapato kwa Serikali, kukuza utaalamu wa ndani, urahisi wa kukarabati (after sales service) bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kukuza matumizi ya malighafi zinazopatikana hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, mataifa yaliyoendelea kiviwanda hayakuendelea nakufikia yalipo kwa bahati mbaya yalifikia hatua hiyo kwa kujenga uwezo wake wa ndani, kwa kujenga mazingira ya kutumia bidhaa zake na kuwapa wataalamu wake wa ndani fursa ya kujenga uzoefu na uwezo hata kwa kutoa ruzuku inapobidi.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati Mhe Mary Nagu akiwa Waziri kwa wizara hii, alianzisha kampeni ya *“buy Tanzania use Tanzania”*, hii ni kauli mbiu yenye maana kubwa sana kiviwanda. Hiyo kaulimbiu imeishia wapi?, continuity ya mambo haipo katika nchi yetu kila waziri akiondoka anaondoka na mafaili yake na anayekuja anakuja na mafaili yake. Hii ndiyo Serikali ya CCM.

## 2.6. Kila siku nchi inanza upya.

**Mheshimiwa Spika**; mwenendo huu unaifanya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni irudie maneno yake ya mwaka jana na ni nayanuku “...Miaka mitano ijayo ya Mhe. Rais Magofuli inayotumia ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, haina jambo jipya katika Maendeleo ya Sekta ya Viwanda hapa nchini. Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 inazungumzia Maendeleo ya sekta ya viwanda katika muktadha ule ule ulioshindwa kuzaa matunda kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita. Ilani hiyo ya CCM inasema kuwa;

*“Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2015–2020, Chama Cha Mapinduzi kitalelekeza Serikali kuweka nguvu kubwa katika kukamilisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda Awamu ya Tatu (2010–2020) ambayo malengo yake ni kuiwezesha Sekta ya Viwanda kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu kama ilivyoanishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025...”*

*Mheshimiwa Spika, Mh Rais wa awamu ya tano alishaweka wazi msimamo wake kuwa anajitambua na haelekezwi na mtu yeyote cha kufanya, ni imani ya kambi rasmi ua upinzani Bungeni kuwa sasa Nchi inaendeshwa kwa mawazo na utashi wa Mh Rais John Pombe Magofuli na ndio maana ametamka mara kadhaa kuwa anayo kazi ya kunyoosha nchi kwanza; maana yake ni kuwa watangulizi wake waliipinda nchi sana. Msimamo huu kwa kiasi kikubwa siyo sahihi kwa kuwa huo ni uimla jambo ambalo limeanza kuvuruga uchumi wetu na kuondoka katika vipaumbele tulivyojipangia na kuanza mtindo wa kubahatisha. Ushauri wetu ni kama ule wa Rais mstaafu wa awamu ya nne kuwa yafanyike mapya ya kutupeleka mbele siyo mapya ya kubomoa.*

### 3.0 SERIKALI KUPOTEZA DIRA KATIKA SERA ZA BIASHARA NCHINI

#### 3.1. Mkanganyiko wa Mwelekeo wa Sera Kitaifa

**Mheshimiwa Spika**, katika miaka ya 1990 Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania ilianza kutekeleza mageuzi makubwa ya kiuchumi (Economic reforms) kwa kubinafsisha mashirika na viwanda vyote vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali na vilivyokuwa havifanyi vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la kufanya hivyo ni kuiondoa Serikali katika uendeshaji wa moja kwa moja wa shughuli za uzalishaji na Biashara na kuipa nafasi zaidi ya kutoa huduma za jamii, kujenga miundo mbinu, kutunga sera na kujenga mazingira wezeshi na rafiki kwa sekta binafsi na kuwekeza katika mashirika na viwanda vya kimkakati vinavyoweza kuchochea mageuzi ya kiviwanda katika Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya takribani miaka 27 toka sera hii ianze kutekelezwa, sasa, Serikali ya awamu ya tano ya CCM imeamua kurudi nyuma na kuanza tena kushiriki moja kwa moja katika shughuli za uzalishaji/kiuchumi na Biashara. Mfano mzuri na hai ni tangazo la Serikali kuwa nyumba zote za Serikali zitajengwa na TBA na inasemekana pia ipo nia ya kutaka SUMA JKT ipewe kandarasi zote za ujenzi wa Barabara za Serikali jambo ambalo limeleta hofu kubwa katika sekta hii ya ujenzi ambayo ina mchango mkubwa katika mafanikio tunayojivunia leo.

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya Waziri wa ujenzi, uchukuzi na mawasiliano Mh Prof. Makame Mbarawa (MB) alilieleza Bunge lako tukufu kuwa makandarasi waliosajiliwa ni 8,475 na alieleza mipango mbalimbali ya kuwa endeleza makandarasi hao. Aidha alieleza kazi nyingi sana zinazofanywa na TBA ambaye ni wakala wa majengo wa Serikali na na ukweli si Mkandarasi lakini yeye sasa ndiye anayetakiwa kufanya kazi zote za ujenzi wa majengo ya Serikali. Swali la msingi hapa, hivi hawa wakandarasi anaowazungumzia Mhe Mbarawa watafanya nini na wapi?

Ikumbukwe kuwa hawa wanaajiri wataalamu wetu na wanalipa kodi mbalimbali kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine ni uamuzi wa Serikali kuamua kuingia katika biashara ya Ndege kwa yenyewe kununua ndege 2 na tayari imeshaagiza nyingine nne (4) kwa gharama ya dola za marekani 231.2 tena kwa fedhaa taslimu kinyume kabisa na utamaduni uliozoeleka Duniani kote kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, maamuzi yote haya siyo sahihi kiuchumi kwa kuwa sekta binafsi ni mdau mkubwa na muhimu kwa uchumi wa Taifa lolote.

**Mheshimiwa Spika**, Mahali pengi Duniani/kiulimwengu sera za aina hii zimeshindwa na Serikali nyingi zimeamua kuchukua mkondo wa Serikali kujenga mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuendesha uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iliachie soko lifanye kazi yake, Serikali ijenge mazingira wezishi na rafiki kwa kutunga sera safi, sheria na kuzisimamia kikamilifu, kuondoa urasimu usio na tija, kulinda wawekezaji wa ndani kwa wivu mkubwa na kwa uangalifu wa hali ya juu kwa kuzingatia sheria, kanuni na mikataba ya kimataifa. Ni kwa kufanya hivi ndio tunaweza kupata akina; Ali Mufuruki, Dr Reginald Mengi, Mohamed Dewji, Said Salim Bakhressa na wengi zaidi kama wawekezaji wazawa na kuingia katika uchumi wa kipato cha kati.

**Mheshimiwa Spika**, katika randama ya Wizara yenyewe imekiri kuwepo na changamoto nyingi katika mazingira ya uwekezaji katika sekta ya viwanda na biashara kama "...uwepo wa kanuni nyingi, uwepo wa wakusanyaji ushuru wengi wa ada mbalimbali, uwepo wa taasisi nyingi za udhibiti (karibu 18), uwepo tozo nyingi za kibiashara (takribani 40) ambazo zinaweza kushawishi rushwa, na uwepo wa gharama kubwa za wadhibiti hususani kupata usajili wa biashara, VAT, ushuru wa ndani na uthibitishwaji wa ubora wa bidhaa..."

### 3.2 Matamko ya Viongozi yasiyoendana na Sera za Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa na viongozi wa Kitaifa ambao hutoa matamko holela yasiyoendana na sera zilizopo, matamko ambayo kimsingi yanayumbisha utulivu wa mazingira ya biashara nchini na kuathiri pato la Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, matamko hayo yameonyesha mtazamo hasi kwa sekta binafsi kwa kuwa hayazingatii sheria zilizopo, sera, uwekezaji uliokwisha fanywa na mdau katika sekta mbalimbali. Mfano uamuzi/agizo la Mh. Rais la kufuta leseni ya Mtafiti wa madini katika eneo la Geita eti kwasababu tu alilalamikiwa na Wananchi kwenye mkutano wa hadhara. Serikali kuzuia kusafirisha mchanga ghafla tena tayari makontena yakiwa yameshafika bandarini kana kwamba yalikuwa yanatoroshwa.

**Mheshimiwa Spika**, matamko mengine ni pamoja na marufuku ya Serikali juu ya matumizi ya pombe ya Konyagi inayopatikana katika vifungashio vinavyojulikana kama viroba kuanzia tarehe 01/03/2017 jambo ambalo limewagharimu Watu wengi uchumi wao hadi kujua nimkumbuke mwananchi wa jimbo langu Ndg Peter John Mselia aliyepoteza maisha katika sekeseke hili, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Matamko yote niliyoorodhesha hapo juu ni maamuzi yasiyo shirikishi na pia hukiuka mkataba na kuendelea kuleta hofu na maswali mengi kwa wawekezaji katika Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Uwazi katika Uendeshaji wa Biashara nchini ndio msingi wa kukusanya mapato halisi bila kudanganywa na wawekezaji. Uwazi hauanzii kwenye usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi bali uwazi huanzia katika Mikataba ya Kibiashara, lakini Serikali hii ya CCM bila kuzingatia ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni uliotolewa mara kwa mara kuhusu kuweka wazi mikataba tata baina ya Serikali na Makampuni ya Uchimbaji madini. Kwa mfano wakati dhahabu ndio inaongoza kibiashara na kunachangia asilimia 21 ya mauzo ya bidhaa zote nje ya nchi

kwa takribani dola bilioni \$1.42, Serikali inarukia ejenda ya kuzuia mchanga wa madini kuuzwa nje ya nchi, kuikosesha nchi mapato bila kwanza kuweka wazi mikataba ya uchimbaji, ambayo ndio chanzo cha nchi kupoteza mapato mengi.

### **3.3 Kushuka kwa mauzo nje ya nchi (Exports) kinyume na malengo ya Sera ya Taifa ya Biashara**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Biashara nchini inaongozwa na Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 iliyobuniwa na Serikali ya CCM, ambayo dalili za kisayansi zinaonesha kuwa imechoka kiakili katika kuisimamia Sera yake yenyewe. Tafiti mbalimbali duniani na nchini zinaonesha kuwa Sera hii pamoja na utekelezaji wake haifanyi vizuri katika Maendeleo ya Sekta nzima kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Sera hii ya Taifa ya Biashara katika dira yake inaweka mkazo kwa Sekta nzima ya biashara kuwa ni kuugeza uchumi kuwa wa uzaji wa bidhaa nje ya nchi (export-led); Dira ya Sera hiyo inasema, nitanukuu:-

*"... to transform the economy from a supply constrained one into a competitive export-led entity responsive to enhanced domestic integration and wider participation in the global economy through national trade liberalisation"* Tafiri yake ya Kiswahili ni kuwa:

*"...kubadilisha uchumi kutoka katika vikwazo vya usambazaji kwenda kwenye ushindani wa mauzo ya bidhaa nje ya nchi yatakayowezesha maingiliano ya ndani na ushiriki mkubwa wa uchumi wa dunia kupitia biashara huria kitaifa"*

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini kuwa msingi mkuu wa Sera ya Biashara ya Taifa ni **"mauzo ya bidhaa nje ya nchi"** yaani **"exports"**. Msingi ambao ujenzi wake kwa vitendo umekuwa ni kitendawili kikubwa kutokana na Serikali hii ya CCM kushindwa kwa vitendo kuimarisha uzalishaji wa bidhaa na huduma ndani ya nchi ili hatimaye kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Ripoti ya Shirika la **Trading Economics** iliyochapwa mwaka 2017 katika takwimu zake zimeonesha kuwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi (Exports) yameshuka kutoka **Dola milioni 932.90** mwezi Januari, 2016 mpaka **Dola milioni 854** mwezi Disemba, 2016. Wastani wa mauzo ya bidhaa nje ya nchi uliendelea kubakia kuwa **dola milioni 549.16** kutoka mwaka 2006 mpaka mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2017 iitwayo **“Ease of Doing Business Tanzania”** (Wepesi wa Kufanya Biashara Tanzania) imeripoti kuwa Tanzania imeshika nafasi ya 180 kati ya 190 (nafasi 10 kutoka mkiani) katika wepesi wa kufanya biashara baina ya mipaka ya nchi na nchi (Trading Across Borders)

**Mheshimiwa Spika**, kukamilisha nyaraka za mauzo ya bidhaa nje ya nchi hapa kwetu Tanzania inachukua saa 96 (karibuni siku 4) wakati Botswana huchukua takribani saa 8 tu, na Kenya majirani zetu huchukua muda wa saa 21. Kushuka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi kumeendelea kushika kasi hasa katika kipindi amacho Serikali ya awamu ya tano ipo madarakani.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa taarifa mbele ya Bunge lako tukufu juu ya hatua inazozichukua kuhakikisha inaongeza kiwango cha mauzo ya bidhaa nje ya nchi (Exports). Tunaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaboresha mazingira ya biashara katika mipaka ya nchi na nchi (Trading Across Borders). ili nchi yetu iendelee kuaminiwa na wawekezaji wa ndani na nje ni lazima sera na sheria zetu za biashara ziaminike, ziheshimiwe na ziwe shirikishi (Predictable and participatory).

### **3.4 Uratibu Mbovu wa Sekta ya Viwanda na Biashara**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeshindwa kwa kiwango kikubwa kuratibu vyombo vyake vinavyotoa huduma mbalimbali katika wizara ya viwanda, biashara na uwekezaji hususani vile vya udhibiti na uratibu. Yapo malalamiko mengi yanayoonyesha kuwa vyombo/ wakala wa Serikali

wamekuwa wakiongeza urasimu na gharama zisizo na tija na hata kusababisha kufa kwa miradi kadhaa au kushindikana kwa miradi kadhaa nchini mfano mzuri ni mgogoro unaokinyemelea kiwanda cha Tanga Cement PLC

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kiwanda cha Tanga Cement PLC kukidhi vigezo vyote vya kisheria kama vilivyowekwa na TIC kiwanda hiki kilitambuliwa kama mradi wa kimkakati na hivyo Serikali kupitia TIC ikatoa vivutio kadhaa vikiwemo msamaha wa kodi kwa wataalamu washauri toka nje ya nchi, kodi ya zuio (withhold tax) kwa manunuzi ya mitambo na vipuri vyake na mwaka 2009 mkataba ukaingiwa kati ya Serikali (TIC) na mwekezaji. Kiwanda hiki kilipata mkopo wa kujenga mradi huu toka taasisi za fedha za Afrika Kusini na mikataba yote iliingiwa kwa kuzingatia unafuu uliotolewa na Serikali kupitia TIC lakini taasisi nyingine ya Serikali (TRA) ilikuja kufanya ukaguzi na kutaka kodi zote zilipwe ikiwa ni jumla ya Shilingi. Bilioni 17. Madai ya TRA ni kwamba makubaliano ya Tanga Cement PLC na TIC hayakuwekwa kwenye gazeti la Serikali (GN) hivyo kisheria hayatambuliki jukumu ambalo lilipaswa kufanywa chini ya Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika** Kiwanda hicho kwa sasa kipo kwenye mkanganyiko mkubwa kutokana na msimmo huo wa TRA kwani fedha hizo zinazodaiwa hazipo na wataalamu washauri waliojenga walishalipwa na wanaoendelea na ushauri wanao mkataba wenye punguzo la Kodi hizo na ni jambo la kisheria ambalo kulivunja lina athari zake kubwa.

**Mheshimiwa Spika** huu ni mfano unaotokana na Serikali kutokuwa na uratibu miongoni mwa vyombo vyake. Kiwanda hiki hakina kosa ila kinabebeshwa mzungo na matokeo yake kitayumba na malengo yaliyokusidiwa kupotea kabisa kwa uzembe wa Serikali yenyewe ambayo ina jigamba kujenga mazingira rafiki na wezishi kwa ustawi wa kauli yake mbiu ya Tanzania ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ichukue hatua za haraka na za makusudi kutatua tatizo hili kukinusuru kiwanda hiki muhimu. Itakuwa fedheha



sana kwa Serikali inayojitanabaisha kwa kauli mbiu ya Tanzania ya Viwanda kuongeza gofu jingine jijini Tanga ambalo tayari limeshaelemewa na magofu ya viwanda vingi vilivyouawa na Serikali za CCM awamu zilizotangulia.

**Mheshimiwa Spika** kana kwamba haitoshi kiwanda hiki kinaandamwa na tatizo lingine linalosababishwa na Serikali pia. Tanga cement PLC kilitambuliwa kama kiwanda cha kimkakati kwa lengo la kutengeneza Clinker ambayo ni malighafi kwa ajili ya viwanda vya cement nchini hasa vile vidogo vidogo

**Mheshimiwa Spika**, kutekeleza jukumu hilo mahitaji ya nishati ya umeme ni makubwa sana yanaweza kuchukua asilimia 70 ya uendeshaji wa kiwanda hicho. Umeme unaweza kuwa unaotokana na Maji (TANESCO) au Gesi au makaa ya mawe. Umeme wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi ndiyo nishati ya umeme wa uhakika na nafuu kwa kiwanda hicho lakini bila kujali ustawi wa kiwanda hiki Serikali imepiga marufuku uagizaji wa makaa ya mawe toka nje jambo ambalo limekiacha kiwanda hicho na chaguo la kutumia umeme wa Tanesco ambao hauaminiki na ni ghali sana au kununua makaa ya mawe hapa nchini ambayo nayo hayapatikani kwa kadiri ya mahitaji na kwa wakati lakini pia ni ghali sana kutokana na gharama za usafirishaji kutokana na miundombinu ya inayotumiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kukaa na wadau wa viwanda vya cement nchini na kukubaliana namna yenye tija ya kututua mikanganyiko hii ambayo kimsingi inaweza kuua baadhi ya viwanda vyetu vingi vya cement hapa nchini na dhamira safi ya Serikali ya awamu ya tano ya kujenga viwanda na kupunguza uhaba wa cement nchini jambo litakalosababisha bei ya bidhaa hii kuwa ya juu kinyume na matarajio.

#### **4.0 SEKTA YA BIASHARA**

##### **4.1 Mazingira Magumu ya kufanya Biashara nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Ripoti ya **Ease of Doing Business Tanzania**

**2017** imeonesha kuwa Tanzania imeongeza ugumu zaidi katika hatua za kuanzisha biashara kwa kuongeza tozo za usajili. Jambo hili linaathiri juhudi za kuongeza ajira kwa vijana wetu. Tanzania imeshika nafasi ya 135 kati ya 190 katika wepesi wa kuanzisha biashara mpya. Unapokuwa na ugumu wa kuanzisha biashara, unawafanya wajasiriamali wasifanye shughuli rasmi ya kuingiza mapato yao na mapato ya Serikali, na hivyo kupunguza kiasi cha ajira zitokanazo na biashara rasmi.

**Mheshimiwa Spika**, ili mjasiriamali aanzishe biashara Tanzania anatakiwa kuruka vihunzi 9 vya utaratibu wa usajili ndani ya siku 26 na gharama ya asilimia 21.5 ya mapato ya Mtu mmoja kwa mwaka (per capital income). Biashara za ujenzi wa majengo ikiwemo uuzaji wa vifaa vya ujenzi unakabiliwa na changamoto kubwa ya muda mrefu unaotumiwa kutoa Kibali cha Ujenzi (Construction Permit). Utafiti wa Ease of Doing Business 2017 unaonesha kuwa inachukua takribani siku 205 na taratibu 18 ili mfanyabishara apate kibali cha ujenzi. Kuingiza umeme kwenye biashara mpya kama vile kiwandani inachukua siku 109 na hatua 4 za ukamilishaji wa nyaraka mbalimbali. Kupata hati ya nyumba kwa ajili ya biashara mbalimbali inachukua hatua 8 ndani ya siku 67 kukamilisha mchakato wa kupata hati hizo.

**Mheshimiwa Spika**, nchini Rwanda, ambako ndiko Serikali ya awamu ya tano inapendelea sana kwenda kuchukua ushauri wa masuala mbalimbali ikiwemo jinsi ya kukusanya kodi, inachukua muda wa siku 1 tu kufungua Kampuni bila kulipia gharama zozote zile. Hapa nchini inachukua siku 4 kufungua kampuni na ada inayotozwa ni kati ya Shilingi 20,000 na 440,000 jambo linazuia biashara nyingi kurasimishwa, ajira kupotea na sekta binafsi kuendelea kudumaa.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mazingira magumu ya kuanzisha na kuendeleza biashara nchini, utafiti uliofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2012, (National Baseline Survey Report – Micro, Small and Medium Enterprises in Tanzania) unaonesha kuwa asilimia 96.4 ya biashara za chini (Micro-Enterprises) hazijasajiliwa na BRELA, na asilimai 84.4

ya biashara ndogo (Small Enterprises) hazijasajiliwa na BRELA, huku asilimia 63 ya wafanyabishara waliohojiwa wakisema hawajui chochote juu ya masuala ya usajili wa biashara.

**Mheshimiwa Spika**, hii ni ishara kuwa mazingira ya kuanzisha biashara nchini sio rafiki kiasi cha kuwa na kiwango kikubwa cha biashara zinazoanzishwa bila kusajiliwa rasmi. Ni ishara pia kuwa mipango ya Serikali haiwezi kuwafikia kundi hilo kubwa la wafanyabiashara nchini ili kuboresha mazingira yao ya biashara na kuongeza mapato ya Serikali kwa namna itakayofaa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuboresha mazingira ya kuanzisha biashara kwa kupunguza idadi ya siku mpaka kufikia siku moja (saa 24) na kuondoa tozo za usajili wa makampuni ili kuchochea wajasiriamali kufungua makampuni kwa wingi na kuongeza ajira kwa Watanzania. Aidha, tunaitaka Serikali kuweka mazingira rafiki na yanayovutia wafanyabisahara wa kada zote kusajili biashara zao kwa namna itakayoiwezesha Serikali kubaini wafanyabishara walipo ili kuwapelekea Maendeleo kwa wepesi na haraka zaidi, tofauti na ilivyo hivi sasa, ambapo ni vigumu mipango ya Serikali kuzifika biashara ndogo ndogo zaidi ya asilimia 90 ambazo hazijasajiliwa na kutambuliwa.

#### **4.2 Kufungwa kwa Biashara zaidi ya 2,000 nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Waziri Uchumi na Mipango, Mhe. Dr. Philip Mpango alinukuliwa na gazeti la Mwananchi, tarehe 3 Januari, 2017 akikubali kuwa Serikali imebaini kuwa karibu wafanyabiashara 2,000 wamefunga biashara zao. Gazeti hilo la Mwananchi, lilimnukuu mwenyekiti wa Wafanyabiashara nchini, Bw. Johnson Minja akidai kuwa kufungwa kwa biashara hizo kunatokana na Serikali kutosikiliza kilio cha muda mrefu cha wafanyabiashara, na kuwa Serikali imeweka mazingira magumu sana ya kufanya biashara hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Suala hili la kufungwa kwa biashara nchini limetolewa angalizo na Shirika la Fedha la Kimataifa

(IMF). Ripoti ya IMF kuhusu utekelezaji wa Sera Tanzania (Policy Support Instrument for Tanzania) iliyotolewa tarehe 9 Januari, 2017 imeionya Tanzania kuwa moja ya masuala yanayohatarisha ukuaji wa uchumi ni pamoja na *“kuyumba kwa sekta binafasi kutokana na mikakati mipya ya Serikali ya awamu ya tano”* (private sector uncertainty about the government’s new economic strategies.)

**Mheshimiwa Spika**, kama biashara 2,000 zilizofungwa wastani kila biashara inaajiri watu 5, inamaanisha kuwa ajira 10,000 za Watanzania zimepotea kutokana na sera mbovu za uratibu wa biashara nchini zinazosimamiwa na Serikali ya awamu ya tano. Serikali imevuruga mazingira ya biashara nchini na hivyo kupelekea wananchi wengi kuishi maisha ya dhiki na taabu.

**Mheshimiwa Spika**, muendelezo wa sera hizi zinagharimu ajira na biashara nchini ni kinyume cha ushauri uliotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa – IMF tarehe 14 Aprili, 2017 Tanzania kuifikia malengo ya uchumi wa kati sharti iwe na sekta binafsi yenye nguvu na yenye mazingira bora ya biashara. Ni wazi kuwa kudorora huku kwa biashara na kuendelea kufungwa kwa biashara nchini ni ishara kuwa Serikali ya awamu ya tano haielewi inataka kulipeleka wapi Taifa letu kwa kuendelea kuharibu mazingira ya biashara nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa taarifa za kina kwanini biashara zaidi ya 2,000 zimefungwa nchini. Aidha, tunaitaka Serikali iseme kuwa ni hatua zipi inazozichukua ili kuondoa mdororo wa biashara nchini na hatua zilizochukuliwa kuzuia kuendelea kufungwa kwa biashara nyingine nchini.

#### **4.3 Hali duni ya Wafanyabiashara wadogo pamoja na Machinga**

**Mheshimiwa Spika**, Taifa letu limekosa dira muafaka (a right vision) juu ya kuendeleza watu wake kupitia sekta isiyo rasmi iliyojaa wafanyabiashara wengi wa biashara ndogo ndogo maarufu kama wamachinga. Kwa ufupi, Tanzania kwenye

sekta ya Biashara ni Taifa la wachuuzi, ambao kwa muda mrefu biashara zao imekuwa ikiathiriwa na ukosefu wa dira muafaka ya Serikali kuhusu biashara ndogo ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inaendelea kusisitiza kuwa 'Maendeleo ni ya watu na sio ya vitu' hivyo ni jukumu la Serikali kuangalia Maendeleo ya kila mtu mmoja mmoja kwa makundi yao kama vile ilivyo kwa kundi la wafanyabiashara ndogondogo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali pamoja na kufanya tafiti mbalimbali kupitia mashirika yake mbalimbali lakini inashindwa kuzitumia tafiti hizo kwa umakini wakati wa kupanga vipaumbele kwenye sekta ya ukuzaji wa biashara kwa ajili ya Maendeleo ya watu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Moja ya tafiti ambazo hazitumiki ipasavyo na kwa kiwango cha kuridhisha katika kupanga Maendeleo ya wafanyabiashara ndogo ndogo ni pamoja na utafiti uliofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2012 juu ya Sekta ya Biashara za Chini, Ndogo, na Biashara za Kati (National Baseline Survey Report – Micro, Small and Medium Enterprises in Tanzania).

**Mheshimiwa Spika**, Utafiti huo ulibaini kuwa vijana wa Kitanzania wenye umri kati ya miaka 25 na 34 ndio kundi kubwa kwa asilimia 36 linalojihusisha na biashara ndogo ndogo nchini, wakati kwa ujumla wake asilimia 14.6 hawajawahi kumaliza elimu ya shule ya msingi, na asilimia 73.5 ndio wamemaliza elimu ya shule ya msingi na asilimia 72.1 katika maisha yao yote hawajawahi kabisa kupata mafunzo yoyote kabla hawajaanza biashara. Bila kuwa na 'picha kubwa' yaani maono makubwa ya kuliangalia taifa letu miaka 100 mbele, taifa haliwezi kupiga hatua za Maendeleo ya kibiashara kwa haraka, bali tutaenda kwa kusuasua kama ilivyo hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Ukisoma kitabu cha randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 fungu namba 60 hakuna malengo ya kushughulikia masuala

ya wafanyabishara ndogo ndogo. Katika hali kama hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitarajia Wizara ya Viwanda na Biashara katika malengo yake kwenye sekta ya biashara katika mpango wa taifa na katika bajeti ya mwaka 2017/2018 itoe kipaumbele kuboresha mazingira ya wafanyabiashara ndogo ndogo kulingana na tafiti zilizofanywa huko nyuma, jambo ambalo halijapewa umuhimu na Serikali.

## 5.0 SEKTA YA MASOKO

**Mheshimiwa Spika**, dhana ya masoko ina uhusiano wa moja kwa moja na aina na ubora wa bidhaa zinazozalishwa na uwezo wa mtu kufanya mahusiano ya kibiashara. Kwa muktadha huo, masoko hayatafutwi kwa kuangalia siasa za washirika wako tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ili kupata masoko kama ni ya bidhaa zako haina maana kwamba uzuie bidhaa za mshindani wako. Unachotakiwa kufanya ni kuzalisha kwa ubora uliozaidi na pia bei yake iwe ni shindani kwa kulinganisha na bidhaa kama hizo za mshindani wako.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Taifa letu halizalishi vya kutosha bidhaa za ndani hivyo manunuzi ya bidhaa nje ya nchi (imports) ni makubwa zaidi ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi (exports). Takwimu zinaonesha kuwa mauzo yetu ya bidhaa nje ya nchi yameshuka kwa asilimia 5.0 ambayo ni sawa na shilingi Trilioni 8.22 wakati uagizaji wa bidhaa nje ya nchi ukiongezeka kwa asilimia 8.9 ambayo ni sawa na Shilingi Trilioni 19.90.

**Mheshimiwa Spika**; Sera mbovu za biashara zilizo asisiwa na Serikali hii ya CCM hazijaweza kumudu kuiondoa nchi katika hali mbaya kama hiyo. Nchi yetu imekuwa tegemezi na haizalishi vya kutosha kiasi cha kuagiza kutoka nje ya nchi hata chakula kama sukari, mchele, ngano na mahindi, samaki, matunda mazao ambayo yalipaswa kupatikana kwa wingi hapa nchini na hata ziada ya kuuza nje.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa sasa Tanzania inanunua mchele kutoka katika mataifa ya China, India, Indonesia, Pakistan na Vietnam, wakati uzalishaji wa ndani ukiwa mdogo ambapo asilimia 18 ya familia zinazojihusisha na kilimo ndio hulima zao la mchele. Jiji la Dar es Salaam pekee hutumia asilimia 60 ya mchele unaozalishwa ndani wakati asilimia 30 huliwa na wakulima wenyewe na asilimia 10 inayobakia huingia katika soko la ndani hasa maeneo ya mikoani. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya Global Agricultural information Network iliyotolewa tarehe 21 Machi 2016 kama ilivyoandaliwa na Benjamin Mtaki na kuidhinishwa na Kate Snipes.

**Mheshimiwa Spika;** ni aibu kubwa kwa nchi yetu kuagiza mchele kutoka mataifa mengine wakati tuna mito inayotiririka maji mwaka mzima, tuna ardhi kubwa yenye rutuba, na vijana wetu wana nguvu za kuzalisha ila Serikali haijatilia maanani aibu hii mbele ya uso wa ulimwengu. Taifa linashindwa kuzalisha ngano na badala yake thamani ya manunuzi ya ngano nje ya nchi yaani **“imports of wheat”** yamefikia dola milioni 225 kwa mwaka kwa mujibu wa Global Agricultural information Network.

**Mheshimiwa Spika;** Ununuzi wa bidhaa nje ya nchi (imports) unachangia katika kuporomosha thamani ya Shilingi ya Tanzania kiasi cha kulifanya taifa letu kupoteza hazina yake ya fedha za kigeni na kuongezeka kwa pengo kubwa katika urari wa biashara. Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani imeporomoka kutoka shilingi 1,754.7 Januari 2015 mpaka kufikia Shilingi 2,335 mwezi May 2017. Sababu zinazotajwa na Serikali kuchangia uporomokaji huo ni pamoja na kupungua kwa mauzo ya nje ya nchi. Hapa Serikali imeendelea kukiri udhaifu wake kuwa inashindwa kabisa kusimamia thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani katika soko la dunia

**Mheshimiwa Spika,** *“nchi yoyote inayotaka kujitegemea kibajeti lazima iimarishwe na bidhaa zake zilizoongezewa thamani na kuuzwa nje ya nchi”* hii ni kauli ya mtendaji mkuu wa TPSF

## 6.0 SEKTA YA UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Sera ya Uwezeshaji ya Taifa ya mwaka 2004 pamoja na sheria ya usimamizi wa sheria hiyo ya mwaka 2004 vililenga kuhakikisha kwamba watanzania waliowengi wanapata fursa ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwenye sekta mbalimbali. Mataifa mengine yamefanya hivyo, mfano; Afrika Kusini mwaka 1994 baada ya kumalizika kwa Ubaguzi wa Rangi walianzisha sera ya kuwawezesha Waafrika wazawa *Kiuchumi (Broad-Based Black Economic Empowerment (B-BBEE))*,

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wetu, Sheria na Sera za Uwezeshaji na Uwekezaji ni dhahiri vimeshindwa kukidhi matakwa tarajiwa, imebaki makabatini badala yake Serikali ya awamu ya tano ni kama imetangaza vita na watanzania wazawa pale walipojaribu kutafuta fursa za kuwekeza kwa kuwaona kama maadui wa uchumi wetu na haya yanajidhihirisha jinsi wafanyabiashara wanavyosumbuliwa na kutengwa katika shughuli ambazo wameandikishwa kihalali.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inawachukulia wafanyabiashara kama mahasimu wake nasio kama wadau muhimu, hata uamuzi wa Serikali wa kuondoa pesa zake na za mashirika katika benki za biashara ni katika mtazamo huo hasi ambao unawanyonya wafanyabiashara na na mazingira ya biashara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza katika mazingira kama hayo, Sera na sheria za uwezeshaji zinawasaidia vipi watanzania katika kushiriki na kumiliki sekta mbalimbali za uchumi wa nchi yetu? Ni dhahiri kuwa Serikali imeshindwa kuwasaidia Watanzania kuingia katika biashara kubwa kwa makusudi au kwa kukosa uwezo wa kujenga mazingira wezeshi kwa Watanzania kuwekeza na kuwa sehemu ya wamiliki wa uchumi wao. Serikali za CCM zimeshindwa kabisa kutumia ardhi na rasilmali asilia za nchi yetu kama mtaji kwa watanzania katika ubia na wawekezaji wa nje.

## 6.1. TIC NA UWEKEZAJI WA KUSUASUA NCHINI



**Mheshimiwa Spika**, Hali ya uwekezaji nchini hairidhishi hata kidogo hii ni kutokana na marekebisho ya mara kwa mara ya sheria zinazosimamia vivutio vya uwekezaji, urasimu, rushwa, ukosefu wa uratibu wa kiSerikali n.k

**Mheshimiwa Spika**, Sababu nyingine zinatokana na utawala mbovu kama ucheleweshaji wa vibali mbalimbali vya kuwasaidia wawekezaji kuendeleza miradi yao, umeme usiokuwa wa uhakika, ubovu na urasimu wa usafirishaji na bandari ya Dar es salaam kuwa na urasimu uliokithiri, migogoro ya ardhi isiyotatuliwa, mlolongo wa kodi na ufanisi duni wa wakala wa Serikali, bodi za mazao na riba kubwa zinazotowwa na taasisi za fedha na rasimali fedha zisizokidhi mahitaji ya TIC mfano 2017/2018 TIC haikutengewa hata senti moja kama OC.

## 7.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**; Msimamo wa Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA/UKAWA iliyouzwa na Mgombea Urais wa CHADEMA/UKAWA Mheshimiwa Edward Lowassa tuliwaahidi Watanzania kuwa katika kipindi cha miaka mitano yaani 2015 – 2020 naomba kunukuu tamko la Ilani, alisema kuwa<sup>1</sup> ***“Tutainua mchango huu wa sekta hii muhimu (ya viwanda) ufikie siyo chini ya asilimia kumi na tano (15%) katika miaka yetu mitano ya kwanza”***. Tutafanya hivyo kwa:

- 1) *Kuimarisha sekta ya viwanda kuwa mhimili wa uchumi kwa uzalishaji wa bidhaa na ajira endelevu;*
- 2) *kuingia mikataba ya kuleta teknolojia ya kutengeneza bidhaa badala ya kuleta bidhaa;*
- 3) *Kuhakikisha kuwa ndani ya miaka mitano asilimia (75%) ya mali ghafi zote za Tanzania zinasindikwa kabla ya kusafirishwa nje ili kuongeza mapato na ajira ya mamilioni ya vijana;*
- 4) *Kutoa kipaumbele na vishawishi maalum kwa viwanda vya kuendeleza kilimo. Kwa mfano, tutaendeleza viwanda vya mbolea kulingana na mahitaji ya taifa na uuzaji wa ziada ya bidhaa hiyo nje ya nchi; pili viwanda vya kutengeneza mbegu bora na madawa ya kilimo;*

---

<sup>1</sup> ILANI YA CHADEMA/UKAWA Ukurasa wa 45.

5) *Kufufua na kuongeza viwanda vyetu vya nguo ili tuweze kusindika kiwango kitakachofikia asilimia sabini na tano (75%) ya pamba inayozalishwa Tanzania.*

6) *Kuimarisha na kukuza usindikaji wa mazao ya katani, kahawa, tumbaku na chai ili kuhakikisha ongezeko kubwa la thamani katika mazao haya na ongezeko kubwa la bidhaa zinazotokana na mazao haya.*

**Mheshimiwa Spika**, Serikali za CCM kwa utamaduni wake wa kutaka kuonekana inafanya imekuwa ikijiwekea vipaumbele vingi na wasivyoweza kutekeleza au visivyona mchango mkibwa katika mageuzi ya kiviwanda yanayoelezwa na dira ya Taifa au kutokana na kujaribu kushika kila kitu na mwishowe kushindwa vyote. Tunataka utamaduni huu sasa ukome kwani unaliingizia taifa hasara kwa kutenga fedha kidogo kidogo kwenye miradi na hatimaye kushindwa kukamilisha miradi husika kwa wakati na huku gharama za miradi zikikua maradufu kutokana na mabadiliko mbalimbali na kwa wakati mwingine kulipa watumishi wasiokuwa na kazi ya kufanya kutokana na kutokuwepo kwa fedha za kutekeleza majukumu yao. Haya ni malipo hewa yanayotokana na mipango hewa. Tanzania kwa sasa itakuwa na umeme wa gesi, maji na umeme wa makaa ya mawe ambapo umeme wa makaa ya mawe utakuwa msaada mkubwa kwa nchi kwani hautegemei tabianchi kama ilivyo vyanzo vingine vya umeme.

**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni**, inasisitiza na kuendelea kuishauri Serikali kuwa bado inaweza kubadilisha mwelekeo wake kwa kuzingatia msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Maendeleo ya Sekta ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha.

.....  
**ANTHONY CALIST KOMU (MB)**

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI-  
WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

**17.05.2017**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na uchangiaji, kuna mambo mawili; la kwanza kama ambavyo kwenye Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Bobali alipongezwa kwa Hotuba nzuri, Mheshimiwa Antony Komu kipekee naye anapongezwa kwa hotuba ambayo haijakuwa na miongozo, taarifa wala utaratibu. Ahsante sana, nadhani huo ndio utaratibu mzuri alioelekeza Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja hapa kutoka kwa *Captain* wa Bunge *Queens* yaani wachezaji wa mpira wa pete au *netball* anawatangazia kwamba wanawake wote wa Bunge hili wanaotaka kujiunga na timu hiyo ya Bunge *Queens* wawe wanahudhuria mazoezi uwanja wa Jamhuri saa 12.00 asubuhi. *Captain* wetu ambaye ni Mheshimiwa Halima Mdee anatumkumbusha kwamba kutakuwa na ziara za mechi za majaribio. Kwa hiyo, mchezaji kama atakuwa hahudhuri mazoezi maana yake kwenye hizi ziara hatokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnasisitizwa mwende huko, wanawake, hajasema kama wanaume wanaweza kucheza huu mchezo, lakini Wabunge wanawake mnasisitizwa kwenda huko ili aweze kusuka vizuri kikosi. Pia mtakumbuka Mheshimiwa Spika alitangaza kwamba, Bunge la Tanzania safari hii tutakuwa wenyeji wa michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo kama kawaida kwa wachezaji wa Bunge Mheshimiwa Spika, akiwepo uwanjani huwa wanashinda michezo yote, sasa tusije tukajikuta safari hii, Mheshimiwa Spika anakuwepo halafu makombe yanaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndio msisitizo wa tangazo la *Captain* wa Bunge *Queens*. Baada ya hayo Waheshimiwa Wabunge tutaendelea. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha hapa ya wachangiaji kutoka vyama mbalimbali, tutaenda kwa utaratibu ufuatao:-

Tutaanza na Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Silvestry Koka ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niwe wa kwanza kuchangia katika hotuba hii ya Viwanda na Biashara. Kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote na watendaji wa Wizara mbalimbali kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza Ilani ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia hapa hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ukurasa wa 24. Hivi Mkuu wa Nchi ndiye baba, Rais, amepita mahali wananchi wamelalamika akatoa jibu kwamba atawasaidia, sasa hapa wanasema kwa nini alitoa majibu ya papo kwa papo kule wapi na nini, walitaka afanye nini? Watu wamemlalamikia Mheshimiwa Rais, si lazima ndio awape majibu wanasubiri na kwenye Ilani ya CCM tulisema tutatekeleza tutatoa majibu ya kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo vile vile Bunge lako hili tumesema kwamba kuna baadhi ya mikataba hasa ya madini sio mizuri tulisema hapa, sasa imetekelezwa tena tunalalamika tunasema kwa nini michanga na kadhalika, aaa. Serikali imeunda Kamati ya kushughulikia, tuiache Serikali ifanye kazi yake. Kwa hiyo naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya Wizara hii, juu ya fidia iliyoko katika Soko Kuu la Kimataifa katika Mji wetu wa Makambako. Kitabu cha bajeti, kilichopita cha 2016/2017, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi wa Makambako na Mheshimiwa Rais alipopita pale aliwaambia fidia hii mtalipwa; na alipokuja Waziri Mkuu alisema majibu nitarudi nayo mimi ya kuwalipa fidia wananchi wa Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabisa Serikali ione maana kwenye kitabu hiki cha bajeti ambacho kiko hapa, cha 2017/2018 haipo tena, hazijawekwa. Kwa hiyo niombe Serikali itekeleze na mwisho ni mwezi huu Juni, niombe sana Serikali ihakikishe inalipa fidia za wananchi wa Makambako, vinginevyo mimi kama Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa leo nitashika shilingi kama nitakuwa sijapata majibu maana kwenye bajeti ya 2017/2018 hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali ihakikishe inalipa fidia ya wananchi katika maeneo ya Makambako. Wananchi hao wamekaa kwa muda mrefu, hawawezi kufanya kitu chochote wala kuendeleza wala kufanya kitu chochote katika maeneo yale na Serikali ilisema italipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri uko hapa na nilikutana na Waziri wa fedha akanihakikishia tutalipa fidia, nikuombe Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya viwanda uko hapa nimwombe ahakikishe wanasimamia kulipa fidia katika eneo hili la Makambako. Vile vile katika fidia, wako hawa watu wa ujenzi, kuna mradi unaojengwa pale, *one stop center* ambao unajengwa katika eneo letu la Makambako, vile vile nao wanahitaji kulipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kupitia hili nimwombe sana wahakikishe wanawasiliana pia katika Wizara hii nyingine ambayo kuna fidia mbili hapo, kuhakikisha tunalipa fidia ya Mji wetu wa Makambako ili wananchi wa mji ule waendele sasa kuwekeza viwanda na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, limezungumzwa kwa uchungu sana suala Liganga na Mchuchuma. Suala hili limezungumzwa kwa miaka mingi, mpaka tunajuliza kuna tatizo gani sisi watu wa Kusini kule? Kuna tatizo gani na ni uchumi mkubwa katika Mkoa wa Njombe na Kitaifa kwa ujumla, lakini mpaka sasa hatujaona hapa nini ambacho kinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuja Waziri Mkuu tumekwenda pale Liganga mwaka huu, wale wawekezaji wametenga hela za kulipa fidia, wale wawekezaji wako tayari na Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema Kamati maalum itaundwa ya kuona je, zile fedha zilizotengwa, bilioni kumi na tatu, zinaendana na fidia ile?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimuulize Mheshimiwa Waziri, mpaka sasa wamefikia wapi juu ya kulipa fidia ya Liganga na Mchuchuma ili mwekezaji yule aweze kuendelea na shughuli ile kwa sababu fedha zipo? Ni uchumi mkubwa sisi tunaoutegemea sana katika Liganga na Mchuchuma na mwekezaji yule tunamkatisha tamaa maana sasa hatuelewi nini kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Serikali ihakikishe kwamba inalipa fidia kwa sababu fedha zipo mwekezaji anazo yeye mwenyewe na kuhakikisha wawekezaji wale wanaanza na walikuwa tayari kuanza. Bajeti iliyopita mlituambia mwaka huu wa 2016/2017 mwekezaji ilitakiwa aanze, nini kimechelewesha? Tupate majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, leo katika Wizara hii kwa kweli inafanya kazi nzuri ya kuhakikisha viwanda vinajengwa katika nchi yetu na ndio uchumi. Tukiwekeza kwenye viwanda tutapata ajira na kadhalika. Nakubaliana kabisa Mheshimiwa Mwijage anafanya kazi nzuri pamoja na watendaji wake na Naibu Waziri, lakini nirudie tena, nasema kwa uchungu kabisa, wale watu wa Makambako hivi sasa wako njiani wanakuja, kwa hiyo jioni Mheshimiwa Mwijage anao na Mheshimiwa Waziri Mkuu jioni atatakiwa akutane nao, kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema majibu nitarudi nayo mimi, sasa wanakuja. Nimwombe jioni ahakikishe anakutana na hao watu wa kutoka Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linanipa tabu, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu nitakaposhika shilingi juu ya kulipa fidia ya watu hawa mniunge mkono,

kabisa, yaani Mbunge mwenzenu napata tabu juu ya watu hawa kulipwa fidia. Kwa sababu kwenye bajeti humu ya mwaka huu hazimo sasa maana yake mpaka mwezi Juni hii zilitakiwa ziwe zimeshalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage sijui nisemeje, wale watu wananipa tabu kwa kweli. Yaani nakosa raha juu ya kulipa fidia hizi, niombe sana Serikali yangu. Mheshimiwa Rais alishasema fidia ilipwe sasa nini? Yamechukuliwa makaratasi yote yanayotakiwa ya wale watu, wako 274 yako kwenu Hazina na Mheshimiwa Mwijage anayo.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

#### **T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga subiri upokee taarifa, Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa mchangiaji ambaye anachangia sasa kwamba malalamiko ambayo anayatoa katika Jimbo lake alitakiwa apeleke katika Chama cha Mapinduzi ambacho mpaka leo malalamiko hayo ambayo anayasema Serikali ya CCM imeshindwa kuyatekeleza, hapa sio mahali pake.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa, tuseme kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani ngoja taarifa yake tuimalize kwanza, halafu nitakuruhusu.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anapotosha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unajua tungekuwa tunaielewa kwamba Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani tunatekeleza Ilani ya CCM tusingesema hivyo. Wote hapa tunatekeleza Ilani ya CCM ndiyo tuliopata ridhaa, ndiyo maana naiambia Serikali yangu ya CCM itekeleze Ilani ambayo tulishaiambia. Kwa hiyo wote humu tunatekeleza Ilani ya CCM. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa Mheshimiwa Deo sasa naomba upokee taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Ridhiwani.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi taarifa yangu nampelekea yule msemaji kule...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Aaaa, tulieni, mmegusa eneo langu lazima niseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba humu ndani tumeletwa na wananchi kuja kuiambia Serikali ya Chama cha Mapinduzi, juu ya mambo ambayo wananchi wetu wametutuma. Kwa hiyo yeye kama anayo Serikali nyingine ambayo anaiambia huko, ajue humu ndani wote tumeletwa kuja kuzungumzia masuala ya chama chetu na nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa kwa Kanuni zetu kwa sababu Mheshimiwa Rhoda Kunchela ulikuwa huchangii, tutaendelea. Mheshimiwa Deo Sanga malizia muda wako.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana, nadhani ameelewa humu ndani wote tunatekeleza Ilani ya CCM, ndiyo inayosimamiwa na ndiyo maana tunaiambia Serikali sasa yale mambo ambayo iliahidhi iweze kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimalizie tu kwa kusema Mheshimiwa Mwijage na watendaji wake,



wamenielewa nilichokisema, niombe sana kuhakikisha mpaka Juni, angalau wale watu tuwalipe fidia zao kama ambavyo tulikuwa tumeahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya nikushukuru sana, niishukuru Serikali, nimshukuru Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanga. Sasa tutamsikia Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Silvestry Koka atafuatia, halafu Mheshimiwa Nape Nnauye ajiandae.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya, amefanya kazi kubwa ya mfano. Nijenge hoja ya kumpongeza, maana yake wengine watasema kwa nini wanapongezana; mimi nampongeza Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kwa mwaka huu kwa Mkoa wa Tabora; amefanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ameamua kupeleka maji katika Mkoa wa Tabora kutoka *lake* Victoria, hiyo pongezi ya kwanza. La pili, ametengeneza barabara ambazo ziko kwenye mpango na ambazo zimekamiliika tangu akiwa Waziri. Kubwa zaidi, amefanya kazi kubwa mno ya kuleta usafiri wa ndege katika Mkoa wa Tabora, hayo yote lazima nimpongeze. Si hilo tu, ameleta tena *standard gauge* ambayo itapita Tabora, mimi bado nitaendelea kumpongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutangaza viwanda na biashara kwa ajili ya kuondokana na umaskini kwenda kwenye lengo la uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba sasa niende kwenye hoja. Hoja yangu nzito kabisa nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Viwanda kwamba mimi nilikuwa Mbunge mwaka 2000 mpaka 2010, hilo kwanza alielewe, kwa hiyo ninapochangia hapa kuzungumza haya ninayoyasema ayazingatie ayafuatilie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Kiwanda cha Manonga cha Usindikaji wa Mbegu za Pamba, kiwanda hiki kina historia yake, hawa wawekezaji wanambabaisha wanamtapeli, aende kwa kina, Rajan alikuwa mbabaishaji. Tumeanza kuzungumza kuhusu kukifufua kiwanda hiki ajenda ni ubabaishaji tu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, nakuheshimu; wakati anajibu swali la Dkt. Kafumu alisema yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, alisema hivi huyu mwekezaji inaonekana hana nia ya kuja kuwekeza au kukifufua kile kiwanda, sasa kigugumizi cha nini? Kwa nini asiamue akawapa Igembensabo ambao wapo na wanaweza kufanya kazi hiyo? Haya nayo yanachangia kuwafanya wananchi wa Tabora, vijana pamoja wakulima kurudi nyuma. Kwa hiyo, naomba hilo Mheshimiwa Waziri, mimi nitamfuata mpaka Ofisini kwake ili ajue uchungu wa wananchi wa Tabora. Maana alilijibu kama vile suala hili kama lipo lipo tu, lakini nimwombe alifuatilie kwa kina, lina uchungu sana na wananchi wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora kimepoteza ajira za vijana wa Mkoa wa Tabora wote na mikoa jirani kwa uzembe. Hivi hawa wawekezaji kwa nini mnawaogopa? Mpelekeeni Mheshimiwa Rais, atayatumbua haya ili angalau na sisi tuonekane katika nia ya Serikali ni kupeleka viwanda. Kiwanda cha Nyuzi cha Mkoa wa Tabora ambacho kiko Manispaa kina historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuwepo Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Misigalo alishika shilingi katika jengo

hili miaka ile. Kwa hiyo, alipolipeleka hilo wananchi wakaona anafaa bora aendelee akakaa vipindi viwili. Kwa matokeo hayo mpaka leo hakuna Mbunge anayekaa vipindi viwili kwa Mkoa wa Tabora kwa sababu hakuna wanachokiona tunachofanya. Sasa na mimi ili niweze kurudi tena lazima tupambane mimi na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mkoa wa Tabora kutokuleta wawekezaji ni makosa, tunazo fursa zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Tabora inaongoza katika nchi hii kwa ulinaji wa asali, hilo nalo alizingatie na lazima niseme fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba kuna nta ya kutosha, tumbaku ya kutosha, pamba ya kutosha, maembe ya kutosha pamoja na karanga za kutosha; na maeneo ya kuwaweka hao wawekezaji yapo na alishakiri mwenyewe, alikuwa anatuletea wawekezaji, lakini juzi wakati anajibu swali alisema hivi, aah wale wawekezaji tena hawapo. Hivi akisema hawapo kwa mtu wa chini kabisa kule inaonekana Serikali haitendi haki, kwingine wanapeleka wawekezaji, kwingine hawapeleki wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kiwanda cha nyama, mifugo ipo, zamani pale tulikuwa Kiwanda cha Maziwa, kwa hiyo ukileta Kiwanda cha Nyama kitahudumia Singida, Shinyanga, Mbeya na Kigoma, lazima watapita pale. Hata hivyo si hilo tu, Tabora iko kati; kwa nini nasema iko kati, ukiwatangazia wawekezaji ukasema Tabora kuna fursa zifuatazo, watauliza kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema Tabora iko kati; ukiichukua Mbeya kuleta kutoka Zambia wapo pale watafika Tabora, ukitoka DRC lazima apite Tabora, ukitaka kwenda Burundi lazima apite Tabora, anapokwenda Rwanda lazima apite Tabora, anakwenda Uganda lazima apite Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, akiwekeza pale atakuwa na mfumuko wa kupata soko mpaka Afrika Kusini, kwa sababu hii ni *center* ambayo inafungua; kama anavyofanya Mheshimiwa Rais wetu anafungua barabara. Kwa hiyo hayo ndiyo nimesema nimfafanulie Mheshimiwa Waziri ili angalau aone uchungu tunaopata sisi Wanatabora na yeye aupate.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Tumbaku nilifikiri atakitaja leo humu, hakuna chochote alichokitaja ambacho nilimwomba mwaka 2016/2017, hakuna alichoweka humu. Leo ningepata majibu wala nisingechangia, sana sana ningefanya kumpongeza, anafanya kazi nzuri sana lakini si maeneo ya Tabora na Kigoma, majirani zangu wananiambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine, hili ni la jumla, tuna tatizo sasa hivi la wawekezaji wa viwanda kuhusu sukari. Tuna tatizo la sukari tusijibu tu bla bla hapa; sukari sasa hivi ni tatizo kwa nchi nzima na kuna wenye viwanda ambao si waadilifu na si wazalendo. Sukari imekamatwa Kagera ambako anatoka Mheshimiwa Waziri, hivi imekamatwaje na imeuzwa na nani, ambayo ilikuwa inavuka wanaipaki kupeleka Kenya. Sasa hebu aniambie Tanzania tukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, suala la sukari ajiulize kwa nini wanafanya vitu vya namna hii hususan unapoanza mwezi wa ramadhani? Maana ni keshokutwa tu, wanamchafua Rais wangu, hiyo ni hujuma ili wamsaliti lakini hawezi kusalitika, tunamuunga mkono hata yawe mapambano lakini sukari kwa nchi hii itapatikana na Mheshimiwa Waziri Mkuu alishasema. Kwa hiyo nimwombe afuatilie suala hili, nendeni kwenye *godown* hawa watu mnawaogopa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nimwombe, mikataba ya ubinafsishaji wale waliobinafsishiwa, waliopewa wale wa Kiwanda cha Nyuzi cha Manonga anipe majibu. Kwa nchi nzima viwanda vyote vile vije hapa, kwani kuna

tatizo gani kuwanyang'anya? Mheshimiwa Lukuvi hapa ananyang'anya hati na kadhalika kwa nini Wizara ya Viwanda isifanye hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe, nimesema kwa hisia na uchungu kwamba nchi hii tusipopambana, nchi hii tusipoielekeza watamlaumu Waziri wa viwanda lakini utekelezaji wake utakuwa haupo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hawa watu awanyanga'anye hizo nanii zao kwani lazima?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Nchemba muda wako umemalizika, ahsante sana.

**MHE. MWANNE I. NCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Nape Nnauye atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudi ambazo zimeanza kuonekana za kufufua viwanda na hasa kwa kweli viwanda vya korosho. Jimboni kwangu kuna kiwanda wamefufua, lakini na maeneo mengine tumeanza kuona juhudi hizi zinakwenda na nadhani hatua walizochukua zinakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba naunga mkono, vile viwanda vilivyobinafsishwa na havikufanya vizuri, kwa sababu mikataba ipo na wengi hawakufanya sawasawa na mikataba na ukisoma ripoti zote

zinaonyesha kwamba, wengi walipobinafsishiwa viwanda hivyo, wakavitumia wakaenda wakakopa na pesa zile zikaenda maeneo mengine. Mheshimiwa Mwijage aache upole, achukue hatua tuwadhibiti watu waliofanya kinyume na tulichokubaliana. Pamoja na kazi nzuri ambayo mmeanza kufanya, ningeshauri maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza Mheshimiwa Mwijage tuna shida kubwa ya tafsiri tuliyonayo juu ya nini tunakiita ni kiwanda. Ukiangalia maeneo mengi ukitaja idadi ya viwanda ambavyo vimeanza kujengwa watu wanaangaliana usoni, kwa nini? Kwa sababu tunalo tatizo la tafsiri ya pamoja ya kukubaliana hivi kiwanda hasa ni nini? Ni lile dubwashika kubwa au hata nikiwa na karanda kangu bado tunakaita viwanda, ndiyo maana Mheshimiwa Waziri akitoa idadi ya viwanda hapa aasema elfu tano, elfu kumi, elfu ngapi, wakati mwingine watu wanaangaliana wanapata mashaka na tunachokisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Mwijage kwenye hitimisho lake hebu tuzungumze tunaposema viwanda tunamaanisha nini, tukikubaliana hapa, tutakwenda vizuri. Niliwahi kukutana na wanahabari nikiwahamasisha wazungumze juu ya viwanda. Wakaniambia lakini Nape hata ninyi wenyewe hamna tafsiri moja, sasa tukizungumza tunazungumza nini hasa. Nadhani hili la kwanza kubwa litatuweka mahali pazuri, tunaposema kiwanda tunamaanisha nini, tukikubaliana hapa sasa tutasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Mwijage viwanda ni ukombozi na hasa kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa sababu bado maskini sana. Ukombozi wowote una vita na una vita hasa kwa wale ambao wanafaidika na mfumo wa kutokuwepo kwa viwanda. Hapa nitatoa mfano, tumekuwa tukizungumza juu ya ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Lindi, pale Kilwa. Taarifa tulizonazo, Mataifa makubwa yenye *interest* na mbolea katika nchi hii yanapambana kuhakikisha kiwanda hicho hakijengwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo ambalo hatutakubaliana nalo Mheshimiwa Mwijage ni pamoja na kuruhusu vita hii iendelee kutuumiza; Wanakusini wanapigana kwa maslahi yao na kama Serikali mtayumba kwenye hili, Wanakusini hatutakubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishalizungumza, mlishakubaliana, mwekezaji alishapatikana na utaratibu uko wazi, sasa vita hii ya wakubwa isituumize, wakapigania nje ya Lindi lakini tunakitaka kiwanda cha mbolea Lindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine, moja ya jambo linalopigiwa kelele na wawekezaji ni vitu vinavyoitwa vivutio (*incentives*), vinavyowavutia kuja kuwekeza kwenye nchi yetu. Mjadala katika nini vitumike kama vivutio vya kuwekeza inachukua muda mrefu sana na hata katika *ranking* za urahisi wa uwekezaji katika nchi yetu, katika jambo linaloturudisha nyuma ni pamoja na mjadala juu ya vivutio.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua mjadala uliokuwepo juu ya bomba la mafuta, mjadala juu ya viwanda vya uunganishaji wa vipuri mbalimbali katika nchi yetu, suala la vivutio nadhani ni tatizo kubwa. Sasa umefika wakati Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Awamu ya Tano fikirieni kutengeneza vivutio ambavyo tunakubaliana navyo, kwamba wanaokwenda kwenye mjadala waende wakiwa wanajua, huu ndio msimamo wa nchi katika kutoa vivutio katika uwekezaji ili tupunguze muda wa mjadala; kwa sababu wapo wawekezaji wengi wana pesa zao; anakuja akiona mjadala unachukua muda mrefu anaondoka, kwa sababu hatujaweka vipaumbele katika vivutio tunavyotaka kuviweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali; umefika wakati kaeni kubalianeni; hivi ndivyo vivutio tutakavyovitoa, vikitokea vya ziada hivyo ndivyo viingie kwenye mjadala, vinginevyo tutashindwa kushindana. Kama mtu anakwenda Rwanda anatomia masaa machache anapata mkataba yuko tayari kuwekeza, halafu akija kwetu

anachukua miaka miwili au mitatu, watatukimbia; na wakitukimbia maana yake nchi kinachozungumzwa hakitatekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mchango wa sekta binafsi na kuna watu wamezungumza hapa. Nataka kushauri Serikali yangu, hebu tusiingie kwenye mtego wa kuiingiza Serikali kwenye uwekezaji wa viwanda, tuwaachie sekta binafsi. Kazi yetu iwe ni kuwatengenezea mazingira mazuri ya kuwekeza. Dunia ya leo tukitaka kwenda wenyewe tutakwama, lakini tukiwatengenezea mazingira mazuri inawezekana, mchango wao ni mkubwa, tutengeneze mazingira ikiwemo vivutio, lakini pia waone kwamba hili ni eneo sahihi la kuwekeza. Mtaji wa mwanzo wa amani na utulivu tunao, lakini haya maeneo mengine lazima tuyawekee kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni suala kubwa sana la kuhusisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu, ni suala la msingi sana. Tusipolihusisha tutawaacha watu wetu nyuma na haya maendeleo hayatakuwa na maana kabisa, kwa hiyo, ni lazima tuhusishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo moja la kuhusisha ambalo nadhani tushauriane, Serikali, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Elimu pengine na TAMISEMI kupitia VETA, tuangalie tunawatengeneza akina nani kwenda kufanya kazi kwenye hivi viwanda? Vinginevyo tutajikuta tunaanzisha viwanda na mwisho wa siku wanaokuja kufanya kazi si vijana wetu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna mtaala wa VETA ambapo nchi nzima mtaala ni huo mmoja, lakini mazingira yanatofautiana. Ukienda Lindi na Mtwara mahitaji yetu ni kuwatengeneza vijana wetu wakafanye kazi kwenye mafuta na gesi, lakini mtaala wa kwao ni sawasawa na mtaala wa Bukoba, mazingira ni tofauti. Wa Bukoba wafundishwe kuchonga mtumbwi na kuvua samaki, lakini wa Mtwara na Lindi wafundishwe namna atakavyofanya kazi kwenye



mafuta na gesi. Sasa nadhani tufikirie namna ya kutengeneza mtaala kwa mujibu wa mahitaji ya ukanda na shughuli za kiuchumi zilizoko kwenye eneo husika badala ya kuendelea na utaratibu wa sasa hivi wa mtaala mmoja kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tukienda hivi maendeleo ya viwanda pamoja na kuongeza thamani ya mazao yetu, lakini pia utakidhi haja ya wale wanaokwenda kufanya kazi. Ukienda leo pale Mtwara kwenye utafiti wa gesi na mafuta pana shida, mpaka walinzi wanaajiriwa kutoka Kenya, wanaajiriwa kutoka Uganda. Hivi hatuna vijana wetu pale tukawafundisha Kiingereza kidogo na kuwafundisha *discipline* ya kufanya kazi pale?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani VETA inaweza kuboreshwa zaidi kutoka hapa ilipo ikawaandaa vijana wetu wakakidhi haja ya soko la huko tunakokwenda. Tukifanya hivyo tunaambatanisha maendeleo ya viwanda pamoja na maendeleo ya wananchi wetu na tukifanya hivyo naamini hatutakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua iko nia njema ya Rais wangu, najua iko nia njema ya Serikali ya Awamu ya Tano, lakini hebu tuhusianishe basi haya tunayoyafanya yapate tafsiri sahihi, tuweke vigezo sahihi, vile vile tuyahusianishe na maendeleo ya watu wetu. Tukifanya hivi mambo yetu yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yake na kwa kweli mambo yake nadhani yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi, leo ntaongelea kodi. Mheshimiwa Mwijage anafanya kazi nzuri sana kutafuta

wawekezaji, lakini wawekezaji ili waweze kuja Tanzania ni lazima tuangalie mfumo wetu wa kodi. Mfumo wetu wa kodi si rafiki kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijenga kiwanda ukataka wakati unajenga uanze kupata kodi haiwezekani. Duniani kote wameondoka kutoza kodi kwenye *production*, unatoza kodi kwa yale yatakayotokea baada ya ku-*produce*. Sasa sisi tunataka mtu anafika siku ya kwanza tu na kodi ianze, matokeo yake Tanzania hatutabiliki katika mazingira ya uwekezaji. Mabadiliko ya Tanzania yanakuja kila mwaka; mwaka huu tutasema tunaondoa vivutio, mwaka kesho vinarudi, mwaka kesho kutwa vinaondoka, hakuna ambaye anaweza akaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawapa mfano wa vitu vichache. Mwaka 2009 tuliondoa vivutio kwenye kodi ya *deemed capital goods*, uwekezaji ukashuka. Mwaka uliofuata tukarudisha, uwekezaji ukapanda. Hata hivyo, sisi tuna *TIC* ambayo inatoa *certificate*, lakini *TIC* inatoa *certificate* ambayo Waziri wa Fedha haitambui. Sasa, tuko kwenye Serikali moja, niwaombe watu wa Serikali; Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Waziri wa Fedha tukubaliane vivutio gani vinawekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia hapa Mzee Deo Sanga anaongelea habari ya Mchuchuma na Liganga, Mzee Sanga tatizo ni vivutio, utapiga kelele, lakini haiwezekani; kwa sababu *TIC* wamewapa vivutio, Waziri wa Fedha hajakubali, sasa tunafanyaje? Kwa hiyo, niwaombe na ningekuwa na muda ningesema hata vifungu ambavyo vinakubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *VAT*; Sheria yetu ya *VAT* haitambui suala la bidhaa za mtaji na *capital goods* na *deemed capital goods* hawatambui. Juzi walikuja wale ambao wanatengeneza magari Kenya, *Volkswagen* walitaka kuja Tanzania, walikutana na Mheshimiwa Mwijage

mmekubaliana weee, walipofika sasa kwenye vivutio, Waziri wa fedha akaweka nanga, wakaondoka. Mwisho wake sasa tunamlaumu nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema kwamba naamini nia ya kuleta uwekezaji ni njema, nia ya kukuza viwanda ni njema, lakini nia njema hii tuipeleke kwenye sheria ili hadi kuanzia chini Mkuu wa Wilaya mpaka mtu wa juu aongee kivutio cha namna moja. Unapooengelea Tanzania tukisema vivutio, *across the country* tunaongea jambo moja. Leo kuna vivutio vya Mwijage, kuna vivutio vya *TIC* na kuna vitutio vya Waziri wa fedha inawezekanaje kwenye nchi moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana sana na matokeo yake sasa ya kutokuwa na kutabirika; moja, wawekezaji mahiri hawawezi kuja Tanzania; mbili, wawekezaji walioko kwenye sekta ambazo bidhaa zake hazitambuliwi na *VAT* hawawezi kuja Tanzania; na tatu, tumeumiza usafirishaji na *tourism in Tanzania*.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafirishaji mwaka 2015 wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne tulikuwa na malori 23,000 yanafanya kazi kwenda kupeleka mizigo, leo yamebaki malori 11,000 kwa sababu gani kwa sababu ya *VAT* kwenye *auxiliary* basi, kwa sababu gani kwa sababu ya *single custom* ya Congo, sasa tunaumumiza nani? Naomba Serikali mkae, sheria zetu tuzioanisha ili ziweze kufanya kazi ili tuweze kwenda mbali katika kujenga uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mifano michache; nimelisema hili la Mchuchuma nadhani wenzangu wamelisema. Ethiopia, Dangote alikwenda Ethiopia akapewa vivutio, akapewa na bei ndogo sana ya umeme watu wakashangaa akazalisha *cement*, bei ya mfuko wa *cement* ikashuka kwa 60%. Watakaofaidi ni watu gani? Ni wa Ethiopia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakosa kodi hapa unapata kule mbele, *production* ikiwa kubwa watu watajenga nyumba sana watu watanunua *cement*, tutapata tu kule mbele, *unless* mtuambie hii shule ya uchumi mliyosoma nyie ni ipi ambayo wengine hatuijui? Mtuambie leo. Ningetamani Mheshimiwa Waziri wa Fedha awepo hapa leo, asimame atuambie shule yake ya uchumi ambayo wengine wote hatuijui ni ipi? Maana haiwezekani tunaenda huku tunarudi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la ngozi na Mheshimiwa Mwijage amekwenda Ethiopia, Ethiopia leo ni *big exporter* wa *product* za ngozi kwa sababu gani? Nendeni m-*google* wanatoa *incentive*, wanatoa *tax holiday* kwa asilimia nyingi sana, lakini matokeo yake *export* imeongezeka, dola inakuja nyingi *in the country* wana-*manage their economy*. Sisi tunataka tupate kodi leo kabla haiwezekani haiko dunia unayoweza ukapata kodi kabla hujazalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini juzi kwenye suala la wafanyabiashara Mheshimiwa Rais amesema maneno yafuatayo:-

Rais amewaambia Watanzania mkishindwa kujenga viwanda, mkishindwa kufanya uwekezaji Tanzania wakati wangu, hamtoweza wakati mwingine wowote. Sasa maneno makubwa haya ya Mheshimiwa Rais yawekeni kwenye sheria, kayawekeni kwenye utekelezaji, maana tutaonekana huku tunaongea maneno mazuri, ukija na fedha zako unanza kupigwa maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna ardhi, Tanzania tuko *well located as a country*, tuna madini, tuna *gas*, tuna misitu, tuna *tourism*, kutokwenda kwa kasi hatuna maelezo na hatuna maelezo kwa sababu moja tu, kwa sababu hatuna vivutio, hatuna *strategy*. Ukisoma mkakati wetu mzuri sana na sisi Mungu alitujali, ukisoma *development plan* ya miaka mitano, ya mwaka mmoja *superb*, ukisoma ripoti hapa ya Mwijage *superb* lakini nenda kwenye utekelezaji hapo ndio penye mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Waziri akae na wenzake Serikalini waviangalie hivi vivutio, waangalie haya mazingira ya uwekezaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba muda wako umekwisha malizia sentensi.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningesema habari ya *NEMC, NEMC* nayo ni kikwazo kwenye uwekezaji nchini *NEMC*, inakwaza nchi hii...

**NAIBU SPIKA:** Haya. Ahsante sana, Mheshimiwa Peter Serukamba muda umekwisha sasa.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha subuhi. Nitasoma kwenu majina machache tutakayoanza nayo mchana halafu nina tangazo moja kutoka kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, hawa ni baadhi ya wachangiaji wetu wa mchana.

Kuna tangazo hapa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Shirika lake ama Shirika lililo chini ya Wizara yake la *TEMDO* limeleta viwanda kwa ajili ya maonesho. Jamani hili ni tangazo tafsiri atatoa kesho wakati akimalizia, lakini kwa leo ameleta viwanda kwa ajili ya maonesho, eneo ni karibu na *canteen*. Aina ya hivyo viwanda alivyoleta ni nne. Aina ya kwanza, ni *sunflower seed processing*; ya pili, *hospital solid waste incinerators*; ya tatu ni *cooling cabinets mortuary*; na ya nne

ni *biomass brickating machine*; anawaomba tutembelee hivi viwanda ambavyo viko karibu na eneo la canteen.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji. Kuna majina niliyataja asubuhi kwamba yangeanza sasa hivi. Tutaanza na Mheshimiwa Zacharia Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoongoza nchi yetu na kwa jinsi anavyosimamia utendaji wa Serikali tangu aingie madarakani. Ni kiongozi wa mfano na katika mifano yake halisia ameweza kuipeleka nchi na kuweza kuongoza na kutoa dira sahihi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kufika wakati huu wa sasa sisi Wabunge wote. Pia nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote na mimi mwenyewe, wana-Mbulu na Watanzania kwa ujumla kutoa pole nyingi kwa ndugu zetu, marafiki na jamaa wote waliopatwa na hali mbalimbali ya kupoteza ndugu zao katika nyakati tofauti kwa matukio ambayo hatujaweza kuyazoea. Mwenyezi Mungu aendelee kuibariki nchi yetu tuweze kupata hatua nyingine nzuri kwa baraka zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Baraza la Mawaziri,

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe na watendaji wote wa Serikali kwa jinsi ambavyo wanajitahidi kutekeleza majukumu yao na kuwapa Watanzania fursa sahihi na nia njema ya kuweza kufanikisha malengo mahsusi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa mchango mchache ambao natarajia kuzungumza katika Bunge hili kwa nafasi hii ya viwanda. Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kuiaa Serikali; uanzishwaji huu wa viwanda tunaouanzisha hivi sasa ningependa kushauri Serikali ijikite katika hali halisi ya kila Kanda kuwa na kiwanda ili maendeleo yetu yaweze kuendana na sehemu mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna baadhi ya maeneo yatakuwa yamekosa fursa ya kupata viwanda kutokana na hali halisi ya jiografia, rasilimali zilizoko na fursa nyingine za hali ya kupatikana kwa malighafi. Niseme tu kwamba kwa namna yoyote ile tufanye pia utafiti katika nchi yetu ili pia tuweze kuona ni maeneo gani kwa nchi yetu yanaweza kuwa na malighafi ili yale maeneo ambayo hayatapata uwekezaji wa viwanda na fursa za kujengewa viwanda basi waweze kuzalisha na kupata fursa ya kuwa na malighafi ambayo itaendeleza nchi yetu katika hali hii ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo yetu iboreshwe katika uzalishaji na uingizaji wa bidhaa. Nizungumze tu kwamba tukio lile la kuondolewa kwa simu feki katika nchi yetu liliumiza Watanzania wote, Watanzania walikuwa wanahangaika, wakapata simu, wakawa wanamiliki lakini mwishoni tukajikuta simu nyingi zinazomilikiwa hazitaweza kukidhi haja. Pamoja na pombe zingine zilizofutwa katika ile hali ya kawaida ambayo ilionekana si nzuri kwa matumizi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ambayo tusipoidhibiti katika uanzishwaji wa viwanda hivi na tusipoboresha mfumo wa Mamlaka ya Chakula na Dawa nchini, tutakuta tumeanzisha viwanda vingi lakini bidhaa ambayo

inazalishwa itakuwa ni bidhaa ambayo pia Watanzania watakuwa wametumia katika hali ambayo si sahihi. Hivi sasa si kweli, hata tuliotumia simu na wale Watanzania wote na waliotumia viroba na pombe mbalimbali na madawa lazima wamedhurika. Si rahisi kwa mara moja tukatambua madhara yake ni kwa kiasi gani, lakini ni vizuri tutakatazama upya mifumo yetu, tukafanya vizuri na tukaweza kuona viwanda vyetu vya ndani vinahimili mashindano au ushindani wa bidhaa kutokana na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi bila viwanda haitawezekana, lakini kuwa na viwanda bila kuwa na watu wenye taaluma ni kazi moja ngumu pia. Nitoe rai kwa Serikali, tuweze kupitia vyo vyetu vya VETA, vyo vya ufundi stadi kuandaa watumishi wa kada za kati na kada za chini ili waweze kupata nafasi za ajira na waweze kunufaika kama watumishi katika viwanda ambavyo tunatarajia kuanzisha. Bila kuwa na Watanzania hawa wenye taaluma ya chini na ya kati, basi viwanda tutakavyoanzisha vitakuwa vinamilikiwa na watu wa nje na pia tutakuwa tunatafuta watumishi wa kada za chini kutoka nchi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niweze kusema tu kwamba, kwa ujumla usimamizi wa kodi haujakaa vizuri kwenye viwanda ingawa suala hili ni la Wizara ya Fedha. Viwanda vyetu vingeweza kuzalisha bidhaa nzuri zenye kuhimili ushindani zikaingia kwenye mfumo na mfumo wa ukusanyaji wa kodi ukatazamwa, basi Tanzania ingeweza kuwa nchi ya mfano katika kukusanya na nchi ya mfano katika kuelekea uchumi kupitia viwanda ambavyo tutaanzisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine utafiti ufanyike ili tujue ni maeneo gani yanakuwa na malighafi na maeneo gani yanaweza kuwa na fursa za uanzishwaji wa viwanda kutokana na rasilimali zitakazokuwepo katika maeneo hayo, pia katika yale maeneo ambayo kwa namna moja au nyingine tunaweza tukawa tumepata mwingiliano wa kiuchumi kwa maana ya yule anayezalisha, yule mwenye malighafi na yule mwenye kutokewa na fursa hii ya kupatikana kwa kiwanda. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kusema kwamba, Watanzania si kwamba hawapendi mali inayozalishwa Tanzania, ni pale baada ya mtumizi anapoonza mali au bidhaa iliyotoka nje ina thamani kubwa kuliko ile iliyoko nchini. Kwa vyovyote, lazima yule ambaye ananunua au mlaji au mtumiaji atakuwa na taswira nyingine tofauti ya kuona kwamba pengine ile ya nje ni bora zaidi kumbe hata sisi tuna bidhaa bora na nzuri zaidi, tatizo ni pale tu tunaposhindwa kudhibiti ubora unaotakiwa katika hali ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutazame pia wakati huu tunafufua viwanda, je, ni kwa kiasi gani tumefanya utafiti kwa nini viwanda hivi awali vilipotea au vilishindikana kuendeshwa au vilipata kukwama na hatimaye kushindwa kujiendesha? Kwa vyovyote vile bila utafiti, bila mapitio tunaweza tukaanzisha na mbele ya safari kukaja tena wimbi lingine la viwanda hivi kupotea na hatimaye nchi yetu kupiga *mark time* au kutokuwa na hatua ambayo si nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine kwa namna moja au nyingine naweza nikazungumza jambo lisiwafurahishe Watanzania. Tukiwa watu wa kuamini mambo mepesi, yasiyo na tija, ambayo hatuyafanyii utafiti, mambo ambayo rasilimali wataalam hawatumiki kama sehemu ya Watanzania waliopata fursa ya kupata taaluma hiyo, basi kwa vyovyote vile si rahisi tukawa na viwanda ambavyo ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza kwanza Mheshimiwa Rais na vilevile kuwapongeza Wizara kwa jinsi wanavyohangaika. Pia tunaomba sekta hii muhimu sana itakayoajiri Watanzania wengi, ipate fedha katika Bajeti ya Mwaka huu kwa asilimia 100 ili fursa hii ya viwanda kupanda na kupata nafasi nzuri, iweze kuwafikia Watanzania na Watanzania waweze kunufaika na fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapitisha bajeti, mwakani tunatarajia kuona kwamba angalau kile tulichopitisha kuna asilimia pengine 100 au 80 kwenda mbele ipelekwe kwenye malengo mahsusi yaliyoanzishwa au yanayoanzisha viwanda ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini nikitegemea yale yote yaliyokusudiwa yanapata fursa ya kutengewa fedha na kufanikiwa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga ajjandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Mwijage ni kaka yangu na mara nyingi tumekuwa tukiwasiliana na leo nataka nimkumbushe tu mambo machache ambayo tungependa Mheshimiwa Rais lakini pamoja na Taifa liyafahamu. Kwanza kabisa nimfahamishe kwamba mwaka wa jana wakati fulani Mheshimiwa Waitara alichangia akimtaka CAG kwenda kufanya ukaguzi maalum Chuo cha Elimu ya Biashara, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, CAG amekwenda kukagua amekiri lakini bahati mbaya sana ukaguzi huu umefanyika Chuo cha Dodoma pamoja na Chuo cha Mwanza, Dar es Salaam ambako ndiko kwenye upotevu wa zaidi wa Sh.400,000,000 ukaguzi haujafanyika. Taarifa za CAG ni hizi hapa, naomba apatiwe *copy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri mambo machache. Tunatamani sana kuwa na viwanda Tanzania, lakini Sera yetu bado haijabadilika. Ukiangalia kimtazamo, wawekezaji wengi wanashindwa kuja Tanzania kwa sababu ya kodi. Kodi nyingi zinatozwa kabla mtu hajawekeza hata kitu kimoja; atakutana na watu wa ardhi, watataka pesa kutoka kwake,

atakutana na watu wa *NEMC*, atataka pesa kutoka kwake. Sasa tunawavutiaje wawekezaji kama vyanzo au vivutio vya uwekezaji ni vichache au vilivyokuwa na misongo misongo? Kwa hiyo, tuangalie namna bora ya kufanya, *NEMC* pamoja na watu wa ardhi waone namna ya kutoza kodi ikiwezekana baada ya mtu kuwekeza katika mazingira fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nataka nimkumbushe lakini pia tumsaidie Mheshimiwa Waziri kumkumbusha Mheshimiwa Rais; alipokuja Mtwara wakati anaomba kura, alisema atahakikisha viwanda vya korosho vinafanya kazi. Sasa hivi tuna mwaka mmoja takriban na nusu viwanda vile havijaanza kufanya kazi na hatujaona juhudi zozote zinafanyika angalau kuwatafuta wale watu ambao walipewa viwanda na Serikali ili waviendelee. Vile viwanda sasa vimegeuka kuwa maghala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tafiti mbalimbali zimefanyika ambazo zinaonesha kabisa kwa kutumia tu korosho iliyoko Mtwara sisi tunaweza tusiwe watu tunaohitaji viwanda vingine vyovyote. Korosho yetu ina uwezo wa kututoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hii *paper* hapa mbele yangu inasema; *justification for cashew value addition in Tanzania*. Hii karatasi nitaiteta kwako lakini ina mambo mengi sana humu ndani ikiwa ni pamoja na kuonesha faida mbalimbali zinazoweza kupatikana baada ya kuwa na kiwanda cha korosho; kwa sababu unapozalisha korosho zile *cashewnut kernels*, zile korosho za ndani ni asilimia 25 ndiyo ambayo inatumika na inasafirishwa kwenda nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule inakokwenda wanapata maganda ya korosho ambayo ni asilimia 50 – 60 na saa zingine inafikia 70 – 80 ya maganda ya korosho. Sasa faida za maganda ya korosho. Sasa, faida ya kwanza kabisa maganda yanaweza yakatumika kutengeneza *break lining* kwa ajili ya magari. Maganda ya korosho yanaweza yakatumika kutengeneza vilainishi vinavyotumika kwenye nchi zenye joto kali, maganda ya korosho yanaweza

yakatumika kutengeneza vipodozi (*cosmetics*). Nadhani ukiangalia watu wa Mtwara wengi utaona wamejichora alama fulani za korosho, maana yake kwamba inaweza kubadilisha ngozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tukiangalia maganda haya haya ya korosho (sina hakika sana) lakini ilikuwa inasadikika Mheshimiwa Rais alifanya *research* yake kwa kutumia maganda ya korosho akisema kwamba maganda ya korosho ni dawa nzuri sana ya kuuu vidudu kuliko hizi dawa mnazozingiza kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia maganda ya korosho yanaweza kutengeneza *ceiling board*. Sasa niombe Wizara wafufue viwanda vilivyoko Mtwara; hii sehemu waliyoitaja ndiyo inayoingiza pesa nyingi kwenye korosho kuliko hizi korosho chache wanazozitegemea ambazo ni asilimia 20 – 25. Kwa hiyo, waone namna watakavyofanya kuhakikisha viwanda vile vya korosho Mtwara vinafufuliwa kwa ajili ya kuongezea pesa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako tu mwaka huu Tanzania au korosho ya Tanzania ndiyo limekuwa zao la kwanza lililoingizia mapato makubwa Taifa hili. Sasa tuone hicho tunachokipata ni asilimia 25 tu ya hali halisi. Tulete viwanda, tuwatafute wawekezaji waje kuwekeza ili waweze kuzalisha tupate hivi vitu vingine. Hizo *break lining* zinazotoka India, China nyingine zinatengenezwa kwa kutumia maganda ya korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tanzania miaka ya 60 na 70 tulikuwa na viwanda vya kutosha tu maeneo ya Mtwara, Lindi, Ruvuma pamoja na Pwani, bahati mbaya vile viwanda vililuzwa na watu wanavifanya maghala. Sasa tunaamua kuondoa korosho zetu tunaziua tunapeleka nchi za nje. Kule wenzetu wanakwenda kutengeneza hivi vitu ambavyo wanarudisha kwetu kuiuza. Faida ya korosho si kwenye ubanguaji ni mazao yanayotokana na ile korosho baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwongezee Mheshimiwa Waziri kitu kingine ambacho Watanzania wengi hawakifahamu na Mheshimiwa Waziri naomba achukue hili *very serious*. Kuna pombe inazalishwa kutokana na mazao ya korosho (bibo), ile pombe jina lake halisi inaitwa *nipa*. Watanzania walio wengi wanatumia hii pombe, inafahamika kwa majina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Sheria hii inaitwa *Intoxication Liquors Act 1968*, ilitambua pombe mbalimbali za kienyeji katika maeneo yao. Sasa sisi kule kwetu tunatengeneza pombe inaitwa *nipa* kama nilivyoeleza, lakini inatambulika kama pombe ya Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tafsiri yake inasema hivi – Moshi *means the distilled liquor commonly known as Moshi*, Kitaifa, lakini pia watu wa Mtwara pamoja na Lindi tunaita *nipa or piwa* – watu wa Moshi. Sasa nimwombe; hii haijawahi kuharamishwa hata siku moja na hakuna Sheria yoyote iliyobadilishwa na kuharamisha hii pombe ya *nipa* Tanzania. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea hivyo kwa sababu kuna faida kubwa inayopatikana kwenye mabibo. Kwa mfano tu mwaka huu mabibo zaidi ya tani milioni moja na laki tatu yamezalishwa, lakini yametumika kiasi kidogo sana, watu wanakula wanatupa. Sasa tukiamua kuchukua hatua tukaenda mbele, tunaweza kupata *wine*, tunaweza kupata pale ndani hizo *whisky* na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, hii *nipa* ikiwa *distilled*, kwa sababu jukumu la Mheshimiwa Waziri kadri ya Sheria iliyoko hapa mbele ni wewe unatakiwa kutoa leseni kwa wapika *nipa*, si wapika gongo, wanaopika *nipa* inayotokana na mazao ya shambani; kama ambavyo iko kwa watu wanaopika *nipa* hiyo hiyo jina lingine tuseme Moshi wanaita *piwa* wanawauzia kiwanda cha *K-Vant* wanatoa pale ndani *spirit*. Ile *spirit* inatumika hospitalini kwa shughuli mbalimbali. Kwa hiyo inakuwa *distilled* vizuri, inakwenda kutumika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kule kwetu tunatambua, watu wengi wanafahamu, sisi tunauza ile nipa kwa chupa moja ya fanta Sh.500, ile chupa ya bia Sh.1,000. Wakiamua sasa kuigeuza ikawa zao la biashara wananchi wakapewa leseni, wataipika vizuri si mafichoni kule ambako inatoka ikiwa chafu kwa sababu hawatunii vifaa vizuri. Itakapokuja hapa mbele itapata bei nzuri, hawatakunywa wale watu, hawataweza kununua, lakini itakwenda kutumika kuongeza na kukuza kipato cha wakulima. Pia wakati huo huo itasaidia kwenye hospitali zetu, sisi tunafanya *importation* ya *spirit* kutoka maeneo mbalimbali, *spirit* hii inapatikana kwenye *nipa*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hizi hapa. Mara ya kwanza kabisa lilijadiliwa jambo hilo la ilisainiwa hii hapa na marehemu Mheshimiwa Mzee Kawawa. Mara ya pili imejadiliwa tena hii limesaini na wakati huo Katibu wa hili Bunge ambaye alikuwa Mzee Msekwa. Baadaye Mheshimiwa hayati Nyerere Baba wa Taifa naye alisaini, hawakuharamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilipoanza kuharamishwa hii ni pale ambapo mlianza kuiita, kuna jina waliita wataalam, unajua wanasema ukitaka kumpiga mbwa, mpe jina baya. Wakaanza kuita inaitwa *illegal illicit alcohol*, hii sasa ndiyo gongo. Hata hivyo, sisi kwetu hatutengenezi gongo, tunatengeneza *nipa pure*, inatokana na mazao ya shambani. Tuwaruhusu wale watu wajiongezee kipato, kwa sababu ni kweli inafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwijage akija kule nyumbani hata mimi nitamtafutia kichupa kidogo cha *nipa* aonje ladha yake ambayo inafanana na *whisky*, hizi tunazo *import* kutoka nchi mbalimbali, tunazileta Tanzania tunazitoza kodi wakati tunapoteza mapato kule kwa wakulima, lakini pia pamoja na kuwaongezea kipato wakulima wetu. Kwa hiyo, kuna hii *research* nimeweka hapa kwako. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo hilo bibo ni zuri zaidi kuliko ilivyokuwa pamoja na hizi *citrus fruits*, ina *vitamin c*

mara tano zaidi. Sasa kwa nini tusiache wale wananchi wakajipatia kipato kutokana na hivi vitu? Sheria iko wazi, ikiwezekana Mheshimiwa akija hapa awaombe radhi Watanzania waliofungwa kwa kutumia mazao yao ya shambani kutengeneza pombe ambayo inaitwa haramu wakati pombe hiyo haijawahi kuharamishwa, ni sehemu ya kuongezea kipato wakulima. Kwa hiyo, naona unamwonesha Mheshimiwa Mwigulu hapo awataarifu polisi wake, lakini na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda ana jukumu la kutoa leseni kwa watengenezaji wadogo wadogo ili waweze kufanya vizuri, wakauzie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti umekamilika Chuo cha Kilimo Naliendele, wanasubiri tu sasa kununua hivi vitu kutoka kwa wakulima wa korosho. Bei ya korosho inaweza ikashuka muda wowote na faida ya korosho inapatikana kwenye mazao mbadala. Mwaka huu tumefanikiwa kuuza mpaka Sh.4,000 lakini niseme tukiamua sasa kuwaachia wakulima wakawa huru wakafanya jambo hili kwa Mheshimiwa Waziri kuwapa leseni, kilo moja ya korosho na mazao yake wanaweza kupata mpaka Sh.6,000 au 7,000 na haitashuka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu hasa ni kuonesha *economic importance of cashewnuts* na *chain* nzima ya korosho. Naomba Mheshimiwa Waziri alichukulie hili *very serious* na nitakwenda ofisini tuweze kulijadili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga hoja ya Upinzani. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe, hapa kuna hoja moja tu, kwa hiyo ahsante kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (Kicheko/Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, ametaja vipodozi hapa, nikawaza Mheshimiwa Waziri wa Afya itabidi atuelekeze vizuri maana usije ukatuweka matatani. (Makofi)

Mheshimiwa Silvestry Koka, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajandae.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa utendaji usiochelewa. Nasema hivyo kwa sababu tulisimama hapa na tukasema tunahitaji Rais na Serikali ambayo inafanya maamuzi hata kama ndani yake kutakuwa na makosa madogo madogo, naye anafanya hivyo na nina imani tutakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri aikumbuke Kibaha. Tunalo eneo lapata hekta 1,500 lililotengwa kwa ajili ya viwanda na yeye kama alivyo imara kutoa viwanda basi namuomba atoe viwanda hadi eneo hili liweze kukamilika na namuunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Tanzania ya Viwanda ni jambo linalowezekana na nia nzuri ya Serikali iliyonayo inawezekana endapo kwa uhakika tutakwenda kuondoa kero na matatizo mbalimbali ambayo yanaturudisha nyuma kwenda kufanikiwa katika azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na azma hii tunaiomba Serikali iendelee kutengeneza mazingira bora na rafiki zaidi na wawekezaji na wafanyabiashara. Tunaiomba Serikali iondoe kero mbalimbali ikiwa ni pamoja na tozo za aina moja ambazo sasa zinatozwa na taasisi ambazo ni za usimamizi (*Regulatory Authority*) utakuta taasisi mbili au tatu zinatoa tozo ambazo zinafanana kwa wafanyabiashara. Hili ni tatizo na ni kikwazo katika uanzishwaji wa viwanda na uendeshaji wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kero nyingine kubwa ambapo viwanda vyetu vya ndani vinapozalisha vinashindwa hasa kushindana na mali zinazotoka nje ya nchi. Hii ni kwa sababu baadhi ya malighafi na utaratibu mzima



wa mchakato wa uzalishaji katika viwanda vya ndani vinatozwa kodi, ikiwa ni pamoja na kodi ya VAT. Hii inafanya mali zinazozalishwa na viwanda vya ndani zishindwe kushindana na mali kama hizo zinazotoka nje kwa sababu wao katika uzalishaji hawalipi kodi hizo. Hili ni tatizo kubwa na ningepomba sasa Serikali kupitia Wizara yake ilitazame na kulifanyia kazi ili tuweze kushamirisha nia na madhumuni ya viwanda Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu ni wajibu wa Serikali kulea wafanyabiashara na viwanda, kwa sababu kimsingi Serikali inamiliki asilimia 30 ya makampuni na biashara zote zilizopo ndani ya nchi. Ndiyo maana siku ya mwisho biashara zote zinawajibika kulipa asilimia 30 ya faida inayopatikana na shughuli nzima ya uzalishaji au ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali kulea, kutunza na kusaidia ili siku ya mwisho iweze kufaidika na kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Vivyo hivyo, kwa wafanyabiashara na wazalishaji wanatakiwa wawajibike kwa Serikali na wananchi kwa kutimiza taratibu zote kwa mujibu wa sheria zinazowahusu ikiwa ni ulipaji wa kodi na mengineyo ili kila mmoja aweze kufanya linalofaa na tuwe tunapata *win win situation*; kwa maana hakika mtu ambaye ana asilimia 30 kama na yeye hutamtimiza haki ni wazi kwamba biashara haitaweza kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ameonesha nia ya dhati ya kuwasaidia Watanzania, wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania. Katika mkutano wa *Tanzania Business Council* uliokaa tarehe 6 mwezi huu, Mheshimiwa Rais alitamka wazi kwamba yupo tayari kuendelea kuwasaidia wawekezaji kwa kuwapa *incentives* mbalimbali ikiwa ni pamoja na *tax holiday* ilimradi uwekezaji huo unalenga kunufaisha na kuisaidia nchi, Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla wake. Kwa hiyo, ni wazi kwamba nafasi ipo kazi ni kwetu sisi wawekezaji na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hili ameliweka wazi na amewaagiza watendaji waende wakalitekeleze. Rai yangu kwa wawekezaji, tusilale, rai yangu kwa wafanyabiashara, tusilale. Hatuna sababu ya kuendelea kupata vikwazo kwa sababu Rais amekwisha tamka wazi na yupo tayari kufanya maamuzi yoyote ili lengo na madhumuni ya kuwaunga mkono wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na hata wa nje likamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nichukue nafasi hii kutaka mamlaka zote husika ikiwa ni pamoja na Wizara mbalimbali ziweze sasa kushirikiana na kuhakikisha kwamba azma hii inakwenda kukamilika na tunasonga mbele katika kuimarisha viwanda na vile vile biashara na hatimaye uchumi na maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi sana nizungumzie madeni kwa kuwa kimsingi yanahusika moja kwa moja na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu mzigo mkubwa wa madeni ya nje na madeni ya ndani ambao Serikali inao, lakini naiomba sana Serikali katika utaratibu wake, ijikite sasa kupunguza mzigo wa madeni ya ndani. Lengo ni lile lile, madeni ya ndani yatakavyolipwa wafanyabiashara na wawekezaji wataendelea kuwekeza na matokeo yake manufaa yale yatakuwa ni kwa ajili ya Serikali na wananchi kwa ujumla wake, ina maana Serikali itaendelea kukusanya kodi kutokana na ile pesa kuingia kwenye mzunguko. Athari ya kupungua kwa ajira itaondoka, maana yake ajira zitaongezeka na hatimaye Serikali itafaidika zaidi pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali itapata fursa ya kutumia mitaji ya wafanyabiashara na wawekezaji katika kutekeleza malengo na mambo mbalimbali ya maendeleo. Pamoja na hilo uwekezaji wa ndani utaweza vile vile kuvutia zaidi uwekezaji wa nje ambao tunauhitaji ili kwenda kuimarisha uchumi wetu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulipwa kwa madeni ya ndani kutaisaidia Serikali kupata huduma na bidhaa kwa bei nafuu, kwa sababu kunapokuwa na *tendency* ya Serikali kuchelewa kulipa huduma na bidhaa zinazotokana na wafanyabiashara na za uzalishaji wa viwandani, maana yake ni kwamba kinachofuata huduma zile Serikali itaendelea kuzipata kwa bei ya juu na huku wafanyabiashara wakihofia kwamba ukifanya biashara na Serikali, basi fedha zako zitakaa muda mrefu na ikiwa umezikopa matokeo yake utapata matatizo makubwa. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba bei zitakuwa ni kubwa na hatimaye hatutafikia malengo ya kubana matumizi na kwenda sambamba katika utoaji wa huduma katika serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba tutasaidia wafanyabiashara wetu, maana wengi tayari wapo kwenye matatizo makubwa na mabenki. Wengine wanafilisiwa na wengine wanapoteza mali zao. Kwa hiyo kwa kuanza kuwalipa wafanyabiashara wa ndani ni wazi kwamba tutachangamsha uchumi na hatimaye wananchi watafurahia na tutasonga mbele kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya ndani yakilipwa itawasaidia vile vile Watanzania wengi ambao wanadaiwa kodi waweze kuzilipa kwa wakati na hatimaye siku ya mwisho itakuwa ni *win win situation* kati ya wafanyabiashara, wawekezaji na Serikali na kimsingi fedha nyingi zitatumika katika kuwekeza na hatimaye tutafikia malengo ya viwanda, ajira na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na haya machache ya kuishauri Serikali yangu, inaunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Deo Ngalawa ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kusimama katika Bunge hili Tukufu ili niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na Mkoa wa Tabora. Siku zote mcheza kwao hutunzwa. Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Tabora siku zote wamekuwa wakipiga kelele kuhusiana na suala zima la viwanda, Mheshimiwa Waziri Mwijage anafahamu, watendaji wake wote wanafahamu na wakati wote wamekuwa wakitupa ahadi za kwamba watatuletea wawekezaji katika mkoa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora kuna Kiwanda cha Nyuzi, kiwanda hiki alipewa mwekezaji mwenye asili ya Asia. Baada ya mwekezaji huyu kupewa kiwanda kile kitu kikubwa ambacho ameweza kukifanya katika kiwanda cha nyuzi ni kuondoa mitambo yote iliyokuwepo pale kwenye kiwanda kile kuisafirisha na kuipeleka kwao na kutuachia *hall* pale katika kiwanda kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hili kwa sababu nina ushahidi nalo. Ukienda katika kiwanda kile huwezi kumkuta mfanyakazi hata mmoja zaidi ya Wahindi wawili ambao wanazunguka katika kiwanda kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kile hakinufaishi vijana wa Tabora, hakinufaishi wazawa wa Tabora na wala hakinufaishi wanawake wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa mwekezaji huyu aliamua kwenda mbali zaidi hadi kuamua kuuza majengo yaliyokuwa yanamilikiwa na kiwanda kile. Leo majengo yale yanatumiwa na Ofisi ya Uhamiaji pale juu, ukienda pale kwenye barabara ya Kilimatinde kuelekea kule njia ya kwenda Jimbo la Igalula utaona yale majengo. Juu wameweka ofisi ya uhamiaji chini yapo magofu tu ambayo haieleweki yanafanya kazi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini basi watamwondoa mwekezaji huyu, watuletee mwekezaji mwenye nia thabiti ya kuwekeza katika Kiwanda cha Nyuzi? Malighafi za uwekezaji katika kiwanda kile zipo kwa sababu Tabora tunalima pamba, lakini pia majirani zetu wa Kahama, Shinyanga na maeneo mengine yanayolima pamba tunayopakana nayo yanaweza kufikisha malighafi zile kwa urahisi na kile kiwanda kikaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kutuletea mwekezaji imeshindikana, kiwanda tunacho, mwekezaji waliomuweka hafai, tunaomba sana waende wakapitie kiwanda kile wakiangalie, tukifufue kiwanda cha nyuzi na sisi wananchi wa Mkoa wa Tabora tuweze kunufaika na rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora kuna jengo la *SIDO*. Kwa masikitiko makubwa sana jengo hili haijawahi kuwanufaisha hata siku moja wakazi wa Mkoa wa Tabora. Matokeo yake leo hapa ninavyozungumza, *SIDO* Mkoa wa Tabora wamekodisha kwa Mratibu wa Mafunzo wa *VETA* bwana Kaali ambaye ameweka ofisini yake pale na kutengeneza furniture na kuziua. Hivi ndiyo yaliyokuwa malengo ya *SIDO* hayo ama ilikuwa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba Mheshimiwa Waziri aje anipe majibu ya kunitosheleza ili niweze kujua kwa nini *SIDO* imepewa mwekezaji eti yeye ndiye anatengeneza makochi yake pale na *furniture* zake halafu Watanzania wa Mkoa wa Tabora, hawanufaiki na hiyo *SIDO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia ya nyumbani kwetu, sasa naomba nizungumze mambo mengine kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wenye viwanda, wamekuwa na malalamiko mengi siku zote na kwa bahati nzuri mimi mwenyewe ni mmoja kati ya wajumbe

wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira na siku zote malalamiko haya yalipotufikia tumekuwa tukiyafikisha sehemu husika, lakini bado kumekuwa na maendeleo ya kulalamika kwa wafanyabiashara hawa kwamba mambo wanayoyahitaji kwa kweli hayatekelezwi sawasawa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema tunakwenda kwenye nchi ya viwanda tunakwendaje kwenye nchi ya viwanda walioopo sasa yale wanayolalamikia hayafanyiwi kazi ipasavyo? Tutegemee kulete wawekezaji wengine ili waweze kufanya kitu gani kipya ambacho kitawavutia wale watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iweze kuangalia hawa wafanyabiashara wetu wenye viwanda nchini. Sasa hivi wafanyabiashara wenye viwanda nchini ndio wamekuwa kama vile wanatakiwa wafanye kila jambo. Kosa dogo mfanyabiashara anakwenda kutozwa faini badala mfanyabiashara huyu kupewa maelekezo nini afanye lakini imekuwa wakifika *NEMC* ni milioni 50, akifika Waziri ni milioni 30, sasa hawa watu watafanya kazi hii kwenye mazingira yapi? Tunawakatisha tamaa, hawa wafanyabiashara wanahitaji kuwekeza, lakini wanashindwa kutokana na mlolongo wa mambo ambayo yanawakera.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfanyabiashara yoyote au mwekezaji anapotoka nje lazima apate mwenyeji kutoka ndani ajue mwenzetu amefikia wapi, anafanya nini kuendeleza kiwanda chake, sasa mwisho wa siku itafika mahali ataanza kuambiwa mabaya kwanza halafu ndipo aambiwe yale yaliyo mema. Zaidi ya amani na utulivu ambayo ataambiwa ndilo litakuwa jambo la kwanza mengine ataambiwa hapo ukifanya hivi tayari, ukifanya hivi tayari, mambo yanakuwa si mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kilichopo hapa Dodoma (*Dodoma Wine*) huyu mwekezaji anafanya kazi nzuri kweli kweli, mwekezaji huyu ana wateja wengi kweli kweli, lakini anashindwa kuzalisha kwa ufanisi kwa sababu kila

kukicha akifungua ofisi yake watu wa Halmashauri hawa hapa, akifungua ofisi NEMC hawa hapa, akifungua ofisi watu wa mazingira hawa hapa. Wote hawa kila mmoja anakwenda kwa wakati wake na anahitaji fedha kutoka kwa huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo tukumbuke huyu ameajiri, huyu anatakiwa kulipa kodi ya Serikali, huyu anatakiwa kufanya mambo kibao katika nchi hii, anafanyaje biashara zake? Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hawa wawekezaji wetu wachache tulionao ambao ni waaminifu, waweze kuangaliwa mazingira yao ya kufanyia biashara zao ili waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *General Tyre* kimekuwa ni hadithi za Alfu Lela Ulea. Niseme tu Mheshimiwa Waziri tulikwenda tumetembelea na waliahidi kwamba kiwanda hiki kingefanyiwa upembuzi yakinifu. Mwaka wa jana bajeti yake ilikuwa Sh.150,000,000 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, leo imeandikwa Sh.70,000,000, sijui ni kwa ajili ya nini, kwa sababu ni pesa ndogo sana ambayo haiwezi kwenda kufanya huo upembuzi yakinifu ambao wanasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo majibu mengine ambayo tumepata ni sasa hivi wanatafuta mwekezaji, kwa hiyo mwekezaji mwenyewe ndio atakayekwenda kufanya huo upembuzi yakinifu. Tunasema ni hadithi za Alfu Lela Ulela kwa sababu haya mambo yameanza kusemwa tangu tukiwa wadogo tunasikia *General Tyre* mpaka leo bado tunaisikia *General Tyre*.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye viwanda wana malalamiko makubwa sana kuhusiana na umeme usio wa uhakika, umeme unakatikatika wakati wowote. Sasa wale wanapokuwa wameshawasha mashine zao, umeme ukikatika kwa ghafla, ukija kurudi unawasababishia hasara kubwa sana katika mitambo yao kwa sababu umeme unavyorudi haujulikani umerudi kwa nguvu ya aina gani. Kwa hiyo nimwombe Sana Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana

na Mheshimiwa wa Nishati waangalie kwa kiasi kikubwa ili kuona ni jinsi gani wanavyoweza kuwasaidia wafanyabiashara kwenye suala zima la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na ziara katika Mkoa wa Tanga. Tanga ni moja kati ya mikoa inayoongoza kwa kuwa na viwanda vingi vingi sana, lakini pale Tanga umeme wa uhakika haupo. Hizo *megawatt* walizopewa na *TANESCO* haziwatoshi kuweza kuendesha shughuli za viwanda. Kwa hiyo, naomba sana wauangalie mkoa ule ili uweze kufufua vile viwanda na tayari watu wameanza kuamka kuvifufua; waweze kuleta ajira kwa Watanzania hasa vijana na wanawake ambao hawana ajira za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wenye viwanda hasa hao wanaofanya biashara ya *cement* wamekuwa na malalamiko juu ya upendeleo, kwamba kuna baadhi ya wafanyabiashara wanapendelewa kwenye masuala mengine na wao hawapewi upendeleo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Tanga Cement* wanatengeneza *clinker* ambayo inatengeneza *cement*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi, nimshukuru Waziri Kivuli wa Kambi rasmi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri. Ahsante, *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tutaendelea na Mheshimiwa Riziki Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ngalawa na Mheshimiwa Balizi Adadi Rajabu ajiandae.



**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyenijaalia kupata afya njema na kuwepo katika kuchangia hoja iliyokuwepo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mtanzania na napenda maendeleo ya Tanzania na napenda Watanzania iwe mweusi, iwe mweupe, mwenye rangi ya kijani, tuwe na maendeleo ambayo yanawiana. Nataka nitoe pongezi zangu za dhati kwa baadhi ya wawekezaji wa Kitanzania ambao wameonesha kuwa wana uwezo wa kuweza kufanya biashara na wana uwezo kuingia katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Mwezi Aprili, kulifanyika mkutano mkubwa sana Nairobi wa *African Urban Transport*. Nataka kuwapeni taarifa Wabunge mwendo kasi *UDAT* imepata tuzo namba mbili. Yule ni Mtanzania kama ana mahali amekosea basi inabidi arekebishwe lakini ameonesha uwezo mkubwa na wameambiwa Wakenya, Waganda, Wazambia, Waethiopia na tumewaona wamekuja kujifunza Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo maendeleo ambayo unayaona yakiwekezwa kwa ngozi nyeusi na Watanzania basi maendeleo haya yatakuwa yana uwiano, na pesa yetu badala ya kuipeleka nje, itabakia Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze tena Reginald Abraham Mengi na yeye ameonesha uwekezaji wake unamsaidia na unamgusa mtu mwenye ngozi nyeusi na ajira kubwa zinakwenda kwa watu wenye ngozi nyeusi. Nampongeza Bakhresa, kazi yote na fedha zinazopatikana za Bakhresa zinabakia Tanzania na unaona hata nyumba zao na *investment* zao zinawagusa Watanzania na wengineo. Hii maana yake Nigeria waliwatengeneza watu weusi 150 mmojawapo akiwa Dangote ambaye anakuja kuwekeza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaingia katika ulimwengu wa viwanda, tumewaandaa vipi Watanzania wenye ngozi nyeusi ambao ndio maskini zaidi ili waweze kuingia katika uwekezaji? Ni matumaini yangu, tusijibeze sisi wenyewe tunaweza. Mwanzo hatukuwa na elimu lakini sasa hivi tumepata elimu, watoto wetu hawa baadaye ndio wataokuwa akina Dangote wa Tanzania. Tusiwakatishe tamaa tuwape nguvu ili wazidi kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi, Mtwara na Ruvuma tumeonesha mabadiliko makubwa sana. Mwaka jana nilimuuliza swali la papo kwa papo Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu tozo na kero ya korosho. Katika usimamizi bora unaofanyika tumepata korosho kilo moja kwa Sh.3,800, ilikuwa ni dhahabu ya kijani imewezesha kuingizia Tanzania dola za Kimarekani 346,000,000 katika mnada wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hizi ukizigawanya au ukazipigia hesabu kwa *Tshs* tumefanya mafanikio makubwa sana. Tumedhulumiwa kwa muda mrefu na wafanyabiashara wa mazao. Ningeomba *speed* hii iliyokwenda kwenye korosho iende kwenye kahawa, tumbaku, ufuta, mbaazi na alizeti ili Watanzania hawa ambao ni maskini waweze kufarijika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la korosho linastawi Pwani yote mpaka Zanzibar. Tuko kwenye Muungano, tusiache Zanzibar nyuma katika kuondoa umaskini tukawa sisi peke yetu tunaendelea. Hii korosho inapatikana Madagascar, Comoro na Seychelles. Nilitegemea kwa upendo wetu tuliokuwa nao katika Muungano basi na korosho ipelekwe na kuhamasishwa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, korosho yetu imeingia dosari kubwa kwa wafanyabiashara ambao wana mazoea. Baada ya kuona tumepata soko la Vietnam wafanyabiashara wakubwa wa mazao wamezuia makontena wanaya-*hold* ili yule anayenunua korosho asizipeleke tena nje, hii ni dhuluma

kwa Watanzania. Wamekuwa matajiri kwa kupitia Tanzania, leo wao wanakuwa matajiri hawataki waone uchumi wa Tanzania unaruka kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri mwenye dhamana aliangalie hili na awaangalie wanaofanya mchezo huu, uishe. Hili ni tambazi, maana kama ni jipu limevilia limekuwa ni tambazi, nataka tuhame kutoka katika majipu tuyapasue matambazi ambayo yamezoea kutukamua na kutunyonya nchi hii ili tusiweze kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ambavyo vilibinafsishwa nataka aniambie Mheshimiwa Waziri, je, hivi viwanda vimebinafsishwa au vimeuzwa? Kama vimeuzwa nani amenunua na kama amenunua mbona havifanyi kazi zaidi ya miaka 20?

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza ndugu yangu Mwambe, huyu Mwambe ana uchungu na korosho. Kiwanda cha Lindi kimefungwa, Kiwanda cha Mtwara kimefungwa, Kiwanda cha Masasi kimefungwa, Kiwanda cha Newala kimefungwa, Kiwanda cha Kibaha kimefungwa, wao wanachukua zile korosho wanakwenda kupeleka ajira kwao, kwa nini? Hamwoni kama Mkoa wa Lindi hakuna kiwanda hata kimoja? Tutapataje utajiri katika hali ngumu ya kimaskini kama hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefikia mahali tunajiliza hivi Lindi kweli mkoa wenye majimbo nane hatuna kiwanda hata kimoja. Kama Waziri ananibishia, aniambie Lindi kuna kiwanda fulani, hakuna, vyote havifanyi kazi, ina maana tunatengeneza umaskini Mkoa wa Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Uwekezaji. Nimeangalia katika makosa ambayo tumeyafanya nchi hii ni kwamba hatuna sera. Kama hatuna sera tumeingiaje katika uwekezaji wa viwanda? Tunakwendaje na maendeleo ya viwanda wakati hakuna sera? Sera ni usukani, utatoa sheria, taratibu na kanuni, hatuna. Sasa hivyo viwanda 200 vinavyokuja sheria gani

itasimamia? Utaratibu gani utasimamia? Kanuni gani itasimamia? Tutarudi kule kule. Hivyo naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuleta majibu aniambie kwa nini sera ya viwanda haijakamilika mpaka leo. Tunakwenda katika ulimwengu wa viwanda, tunaendaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda mpaka kwenye madini. Tulienda katika Idara na Maendeleo ya Madini bila kuwa na sera. Tullitembelea Buzwagi hakukuwepo na sera, wamechimba mahandaki, watu wengine wameshamaliza kuchimba madini, tumeachiwa malaria katika Mikoa ya Geita, Simiyu na Mara. Ndicho tunachokataa hiki, tunataka sera ije iweze kuwakamatia wale ambapo katika upande wa *environmental impact assessment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifikie mahali tujiulize tumelogwa na nani? Wanatuambia wenyewe, nilikaa na mtu mmoja akaniambia Tanzania *is a sleeping giant* na tunajitambua kabisa kama tuko *sleeping giant*. Kama tungekuwa si *sleeping giant* tungekuwa na sera sasa hivi, lakini mpaka leo tunakimbizana na viwanda lakini hakuna sera. Leo unaposema mimi mtaalam unakuja kunielimisha nini wakati huniambii nitafanya nini? Nenda *TPDC*, walikuja kwenye Kamati wakiwa hawana sera, *strategic plan*, wala *action plan*, kutakuwa na *commitment* hapo?

## T A A R I F A

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida naona Waziri anataka kutoa taarifa.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sikupaswa kujibu lakini neno linalozungumzwa lina uzito, huwezi kuingia kwenye shughuli ngumu kama hizi bila sera au mkakati. Ujenzi wa uchumi wa viwanda unaendeshwa kwa sera ya viwanda iliyoinduliwa mwaka 1999 inakwenda mpaka mwaka 2020. Chini yake iko mkakati *//DC* ulioinduliwa tarehe 11 Desemba, 2011 unakwenda mpaka 2025, kuna sera, kuna mkakati.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh naomba ukae tumalize hii taarifa kwanza halafu na wewe utapewa nafasi. Mheshimiwa Lulida unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mheshimiwa Waziri mimi ni shangazi yangu, siipokei. Kwa nini siipokei? Kwanza hata kwenye kwenye *computer* kuna *update* ikiwa 1996 sasa hivi tunazungumza mwaka 2017 *update* ngapi zingepatikana sasa hivi? Maana *computer* tulianza na *Microsoft* tunaenda *excel*, tumekwenda mambo chungu nzima, leo anaturudisha nyuma katika *analog*, tunakwenda katika *digital* sasa hivi katika ulimwengu wa kisasa wa maendeleo ya viwanda, sikubali hoja yake. *(Makofi)*

## T A A R I F A

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida, Mheshimiwa Ally Saleh anataka kutoa taarifa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba kama sera ni ya mwaka 1996 unataka kutuletea leo kwenye viwanda vingi, *we are planning to fail. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh, kwa kuwa Waziri hakuwa mchangiaji, alikuwa ni mtoa taarifa, basi Mheshimiwa Lulida ataendelea, Mheshimiwa Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Ally Saleh, namwambia kitu kimoja, bahati nzuri nilikwenda Lima Peru, nimetembelea mpaka Mexico walifanya makosa haya sasa hivi zile nchi ziko *polluted* kwa vile hawaku-*update* hizi sera zao, wakajiingiza katika mikataba na sheria mbovu na kuiweka nchi katika umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia madini. Leo tunaletewa na *STAMICO* kuwa kuna baadhi ya mashirika ambayo yameingia ubia na madini, kwa vile hakuna sera, amefanya *feasibility study* na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulida malizia sentensi kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru, sina lingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DEO F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, najikita moja kwa moja kwenye Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Ikumbukwe katika Bunge lako tarehe 19 mwezi wa Nne niliuliza swali Liganga na Mchuchuma, fidia kwa waliopisha maeneo itakuwa ni lini? Nikajibiwa kwamba italipwa mwezi Juni, 2016. Pia Bunge lako lilitaarifiwa kwamba Mradi wa Liganga na Mchuchuma ungeweza kuanza mwezi Machi, 2017. Sasa kitu ambacho nakiona ni kwamba, Serikali haina dhamira ya dhati juu ya Mradi wa Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kufuatilia maelezo ya Mheshimiwa Waziri, naomba ninukuu kwa kusoma, Mheshimiwa Waziri anasema:-

*"Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Wizara kupitia NDC iliendelea na majadiliano juu ya mauziano ya umeme kati ya Shirika la Umeme TANESCO na kampuni ubia. Mfumo uliokubalika na pande zote mbili ni mwekezaji kujenga mtambo wa kufua umeme, kumiliki na kuendesha, (build, own and operate). Mauzo ya umeme kwa TANESCO hayajumuishi gharama za uwekezaji kuhusu ujenzi*

*wa mradi. Kamati ya Taifa ya uwekezaji imepitia kwa mara nyingine vivutio vilivyombwa na mwekezaji kwa lengo la kutafuta manufaa zaidi kwa Taifa katika mradi huo”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mradi wa Liganga na Mchuchuma umewekwa kama ni mradi kielelezo (*flagship project*). Hata hivyo, kitu ambacho nakuja kukiona hapa inaonekana kwamba hakuna *master plan* ya mradi huu kuanza. Leo hii tunauzungumzia hata fidia haijalipwa, wakati mwekezaji anasema tayari ana hela za kulipa, lakini sisi kama Serikali yenyewe inazungumza kwamba bado wanaendelea na mazungumzo juu ya *power purchase agreement* kati ya mbia na *TANESCO*. Sasa najiuliza pana tatizo gani? Kwa sababu tungepewa *schedule of activities* mpaka mradi ku-*take over*, lakini leo hii bado tunazungumzia kwamba tunaendelea na majadiliano sasa tujulize haya majadiliano yataendelea mpaka lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia Wizara hii mwaka wa jana tulizungumza kwamba tungepewa *road map*. Ifike mahali kwamba tujue kwamba mwezi huu mpaka mwezi huu, mwaka huu mpaka mwaka huu *activity* fulani inafanyika ili tuweze kujua kwamba itakapofika muda fulani mradi huu uwe ume-*take over*. Hiyo tulikuwa tunaizungumza hivyo kwa maana ya tuweze kum-*pin* mtu ambaye anatuletea shida hapa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kama tunaamua kuzungumzia tu kwamba tutaendelea tu na majadiliano itafika 2020 huu mradi haujaanza, fidia haijalipwa, hayo makubaliano ya *TANESCO* hayapo, hizo *incentives* ili Serikali ije itoe *GN* haziatakuwepo. Kwa hiyo, napenda kusikitika kwamba huu mradi hatujauwekea kipaumbele. Inawezekana zipo *incentives* ambazo zinatakiwa na mwekezaji lakini vile vile lazima tuangalie *multiplier effect* ya mradi wenyewe upoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unaleta ajira 33,000, hiyo hatujaiangalia, lakini tunaangalia zile *taxation*

tu za mwanzo. Ifike mahali; kwa sababu Baraza la Uwekezaji Mwenyekiti wake ni Waziri Mkuu, kwa hiyo, maana yake huu mradi unafahamika vizuri. Kama kuna shida basi tujue kwamba huu mradi haufanyiki ili watu waendeleo na mambo mengine. Leo hii ndugu zetu wa Ludewa kule wamepisha mradi lakini fidia hawana, maeneo yale yanashindwa kuendelezwa, yanashindwa kulimwa, lakini hakuna tamko lolote la Serikali ambalo linawapelekea sasa wananchi wale wafanye nini. Mwekezaji anasema hela anayo, kama hela ya mwekezaji inaleta shida, basi Serikali ingebeba jukumu la kulipa fidia huku ikiendelea na hayo mazungumzo ili iwafanye wale watu waendeleo na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijaribu kuangalia licha ya ajira 33, 000 zitakazokuwa zimeletwa na mradi huu, tunatarajia kwamba huu mradi ungeweza kuleta *population* ya watu wasiopungua laki tatu ndani ya eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuja kwa mradi huu maana yake ungeweza kuanzisha viwanda vingine kwa ajili ya kuweka *value addition* ya mazao yanayolimwa na mikoa na wilaya jirani. Hata hivyo, inaonesha ni kwamba Serikali yenyewe ime-*base* tu kwenye maeneo machache, kitu ambacho na chenyewe si sawa kiuchumi. Ifike mahali kwamba hiyo *tax* kwa mfano tukii-*wave*, kuna *impact* nyingine kwa jamii kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza kwamba huu mradi haupewi kipaumbele kwa sababu pia unakuta hata ile miundombinu yenyewe haijawekwa. Leo hii tuna barabara inayoenda kwenye chuma cha Liganga, barabara ya kutoka Mkiu kuelekea Madaba, mpaka leo hii tunaambiwa tunafanya *rehabilitation* hakuna utaratibu wowote kusema inaingia kwenye upembuzi yakinifu, iende kwenye usanifu wa kina, barabara zijengwe ili kwenda kwenye huo mradi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nchi inazungumza haina chuma, lakini chuma kimelala pale Liganga, leo



chuma tunaagiza. Kwa hiyo ikifika mahali unakuta sasa hivi vitu vinasuasua. Tumezungumzia juu ya Reli ya Mtwara kuja Mbamba Bay kutoka Mbamba Bay inakuja Mchuchuma inakwenda Liganga; sijajua utaratibu ukoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unaweza kuona kwamba Serikali na yenyewe inakwepa. Kama tatizo ni mwekezaji, basi ifute huo utaratibu ili tujue kwamba huu mradi haupo tunatafuta mwekezaji mwingine ili tuweze ku-move, kwa sababu haiwezekani miaka mitano, sita tunazungumzia Liganga tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Liganga kwa mara ya kwanza imezungumziwa mwaka 1929. Sasa mwaka 1929 mpaka leo tunazungumza tu Liganga, wazee wetu wanakufa, watoto wetu wanakufa sisi wote tutaenda tutakufa Liganga itaendelea kubaki palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozunguzia uchumi wa viwanda Tanzania huwezi ukaiondoa chuma cha Liganga na huwezi kuondoa makaa ya mawe Mchuchuma. Makaa ya mawe Mchuchuma yanatoa megawati 600, leo nchi inatumia megawati 1050... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo muda wako umekwisha.

**MHE. DEO F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajiandae.

**MHE. BAL. ADADI M. RAJABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kupata muda huu kuweza kuchangia hii hoja muhimu sana ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Awamu yake ya Tano, kwa kuweka msisitizo mkubwa sana kwenye viwanda. Viwanda ni kitu muhimu sana kwenye nchi yoyote na ndiyo vinavyokuza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukurani hizo lakini mtakumbuka kwamba viwanda vingi kwenye hii nchi vilikuwa Tanga. Tanga ilikuwa ni kitovu cha viwanda, lakini viwanda sasa hivi Mkoa wa Tanga vimekufa kabisa. Sasa nilitegemea Mheshimiwa Waziri alipoingia madarakani kitu cha kwanza kingekuwa ni kufufua vile viwanda vya Tanga ambavyo vilikuwa zaidi ya 1000. Kwa hiyo, tulitegemea kuna mikakati madhubuti ya kufufua vile viwanda. Kulikuwa na viwanda vingi tu vya chuma, sabuni, mbolea na vitu vingi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi sijaona juhudi zozote za kufufua vile viwanda, lakini namshukuru kwa kutuletea kiwanda kikubwa sana ambacho kitaweza kutoa tani milioni saba kwa mwaka, Kiwanda cha Hengya na nimeambiwa kufuatana na taarifa yake kwamba wawekezaji wenyewe wako hapa Bungeni. Nawashukuru sana na nawahakikishia kwamba, wawekezaji hao waje Tanga na hawatapata matatizo yoyote na najua kabisa Mkuu wetu wa Mkoa wa Tanga yuko China kwa ajili ya ku-*facilitate* kiwanda hicho kiweze kuja Tanga. Karibuni sana Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muheza sasa hivi sisi tumeshajitayarisha, tuna ardhi kubwa sana. Tuna ardhi ambayo sasa hivi tunasubiri mtuletee viwanda, tunafanya juhudi kubwa sana za kutafuta viwanda vya matunda; kutafuta wawekezaji wa viwanda vya mihogo pamoja na viwanda vya kuwekeza mipira, hizi pilipili manga pamoja na karafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ardhi tunayo na nilishamwambia Mheshimiwa Waziri na tujitahidi kwa uwezo tuweze kupata wawekezaji wa kuweza kusaidia kupata hivi

viwanda hasa vya matunda pamoja na mihogo. Juhudi bado zinaendelea na mazungumzo bado yanaendelea na *insha Allah* pengine tunaweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamefunguliwa viwanda vingi hapa karibuni, viwanda vya matunda, lakini ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, wawekezaji wanapokuja asiwaelekeze kwenye sehemu moja tu, ajaribu kuwaelekeza kwenye sehemu zile ambazo zao linatoka. Zao la matunda linatoka Tanga (Muheza). Kwa hiyo, ningeshukuru sana alete wawekezaji au wa mihogo Muheza, tunayo ardhi kubwa sana kwa ajili ya viwanda na kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TIC* au *EPZA*. Vituo hivi ni muhimu sana kwenye nchi yoyote ile. Vituo vya *TIC*, *EPZA*, panapotokea ukorofi, ucheleweshaji wowote kwenye vituo hivyo, wawekezaji hapa ndipo wanapoweza kutoroka na kuondoka kwa kuwa vituo hivi ndivyo vinavyopokea wawekezaji. Sasa, niliwahi kuzungumza mwaka jana hapa kwamba, Kituo cha *TIC* lazima pawe na *Land Bank*, mwekezaji anapokuja hataki usumbufu, yeye anataka kuambiwa maeneo ni haya, ni haya, ni haya, wekeza hapo. Sasa utaratibu wa kusema watu binafsi ndio wawekeze pale, una *land* yako unakwenda kuingiza kwenye *TIC* inaleta usumbufu. Ni lazima Serikali sasa hivi kuptia Wizara ya Ardhi itoe ardhi *TIC*, ni lazima itoe ardhi *EPZA* ili mwekezaji akija aende moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho mimi kwenda *TIC* baada ya kupeleka wawekezaji pale, kulikuwa na vibali zaidi ya kumi na tano. Sasa sijui sasa hivi hivyo vibali vimefunguzwa kwa kiasi gani, lakini unaposema *One Stop Centre* ni lazima iwe *One Stop Centre* kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda *Mauritius Enterprise*, wao wana-*time frame*; mwekezaji anapokwenda pale ilikuwa *2400Hrs* lakini wamefunguza mpaka *0600Hrs*; kwamba kila kitu *Residence Permit*, *Working Permit*, viwanda, sijui leseni vyote vinafanyika katika siku moja. Sasa mwekezaji

anataka kitu kama hiki na ndiyo maana kwenye ripoti za *transparent international* dhidi ya *good governance* na *corruption*, Mauritius na Botswana wamekuwa wanaongoza kwa miaka mingi na ni kwa sababu ya *TIC* yao, *Mauritius Enterprise*, ukienda Botswana *TIC* yao, hakuna usumbufu watu wanapata vibali mara moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeshauri kwamba, Mheshimiwa Waziri aangalie vibali gani pale vinaleta usumbufu, atoe vile vibali weka vibali vichache. Mwekezaji hapendi usumbufu atoke hapa aende sijui biashara, atoke hapo aende sijui *immigration*, atoke hapo aende wapi! Anataka kila kitu akikute pale pale na hapo ndipo tutakapoweza kupata wawekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna taarifa wawekezaji wanaondoka, ni kweli? Ningependa hiyo taarifa labda Mheshimiwa Waziri aje ui-*clarify* wakati atakapokuja ku-*wind up* kama kweli wawekezaji wetu wanaondoka kwa sababu ya huu usumbufu ambao ni *unnecessary* ambao upo sehemu mbalimbali? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba Kiwanda cha Kamba, Tanga kina mashine nzuri na kinatoa mali ambazo zinanunuliwa hata nchi jirani. Nikaomba kwamba, Serikali sasa hivi basi iwape zabuni wale Kiwanda cha Kamba, wanatengeneza mazulia mazuri sana, ili mazulia yote ambayo yanatengenezwa, basi wapewe zabuni Tanga ili waweze kuzalisha na kuweza kuinua kile kiwanda. Sasa hivi kinatoa vizuri na kinataka kuleta mashine nyingine ambazo ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kushauri tu kwamba, ili kuleta wawekezaji, najua kwamba wanatumia Mabalizi nje, lakini ni vizuri wakaweka ma-*trade attachee* kwenye sehemu zile chache ambazo wanaona kwamba, kuna wawekezaji wengi ambao wanakuja. Wapeleke hawa ma-*trade attachee* watakaa kwenye Ofisi za Ubalizi na watakuwa *specifically* kazi yao iwe ni hiyo na wawape *assignment* kubwa, tutakuwa hatupati hasara,

lakini nina hakika kabisa kwamba kuwepo kwa ma-*trade attachee* kwenye Balozi zetu kutasaidia sana badala ya kuwaachia hilo jukumu Mabalazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare ajjandae.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika Wizara hii muhimu sana ya Viwanda na Biashara. Mimi kama mama na mzazi naomba nichukue fursa hii kuwapa pole familia zote za wale vijana wetu waliofariki pale Karatu, zaidi ya 33 na Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema, peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Komandoo, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Kauli Mbiu yake mahiri kabisa ya kwamba 'Tanzania ya Viwanda Inawezekana'. Amekuja na *good spirit* ya uchumi wa viwanda na nina hakika kabisa tukimuunga mkono kwa vitendo inawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na naelewa kabisa kwamba Serikali haijengi viwanda, Serikali ina-*facillitate* viwanda. Hata hivyo, pamoja na hayo nataka kujua, Serikali inapoingia katika miradi ya kimkakati kama vile Liganga na Mchuchuma, nime-*declare interest* mimi natoka mikoa ya huko, lakini Serikali hii haitoi *GN (Government Notice)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni kwamba, miradi mingi inasimama. Haijulikani miradi hii itanza lini? Miundombinu haieleweki, *Power Purchase Agreement* zake hazieleweki. Namwomba kaka yangu Mheshimiwa Mwijage

pamoja na kujieleza vizuri sana, lakini atulettee majibu yenye tija atakapokuja ku-*wind up* hapa juu ya suala zima la Mradi ule wa Liganga na Mchuchuma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala zima la kodi. Kodi za VAT kwa wawekezaji wenye viwanda nchini ni tatizo kubwa sana. Wawekezaji hawa wanachajiwa VAT kwenye utengenezaji wa bidhaa za ndani, lakini cha ajabu na cha kusikitisha sana ambacho ambacho nashindwa kuelewa mpaka kesho, bidhaa hizi zinazokuwa *imported* kutoka nje hazina VAT. Sasa nashindwa kuelewa kabisa hapa, hivi tunauwa hili soko la ndani ama tunajanga? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni kwenye hizi *textile factories*, hata hapa Dodoma kwenyewe kuna kiwanda cha *gypsum* mpaka kimefungwa kwa sababu hozohizo ambazo mimi ninazitoa. Naamini inawezekana kabisa *buy Tanzania use Tanzania*, tujivunie *products* zetu za hapa nchini jamani, inawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la hii *NEDF (National Enterpreneurs Development Fund)*. Hii pesa Serikali inahitaji iipe Wizara kwa nguvu sana kwa sababu, inasaidia sana kuinua wafanyabiashara wadogo wadogo. Hivyo tunaomba Serikali itilie mkazo suala zima hili la *NEDF* na hii itasaidia kuleta kile kitu tunaita *One District One Product*, kwa sababu yote haya yanawezekana tukiwa na mikakati thabiti na yenye tija kwa vitendo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya yote mwenzangu pale Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Balozi Adadi amezungumza. Tunazungumzia ukuaji wa viwanda, mimi natoka Mbeya, kule kwetu Mbeya kuna viwanda vingi sana vimekufa yamebaki ni magofu tu. Tunaelewa kabisa ufufuaji wa viwanda uko chini ya *TR*, lakini pamoja na hayo tunataka Serikali itupe mkakati wa ufufuaji wa viwanda hivi umefikia wapi kwa sababu kule kwetu Mbeya majengo yale yamebaki ni magofu, rasilimali zinapotea bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya yote ni suala ambalo halieleweki, tunahitaji Mheshimiwa Waziri hata kama iko chini ya *TR* tulettee mkakati mzima wa Serikali juu ya ufufuaji wa viwanda ili twende na dhana nzima ile inayosema ukuaji wa viwanda, ufufuaji wa viwanda na ujengaji wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine ninayozungumza kule kwetu *Mbeya Textile* ni magofu, *Tanganyika Packers* magofu, Sijui kutengeneza sabuni vyote hivyo ni magofu, ni magofu, ni magofu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenyewe unaelewa, hii ni hasara; hata zana za kilimo; ni hasara kubwa. Rasilimali zetu zinapopotea bure ina maana Serikali yetu hii yenye nia njema ya Awamu ya Tano tunakuwa hatufikii zile ndoto zetu tunazosema ukuaji wa viwanda. Kama ikishindikana *worse to worse* pia tupate *PPP, provided* tunaweza kupata ile *win win Situation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nisigongewe kengele, naunga mkono hoja hii ya Biashara na Viwanda, lakini kaka yangu Mheshimiwa Mwijage akija hapa atulettee majibu ambayo yana tija kwa vitendo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, viwanda Mkoani Mbeya nadhani umesikia hapo.

Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete! Atafuatiwa na Mheshimiwa Getrude Pangalile Rwakatara, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kupongeza sana juhudi zinazofanywa na Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hakika maneno haya hata kama kuna mtu anasema kwake hayajafanyika, lakini Chalinze wanaopita kwenye barabara wameshayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nimeona kwenye TV hapa wawekezaji wangu wamekuja. Ningependa nitambue uwepo wa bwana Jack Feng na ndugu yangu Beda kwa kweli, wananifanya leo hii ninaposimama hapa na ninapotazama kitabu hiki natamba na Mheshimiwa Mwijage anatamba ni kwa sababu yao. Nawashukuruni sana. Kama mnavyoona kwenye TV pale bwana Jack Feng na bwana Beda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mazuri ambayo Serikali yangu imeendelea kufanya, lakini bado zimebakia changamoto na yako maeneo ambayo mimi kwa nafasi yangu kama Mbunge ningependa nitoe ushauri maana maongezi yangu leo yamejikita sana kwenye ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, viwanda na maji. Kule kwangu mimi viwanda vyangu vyote ninavyotengeneza vyote vinahitaji maji. Tunapozungumzia viwanda vya vigae, mahitaji ya maji ni makubwa sana, lakini pia, nazungumzia viwanda vya mazao yanayotokana na matunda, mahitaji ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameeleza katika Hotuba yake ya Bajeti juu ya ukubwa wa viwanda hivi na vitu ambavyo vitaendelea kuchukuliwa pale. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri na huu ni ushauri wa dhati kabisa toka moyoni mwangu Wakae na Waziri wa Maji waulizane juu ya jinsi gani lile jambo linalokabili Kiwanda cha *Sayona Fruits Processing* pale Mboga, watakavyoweza kulimaliza. Mheshimiwa Waziri wa Maji ametoa ahadi alipokuwa anafanya majumuisho ya hotuba yake akisema kwamba jambo hilo tutaliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Waziri anaweza kwenda mbio sana, hebu ajaribu kukamatana na Mheshimiwa Waziri wa Maji ili tuweze kulifikisha jambo hili pazuri na ile ahadi ya kusema kwamba mwezi wa 10 Mungu akijalia Mheshimiwa Rais aje Chalinze kuja kuzindua kiwanda kile iwezekane. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia, tulifanya mazungumzo na wenzetu wa TWYFORD ambao wanaonekana kwenye TV hapo; kwamba kubwa zaidi ambalo wao wanalitaka ni Serikali iwape ruksa ya kuweza kuchukua maji kutoka Mto Ruvu ili waweze kuyavuta mpaka pale kwenye kiwanda chao, lakini pia waweze kutengeneza maji ambayo watayafikisha katika maeneo mengine ya Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Waziri ni binadamu sana, najua kwamba katika kuwapa kibali hicho hatowasahau wananchi wa Kata za Vigwaza, Pera pamoja na Bwilingu kwa sababu maji hayo yanayohitajika yakienda kiwandani kama hayatakwenda kwa wananchi huenda tukakuta siku moja mwekezaji analalamika kwamba, maji hayaendi kwa sababu wananchi wametoboa mabomba. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili aliwekee mkakati mzuri ili tuweze kufanikisha haya mambo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo liko jambo la Bandari ya Bagamoyo. Mheshimiwa Waziri nimetazama kitabu chake chote hiki, hakuna sehemu ambayo amezungumzia Bandari ya Bagamoyo na viwanda vinavyotakiwa vijengwe katika *Special Economic Zone*. Si hilo tu, Mheshimiwa Waziri wakati anatoa pale ambayo mimi naiita *summary* ya kitabu hiki amejitahidi kuelezea Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nimuulize swali Mheshimiwa Waziri niamini yapi, niamini aliyoyasema akiwa pale au niamini ambayo amendika kwenye kitabu hiki? Hili ni jambo ambalo Wanabagamoyo wangependa sana kulijua kwa sababu, uchumi wa maeneo ya Bagamoyo na Tanzania kwa ujumla wake unategemea sana uwepo wa bandari ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba mwekezaji yuko tayari kwa ajili ya kulipa lile, lakini kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri

nabaki na maswali ya kuuliza lini fidia hizo za wananchi wale wa Pande, Mlingotini na maeneo mengine ya Kata ya Kiromo wataweza kulipwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata kama wanataka kulipa ni jinsi gani anakuja kulipa mtu huyo? Kwa sababu fedha hizi ambazo tunazungumza hapa ni fedha za mwekezaji, lakini mwekezaji huyu anapata wapi taarifa juu ya mahitaji ya watu wale? Vile vile anaweza vipi kutambua watu wale kwa sababu niliposikiliza maneno yake naona kama kuna utaratibu wa Serikali kujitoa na kuliacha eneo lile ambalo sisi Wanatanzania tunategemea kwamba, liwe ndio sehemu ya ukombozi mkuu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Waziri amezungumza juu ya mambo mengi ambayo nchi yetu inafanya. Hata hivyo, viwanda hivi vinavyojengwa katika eneo la Chalinze *in particular* ni viwanda vikubwa sana, lakini mwekezaji wangu, kwa mfano Sayona ambaye anajenga kiwanda kikubwa cha matunda ambapo ndani ya kitabu chake ukurasa wa 23 ameeleza juu ya ukubwa huo, lakini pia ameeleza juu ya umuhimu wa kiwanda hicho, lakini mwekezaji huyu anahangaika mpaka leo kutafuta *Strategic Investment Certificate*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anajua, kwa wawekezaji ambao watahitaji bidhaa za Tanzania nzima, kwa wawekezaji ambao watatoa ajira zaidi ya watu 29,000, kwa wawekezaji ambao watachukua matunda na watatoa *production* ya lita zaidi ya milioni mia mbili kwa mwaka, huyu mtu ana kigezo chote cha kupewa *Certificate* ya *Strategic Investment*. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake atueleze sisi Wanachalinze na Watanzania kwamba, amejipangaje katika kuhakikisha kwamba, mwekezaji huyu anapewa hiyo *Certificate* ili mambo yaende vizuri katika eneo lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio mwisho kwa umuhimu, Mheshimiwa Waziri kuna Kiwanda cha Nyama cha Ruvu, kimekufa na hakuna dalili ya kufufuka. Mheshimiwa

Waziri anajua wakati kaka yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba akiwa kwenye Wizara ya Kilimo, nilipata nafasi ya kwenda naye pale kwenye kiwanda akaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, Serikali katika kuonesha kwamba, iko tayari kuhakikisha kwamba kiwanda kile kinafufuka ilinunua mashine nzuri kwa ajili ya kuja kufunga ili kiwanda kiweze kufanya kazi, lakini la kushangaza kiwanda kile na mashine zilizopo pale havifanani. Kwa hiyo, kukawa na mapendekezo ya kukipanua lakini mpaka sasa hivi hakuna juhudi zozote wala maelezo yoyote katika Kitabu cha Bajeti cha Mheshimiwa Waziri ambayo yanaeleza juu ya mkakati wake kama Waziri au kama Wizara juu ya kuhakikisha kwamba, kiwanda kile kinafufuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwambie tu Mheshimiwa Waziri, tunapolia vilio vya mifugo katika Jimbo la Chalinze, tunapolia vilio vya mifugo katika Tanzania, jibu lake ni kuwa na viwanda vya kusindika na kuchakata nyama kama hivi ambavyo vinatakiwa vifanye kazi. Mheshimiwa Waziri aisaidie nchi yake, akisaidie chama chako, tunahitaji kuweka utaratibu ulio mzuri ili mambo yaweze kwenda vizuri katika Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, maana sisi Wanasiasa tuna mwisho na mwisho kabisa! Sasa hapa mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri katika uwekezaji lazima kuwe na utayari wa Serikali. Utayari huo nimeuona, lakini nataka niuone kwa vitendo. Mheshimiwa Waziri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwani, muda wako umekwisha.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono sana hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Getrude Pangalile Rwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Elibariki Kingu ajiandae.

**MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Namshukuru Jehova Mungu wa Mbinguni, Elishadai, mwenye uwezo wa kunirudisha tena Bungeni. Namshukuru kwa afya na uzima, wote tumeweza kufika salama na kulinda familia zetu, Mungu wetu ni mwema. Bwana asifiwe sana. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Amina! *(Makofi)*

**MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda nimshukuru Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniona, kunikumbuka na kunitewa kuwa Mbunge wa Viti Maalum katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mungu ambariki sana, sana, sana na Mungu amlinde. Namwahidi nitamwomba, Mungu ampe afya njema, Mungu aweze kumpa uongozi bora na kuwe na amani na utulivu kabisa siku zote za uongozi wake. Mungu ampe maisha marefu, aishi akiona vijukuu hadi vitukuu kwa utukufu wa Bwana. Kwa kweli ni mwema, ni mwaminifu; kwa kweli ni mchapakazi, ni jembe; ni komandoo na anaweza. Ahadi yangu kwake sitamwangusha, nitaendelea kumwomba siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena niwashukuru wanawake wote wa *UWT* Tanzania nzima kwa maombi, kwa simu zao za kunitia moyo na kunipongeza. Naahidi pia kwamba nitafanya kazi na *UWT* kwa uwezo wangu wote. Wanawake, kaeni mkao wa kula, nakuja tufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kushukuru Kanisa langu la Mlima wa Moto, Mikocheni 'B', *Assemblies of God* kwa maombi yao; nikianza na Wachungaji, Wazee wa Kanisa na Washirika wote. Ahsanteni kwa maombi yenu. Nashukuru. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Haleluya!

**MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mungu wetu ni mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru familia yangu. Mama yangu mzazi, familia yangu, kaka zangu, dada zangu na watoto wangu wote. Ahsante kwa kunivumilia na kunitia moyo. Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Amina!

**MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Pia naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na pia Watanzania wote, kwa msiba mkubwa tulioupata kwa kupotelewa na watoto wetu kwa ajili ya basi huko Karatu. Mungu aziweke roho zao mahali pema, peponi.

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Nawaombea wazazi wao faraja, nawaombea Mungu awape amani, wakubali yote kwa sababu kazi ya Mungu haina makosa. Bwana alitupa na Bwana ameatwaa, jina la Bwana libarikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii niweze kuchangia katika hotuba hii nzuri ya Wizara ya Viwanda Biashara...

**WABUNGE FULANI:** Waliongea bila kutumia vipaza sauti.

**MHE. DKT. GETRUDE P. LWAKATARE:** Eeh, jamani, mimi Mchungaji, msinitanie! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii niweze kuchangia katika hotuba hii nzuri ya Wizara ya Viwanda Biashara nikianza kumpongeza kwanza kabisa Waziri, Mheshimiwa Mwijage, shemeji yangu. Anafanya kazi

nzuri kwa kweli. Kazi imepata mtu! Siyo mtu amepata cheo, lakini ukweli cheo kimepata mtu sahihi. Anafanya kazi nzuri, tunafurahi na timu yake yote. Yaani kama uhamasis haji, ameufanya, tumeona wawekezaji wakiingia na kutoka Tanzania; tumeona kwamba viwanda vingi vimefunguliwa na hata hivyo tunaona pia juhudi yake, bado anajitahidi. Hata kama watu wakitupa madongo, nasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Jamani, mtoto wa Kihaya anafanya kazi nzuri, tumshukuru. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumtia moyo Mtumishi wa Mungu Mheshimiwa Mwijage pamoja na timu yake ya kwamba aendeleo mbele, azibe pamba masikio; mema ayachukue, lakini yale ambayo ni ya kukatisha tamaa ayaache. Abantu baabi! Wahaya wanasema: "watu wote siyo wema, wengine wabaya." Kwa hiyo, jipe moyo, songa mbele."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa asilia inajulikana kwamba watu wengi humshukuru na kumsifu mtu akifa. Siku ya tanzia ndiyo wanasema ooh, alikuwa hivi, alikuwa hivi. Kwa hiyo, usijali, songa mbele. *Rome was not built in a day, you have tried.* Umejaribu ulivyoweza. Lazima tuanze kidogo, polepole tutapanda, huwezi kuamini, pengine baada ya miaka mitano Tanzania ndiyo itaongoza kwa viwanda vingi kuliko kote *East Africa* nzima. Kwa dira hii tunayoiona tumeridhika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe ushauri kwa sababu kwa kweli kazi ni nzuri sana na mwanga tunauona. Ushauri wangu wa kwanza, ni punguzo la kodi. Jamani kodi Mheshimiwa Waziri ungekaa na Waziri wa Fedha mkaangalia ni jinsi gani mnaweza kutoa *incentive* ya kutosha kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na hata wa nje. Yaani kodi ni kikwazo, kwa sababu kwa kweli ukihesabu, kodi ni nyingi mno. Zinakatisha tamaa, hata mwisho ukijaribu kujumlisha unakuta kwamba faida ni ndogo sana. Inakatisha tamaa wawekezaji na wengine wanafunga kabisa viwanda au wanafunga kabisa biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ya Viwanda inawezekana, lakini pia tuangalie hao wanaowekeza; wanakopa, wana madeni na wana mambo mbalimbali. Kwa hiyo, lazima tuangalie na sisi kama Serikali tuone tunawasaidiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ushauri wangu mwingine, nasema pia ili kuwa na Tanzania ya viwanda, ni lazima kuwe na umeme wa uhakika. Umeme wetu kwa kweli siyo wa uhakika. Kama mnavyoonona, mara nyingi unakatika na pia tozo inakuwa kubwa mno. Hasa ukiwa na kiwanda, ndiyo kabisa, yaani jiandae kulipa mamilioni. Hata kama unatumia *diesel*, vile vile hata *diesel* ni bei. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ni kweli!

**MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Kwa hiyo, unakuta kwamba mwenye kiwanda anakata tamaa, maana yake faida ni ndogo mno. Kama kweli tungekuwa nao bega kwa bega kwa kuwasaidia pamoja na kuhamasisha kuja kuwekeza Tanzania, pia tuwasaidie na wao waweze kupata faida ili walipe madeni yale ambayo wamekopa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rwakatare, muda wako umekwisha.

**MHE. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, atafuatiwa na Elibariki Kingu na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, ajiandae.

**MHE.VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia machache kwenye hii Wizara yetu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya. Natambua wako baadhi ya watu wanabeza yale mafanikio yanayopatikana, lakini hii ni kwa sababu tu kwamba kila mmoja ana uhuru wa kutoa mawazo yake, ndiyo maana anaweza kuzungumza hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi kubwa anayofanya Mheshimiwa Rais, kwanza ya kukusanya mapato, lakini na kusimamia mapato hayo, hiyo tu inaonesha kwamba Rais wetu amedhamiria kuhakikisha kwamba nchi yetu inapiga hatua nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niendeleo kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya. Hata nilikuwa napitia hiki kitabu chake, Mheshimiwa Waziri, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu; moja, nataka tu kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Kiwanda cha *MUTEX* cha Musoma. Kama unakumbuka, kiwanda hiki tumekizungumza kwa muda mrefu, toka mwaka 2005 nazungumzia hatima ya wafanyakazi waliokuwa wa Kiwanda cha *MUTEX*. Wale wafanyakazi baada ya kile kiwanda kubinafsishwa, hadi leo hawajalipwa haki zao. Kwa hiyo, wengine wako pale, hawana namna ya kuishi. Sasa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hili tumeshalizingumza wote, kesho namsubiri tu kwenye shilingi, kama hajatoa majibu sahihi, basi sina namna ya kuweza kuiachia shilingi yake. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni hii Idara au Shirika letu la Viwango (*TBS*). Sasa hivi huko mjini kuna msako mkubwa unaoendelea na wanafanya kazi ya kuharibu zile bidhaa zote ambazo hazikukidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo moja; zile bidhaa zote ni bidhaa ambazo zinapita katika njia halali, lakini hawa watu wetu wa *TBS* wanao wawakilishi kule kutoka kwenye nchi husika ambao wana-*certify* kwamba zile bidhaa



zina haki ya kuingia nchini. Sasa zikishafika humu, mtu kalipa na ushuru lakini kinachofuatia, tunasema hizo bidhaa zote zinateketezwa, yakiwemo mfano, mabati na bidhaa nyingine kama hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati mwingine unajiuliza, hivi kweli hilo bati hata kama basi makosa yameshafanyika, hilo bati ni *gauge* labda tuseme 34 badala ya 32, hivi ukillinganisha na nyasi, ni lipi bora? Kwa hiyo, nilidhani unahitaji utueleze una mikakati gani kuhakikisha kwamba zile bidhaa tunazizua kule kule, kuliko vile ambavyo Watanzania tunaziingiza ndani, halafu zinakuja kutupatia hasara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, naomba nizungumzie suala la viwanda. Ni kweli kwamba hii nchi uchumi wake unaweza ukajengwa na viwanda. Kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri mwenyewe amesema tunavyo viwanda vya aina tatu; viwanda vidogo, viwanda vya kati na viwanda vikubwa.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi binafsi, nisingependa sana tuka-*support* hivi viwanda vikubwa na ninazo sababu za kimsingi ambazo nasema ni vizuri nguvu zetu tukazielekeza kwenye viwanda vidogo. Kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri kwenye *page* ya tisa, yeye mwenyewe ametoa ushahidi hapa akasema, katika Tanzania asilimia 99.5 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeangalia hata katika nchi nyingine, mfano Kenya ni asilimia 98, Malaysia asilimia 97, Ujerumani asilimia 99 pamoja na nchi nyinginezo. Kwa hiyo, huo tu ni ushahidi tosha ambao unadhihirisha kwamba kumbe tunahitaji nguvu kubwa zaidi tuelekeze katika vile viwanda vidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuzungumzia viwanda vidogo bila kuzungumza habari ya *SIDO*. Kwenye *page* ya 68 Mheshimiwa Waziri amesema hivi; "Shirika la *SIDO* ndiyo Taasisi ya Serikali yenye thamani ya kuendeleza viwanda

vidogo nchini.” Sasa kama hivyo ndivyo, Mheshimiwa Waziri ameizungumzia *SIDO* nusu *page*, lakini tunakubaliana kwamba asilimia 99 ya viwanda vya hapa nchini vinapaswa kujengwa au kusaidiwa na *SIDO*. Kwa hiyo, ombi langu la kwanza ni kwamba hebu tuisaidie *SIDO*, tuipe uwezo ili iweze kusaidia hivi viwanda vidogo vidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaambie tu jambo moja, kwamba asilimia kubwa ya kazi inayopaswa kufanyika katika viwanda, ni suala la *packaging*. Labda nitoe mfano mdogo; ukienda hapo sokoni, kuna ile asali imeandikwa “Asali ya Pinda,” tunamshukuru sana Waziri Mkuu Mstaafu kwa kazi nzuri aliyofanya. Robo ya bei ya ile asali ni sawasawa na lita moja ya asali inayotoka Tabora. Hiyo yote ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu ya *packaging*. Kwa hiyo, kumbe tukiendelea kuwasaidia hawa *SIDO*, maana yake ni kwamba watasaidia watu wetu wengi; kwanza, katika kupata mafunzo ya *packaging* na zile bidhaa karibu nusu tutaendelea kuzitumia hapa kwetu nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naendelea kushauri zaidi kwamba Mheshimiwa Waziri tuangalie uwezekano wa kuendelea kuisaidia *SIDO* na kuijengena uwezo. Tena kwa yale mafunzo ambayo wanayapata, yataleta tija zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, juzi tuliona Rais wa Afrika Kusini alipokuja hapa, alikuja na wafanyabiashara wasiopungua 80, lakini kwetu sisi jambo hilo hatulifanyi. Ni ukweli usiopingika kwamba zaidi ya asilimia 80 ya wafanyabiashara ambao tunawafahamu elimu yao kama wameenda sana, ni elimu ya sekondari. Kwa hiyo, ni kwamba viko baadhi ya viwanda vingi wangeweza kuvileta, lakini kwa sababu ya ile *exposure* ambayo wangesaidiwa, wangeweza kufanya vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kubwa, leo Tanzania hakuna *incentives* kwa ajili ya viwanda vidogo, isipokuwa ipo kwa ajili ya viwanda vikubwa. Kwa hiyo, nadhani hilo nalo Serikali ilipaswa ilianganalie, ione namna ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ajjandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba nikishukuru kiti chako kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mfupi katika bajeti hii ya Wizara ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Mwijage na pia naishukuru Serikali ya Chama changu; Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge, nimesoma kitabu hiki cha hotuba ya Kambi ya Upinzani *from page one* mpaka *page* ya mwisho. Ukurasa wa tatu, hotuba ya Kambi ya Upinzani wamesema Serikali ya Chama cha Mapinduzi imechoka kiakili na uwezo wa kufikisha ndoto za Tanzania ya Viwanda, *it is impossible*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kilichojaa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani ni malalamiko, hakuna *alternative* ya nini kifanyike kwa mustakabali wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Mwijage, kuanzia mwanzo mpaka mwisho amejikita kwenye *program, planning, strategy* na namna ya ku-*industrialize* nchi. Kwa hiyo, kama ni watu waliochoka akili, *it is the Opposition Camp* ambao kimsingi *this is nothing! Absolutely nothing!* Malalamiko mwanzo mpaka mwisho. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Very good!*

Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hizi Taarifa uzipuuze ili kusudi niweze kuwapa dozi, ili dawa iweze kuwaingia vizuri. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingu, naomba ukae kidogo upokee taarifa. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

## T A A R I F A

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ni muhimu Mheshimiwa Mbunge akatambua kwamba Taarifa iko kwa mujibu wa kanuni na Bunge hili linaendeshwa kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa Taarifa kwamba kazi ya Kambi ya Upinzani au Chama chochote cha Upinzani katika nchi yoyote ni kuikosoa na kuishauri Serikali iliyoko madarakani. Anaposema kwamba unapolinganisha hotuba ya Waziri na hotuba ya Upinzani, Waziri ndio mwenye Serikali; sisi hatuna Serikali, ila tunaikosoa Serikali iliyoko madarakani.

Kwa hiyo, nataka nimpe hiyo taarifa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei, kwa sababu nilichokisema *from page one to the last page*, hotuba imejaa malalamiko, hakuna *alternative* za *ki-strategy*, mikakati na *source* za kupata *resources* za ku-*industrialize* nchi. Naomba niendeleo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie na Bunge hili nilihakikishie, wengi wanampuuzwa Mheshimiwa Rais John Joseph Pombe...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingu, kuna taarifa nyingine. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Kingu kwamba anatakiwa tu kuelewa kazi ya upinzani; inapoikosoa Serikali halafu ikashindwa kutoa mawazo mbadala kwa mujibu wa utaratibu na yenyewe inaweza kukosolewa pia kwa kutokutoa mawazo mbadala.

Sasa naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Kingu kama hiyo taarifa yangu anaweza kuipokea. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa heshima na taadhima kabisa. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona wawili mmesimama halafu taarifa anayepewa hajaanza kuzungumza bado...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Si ndiyo anazungumza!

**NAIBU SPIKA:** Katika yale mengine huku *Chief Whip* alishasimama, huku amesimama *Chief Whip* mwingine; naomba tuendelee. Mheshimiwa Kingu malizia muda wako. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, wengi wanapuza mikakati ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi katika ku-*industrialize*; lakini nataka nikuhakikishie, ndani ya miaka michache ijayo Rais John Joseph Pombe Magufuli anakwenda kuli-*surprise* Taifa...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** ...kwa kuhakikisha kwamba Tanzania ya viwanda inakwenda kujungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulithibitisha hilo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano, tayari imeshaanza mikakati ya ku-*modernize infrastructure* za nchi. Wenzetu Kenya wamejenga *standard gauge rail* ambayo inatoka Mombasa kwenda Nairobi. Gharama walizozitumia ni Dola bilioni 3.8. Kwa Tanzania, Rais John Joseph Pombe Magufuli anajenga *standard gauge* kwa ukubwa huo huo kwa gharama ya takriban bilioni mbili *US Dollars*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kuonesha kwamba Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli katika ku-*industrialize* nchi amezingatia *three E's* za *economy; Efficiency, Effectiveness and Economy*. Huyo ndiye Magufuli wa CCM na watu wanaotega masikio wakifikiri tutafeli, imekula kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie, mimi binafsi nimesafiri, nimekwenda kutembelea programu mpya;

dada yangu Mheshimiwa Jenista nakupa *big ups* sana, wewe na Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimekwenda Ngerengere; jana hapa tulikuwa tunawatetea wanajeshi, nimejionea barabara zinazochongwa kwa kiwanda kipya cha *five thousand TCD tons*; tani 200,000 kwa mwaka. Nimekwenda Kibigiri, nimejionea programu mpya ya 15 *TCD* kiwanda kinachojengwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Dodoma tunapozungumza, ndani ya miezi mitatu *National Milling* inakwenda kufufuka. Kiwanda cha *National Milling* kinakwenda kuwaka. Tani 60 za unga zinakwenda kuzalishwa na tani 20 za mafuta. Yote ni kazi ya Chama cha Mapinduzi. Taarifa nilizonazo, viwanda vya Mwanza vinakwenda kuwaka na viwanda vyote; *the former National Milling* vinakwenda kuwaka. Wanaosubiri mkono wa mtu uanguke kama fisi, hii imekula kwao. Sisi Chama cha Mapinduzi tunakwenda kujenga viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili; naishauri Serikali yangu ya chama changu, Chama cha Mapinduzi...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama kutaka kumpa mzungumzaji Taarifa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge taarifa sizichukui tena. Nachukua kuhusu utaratibu ikiwa kuna kanuni inavunjwa. Kwa hiyo, kuhusu taarifa naomba mkae.

Mheshimiwa Kingu, malizia muda wako umebaki kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ninaloishauri Serikali yangu ni kwamba wajomba zangu wa Kanda ya Ziwa wameteseka kwa miaka mingi katika kilimo cha pamba. Natoa ushauri Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda wafanye *coordination*. Tunahitaji tuanzishe *large irrigation scheme* za kikanda ambazo zitawa-*accommodate* wakulima wetu wa pamba waweze kuwa

na *sustainable agriculture* ambayo itaweza ku-*provide raw material* kwenye viwanda tunavyotaka kuvijenga. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa kwanza nilifanya *private tour* kwa nchi za Ujerumani, Turkey na Russia; *textile industry* tukiamua kuwa *serious* kaka yangu Mheshimiwa Mwijage, *we have trust and confidence in you*; tukiamua kufanya *fully utilization* ya *resources* tulizonazo, mito na ardhi, nataka niwahakikishie, ajira ya vijana wanaomaliza Chuo Kikuu tunakwenda kui-*curb over just within three years*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa Serikali ya chama changu, tuanzishe *large irrigation scheme*; mito Simiyu tukaitege, mito ya Manonga na Igunga tukaitege, tuvune maji tuwe na *large scale agriculture*. Hii peke yake ndiyo itakwenda kulikomboa Taifa kutokana na adha tuliyonayo ya ukosefu wa ajira kwa vijana katika masuala mazima yanayohusiana na viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tu-*engage protectionism approach* kulinda viwanda vya ndani. Tunalindaje viwanda vya ndani? Hili nalizungumza, nina uhakika huenda hata vyombo vya usalama humu ndani; kuna watu wanataka ku-*temper* na uchumi wa nchi yetu, lazima tuwe *very serious* na lazima tuwe wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, hivi karibuni kuna watafiti fulani kutoka Marekani na nataka niwaambie haya maneno kwa sababu tabia ya Mataifa ya ki-*capitalist* wanapoona nchi changa zinataka kukomaa kiuchumi, wanaanza kupandikiza mambo ya hovyoy ili kutuvuruga. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kingu muda wako umemalizika. Ahsante sana.



**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Kidumu Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mwijage, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana, ameonyesha umahiri wake kwa kujitahidi kuanzisha hivi viwanda ambavyo ametusomea kwenye hotuba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niongee machache kuhusu Mkoa wangu wa Morogoro. Nianze kwa kupongeza. Naishukuru Serikali yetu kwa jinsi inavyoweza Mkoa wetu wa Morogoro kwa viwanda ambavyo vinatarajiwa kujengwa. Ni viwanda vingi kiasi. Nikianza na viwanda vya Nyama, Matunda, Kiwanda cha Sukari ambacho kipo Mkulazi watajenga na Kiwanda cha Mbigili Sukari, watajenga; pamoja na Kiwanda cha Sigara ambacho na chenyewe kitajengwa Morogoro; na bila kusahau *Morogoro Star City* ambapo vitajengwa viwanda mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hivi viwanda viweze kujengwa kwa wakati ili viweze kuajiri hasa vijana pamoja na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimaliza kusema hivyo, kwa Mkoa wangu wa Morogoro kuna viwanda ambavyo vilibinafsishwa na havifanyi kazi. Kwa mfano, Kiwanda cha *Canvas*, Kiwanda cha Ngozi, Kiwanda cha *Ceramic*,

MOPROCO na Kiwanda cha *Juice* ambacho kipo Kingorwila. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amesema kuwa viwanda hivi hasa MOPROCO pamoja na *Canvas* viko karibu kuanza. Naomba viweze kuanza kusudi viweze kutoa ajira hasa kwa vijana pamoja na akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba kuvipongeza na kuwapongeza wale wawekezaji wa viwanda vya Morogoro ambavyo mpaka sasa hivi vinafanya kazi na vinaajiri sana akinamama na hasa vijana, wasichana na wengine. Nikianza na Kiwanda cha Tumbaku; kiwanda hiki kinaajiri akinamama wengi na kinafanya kazi masaa 24. Kwa hiyo, nawapongeza kwa kazi hiyo nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Mtibwa Sukari kinafanya kazi, Kiwanda cha Kilombero K1 na K2 vinafanya kazi; Kiwanda cha Maji ya Udzungwa kinafanya kazi vizuri na Kiwanda cha Nguo kinafanya kazi. Bila kusahau Mazava, ingawa Mheshimiwa Waziri amesema hakifanyi kazi, lakini kinafanya kazi ambapo kuna vijana wengi hasa wa kike, wanafanya kazi kwenye kiwanda hicho. Kwa hiyo, nawapongeza kwa sababu wanasaidia vijana, akinababa na akinamama hasa wa Mkoa wa Morogoro kwa kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo hapa, wananchi wengi Tanzania asilimia 75 wanategemea kilimo, lakini viwanda vya mbolea ni matatizo bado. Naomba kuuliza Mheshimiwa Waziri, Kiwanda Mbolea cha Kilwa – Lindi ni lini kitaanzishwa? Pia hapo hapo, Mheshimiwa Waziri alisema kuwa kuna kiwanda cha Pwani, nacho naomba aelezee kidogo kama ni cha mbolea. *(Makofi)*

Pia namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Mheshimiwa Rais, pia waweze kupanua wigo kwa upande wa viwanda vya kilimo pamoja na pembejeo kwa sababu asilimia 75 ya wananchi wanategemea kilimo na kwenye kilimo ndiyo tunategemea uchumi wa mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema viwanda tunamaanisha mambo mengi. Hatuwezi kuwa Tanzania ya viwanda kama hatuna umeme na hatuwezi kuwa Tanzania ya viwanda bila kutegemea kilimo. Ni lazima tuwe na umeme kwa upande wa nishati na kilimo kwa upande wa malighafi. Pia ni lazima tuwe na maji; huwezi kuwa na kiwanda bila ya maji. Vile vile ni lazima tuwe na ardhi na miundombinu muhimu ikiwepo barabara, reli na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kushirikiana na hizi sekta kusudi tuweze kuanzisha hivi viwanda na Tanzania iweze kuwa Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu fedha za miradi. Kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeona kuwa mpaka Machi mwaka huu fedha za maendeleo ilikuwa ni asilimia 18.92. Ikiwa fedha za maendeleo hazitoki, ni shida sana kufanya maendeleo ya viwanda. Kwa hiyo, nashauri kuwa fedha tunazozipitisha hapa Bungeni ikiwezekana ziweze kutoka na kupelekwa kwa wakati kwenye miradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi nikamaliza bila kuongelea wanawake. Wanawake wa Kitanzania wamejitoa sana kwenye biashara. Wanafanya biashara ndogo, za kati na biashara za Kimataifa, matatizo yaliyopo ni masoko. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iwajengee mazingira mazuri waweze kupata masoko na kuuza bidhaa zao. Pia hapo hapo, naomba waweze kuunganishwa na TBS pamoja na TFDA kusudi mazao yao na bidhaa zao ziweze kuwa na thamani ya kuweza kuuzwa ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wangu wa Morogoro bado una ardhi kubwa. Bado tunaomba zaidi na zaidi wawekezaji hasa kwenye viwanda vya maziwa, kwa sababu bado tunazo ng'ombe na kwenye kilimo bado tuna sehemu kubwa ambayo tunaweza kulima matunda, kuendelea kulima mpunga ingawa kuna wawekezaji, lakini hawatoshi.

Kwa hiyo, naomba sana tuweze kupata hao wawekezaji na madawa ya kilimo pamoja na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *SIDO*; huwezi kufanya viwanda hasa viwanda vidogo vidogo bila ya *SIDO*. Kwa hiyo, naomba sana kuwepo mkakati maalum ambao unaweza ukawaunganisha hawa wafanyabiashara pamoja na *SIDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na Mwenyezi Mungu akubariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Antony Calist Komu ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hii Wizara ya Viwanda na Biashara. Kipekee kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya Wizara hii. Pamoja na pongezi hizo, ninayo maswali hasa katika Mkoa wangu wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nikiangalia bajeti hii ya leo ya 2017/2018, kweli imezungumzia kwa habari ya kuwezesha kuwekeza kwenye miundombinu. Katika ukurasa wa 122 wa kitabu, imezungumzia kwamba Wizara imejipanga kujenga miundombinu hasa ya viwanda katika Mikoa mbalimbali ikiwemo na Geita, Dodoma pamoja na Katavi. Vilevile imejipanga kujenga mabanda ya viwanda kumi katika Mikoa hiyo hiyo ya Dodoma, Geita, Katavi, Manyara na Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kujenga hiyo miundombinu, lakini katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri hajaweza kuzungumzia kabisa habari ya kufufua viwanda. Katika Mkoa wa Geita tunavyo viwanda ambavyo vimekufa.

Kwa mfano, kuna kiwanda cha kuchambua pamba pale Kasamwa. Vilevile katika Wilaya ya Chato tunaona jinsi ambavyo hakuna ambacho amekiandika katika hotuba hii. Kwa hiyo, wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* naomba kufahamu kwamba Serikali inajipangaje kufufua hivi viwanda ambavyo kwa muda mrefu havifanyi kazi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vilipokuwa vinafanya kazi viliweza kuajiri vijana wengi katika Mkoa wa Geita na wengi walinufaika na kufaidika, lakini hapa sijaona. Kwa sababu azma ya Awamu ya Tano ni awamu ya viwanda; na nchi ya Tanzania kuelekea kwenye viwanda, kwa hiyo, ni vyema tuangalie uwezekano wa kuweza kufufua viwanda ambavyo kwa muda mrefu havifanyi kazi ili wananchi katika maeneo waweze kufanya shughuli katika viwanda hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Halmashauri ya Wilaya yangu ya Geita, kuna watu walitoka Wizara ya Viwanda na Biashara, walisema wanataka kuanzisha Kiwanda cha Sukari katika Tarafa ya Butundwe pale Salagurwa, lakini nimejaribu kuangalia kwenye kitabu cha bajeti sijaona mpango wowote katika suala hili. Napenda kupata maelezo kuhusiana na uanzishwaji wa kiwanda hicho katika Tarafa ya Butundwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Mkoa wa Geita hatuna viwanda kwa kweli. Wananchi wameitikia sana huu wito wa kuwa na viwanda katika Taifa la Tanzania na wanasubiri viwanda hivyo. Leo hii tunaona jinsi ambavyo muda unakwenda, lakini hatuoni viwanda. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kabisa anapo-*wind up* hasa katika Mkoa wangu wa Geita juu ya suala la viwanda, tunajipangaje? Tunawekaje mkakati ili wananchi waweze kunufaika na viwanda hivi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kuangalia katika suala la miundombinu; nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali hasa kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kuweka mpango

wa kujenga barabara ya lami kutoka Kahama kwenda Geita kupitia Bukoli. Barabara hii itawezesha kusafirisha bidhaa mbalimbali pamoja na kuwezesha suala zima la viwanda katika eneo la Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba katika upande wa barabara Serikali inajitahidi, napenda pia kuulizia upande wa umeme. Vijiji vingi havina umeme. Kama kweli tuna nia ya dhati ya kufanikisha suala la viwanda, ni vizuri Serikali iweze kuhakikisha sasa inafanya utekelezaji wa mpango wa kuleta umeme hasa vijijini, kwa sababu ni kweli kwamba Serikali ina mpango wa *REA* awamu ya tatu kuleta umeme katika vijiji mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa pia kusikia kutoka Wizara ya Nishati na Madini, waniambie kwamba ni lini sasa watahakikisha umeme unawaka katika vijiji na hasa katika Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Geita ili kuhakikisha kwamba ile azma ya viwanda inaweza kufanikiwa kwa sababu kuna umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wanapokuja mahali, wanaangalia kama kuna miundombinu muhimu inayohitajika; kama hakuna umeme, wawekezaji hawawezi kuja; kama hakuna barabara, hawawezi kuja na kama hakuna maji, haiwezekani wawekezaji wakaja katika eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji, tuna Ziwa Victoria, liko pale. Serikali iwezeshe upatikanaji wa maji ya uhakika ili wawekezaji wanapokuja waweze kukuta miundombinu ikiwa safi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri alizungumzia kiwanda cha kutengeneza matrekta kule *TAMCO*, Kibaha, lakini sasa hajaelezea kiundani kwamba ni namna gani basi wananchi wataweza kupata matrekta kwa ajili ya kuwezesha kilimo? Naomba pia Mheshimiwa Waziri

anapo-*wind up* aweze kuwaeleza wananchi namna tutakavyoweza kupata matrekta ili tuweze kuimarisha kilimo na kufanikisha suala la viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la elimu; nikiangalia Mkoa wa Geita tuna wilaya tano, hatuna hata Chuo cha *VETA* hata kidogo. Haiwezekani tukafikia uchumi wa viwanda bila kuwa na elimu; bila kuwa na *VETA*. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, ishirikiane na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba kila wilaya, sawasawa na Sera ya Taifa ya Elimu na Ufundi Stadi, kwamba kila wilaya inatakiwa iwe na Chuo cha *VETA*. Kwa sasa katika mkoa wetu hatuna Chuo cha *VETA* hata kimoja. Wilaya zote tano hatuna Chuo cha *VETA*. Hata katika mkoa hatuna Chuo cha *VETA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natumia fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri kushirikiana na Mawaziri wengine wa Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI tuhakikishe kwamba tunakuwa na Chuo cha *VETA* katika kila Wilaya katika Mkoa wa Geita ili wananchi, hasa vijana wetu wanaomaliza elimu ya sekondari ambao hawaendelei na masomo mengine, waweze kupata elimu ya ufundi stadi, hatimaye waweze kufanikisha azma ya kuweza kufikia maendeleo ya viwanda. Bila ujuzi, haiwezekani kabisa kufikia maendeleo ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, katika suala zima la maji; napenda kuiomba Serikali kwamba iwekeze zaidi hasa katika miundombinu ya maji. Kwa sababu ukilinganisha na maeneo mengine hakuna maji, lakini sisi katika Kanda ya Ziwa tuna Ziwa Victoria ambapo tukilitumia vizuri tuna uhakika wa kuweza kupata malighafi. Tunalo zao la pamba na mazao mengine ambayo yanakubali. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anapo-*wind-up* aweze kuelezea. Watu wa Mkoa wa Geita wana shauku ya kuwa na viwanda... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Muda wako umekwisha.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Antony Calist Komu na Mheshimiwa Katani Katani ajjandae.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza napongeza hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Komu, Waziri wetu Kivuli, lakini pia napongeza hotuba au mchango uliotolewa na dada yangu, Mheshimiwa Riziki pamoja na Mheshimiwa Mwaifunga pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Kivuli, Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwelekeza ndugu yangu, Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Kingu, ajaribu kuchukua hotuba ya Upinzani ukurasa wa 42 na 43 atajua namna gani *brain ya Oppostion* ilivyo. Hili ndilo tatizo, kwamba watu wengine wanasoma hivi vitabu kwa kutumia miwani ya mbao. Hilo ndilo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba watu wote wenye vitabu vya rangi hii; na kaka yangu Mheshimiwa Mwijage, asome vizuri hotuba ya Upinzani pamoja na Kamati ya Viwanda na Biashara, zitamusaidia sana. Acha maneno ya *sound* hizi nyingine zinazotoka kwingine... (*Makofi*)

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Nafikiri...

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Kanuni?



## KUHUSU UTARATIBU

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lwakatare kaa. Mheshimiwa Ulega, kuhusu utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Kanuni ipi?

**MBUNGE FULANI:** Ataje Kanuni.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, Kanuni ya 68, naisoma pamoja na Kanuni ya 64(a), (b) na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutokupoteza muda, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri Mwijage asiyachukue maneno yale, maana maneno yale kama alivyosema Mbunge aliyetangulia, Mheshimiwa Kingu, ni ya watu waliochoka...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** ...hayana mbadala. Kwa hiyo, yeye asikilize maneno ya watu wanaomshauri asonge mbele. Ahsante sana.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *This is too much bwana!*

**MBUNGE FULANI:** Mnachezea muda wa Bunge ninyi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Ni hivi, Kanuni ya 68 inaruhusu kutoa taarifa ambayo Spika...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** (Hapa aliongea nje ya *microphone*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, kama wewe unajua, kuna ambao hawajui, subiri niwaelekeze. Naomba mtulie, nimeomba kuhusu utaratibu. Kwa hiyo, tulieni niwaelekeze vizuri.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, mnanichelewesha kuzungumza...

**MBUNGE FULANI:** Endelea:

**NAIBU SPIKA:** Siwezi kuendelea, kwa sababu ninyi nanyi mmekuwa Wenyeviti tena. Tusikilizane tafadhali! Tusikilizane na wewe utulie, Mheshimiwa Esther Matiko.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68 (1) inamruhusu Mbunge kuomba kuhusu utaratibu na Mbunge huyu anapaswa kutaja Kanuni iliyovunjwa; na wakati huo Kiti kitatoa kuhusu huo utaratibu kama kuna Kanuni imevunjwa ama hakuna Kanuni iliyovunjwa na mchangiaji anayechangia. Sasa kwa sababu michango itaendelea, kuhusu utaratibu ni tofauti na mtu anayetoa taarifa. Kwa upande wa taarifa, Kiti kina uwezo wa kusema muda unakwenda kikazuia taarifa. Kuhusu utaratibu maana yake, kuna Kanuni inavunjwa na Bunge hili haliwezi kuvumilia Kanuni inapovunjwa.

Sasa nimeombwa utaratibu na Mheshimiwa Ulega kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) akataja na Kanuni ya 64(1) amesema (a), (b) na (c).

Waheshimiwa Wabunge, ukisoma hii Kanuni ya 64 inataka ukiwa unaitumia utaje kitu mahususi ambacho kimevunja Kanuni hiyo. Kwa sababu hiyo, kuhusu utaratibu nilioombwa na Mheshimiwa Ulega, hakuna Kanuni iliyovunjwa na Mheshimiwa Lwakatara, naomba uendele. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Message sent.*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naamini bado dakika zangu tisa zilizokuwa zimebaki, ziko palepale. Matatizo yote haya nafikiri *ambulance* zitatoa watu roho hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua wazi kabisa, kaka yangu Mheshimiwa Mwijage, Waziri wa Wizara hii; Wizara hii ndiyo mlezi wa wafanyabiashara, ni mlezi wa watu wanaotaka kufanya biashara, ni mlezi wa watu wanaotaka kukuza biashara, ni mlezi wa watu wanaotaka kuweka mitaji katika biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahali huwa najiuliza kwamba wakati wa vikao vya *cabinet* kama kweli Mawaziri mnamsaidia Mheshimiwa Rais inavyopasa. Kwa sababu pale inapokuja kutokea kila Wizara kuendesha operesheni zake kivyake vyake bila *coordination* kuonekana kama Serikali inafanya kazi, mimi huwa nachanganyikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunapozungumza, wafanyabiashara wakijua fika kwamba Wizara hii ndiyo mlezi, wanakamatiwa mali, wengine wanakamatiwa magari yakiwa barabarani, eti kwa sababu kuna gari ambayo imesimama miaka sita hajalipa *road license*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kituko kimemgusa Msukuma mmoja alikuwa amepakia samaki anatoka Mwanza anakwenda Dar es Salaam, akasimamishwa na Maaskari gari likapelekwa kituoni. Msukuma akalia akasema kwamba pesa niliyonayo yote imemalizika katika kusafirisha; niko tayari kulipa faini pindi nitakapofikisha mzigo wangu mahali unapokwenda, lakini walimng'ang'ania na samaki wakaoza akaenda kupaki hiyo gari katika kituo. Hii ukiangalia kwa undani ni kukosa busara na akili ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara kama mlezi mama wa wafanyabiashara, naomba ichukue jukumu lake kama mlezi wa wafanyabiashara. Hivi sasa mazingira siyo

rafiki kwa wafanyabiashara. *Policies* zinabadilika badilika, haieleweki! Yaani siku hizi watu wanakaa kwenye TV na redio, hawajui kiongozi akiwa kwenye ziara atazungumza kitu gani. Lolote linaweza likabadilika! *Policies* zinabadilika! Wafanyabiashara hawako tayari kuwekeza kwenye mazingira ambayo hayaeleweki kwamba leo na kesho itakwendaje? Naomba hili mliangalie sana. *Playrole* ya kulea wafanyabiashara, mazingira yawe rafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Bukoba, wafanyabiashara, wajasiriamali waliowekeza kwenye mashine za unga, *TFDA* wamekwenda pale na kufunga biashara ya kusaga unga kwa sababu tu wanataka watu wajenge ma-*godown* au wajenge nyumba kubwa za kuweka mashine kwa kutumia matofali.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli hiyo imesababisha Bukoba Mjini unga umepanda bei kwa sababu ya maamuzi ya mtu mmoja tu. Ukienda Halmashauri, wale wafanyabiashara wanashindwa kujenga hayo ma-*godown* kwa sababu hawajapata vibali toka Halmashauri ambayo ni *owner* wa eneo hilo. Sasa unakuta maamuzi ya mtu mmoja tu yanakuwa tatizo kwa watu wengi na mazingira yanakuwa siyo rafiki kwa wafanyabiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Mwijage, watu wangu wa Kashai, Soko Kuu, Rwamishenye, pale sokoni Kibeta Uswahilini wanataka awaeleze, pesa iko wapi? Pesa imekwenda wapi? Mzunguko wa pesa mbona mbaya? Mtu anapanga nyanya mshumaa, *ntongo*, yaani inaanza ikiwa Azam, inabadilika rangi inakuwa Yanga, mwisho inakuwa Simba na matokeo yake hakuna anayeinunua *ntongo* tena. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanataka kujua pesa inakwenda wapi, mbona kodi wanalipa? Nitaomba kwa lugha nyepesi awaeleze wafanyabiashara pesa imekwenda wapi? Inafungiwa wapi? Kufuli gani hili? Ni kubwa kiasi gani linafungia hela? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yupo kiongozi mmoja aliwahi kusema kweli kwamba jero itaitwa mia tano; buku itaitwa 1,000; na mtu mwenye kifua cha kukaa Dar es Salaam kama atavuka mwezi wa Saba, basi huyo ni mwanaume. Nafikiri huko ndiko tunakoelekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, benki sasa hivi zinashindwa hata kukopesha, hata uwe na nyumba yenye hati, kwa sababu hata zile watu walizokopesha kwa kutumia *collateral* za nyumba, haziuziki; benki zinashindwa hata kuziua. Pesa haizunguki! Pesa haipo!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwijage, akija hapo mbele atueleze, pesa iko wapi? Watu wafanyaje? Waipatie wapi? Waifukuzie wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wa Bukoba walio-*supply* taasisi za Serikali wanadai mpaka sasa hivi zaidi ya shilingi milioni 900 kuelekea shilingi bilioni moja; na kwa bahati mbaya wafanyabiashara hawa, wengi ndiyo wale waliokuwa na nyumba zilizopigwa na tetemeko. Sasa walitarajia hata kale kadogo kalikochangwa na wadau angalau wangekatiwa kidogo. Sasa hivi ni maskini, hawawezi kukopa kwa sababu hawana *collateral*, nyumba zina nyufa lakini pia hawawezi kukopeshana kwa sababu hela iko mikononi mwa taasisi za Serikali, hazijawalipa, wanafanyaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, pia atambue Bukoba imepigwa tetemeko la mwezi wa Kumi; juzi hapa limepiga lingine, mafuriko yamepita! Nashukuru Mheshimiwa Profesa Muhongo atakwenda Bukoba na wataalam wake kuweza kutoa ripoti ya athari ya tetemeko na aina ya miamba, uchunguzi wao. Hiyo itakuwa ni taarifa ya kuhusu tabia za miamba ili tuweze ku-*project* watu wa Bukoba kwamba wanaweza kujenga nyumba za namna gani? Tuletewe michoro ya Japan, ya Australia, ya Paris ili tupewe ushauri wa nyumba za namna gani zinazoweza kuhimili matetemeko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, huyo ni Mheshimiwa Profesa Muhongo, nampongeza sana. Kwa upande wa Mheshimiwa Mwijage, hizi athari za wafanyabiashara ambao sasa, yaani kwanza Bukoba imeshakuwa *dangerous zone...* (Makofi)

(Hapa kengele lilia kushiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lwakatare, ahsante. Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Antony Calist Komu, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani na Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze mchango wangu kwa kueleza masikitiko yangu juu ya kauli ya Mheshimiwa Elibariki Kingu, kijana mdogo ambaye kwa kweli niliamini kwamba angekuwa ni mtu makini, mtu ambaye anasema ukweli na mtu ambaye angekuwa analiongezea hili Bunge hadhi (*value*) kuliko kuzungumza vitu ambavyo kimsingi mtu yeyote anayesikiliza, hataelewa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe umetoa sifa, leo umetoa *complement* kwamba katika hotuba ambazo zimeshatolewa hapa ndani ya Bunge kutoka upande huu, hii ni moja ya hotuba ambazo ni *role model*. Sasa anatokea mtu mmoja anasimama na anasema ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho hakuna kitu chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza huu ni uongo. Maneno kama haya yakivumiliwa ndani ya Bunge hili, maana yake hata hadhi ya hili Bunge na Kiti chako wewe mwenyewe vitakwenda kuathirika.

Kwa hiyo, napenda... (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip!*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane! Mheshimiwa Esther, sijamaliza kuzungumza, kwa nini unaniwekea maneno mdomoni? Unajua ninachotaka kumjulisha yeye? Tuwe tunatulia jamani! Tuwe na utulivu, sisi wote ni viongozi.

Mheshimiwa *Chief Whip*, taarifa nimezizuia, naruhusu kuhusu utaratibu kwa sababu ni uvunjifu wa Kanuni. *(Makofi)*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nilichokuwa nataka kusema ni kwamba waliosoma hiki kitabu kwa sababu wanacho, kina ushauri mwingi sana. Mtu akikushauri, maana yake anakupa *alternative*. Sasa huyu Mheshimiwa Kingu anavyosema hakuna ushauri wowote, ni malalamiko na hakuna mkakati wowote; Mheshimiwa Lwakatare amerejea hapa maeneo ambayo yanaonesha mkakati ambao unaweza ukatumika kama mbadala.

Kwa hiyo, naomba iingie kwenye *record* kwamba Mheshimiwa Kingu amesema uongo na amejaribu kupotosha na kwa kweli kitu alichofanya kinafedhehesha hata Bunge lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komu, kwa namna ile ile ambayo hotuba yako inasema hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni hewa, ina mambo mengi ya hewa, ni namna hiyo hiyo Mheshimiwa Kingu alikuwa anaisema hotuba ya kwako wewe. Kwa hiyo, usije ukatoa maelekezo hapa ya kusema iingie namna hiyo kwenye *Hansard*, hapana. Hayo maelezo ya kuingia kwenye *Hansard*, mimi ndio niliyekaa hapa, naweza kuagiza.

Sasa wewe endelea na mchango wako, lakini *Hansard* haitaondolewa. (Makofi)

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naamini kwamba utakuwa umetunza muda wangu, kwa sababu kwa kweli umetumika ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema na hii ni kauli ambayo nairudia mara kwa mara kwamba ni vizuri Serikali ikaweka vipaumbele vichache. Tukiwa na vipaumbele vichache, maana yake tunaweza kujipima na kujua kwamba tunatoka wapi na kwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi hapa wamezungumza habari ya Mchuchuma na Liganga. Kama tungekuwa tunajiwekea vipaumbele na tukaamua kujua kwamba ni kipi ambacho tunataka kukifanya na kwa wakati gani, haya malalamiko ambayo yameelezwa hapa yasingekuwa yamejitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kulishauri kwa nguvu zote ni suala la Serikali kufanya biashara, kujiingiza katika shughuli za kiuchumi moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Waheshimiwa Wabunge tuwe kitu kimoja na tuishauri Serikali kwa nguvu zetu zote kama Bunge kwamba suala hili ni jambo ambalo huko siku za nyuma lilishafanyiwa uamuzi na baada ya kufanyiwa uamuzi ingekuwa ni busara kama tunataka kutoka hapa tukapata muafaka sasa wa Kitaifa kwamba sasa tunaondoka kwenye utaratibu huu, kwenye utamaduni huu, kwenye sera hii tukaenda kwenye huo utaratibu mwingine wa Serikali kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mchango wa Mheshimiwa Shabiby ambaye alizungumza hapa *from practical point of view* kwamba yeye ni mfanyabiashara na akashauri kwa nguvu zake zote kwamba hata hii biashara



ya ndege ambayo Serikali imeamua kuingia, kama tunataka ifanikiwe, Serikali ikae mbali na hiyo *management* ambayo imewekwa kwa ajili ya kuendesha hiyo biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukichukua mifano kama hiyo, utaona kwamba ni vigumu na haitawezekana kabisa kwamba Serikali ikafanya biashara. Tunao mfano mmoja ambao ni mdogo. Juzi juzi hapa; na bahati nzuri wewe mwenyewe ndio ulihusika kikamilifu, mlikabidhi Serikali shilingi bilioni sita kwa ajili ya kwenda kutengeneza madawati. Wakaamua kutengeneza madawati yale kwa kutumia vyombo vyake vya Ulinzi na Usalama (SUMA JKT na Magezea). Mpaka tunavyoongea hapa siku ya leo, shilingi bilioni sita madawati hayajaweza kukabidhiwa kila mahali ambapo yalipaswa kupelekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe katika Halmashauri yangu ya Moshi hatujapewa hayo madawati kwa sababu tuliambiwa tukachukue hayo madawati kule Nachingwea na watu wengine wengi bado wanadai hayo madawati. Katika utaratibu wa namna hii, unakuta kwamba malengo ambayo yamepangwa hayawezi kufikiwa; hakuna tija wala ufanisi. Huo uamuzi wa Serikali ambao ulikuwa sahihi sana wa kutumia fedha zile wa kwenda kutatua tatizo la madawati, maana yake haikuwezekana. Kwa sababu kama kweli kulikuwa na kero ya madawati, mpaka leo miezi kadhaa hayajafika sasa tunafanya kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia jambo lingine ambalo ni la msingi sana kwenye masuala haya ya viwanda na biashara, hili suala la Serikali kushindana na wadau wa biashara katika nchi; na lenyewe linayumbisha sana uchumi wetu. Kwa mfano, sasa hivi Serikali imeamua kwamba fedha zake zote zitoke kwenye benki za biashara na benki binafsi ziende kukaa Benki Kuu kwa sababu tu wanafikiri kwamba zile fedha za Mashirika au za Serikali zinatumiwa na benki zetu kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini jukumu la Serikali katika kufanya nchi istawi kiuchumi? Mahali pengine Serikali inatoa

hata ruzuku kwa ajili ya benki zisianguke, zifanye vizuri; lakini kwetu pesa ziko pale, hazina kitu chochote ambacho kinainyima Serikali, Serikali inaamua tu kuwa na wivu fulani, kuwa na msimamo ambao ni hasi kwa wafanyabiashara wake na benki zake, zinakwenda kuwekwa Benki Kuu, zinakaa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijiuliza, hivi huo uchumi ni uchumi gani ambao unakufanya wewe uone wivu dhidi ya benki zako kufanya vizuri? Kwa sababu benki zikifanya vizuri, maana yake hiyo ni ajira inayotokana na watu wanaofanya kazi ndani ya benki. Benki zikifanya vizuri, zitakopesha watu ambao watakwenda kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimia Naibu Spika, hata haya aliyouliza Mheshimiwa Lwakatare pesa ziko wapi, niseme pesa ziko Benki Kuu kwa sababu zimeondoka kwenye mzunguko wa kawaida. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaelewa kwamba inao wajibu wa kujenga mazingira rafiki na wezeshi kwa ajili ya watu na sekta binafsi kufanya biashara kama hizo Benki na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maamuzi mengi ya Serikali ambayo yanafanywa bila kujali kwamba biashara au uchumi katika nchi utaathirika kwa kiasi gani. Haya nimeyaeleza kwenye hotuba yangu, lakini napenda nitie msisitizo kwenye jambo hili kwa sababu ni jambo ambalo linaathiri sana biashara na mara nyingi ukikutana na wafanyabiashara, ukikutana na wenye viwanda na wawekezaji, malalamiko yao ni hayo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua jinsi ambavyo Serikali inakuwa au wanakuwa wakali inapokuwa kwamba wanadai labda fedha kwa ajili ya ushuru, wanadai fedha kwa ajili ya kodi...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Komu. Muda wako umekwisha.

Mheshimiwa Katani Katani, atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, tutamalizia na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia nami naomba tu kuwapa maelezo ndugu zangu hao wa upande wa pili kwa maana ya chama tawala, kama Mheshimiwa Kingu na Kaka yangu Mheshimiwa Ulega pale; Serikali hii ya Awamu Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, siyo ukipiga piga maneno ndiyo anakupa Uwaziri, hakupi Uwaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote ukiwaangalia waliopewa Uwaziri, Unaibu Waziri, ni watu makini, wametulia, siyo maneno maneno ya siasa. Sasa kama mnataka Uwaziri kwa namna hiyo, Uwaziri huo haupo na bahati nzuri hakuna *reshuffle*, nimenusa! Kwa hiyo, mnapokuja hapa, muwe na hoja za msingi za kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikubaliane na wewe Mheshimiwa Kingu, sisi Wapinzani tutasema na Serikali ndiyo inatekeleza. Kwa hiyo, unaposema hatuna *alternative*, sisi hatuko kwenye mamlaka. Kweli hatuna *alternative!* Tutashauri tu. Nyeie wenye mamlaka ndiyo mna wajibu sasa tunayoyashauri kuyafanya au kutoyafanya. Sitarajii tukija kwenye Wizara nyingine mtapiga ngonjera hapa na kwaya zenu za vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye michango yangu kuhusu Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

Mheshimiwa Waziri, sisi watu wa Mtwara na Lindi mara nyingi nasema tumesahaulika sana. Nikikukumbusha Mtwara na Lindi tulikuwa na viwanda vya kubangua korosho takribani 11. Pale Newala Mjini tulikuwa na viwanda viwili, Mtama tulikuwa na kiwanda kimoja, Masasi tulikuwa na kiwanda kimoja, Lindi tulikuwa na kiwanda kimoja, lakini viwanda hivi tunavyozungumza, Serikali ya Awamu ya Tatu,

ilivibinafsisha viwanda hivi na baadaye ikaja kuviuza viwanda hivi kwa bei chee. Wengine waliouziwa wamekuja kufanya ma-*godown* viwanda vya kubangua korosho; lakini wengine ni watumishi wa Serikali. Unaona ni dili lilifanywa! Nami naamini Mheshimiwa Waziri yuko makini na Serikali hii ya Awamu ya Tano iko makini, mtakwenda kuvichukua viwanda vile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Newala pale, vile viwanda viwili, bei iliyouziwa haifiki shilingi milioni 300, viwanda viwili! Hebu tukimaliza Bunge hili Mheshimiwa Waziri aende ufuatilie haya ninalomwambia. Sasa wanataka tuwe na Tanzania ya viwanda, viwanda ambavyo Mwalimu Nyerere alifanya kazi kubwa; akaona Kusini kuna fursa ya kuweka viwanda vya kubangua korosho kwa ajili ya kuongeza thamani. Leo korosho tunai-*export* mpaka inatoa ajira. Wahindi wanakuja kununua korosho hapa, *Vietnam* wanakuja kuchukua korosho hapa, tuna-*export* ajira zinakwenda India pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda India, wale Wahindi wanaofanya kazi ya kubangua korosho kazi ambazo Wamakonde wanaweza. Bahati nzuri viwanda vya kubangua korosho havihitaji mitaji mikubwa kama watu wanavyofikiri. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, watu wanakuwa hawamwelewi, lakini mimi namwelewa kweli kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilimtumia *memo* moja nikawa naulizia suala la kiwanda cha sabuni, alinipa *alternative*. Kweli nilipokwenda Kibaha pale, ile thamani aliyoniambia nimeikuta iko hivyo hivyo, shilingi milioni nane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu walitaka kuleta kiwanda cha kubangua korosho chenye thamani ya shilingi bilioni 37, hata India hakuna kiwanda cha namna hiyo. Sasa fursa ya viwanda vile ambavyo vimechukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tatu kwa bahati mbaya, najua kwa bahari mbaya; kuna watu wapiga dili na kuna watu wanakuja kwa

ajili ya kazi; nami naamini Mheshimiwa Waziri umekuja kwa ajili ya kazi. Twende kule maeneo ya Kusini uone viwanda vile vilitolewaje na namna gani tunaweza kuvirudisha ili sisi wakulima wa korosho sasa tunufaike na viwanda vile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka kwangu Kitama, Kijiji nilichozaliwa ukaenda Kijiji jirani cha Miuta, palikuwa na kiwanda pale cha *NDC*; kile kiwanda kimekufa. Ukija Kitama ambapo mimi nipo, pana kiwanda cha kubangua korosho pale, kile kiwanda kinahitaji mtaji mdogo wa kuongezewa. Nasi kwenye korosho umeona taarifa; kwa kupitia *Export Levy* tumekusanya kwa taarifa ya Serikali mpaka mwezi wa Pili mwaka huu zaidi ya shilingi bilioni 980.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya sasa, tumekusanya zaidi ya shilingi trilioni moja kwenye korosho. Sasa pesa zile za *Export Levy* kwa sababu zinakaa tu, uangaliwe utaratibu aidha, hata kwa kupitia *SIDO*, watu wakopeshwe pesa wajenge viwanda vidogo kule.

Mheshimiwa Waziri, Mtwara Mjini pale eneo lile la Mikindani kulikuwa na viwanda pale. Zamani wakati mimi nakua, palikuwa na Kiwanda cha Mashua, Mikindani pale. Vile vile palikuwa na kiwanda cha *Coca Cola* Mikindani pale. Viwanda vie vimepotea na wala hatujui vimepoteaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho, nataka ajaribu kunipa maelezo, vile viwanda vimetekwa, vimekwenda wapi? Maana havipo! Ilikuwa fursa kubwa kwa watu wa Mtwara-Mikindani na maeneo ya Uwanda wa Pwani kwenda kununua vifaa vya uvuvi pale kwa sababu kulikuwa na viwanda pale. Leo tunapozungumza, hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshauri Mheshimiwa Waziri, kwa nafasi yake, najua anaweza; leo wafanyabiashara wakubwa, wawekezaji wakubwa kama Bakhresa anatengeneza *juice*. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge,

*juice* bora kabisa yenye *Vitamin C* ambayo haina shaka kabisa, inatokana na Mabibo ya Korosho. Sasa Mheshimiwa Waziri amshauri mwekezaji yule mkubwa aje Tandahimba pale na Halmashauri inaweza ikampa eneo tu la kutosha aweke kiwanda pale atengeneze *juice* ya matunda na Waheshimiwa Wabunge wapate *vitamin* ya kutosha hapa kwa ajili ya mustakabali wa afya zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, japo kuna wakati walikuja wawekezaji kadhaa na nimwombe Mheshimiwa Waziri ili alifuatilie, ajaribu kuwasiliana na Profesa Aba Mpesha aliyepo Marekani. Wapo wawekezaji wazuri na najua ana mawasiliano nao mazuri, wako tayari kuja kujenga viwanda vya kubangua korosho Tandahimba, lakini kuna watu wanaleta chenga pale katikati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwamini Mheshimiwa Waziri, ni mtu muhimu sana na mara zote huwa nawaambia, mkiwa mnafanya mambo mazuri Watanzania wakayaona, watawapongezeni. Kwa mfano, Kusini ambako viwanda hatuna, barabara hakuna, kila kitu hatuna; umeme shida, maji balaa! Mtakaa mkitegemea CCM mtachaguliwa kwa matatizo haya? Hebu mje mmalize haya matatizo kwanza; myamalize haya mambo! Msije mkafanya Kusini kama *scraper*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazungumzaji wamezungumza hapa, wakati tunazungumza hata suala la reli ile ya kutoka Liganga, ni stori tu. Stori hizi siyo kwamba zimeanza kwenye Serikali yenu. Nimesoma bajeti kipindi cha Awamu ya Nne, kuanzia 2010 historia hiyo ipo kwenye makabrasha; 2011/2012 ipo kweye makabrasha; 2012/2013 ipo kwenye makabrasha; 2014/2015 kwenye makabrasha; mwaka jana (2016/2017) tumepiga makabrasha kwenye Wizara hii; mwaka huu, tumeizungumza tena. Ile ilikuwa inatoa fursa kwa watu wa Kusini kule kote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Mtwara ingefunguka kwa kiwango kikubwa. Mikoa hii ya Kusini; Mbeya, Ruvuma, Njombe, watu wangepanya kazi na ajira

hizi ambazo leo Tanzania ambako kuna bahati mbaya kwamba watu wake hawaajiriwi, eti kwa sababu hawawezi Kiingereza, lakini ukienda Dangote pana Wachina sijui 700 na hawajui Kiingereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya viwanda, kwanza huu utaratibu huu wa Kiingereza, wakija Wachina wasiojua Kiingereza wanaajiriwa na Kiswahili hawajui, wanaajiriwa; Watanzania wenyewe wanakosa fursa kwa vitu vya ajabu ajabu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana, mimi namwamini sana Mheshimiwa Mwijage, nakuamini sana. Namwomba sana aone mambo haya anayafanyia kazi kwa uzuri ili *at least* watu wa Tandahimba na wenyewe wakipata kiwanda cha *juice* pale, wakipata viwanda vidogo vile ambavyo Profesa Aba Mpesha, tayari ana wawekezaji mkononi, watu wale watapandisha thamani ya korosho zao, watapandisha thamani ya mabibo, yale ambayo badala ya kuanika tukapika gongo, tutakunywa *juice* watu mkapata *vitamin C* na mambo yakaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimewataja Wabunge wawili wa kumalizia ili twende vizuri na uwiano. Kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (5) naongeza nusu saa ili hawa Wabunge wawili waweze kumalizia muda wao. Mheshimiwa Zitto Kabwe tutamalizia na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. KABWE Z. R. ZITO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara muhimu sana. Pili, nampongeza sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kwa hotuba ambayo imeweza kuchambua, kukosoa na kutoa mapendekezo ya namna gani ya kuboresha. Vile vile, nampongeza Mwenyekiti

wa Kamati ya Viwanda na Biashara kwa kuleta maoni ya Kamati na maoni ya Kamati ndiyo maoni ya Bunge, kwa sababu Kamati inafanya kazi kwa niaba ya Bunge. Naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri ataweza kuyafanyia kazi yote haya; hotuba ya Waziri kivuli na hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ili kuweza kuboresha kazi ambazo tunafanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 mwezi kama huu tulipokutana kwa ajili ya kujadili hotuba ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Tanzania ilikuwa inauza nje bidhaa za viwanda za thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 1.4 kwa mujibu wa taarifa ya Benki Kuu ya mwezi Machi, 2016. Bidhaa za viwanda ziliingizia Taifa mapato ya fedha za kigeni wakiwa ni wa pili baada ya utalii na wakiwa mbele ya dhahabu ambayo iliingiza Dola za Kimarekani bilioni 1.2; utalii bilioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumekutana mwaka mmoja baadaye kwa kuchukua mwezi Machi, 2016 na mwezi Machi, 2017 bidhaa za viwanda ambazo tunauza nje, zimeshuka kwa Dola za Kimarekani milioni 500 kutoka 1.4 mpaka *0.9 million Dollars*. Sasa tunaposimama hapa na kusema kazi inafanyika, Mheshimiwa Waziri atusaidie kwamba iwapo kazi inafanyika, kuna ongezeko la uzalishaji, ni kwa nini mauzo yetu nje yamepungua kwa kiwango kikubwa kiasi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo mambo ambayo ni vizuri sana Waheshimiwa Wabunge wazingatie. Kwa sababu bidhaa za viwanda zinazouzwa nje zinavyopungua, maana yake ni kwamba viwanda vyetu vya ndani vimepunguza uzalishaji; maana yake ni kwamba kuna watu wapoteza kazi; maana yake ni kwamba kuna mapato ya Serikali ambayo yamepotea. Sasa ndani ya miezi 12, tumepoteza mauzo nje kwa zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 500. Sijui ikifika 2020 kama kutakuwa kuna hata senti moja ambayo tutakuwa tunaipata kutokana na mauzo nje. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tuna tatizo kubwa kwamba tuna viwanda ambavyo vimekuwepo, lakini uwezo wetu wa kulinda viwanda vyetu umekuwa ni mdogo sana. Mheshimiwa Waziri ni shahidi wa malalamiko ambayo anapelekewa kila mwezi ya watu ambao wanaingiza nguo kinyemela katika nchi yetu, wanaingiza mafuta ya kula kinyemela katika nchi yetu, wanaingiza *battery* kinyemela katika nchi yetu, zinakuwa na bei ndogo; na matokeo yake ni kwamba viwanda vya ndani vinashindwa kushindana nao katika soko na tunapoteza ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano mzuri sana; jana niliangalia takwimu za kiwango gani cha *battery* tumeagiza kutoka China kwa miezi sita ya kwanza ya mwaka 2016. Ukienda Idara ya *Customs* ya *China*, utakuta kwamba kati ya Januari mpaka Septemba, mwaka 2016, kwa *records* za *China*, tuliagiza *battery* za thamani ya Dola za Kimarekani milioni 36.5, kwa takwimu za *China*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kuangalia Idara yetu ya Forodha hapa, *battery* ambazo zimeingia nchini na ukilinganisha na *TBS*, *battery* ambazo wamezifanyia ukaguzi kuona ni ngapi zimeingia nchini ni za thamani ya Dola za Kimarekani milioni 5.3. Maana yake ni kwamba, kuna *battery* nyingi sana ambazo zinaingia nchini hazipiti katika njia za kawaida. Viwanda ambavyo vinazalisha *battery* hapa nchini kama *Panasonic* ambavyo vimeajiri watu, vinashindwa ku-*compete* na hizo *battery* zinazotoka *especially China*. Matokeo yake ni kwamba tutaongea humu kuhusu viwanda lakini *in real sense* tunaviua hivyo viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ambayo tungetegemea kuona Mheshimiwa Waziri akihangaika nayo, kwa sababu wahenga wanasema “Ni bora ndege ambaye unae mkononi kuliko ndege ambaye yuko juu ya mti ambaye unataka kwenda kumtungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo nataka kulizungumzia; sisi tuna miradi mikubwa mingi sana,

miradi mingine ni ya mabilioni ya fedha. Kuna miradi ambayo inatoa fedha nje na kutengeneza ajira nje. Kwa mfano, manunuzi ya ndege, tunaposema tunanunua *boeing*, maana yake ni kwamba tunapeleka ajira Marekani. Kuna miradi ambayo inatengeneza ajira ndani na ingeweza kwa kiwango kikubwa kuchochote ukuaji wa Sekta ya Viwanda na mfano mzuri sana ni reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi wa zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni saba kwenye reli. Reli *raw materials* zake ni nini? Sehemu kubwa ni chuma. Unahitaji tani 50 za *steel*, chuma cha pua, kujenga kilomita moja ya reli. Sasa hivi sisi tumewapa Waturuki mkataba. Wataagiza kila chuma ambacho kinakuja kwenye reli yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Deo pale amezungumzia Mchuchuma na Liganga; siyo kama hatuna chuma; tunacho chuma Mchuchuma na Linganga. Kabla ya kuanza kufikiria kutandika haya matararuma ya reli, ilitakiwa tuwe tayari tumejenga uwezo wa kuzalisha kule ili fedha zote zibakie ndani ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashindwa kuelewa; mimi kwa kweli sielewi. Hivi Mheshimiwa Mwijage mnakaa kwenye *Cabinet* Baraza zima, mkajadili hii mipango? Kwa sababu mkikaa, lazima kuna mtu atasema aah, huu ujenzi mimi miradi yangu fulani itaweza kufaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga mabehewa. Mabehewa yana viti. Hivi wamefikiria namna gani ya kuendeleza zao la katani ili viti vya kwenye mabehewa viweze kuwa ni viti vya katani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *concrete*, mmeandaa vipi watu ambao wanazalisha kokoto kwa ajili ya ku-*supply* kwenye reli? Hili ndiyo fungamanisho, kwa sababu una fedha, una dola shilingi bilioni saba zitakazoingia ndani ya nchi, *over a period of five years or seven years*, hizi fedha kama *seventy percent* zinatoka nje, tunafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, angalieni *interior decoration* za mabehewa, ni ngozi. Mmekaa mkafikiria namna gani ya kufungamanisha Sekta ya Ngozi na mabehewa? Haya ndiyo mambo ambayo tungependa kuyaona tukiyajadili. Kwa sababu hizi huhitaji *foreign direct investments*, hizi ni fedha ambazo tayari mnaziingiza. Ni kiasi cha kuingia kwenye mikataba na kuweza kufanya. Kwa hiyo, sasa hivi sisi kwenye reli tutafaidika na nini? Ajira tu! Ajira za vibarua baada ya zile, hakuna kuchochewa kwa... (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu Mkuu wa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda ni Mwalimu wangu wa *Economics*. Mwaka wa tatu amenifundisha *input, output modal*. Sekta zote za uchumi, yaani unachukua sekta, njia hii na njia hii, ukiingiza kwenye *transport* unapata nini kwenye *manufacturing*? Unapata nini kwenye kilimo? Unapata nini kwenye nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sitaki kumwambia Profesa Mkenda kwamba nimrudishie *degree* yake. Kwa sababu yeye ndio Katibu Mkuu *responsible* wa hii Wizara; yeye pamoja na mwenzake Dkt. Meru. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ni mambo ambayo yanapaswa kutengenezewa mkakati, tusipoteze fedha. Kwa sababu ni fedha zetu! Tena tunasema tunajenga kwa fedha za ndani, lakini fedha za ndani zitaenda kutengeneza reli India au China au Uturuki, ziletwe hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwaambia hapa wakati nachangia mchango wa Wizara ya Uchukuzi. Kumbukeni bomba la gesi, kila kitu ambacho kimejenga bomba la gesi kimetoka China. *Nothing* ambacho kimetoka hapa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Wizara wakae upya waangalie, fungamanisho ndiyo *solution*. Tutaweza kupiga hatua kubwa na kuchochea maendeleo makubwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatumia fedha za miradi yetu kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa leo ni hayo tu. Usia wangu ni huo tu, sina mengine ambayo nataka kuyachangia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto. Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mwisho ya kufunga dimba kwenye siku hii ya leo. Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kila mtu ana uhuru wa kutoa maoni yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi kusema, Mheshimiwa Komu alitumia Ibara hii kutoa mawazo yake, yanaheshimika; akasema, Hotuba ya Waziri ni hewa, *the same* alichokifanya Mheshimiwa Kingu kutoa uhuru wake wa mawazo aliposema haina *alternative*. Katika mazingira kama haya tuvumiliane tu. Ukijua kucheka, lazima ujue na kulia. Sindano inapointilia, ndiyo pale pale inapotoka. Kwa hiyo, tuvumiliane tu, tuendele. Kwa hiyo, ili isinipotezee muda, niende kwenye hoja yangu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne na Awamu ya Tano, tuliona mkakati wa kukuza viwanda kwenye Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Nyerere. Ikaenda ikakuza viwanda ikatuachia viwanda vikubwa sana na viwanda vidogo vidogo. Katikati hapa viwanda vikafa na vingine vikauzwa. Hatukuwahi kupata matumaini mpaka ilipofika Awamu ya Tano. Ilipokuwa kwa kauli yake ya kusema sasa Tanzania inakwenda kwenye nchi ya viwanda ili twende sambamba na mpango wetu wa maendeleo ifikapo mwaka 2025 angalau tufike kwenye uchumi wa kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nayasema haya? Nayasema haya kwa sababu tunaona kabisa kuna dhamira ya dhati ya kwenda kule. Kusema ni neno moja na kutenda ni neno lingine. Tukumbuke tunakuja kwenye mkakati huu mkubwa. Kipindi tukiwa na miaka zaidi ya 20 ya kusuasua

kwa viwanda, kwa namna yoyote ile ni lazima tuanze popote, aidha, tumeanza kwa usahihi sana au kwa kukosea, lakini tulipoanza tumeanza sehemu sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hadithi moja inaitwa hadithi ya jongoo na mwana jongoo. Jongoo alizaa jongoo mwana, sasa alipomwona mama yake akitembea, jongoo mwana akamwuliza mama, nina miguu mingi sana nitatembeaje? Jongoo mama akamwambia mwana, anza na wowote. Jongoo mwana alipoanza na wowote akatembea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takribani miaka 20 tumekwama kwenye viwanda, tunauliza tutoke na mguu gani? Mheshimiwa Mwijage, aanze na mguu wowote, mwisho wa siku tutatembea. Tukisema tulie kwenye mkakati, tulie kianze kipi, *in process* tutajua jinsi ya kwenda, lakini ni lazima tuanze na tulipoanza tumeanza sehemu sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema ni sehemu sahihi? Kwa hoja zote za kiuchumi zinafsirika. Hoja ya *input, out put* zinatafsirika vizuri tu. Ndani ya mwaka mmoja, Julai, 2016 mpaka Machi, 2017 vimesajiliwa viwanda 170. Kati ya hivyo, viwanda 54 vipo kwenye hatua ya ujenzi na viwanda 17 vimeanza kufanya kazi ndani ya mwaka mmoja. Huko ndiko tunakosema jongoo anza na mguu wowote, mbeleni huko tutapata njia ya kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, niseme mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema na nitarudia tena kusema. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, tunapotaka kutengeneza viwanda aidha vimekuwa viwanda vikubwa au vidogo, ni *commitment* kubwa ambayo tunaifanya kwenye uchumi wa nchi yetu. *Factors* nne hizi lazima siku zote zituongoze na zituelekeze kwenye kujenga Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni jambo la umeme (*power*), jambo la pili ni watu (*manpower*), jambo la tatu ni *raw materials* na la nne ni mtaji. Haya mambo yote ukiyaangalia ndiyo yanaweza yakatuhakikishia kwamba ndani ya miaka hii mitatu au minne tutakwenda kwenye Tanzania ya viwanda kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejuliza ni kwa kiasi gani kwa viwanda hivi vidogo vidogo ambavyo nchi karibu zote zilizoendelea kama Malaysia, Ujerumani, China, walianza? Walianza na zile asilimia 89 mpaka asilimia 99 viwanda vidogo vidogo (*small scale industry*). Kule majumbani, mtu anaweza akakamua maziwa yake ya ng'ombe akatengeneza siagi, akaenda akauza, ndiko tunakoongelea. Hivi *in process* huko mbele ndivyo vitapelekea kukua kwa viwanda vingine vikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanabeza hivi viwanda vidogo. Niseme, tumeanza sawa sawa, ila inabidi tufanye marekebisho kwenye vitu vifuatavyo: tuna viwanda vidogo vidogo vya SIDO ambavyo vinatengeneza mashine ambazo zinaweza zikawasaidia hawa watu wanaoendesha viwanda vidogo vidogo. Vile vile tuna Shule za VETA; naomba Serikali *i-link* hizi sekta mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anayesoma VETA akifuzu mafunzo yake aunganishwe na SIDO kwa kile alichokuwa amejifunza ili SIDO impatie vitendea kazi kwa mkopo. Anapozidi kuendeleza ile sekta ya ufundi wake ataleta tija na viwanda vidogo vidogo vitakua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tutaimba mpaka jua litakuchwa na kucha kama hatujaona *agriculture* ndiyo sehemu pekee itakayokuza viwanda, hatutatoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuitengeneze ramani ya nchi yetu kwa *zone*. Sehemu wanayolima pamba, sasa tufikirie

kuwa na kiwanda cha *spinning* kwenye maeneo ya pamba. Sehemu wanayolima mahindi, sasa tuwe na *mills* kubwa ya kutengeneza sembe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii watu wa Rukwa, watu wa Songea, watu wa Mbeya na Iringa wanauza gunia moja la mahindi kwa shilingi 40,000 mpaka shilingi 60,000. Likienda kwenye yale makampuni yanayonunua mahindi, pumba ili ulishe ng'ombe wako na mifugo yako, gunia moja la pumba ambalo tunaita makapi ni shilingi 200,000. Tukitengeneza hizi *mills* kwenye haya maeneo, tutakuwa tumewasaidia wakulima na Tanzania ya viwanda tutaiona bila shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maeneo wanalima alizeti. Leo hii mafuta ya *Korie* yanauzwa bei chini, lakini mafuta ya alizeti ya Singida, ya Dodoma mpaka Kibaigwa, unapata shilingi 18,000 mpaka shilingi 20,000 kwa ile galoni la lita tatu. Kwa nini tufike huko? Kuna gharama zinakwenda kwa yule mkulima mdogo ambazo Serikali iki-*intervene*; nilipoongea kwenye eneo la *power*, kwenye kuwakopesha mashine ili waweze kukamua, tutatoka. Ndiyo hiyo hoja tunayoiongea ya *import* na *export* kwa nini vinakuja? Kwa sababu tunavyozalisha kwanza havitutoshelezi na hata kama tunazalisha gharama yake inakuwa kubwa, *automatic* kutokana na hali yetu ya uchumi, tunalazimika kuingiza vitu vya nje kuja hapa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho niseme kuhusu Mchuchuma na Liganga; hapa ndipo kwenye moyo wetu. Ukiuangalia vizuri mradi wa Mchuchuma na Liganga, ndiyo mradi pekee unaofanya Dar es Salaam na Mtwara, Mtwara na Ruvuma, Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya kuja Morogoro itoke katika maana ya reli ya uhakika, chuma cha uhakika na madini mengine. Tunaongelea mwaka huu wa 17, tatizo liko wapi? Kila tukifika tunaongelea Mchuchuma na Liganga, Mchuchuma na Liganga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tunaomba, najua kuna sehemu ataweza kujibibia Mheshimiwa Waziri Mwijage, lakini

nyingine atakuja kujibu Waziri mwenye dhamana. Nawaomba kabisa, suala la Mchuchuma na Liganga, mwaka huu tufunge huu mjadala au halipo; na kama lipo tujue tunatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho tena la mwisho kabisa, nimalizie na la matrekta. Ilikuwa SUMA JKT, ilikuja na vitu vinaitwa *power tiller* na wakulima wakakopeshwa matrekta kwamba sasa tutaondokana na jembe la mkono hatutainamisha tena viuno. Kilichotokea wote tunakijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufanikiwe vizuri, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye sekta hiyo ya *merchanization*, yaani ya kumtoa mkulima kwenye jembe la mkono...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda, muda wako umekwisha.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa michango yetu, kuhusu hoja ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa tangazo hapa kwamba kesho hakutakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho tarehe 18 Mei, 2017, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.54 Usiku Bunge Liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 18 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*